

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 25 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwalishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**  
Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):**

Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA - MSEMADI WA UPINZANI WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni yake Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 324

**Sheria Ndogo Katika Halmashauri**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI (K.n.y. MHE. WILFRED M. LWAKATARE) aliuliza:-**

Kwa kuwa, ziko taratibu zilizowekwa bayana na Serikali kwamba, pindi Halmashauri inapotunga Sheria Ndogo haina budi Sheria hizo kabla ya kujadiliwa na kupitishwa na wahusika zitangazwe na kufikishwa kwa wananchi.

- (a) Je, pale ambapo wananchi wanang'amuwa kuwa Sheria Ndogo katika Halmashauri zao zinatumika kinyume na utaratibu wa kuzipitisha Sheria hizo wanawenza kuchukua hatua gani dhidi ya Sheria hizo au mamlaka iliyopitisha bila kufuata utaratibu?
- (b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Halmashauri zenyetabia kama hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:

- (a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Vifungu Na. 148, 155 na 163 vya Sheria ya Serikali za Mitaa Na 7 ya mwaka 1982 Halmashauri za Wilaya, Mamlaka za Miji Midogo na Serikali za Vijiji sawia vyombo hivyo vimepewa madaraka au Mamlaka ya kifungu cha Sheria ndogo. Aidha, Mamlaka za Miji zimepewa madaraka hayo chini ya Kifungu cha 80 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Na. 8 ya mwaka 1982. Vifungu vyote hivi vinatoa sharti la Sheria ndogo kutangazwa kwa wananchi wakazi wa eneo husika kabla ya chombo chenye Mamlaka ya kutunga Sheria hizo ndogo kupitisha Sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, pale wananchi wanapogundua kuwa Sheria Ndogo zinazotumika katika Halmashauri yao hazikuzingatia sharti hilo la kutangazwa kwao kabla ya kupitishwa na Halmashauri na hatimaye kuidhinishwa na Waziri, wananchi hao wanawenzeza kufungua kesi Mahakama Kuu na kuiomba Mahakama Kuu kufuta Sheria Ndogo hizo au wanawenza kuiandikia Halmashauri husika na kuiarifu ukiukwaji wa Sheria na Halmashauri inapaswa kuzifuta Sheria hizo ndogo.

- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikizielekeza Halmashauri zake zote nchini kuzingatia matakwa ya kisheria wakati wa kuandaa Sheria ndogo mbalimbali ili kuepusha uwezekano wa Sheria hizo ndogo kufutwa na Mahakama pale utakapogundulika ukiukwaji. Aidha, utaratibu huu uliowekwa unaendana na Sera yetu ya ushirikishwaji wananchi katika maamuzi mbalimbali yanayohusu maendeleo yao.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu unataka kwamba wananchi watangaziwe na kwa kufuatana na swali la msingi kwa kuwa katika Halmashauri ya Wilaya Karagwe Madiwani nikiwemo na mimi

tulipinga kupitishwa kwa Pori la Kimisi kuwa *Game Reserve* lakini kinyume chake Serikali ngazi za juu kuanzia Mkoaa mpaka Serikalini walipitisha Pori hilo kuwa *Game Reserve*. Je, hili nalo tunaweza kulipeleka Mahakamani au Serikali ifanye uchunguzi na kutamka kwamba ili kwenda kinyume na wawakilishi wa wananchi? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba sheria ndogo kabla hazijatungwa Mamlaka husika lazima ishirikishe wananchi kwa maana ya kutangaza. Kama utaratibu huo ukikiukwa basi wananchi wale wana haki ama kupeleka Mahakama Kuu jambo hili ama kulirudisha kwenye Halmashauri yao ili itazame upya ile sheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mutungirehi anazo hizi njia mbili zote ziko wazi kuzitumia. Lakini hata hivyo hilo suala la pori, sasa kama Kimisi ni *Game Reserve* ya Taifa, sasa mkitunga sheria ndogo inayopingana na sheria mama, sheria kuu ya nchi hapo mtapata matatizo. Lakini kama eneo hilo liko katika Mamlaka yenu basi njia ni mbili ama Mahakama Kuu, ama kurudisha kwenye Halmashauri watazame upya hiyo sheria.

Na. 325

#### **Hadhi ya Mji wa *Usa River***

**MHE. TALALA BANA MBISE** aliuliza:-

- (a) Je, hadhi rasmi ya Mji wa *Usa River* ni nini hasa?
- (b) Je, ni lini Mji huo utapewa hadhi rasmi ya Mji na ni mpango gani unaofanyika kuuandaa kwa hadhi hiyo na suala la maji litakuwa sehemu ya mpango huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwezi Julai 2005, eneo linalojulikana kama *Usa River* lilikuwa na hadhi ya Mji Mdogo, ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru. Baada ya Serikali kutangaza nia ya kupandisha hadhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kuwa Manispaa, kuanzia mwezi Julai 2005 Mji Mdogo wa *Usa River* nao utakuwa ndani ya eneo la Manispaa ya Arumeru. Kutokana na mabadiliko haya ni wazi kwamba Halmashauri mpya ya Manispaa ya Arumeru itakuwa na jukumu la kuimarisha huduma mbalimbali za kijamii na miundombinu ili kulingana na hadhi ya Manispaa.

Namshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Arumeru wawe na subira wakati taratibu za kuandaa rasmi Manispaa hii zinakamilishwa na Serikali. (*Makofî*)

**MHE. TALALA BANA MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na tunashukuru sana kupewa hiyo hadhi ya Manispaa. Tuliomba ilikuwa ni pamoja na kupata hadhi ya Manispaa ya Arumeru Mashariki ikiwa inaitwa Manispaa ya *Usa River* na Manispaa nyingine ya Ngaramtoni. Je, hiyo bado tutazamie kwamba huenda ikawa hivyo kabla ya mwisho wa Bunge hili? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kwanza shukrani za Mheshimiwa Mbunge, tumezipokea kwa furaha na ombi kwamba sasa lile Jiji la Arusha, Manispaa zake ziwe nyingi zaidi, tuongeze na nyingine ya Manispaa ya Ngaramtoni, naweza kusema kwamba haya mambo yanakwenda hatua kwa hatua kwanza mlikuwa hamna Manispaa kabisa Mheshimiwa Talala Mbise, mlikuwa na Mji Mdogo wa *Usa River* sasa mmepata *promotion* kubwa kabisa sasa ni Manispaa ni hatua, ni awamu. *Inshallah* mbele ya safari kama mji ukiendelea kupanuka namna hii basi na Manispaa nazo zitapanuliwa. Tuwe na subira lakini hatua ya sasa ni nzuri kabisa. (*Makofî*)

Na. 326

#### **Viwanda Vidogo Vidogo vya Usindikaji Matunda na Mboga**

**MHE. EDSON M. HALINGA (K.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakulima wengi sana wanafahamu sana suala la kujikwamua kwa njia ya kilimo cha mazao ya muda mrefu na mfupi na kwa kuwa kutambua hili wakulima wengi nchini wanajishughulisha na kilimo cha matunda na mbogamboga kama vile Maembe, Machungwa, Mananasi, Nyanya, Biringanya, Vitunguu, Karoti na kadhalika. Lakini hali yao inabaki pale pale kutokana na kukosa soko la uhakika na matokeo yake mazao hayo huharibika/kuoza, hivyo kuwafanya waone kwamba Serikali yao haiwajali.

- (a) Je, ni lini Serikali itatambua umuhimu wa kilimo hicho hapa nchini na nguvu za wananchi kwa kujenga viwanda vidogo vya kusindika mazao hayo kwenye maeneo husika ili kuwaepushia wakulima gharama za usafirishaji wa mazao hayo kutafuta masoko sehemu mbalimbali?
- (b) Je, Serikali inaweza kuwapatia /au kuwakopesha vifaa kwenye maeneo yao ili waweweze kuunda umoja na kujenga viwanda vidogovidogo kwa ajili ya usindikaji wa mazao hayo au kujenga masoko maalum kwa bidhaa hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kilimo cha matunda na mboga na viwanda vidogo katika kusindika mazao ili kuyaongezea thamani. Pia, naafiki kuwa ujenzi wa viwanda vidogo utasaidia sana kutatua tatizo la masoko na hata ukosefu wa ajira. Kwa kutambua hivi, Serikali hivi karibuni imepitisha Sera ya Viwanda na Biashara Ndogo na Sera ya Biashara. Hata hivyo, ujenzi wa viwanda hivyo, katika mfumo wa uchumi wa soko, si jukumu la Serikali moja kwa moja bali ni la sekta binafsi, ambayo ndiyo injini ya uchumi wa taifa.

Namshauri Mheshimiwa Mbunge, awahamasishe wananchi wake ama kama Vyama vya Ushirika, kampuni za wananchi au wawekezaji mmoja mmoja kushiriki katika kuwekeza kwenye viwanda vidogo hasa vya usindikaji wa vyakula na matunda na wawasiliane na Ofisi ya *SIDO* ya Mkoa wa Mbeya kwa ushauri wa kitaalam.

- (b) Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Sekta ya Viwanda ndogo, Serikali ilianzisha mifuko ya kuhudumia miradi midogo. Mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Kuendeleza Viwanda na Biashara Ndogo (*NEDF*) unaosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na kuendeshwa na *SIDO*. Hadi kufikia mwezi Desemba 2002, mitaji yenye thamani ya Tshs 4.85 bilioni kwa miradi 14,272 ilitolewa. Wilaya ya Mbozi, ilinufaika na utaratibu huu ambapo miradi 20 ya thamani ya shilingi 8 milioni ilihusika. Serikali inaendelea kujenga uwezo wa *SIDO* ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kuhudumiwa. Katika kipindi cha Bajeti cha mwaka uliopita Serikali ilitenga shilingi 1 bilioni kwa madhumuni hayo na mwaka ujao Serikali imekusudia kutenga shilingi 500 milioni kwa ajili hiyo. Vyama vya Ushirika, kampuni za wananchi na vikundi hivyo waombe Ofisi zetu za *SIDO* Mikoani ili wawaandalie michanganuo na ushauri wa kitaalam ambao ndiyo msingi wa kuweza kupata mitaji ya kuanzisha viwanda vidogo vilivyokusudiwa.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nilitaka atueleweshe kama hii hali ya matunda kama Dodoma hapa sasa yanavyoharibika machungwa, machenza na zabibu hivi haoni kwamba ni hasara kubwa na kama *SIDO* ina uwezo huo kwa nini isifanye kazi hii katika kupunguza hasara na nguvu za wakulima kupotea bure? (*Makofî*)

Je, kuna maana gani ya kuingiza nyanya zilizosindikwa wakati viwanda vidogo kama Dabaga vinasindika nyanya hapa, tuchukue nyanya za Afrika ya Kusini, haoni kwamba zinakatisha tamaa hawa wenye viwanda vidogo vidogo hapa nchini, Serikali itachukua hatua gani? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, katika sehemu yake ya kwanza la kuhusu matunda kuharibika. Tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi hilo tatizo hilo la matunda kuharibika. Lakini nimeeleza jitihada ambazo Serikali inafanya kukabiliana na tatizo hili kwa maana ya kuwezesha wananchi ama mmoja mmoja au katika vikundi kuanzisha viwanda vya kusindika hayo matunda ili yasiharibike, *SIDO* wanafanya kazi hiyo, nimeeleza fedha ambazo Serikali inatenga kila mwaka *SIDO* ili wafanye kazi hiyo vizuri. Katika miaka miwili iliyopita *SIDO* tayari imeshatoa Shilingi milioni 688 kwa ajili ya kusaidia miradi kama hii. Kwa hiyo, jitihada zinaendelea. Hapa Dodoma kesho nadhani Rais atazindua kiwanda cha zabibu hapa Dodoma. Hizi ni jitihada za waziwazi ambazo zinafanyika kukabiliana na tatizo ambalo ni tatizo la kweli. (*Makofî*)

Kuhusu nyanya kwamba zinaagizwa za makopo wakati kuna viwanda kama Dabaga hilo ni kweli, tatizo ni kwamba hivi viwanda kama Dabaga bado si vingi kwa hiyo, havikidhi soko. Kwa hiyo, ule upungufu ambao unatokana na viwanda vyetu vichache havikidhi soko, ule upungufu ndiyo unaofidiwa kwa nyanya kutoka nje kuagizwa.

Lakini siku tukiwa na viwanda vya kutosha tukisindika nyanya zetu za kutosha nafikiri suala la kuagiza nyanya kutoka Afrika Kusini, litapungua kama siyo kumalizika kabisa. (*Makofî*)

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuipongeza sana Serikali kwa hatua yake ya kujenga soko la Kibaigwa la mahindi ambapo sasa hivi mtu akitaka mahindi anakwenda mahali pamoja.

Pili kwa kuwa swalilinahusu masoko na kwa kuwa chini ya Wizara ya Ushirika na Masoko kuna mpango wa kujenga masoko ya Kimataifa ya matunda ya mboga mboga kule Segera Mkoa wa Tanga na Makambako. Je, Serikali inataka tuwaambie nini wananchi kuhusu hili ili wajiendae, kuna ujumbe gani angetaka hasa tuwaambie wananchi wa Mkao wa Tanga hususan wa Lushoto pamoja na Jimbo la Bumbuli? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba Serikali ina mpango wa kujenga masoko katika maeneo yanayoitwa *strategic areas* kule Makambako kwa ajili ya soko la matunda na nafaka, lakini vile vile kule Segera kwa ajili ya matunda yote ya Mkao wa Tanga pamoja kule Lushoto anakotoka Mheshimiwa Shellukindo.

Tunachotaka kuwaambia ni kwamba mipango sasa hivi imeandaliwa isipokuwa sasa tungependa Halmashauri na maeneo yanayohusika waendelee kuandaa mikakati ambayo tunaweza tukishirikiana nayo kwa hiyo, wananchi wajiandae katika kushirikiana na Serikali tutakapojenga masoko hayo. (*Makofit*)

Na. 327

### **Idara ya Maendeleo ya Jamii**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. MARIA D. WATONDOHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu tupate uhuru Idara ya Maendeleo ya Jamii, imekuwa chachu katika kusukuma maendeleo na kuhimiza kampeni mbalimbali, lakini kwa kuwa kada hiyo ya Maendeleo ya Jamii haidhihirishi kuwepo kwake kwa nguvu kama ilivyokuwa hapo zamani:-

- (a) Je, Serikali inafuatilia vipi utendaji wa kada hiyo huko Mikoani?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka kada hiyo hadi kwenye ngazi ya Kata?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Maria D. Watondoha, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, wizara yangu inafuatilia utendaji wa wataalam wa Idara ya Maendeleo ya Jamii huko mikoani na Wilayani kwa njia mbalimbali zikiwemo za kufanya ziara za mara kwa mara katika Halmashauri na kuitia mikutano mikuu ya kila mwaka inayofanywana Wizara ambapo hukutana na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na Halmashauri zote. Aidha wataalam wa Maendeleo ya Jamii walioko Wilayani wanatumwa Wizarani taarifa za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo, taarifa hizo zinaiwezesha Wizara kutoa ushauri na maelekezo ya kuboresha shughuli za maendeleo ya jamii.
- (b) Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuzi wa Serikali wa kupeleka madaraka kwa wananchi, wataalam wa Maendeleo ya Jamii wasaidizi wanaajiriwa na Halmashauri za Wilaya na wanatakiwa kufanya kazi katika ngazi ya Kata na Vijiji ili kuwawezesha wananchi katika kuibua, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kufanya tathmini ya mipango yao ya maendeleo.

Serikali Kuu kupitia Halmashauri za Wilaya, inaendelea na mpango wa kuajiri wataalam wa Maendeleo ya Jamii ili wakafanye kazi kwenye ngazi ya Kata na Kijiji. Hata hivyo hadi sasa bado kuna upungufu mkubwa wa wataalam hao kwenye ngazi ya kata hali hii inatokana na uwezo mdogo wa Halmashauri za Wilaya kugharamia ajira za wataalam hao.

Mheshimiwa Spika, ili kupata wataalam wa kufanya kazi kwenye ngazi ya kata, Wizara yangu inaendelea na jitihada za kuwaandaa wataalam wa maendeleo ya jamii kwa kuwapatia mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii, ngazi ya cheti katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Buhare, Rungembra na Misungwi.

Aidha inawapatia mafunzo ya Stashaha za Juu za Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Maendeleo na upangaji wa miradi shirikishi na menejimenti kwenye Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Mheshimiwa Spika, ili wataalam wa Maendeleo ya Jamii, waweze kupatikana kwenye ngazi ya kata, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na kushauriana na TAMISEMI katika kuzihimiza Halmashauri ziongeze kasi ya kuwaajiri wataalam hao kwenye Kata na Vijiji.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba Halmashauri huko tunakotoka hazina uwezo wa kuajiri hawa watendaji wa Idara hii na sisi katika Halmashauri zetu Idara hii imezorota hawafanyi shughuli za Maendeleo ya Jamii, wanafanya shughuli za mipango.

- (a) Je, huoni sasa kuna haja ya kuchukua watendaji wako kuwarudisha katika Wizara yako uwahudumie? (*Makofî*)
- (b) Kwa kuwa unaboresha sasa vyuo vyako katika maeneo yetu ya Halmashauri zetu tunakotoka. Sasa kama hawa watendaji unao utaendeshaji vyuo vyako hivyo? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka ngazi ya taifa, hadi Kata hadi Vijijini wanafanya kazi nzuri

sana na hii imethibitika katika mradi wa MMEM ndiyo waliosimamia kujenga madarasa wakisaidiana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata na Vijiji kama nilivyosema ni kwamba kwa sababu uwezo wa Halmashauri ni mdogo lakini kuna Halmashauri nyingi zinajitahidi na ndiyo maana hivi sasa asilimia 40 ya Halmashauri zetu tayari zina maafisa hawa wa Maendeleo ya Jamii hadi kwenye maeneo ya Kata na Vijiji.

Kwa upande wa Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao wanaoelimishwa naomba tu kutoa taarifa kwamba katika Chuo cha Tengeru tumetenga kiasi cha asilimia 60 kwa hao Maafisa Maendeleo wa Jamii ambao wako kazini ili waweze kwenda wakajifundishe dhana hii ya Elimu ya Maendeleo ya Jamii.

Kwa hilo, lingine nimelipokea lakini itabidi tukalizungumzie ili tuweze kutoa jibu sahihi. Ahsante sana.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba watendaji hawa ni wachache. Je, Serikali ina mpango gani basi kwa sababu amesema hata kwenye masuala ya MMEM wanashiriki ni kwa sababu gani basi wasipatiwe usafiri hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Wilaya zao ili waweze ili waweze kutumia basi kupitia katika zile kata ambazo hazina Maafisa Jamii na wakati huo huo wakiwa wanasmamia tena shughuli nyingine? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii, wao kazi yao ni mtambuka kwa hiyo, kilichoongezwa ni kwamba wao wakikaa pale Wilayani kazi yao ni kusaidia Idara zote kwa upande Elimu, kwa upande wa kilimo, kazi yao ni kuwahamasisha wananchi ili wajitokeze kufanya miradi iliyopo katika maeneo yao. Kwa hiyo, si kweli kusema kwamba maafisa Elimu hao wameongezewa kazi, wao ni jukumu lao.

La pili kwa upande wa usafiri, tatizo hili halipo tu kwa Idara ya Maendeleo ya Jamii, tatizo hili liko kwa Idara zote. Lakini najua kwamba Mkurugenzi, akisaidiana na watalaamu wake huwa anawasaidia maafisa hawa wote pamoja wanapewa magari au pikipiki ili kwa pamoja wakafanye kazi katika Vijiji na Kata husika. Ahsante sana.

### ***Exchange Rate***

#### **MHE. LEONARD N. DEREFA aliuliza:-**

Kwa kuwa mfuko wa *exchange rate* una madhara kwenye uchumi na maisha ya watu kama ulivyo mfumko wa bei:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isidhibiti mfumko huo?
- (b) Kwa kuwa mauzo ya madini yanaingiza fedha nyingi zaidi ya dola 560 milioni za Kimarekani. Je, kwa nini fedha hizo hazishushi *exchange rate*?
- (c) Kwa kuwa nchi kama China na India pamoja na uchumi wao kuwa ni bora zaidi hawaruhusu uuzaji wa fedha za kigeni kiholela kama tunavyofanya sisi.

Je, kwa nini na sisi tusifanye hivyo kwa lengo la kulinda thamani ya fedha zetu na uchumi wetu kama wanavyofanya hao wenzetu?

#### **NAIBU WAZIRI WA KAZI MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalí la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, thamani ya Shilingi yetu huwekwa na soko na thamani, hivyo hutegemea kiasi cha fedha za kigeni zilizoko katika soko na pia hutegemea hali ya uchumi kwa jumla hivyo mfumko wa *Exchange Rate* kama unavyoelezwa na Mheshimiwa Derefa una maana ya kupungua kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ukilinganisha na dola ya Marekani (*depreciation*).

Kama hivyo ndivyo mfumko huo unasaídia kujenga uchumi wa nchi hii kwani unamsaidia mkulima kwa kumwongezea kipato chake, unaongeza mauzo nchi za nje (*exports*) unaongeza utalii na unasaídia viwanda vya humu nchini kupata masoko ya nje na kuzuia ushindani wa bidhaa kutoka nje.

Kuongezeka kwa thamani ya Shilingi kunamkandamiza mkulima na kunapunguza mauzo nchi za nje na huongeza ununuzi wa bidhaa toka nje na hivyo kuathiri ustawi wa viwanda vya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swalí la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye (a), (b) na (c) kama ififuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Benki Kuu hufuata mfumo unaoitwa *Managed Floating Exchange Rate Regime*, maana yake ni kwamba Benki Kuu hufuutilia kwa makinini mwenendo wa thamani ya fedha yetu katika soko, na mara inapoonekana kuwa thamani katika soko hailingani na hali halisi ya uchumi, Benki Kuu huingilia kati na kurekebisha hali hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, ni sehemu ndogo tu ya mapato ya fedha za kigeni yanayopatikana kutokana na mauzo ya madini, hasa dhahabu. Kwa mfano katika mwaka 2004 zilipatikana shilingi zaidi kidogo ya dola za kimarekani 600 milioni. Katika mwaka huo mauzo yetu yote nchi za nje yalikuwa ni dola za Kimarekani milioni 1,200. Thamani ya bidhaa tulizonunua kutoka nchi za nje ilikuwa dola za Marekani takriban milioni 2,200 hivyo nakisi ya dola za Marekani milioni 1,000 ilijazwa kutokana na misaada ya wahisani pamoja na bidhaa zilizoingizwa na wawekezaji. Kwa hiyo, hata thamani ya shilingi yetu inategemea wahisani na wawekezaji. Kama misaada ya wahisani isingekuweko thamani ya shilingi yetu ingeshuka hata kufikia kiwango ambacho kingelingana na hali halisi ya uchumi na pengine kungekua na ukosefu wa fedha za kigeni. Kwa kifupi, njia pekee ya kuhakikisha kuwa hakuna mfumuko wa *Exchange Rate* ni kuongeza sana mauzo yetu nchi za nje mpaka thamani ya mauzo yetu nje izidi thamani ya ununuzi wetu kutoka nje.

(c) Mheshimiwa Spika, biashara ya fedha za kigeni hapa Tanzania inasimamiwa na sheria ya *Foreign Exchange Act* ya mwaka 1992. Kwa mujibu wa Sheria hiyo kila anayetaka kununua fedha za kigeni hupaswa kununua kutoka benki za bikashara au katika maduka ya fedha za kigeni (*Bureau de Change*) yaliyosajiliwa kuuza fedha hizo, na hutakiwa kutoa maelezo kuhusu kusudio la matumizi ya fedha anazonunua. Matumizi yanayoruhusiwa ni pamoja na matumizi ya safari nje ya nchi, malipo mbalimbali ya nje kama vile elimu, matibabu na ununuzi wa bidhaa za nje. Matumizi ambayo bado yanahitaji kibali cha Benki Kuu ni ya uwekezaji nchi za nje kwa kuwa yanahitaji kuhamisha fedha kutoka Tanzania. Hivyo Tanzania haturuhusu uuzaji wa fedha za kigeni kiholela bali uuzaji unafanywa kwa kufuata sheria. Kimsingi mfumo wa soko huria katika uuzaji wa fedha za kigeni (*current account liberalization*) ulioko Tanzania ambao ulianza mwaka 1996 hautofautiani na ule ulioko India na China. India ilianza kutumia mfumo huo mwaka 1993, miaka mitatu kabla ya Tanzania na China ilianza kuutumia mwaka 1994 miaka miwili kabla ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, mfumo wa thamani ya shilingi yetu hivi sasa unalingana na sera ya kukuza uchumi na kuongeza mauzo nchi za nje.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Napenda niulize kwamba je, Serikali inadhiliti vipi hasa biashara ya *bureau de change* kwa sababu mimi mwenyewe nimewahi kwenda kununua dola lakini ilibidi mpaka nidai ile risiti. Je, ina utaratibu gani wa kudhibiti hii?

Swali la pili, kwa kuwa Benki Kuu ndiyo benki inayotunza rasilimali zote za Taifa hili la Tanzania na kwa kuwa Gavana wa Benki na Naibu wake ndiyo *Board Member* je utaratibu huu unakubalika vipi kwamba yule *Board Chairman* wa Benki Kuu ni yule yule ambaye ni Mtendaji, ni mahali gani Serikali inadhibiti shughuli za Benki Kuu? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli udhibiti wa biashara katika maduka ya fedha unatakiwa uangaliwe na Serikali kwa upande mmoja lakini na wananchi wanavyoyatumia yale maduka. Kwa sababu nakubaliana na Mheshimiwa Derefa upo mtindo kama hutaki risiti wanakuuliza unataka risiti? Hapana, ukisema hapana, unamruhusu yule kutuibia kodi yetu. Kwa hivyo, ningewaomba kuwahimiza Watanzania siyo tu kwenye maduka ya Fedha za Kigeni, hata tunapokwenda kwenye maduka ya kawaida, bidhaa za kawaida, tujenge utamaduni wa kuomba risiti kwa sababu hiyo ndiyo namna pekee ya kudhibiti mapato yetu ya kodi. (*Makofii*)

Juu ya Bodi ya *BoT* kuwemo humo humo tena na Gavana. Huu ni utaratibu tu ambao tumejiwekea ambao sidhani kama unaizua Serikali kufanya kazi yake. Kwa sababu mkumbuke kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, yumo ndani ya Bodi ile. Lakini mara kwa mara Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Waziri wa Fedha, pamoja na Benki Kuu wanakuwa na mahusiano ya karibu katika kuhakikisha kwamba Benki Kuu inafanya kazi zake kwa mujibu wa Kanuni, Taratibu na Sheria na haya ndiyo maana unakuta hata Rais yeye mwenyewe ndiyo kiongozi wa Serikali lakini huyo ndiyo Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri, bado haizuii utendaji wa kazi. Hii inategemea na utaratibu tuliojiwekea katika maeneo fulani na maeneo mengine hilo linaweza kuwa lisiwezekane. (*Mkaofii*)

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na maelezo ya kutosha kuhusiana na tatizo hili la *Exchange Rate* lakini pia kama Taifa Tanzania tunafaidikaje na *Exchange Rate* hasa kuhusiana na matatizo yetu ya bei ndogo za mazao ya wakulima kama pamba na kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA):** Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa *Exchange Rate* unamnufaisha zaidi mkulima kuliko dhana tunayofikiria kwamba unakandamiza. Kwa sababu kama tusingeweka thamani ya shilingi yetu kutokana na hali ya uchumi tuliyonayo mkulima huyu angenunua pembejeo kwa bei kubwa zaidi na kwa hivyo mazao yake moja kwa moja angeshindwa kuhimili ushindani na mazao ya watu wengine kutoka nchi hizi za jirani.

Kwa hiyo, ingawa tunaona kwamba pamba iko bei chini. Hilo ni tatizo lingine la soko la dunia na ndiyo maana mwaka huu unaweza kuona pamba au korosho bei yake imeshuka, wakati mwingine imepanda. Hili halihusiani na thamani ya fedha za kigeni. Lakini fedha za kigeni zinahusiana zaidi na kumsaidia mkulima kuweza kupata pembejeo zake za kilimo, mkulima kuweza kuzalisha kwa bei ya chini zaidi kuliko vile ambavyo

ingekuwa kama tungeamua tu kupandisha thamani ya shilingi yetu bila kuzingatia hali ya uchumi. (*Makofi*)

Na. 329

### **Matumizi ya Kiingereza Mashulenii**

#### **MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa wanafunzi husomeshwa somo la dini ya Kiislam kuanzia shule za msingi hadi sekondari kidato cha nne kwa lugha ya Kiarabu na Kiswahili na wanapofaulu huendelea na masomo yao kidato cha tano na cha sita ambapo hufundishwa kwa lugha ya Kiingereza:-

- (a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha wanafunzi hao kusomeshwa kwa lugha ya Kiingereza badala ya kuendelea kusomeshwa kwa Kiarabu au Kiswahili?
- (b) Je, kuna matatizo yapi ambayo yatajitokeza iwapo wanafunzi hao wataendelea kusomeshwa kwa kutumia lugha ya Kiarabu na Kiswahili?

#### **WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, inaelekea Mheshimiwa Mbunge, anachanganya masomo mawili tofauti: Somo liitwalo Dini au *Religion* ambalo ni la lazima kwa kila mwanafunzi katika ngazi za Elimu ya Msingi na Sekondari na somo la *Islamic Knowledge* ambalo ni somo la hiari (*optional subject*) katika ngazi ya elimu ya sekondari kidato I hadi 4; na linaitwa *Islamic Studies* kidato cha 5 na 6.

Somo la Dini au *Religion* linatakiwa lifundishwe kwa Kiswahili katika ngazi ya elimu ya msingi na kwa Kiingereza katika ngazi ya elimu ya sekondari kwa sababu kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo iliyopitishwa na Bunge hili lugha ya kufundishia elimu ya msingi ni Kiswahili na lugha ya kufundishia elimu ya sekondari ni Kiingereza.

Kwa mujibu wa sera hiyo hiyo somo la *Islamic Studies* inatakiwa lifundishwe kwa lugha ya Kiingereza Kidato kwanza hadi cha nne na vivyo hivyo kwa somo la *Islamic Studies* Kidato cha 5 na Kidato cha 6. Aidha upo uwezekano kwa mwanafunzi anayetaka kuchukua somo la *Arabic* (Kiarabu) ambalo nalo ni mionganii mwa masomo ya hiari (*optional subjects*) katika ngazi ya elimu ya sekondari.

- (b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika kujibu sehemu ya (a) kwa mujibu wa Sera ya Elimu na mafunzo lugha za kufundishia katika shule zetu ni mbili tu:

- (i) Kiswahili kwa miaka 9 ya mwanzo ikiwemo miaka miwili ya elimu ya awali na miaka 7 ya elimu ya msingi; na
- (ii) Kiingereza kwa miaka 9 au 10 inayofuata ikiwemo miaka 6 ya elimu ya sekondari Kidato cha kwanza hadi cha sita na miaka mitatu au minne kutegemea na shahada ile anayochukua mwanafunzi ya Chuo Kikuu. Aidha hakuna somo linaloitwa Dini ya Kiislamu wala viongozi wa dini hawana mamlaka ya kuamua lugha ya kufundishia somo lolote linalofundishwa katika shule. Mwenye mamlaka ya uamuzi huo kwa mujibu wa Sheria ya Elimu iliyotungwa na Bunge hili Sheria Na. 25 ya mwaka 78, ni Afisaelimu Kiongozi ambaye pia anatakiwa kuzingatia maagizo yoyote maalumu au ya kiujumla ya Waziri wa Elimu.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kuna msemo ambaa unasemwa kwamba sasa hivi Serikali inataka kuleta dini mpya kwa sababu ya kuchanganya dini zote kuzifanya kuwa na mtaala mmoja wa dini ya Kiislamu, Kikristo, Kihindu, Kibudha, Kiyahudi na kadhalika na kwa maana hiyo mwalimu yoyote yule anaweza akafundisha katika kipindi hicho cha dini. Jambo hilo ni kweli kutokana na usemi wake aliokuwa anasema yeeye sasa hivi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, nadhani anachozungumzia ni jambo ambalo linafanyiwa kazi na wala halijafikia uamuzi wa mwisho na nadhani Mheshimiwa Profesa Mikidadi amelipata kwa sababu katika kuandaa mtaala wataalam wetu mwenye mamlaka ya kuandaa mtaala wa Taasisi ya Elimu Tanzania hufanya mashauriano ya kina na wahusika wote. Lipo wazo kwamba na sisi kama ilivyo katika nchi nyingine tuwe na somo linaloweza kuitwa *World Religions* (Dini za Duniani) yaani linalofundisha misingi ya dini mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hili ni wazo linalokuja katika juhud ya kutaka vijana wetu katika dunia ya utandawazi wawe na uelewa mpiana na wala haitegemewi somo hilo liwafundishe imani ya kufuata. Somo hilo linatarajiwa liwape ujuzi wa namna ya watu mbalimbali duniani wanavyofuata imani tofauti lakini wanavyoweza kuishi kwa pamoja. Ni zoezi ambalo linafanyiwa na wala hatujafikia mwisho wake na Wizara yangu inaendelea kufanya mashauriano kupitia chombo hicho na viongozi wa madhehebu mbalimbali ili tuuone uwezekano huo. Na nisingependa wananchi wawe na wasiwasi juu ya jambo ambalo bado linafanyiwa kazi. Ni afadhali walijue kwa undani, watoe mawazo, na waione nia njema ambayo Serikali inayo katika zoezi hilo. (*Makofî*)

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kuniona angalau mara ya pili. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, tukizingatia kwamba shabaha ya mafunzo ni kumfanya anayefundisha alielewe lile somo lake na hususan katika masuala ya dini. Hivi tukijua kwamba lugha ya Kiingereza inawapa tabu sana wanafunzi wetu katika ngazi za sekondari hata Chuo Kikuu kwa sasa. Kwa nini mafunzo ya dini yasiendelee hadi ngazi ya kumaliza sekondari ili wanafunzi hao waweze kuelewa kwa Kiswahili badala ya kusisitiza kwamba wakiingia sekondari waanze kufundishwa kwa Kiingereza? (*Makofî*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, anachokisema kwamba lugha ya Kiingereza inawasumbua baadhi ya wanafunzi wetu kuwafanya waelewe. Ni jambo ambalo tumeliona, lipo kweli na hata katika utafiti mbalimbali na katika *feedback* kutoka kwenye soko imeonyesha kwamba vijana wa Kitanzania hasa wenye shahada ya Chuo Kikuu wana mapungufu katika masomo ya lugha na katika kitu kinachoitwa *number skills* yaani ujuzi wa somo la hisabati. Sasa jawabu kwa maoni yangu pamoja na wataalam mbalimbali wa Wizara yangu, siyo kukikimbia Kiingereza. (*Makofî*)

Jawabu ni kufundisha vizuri lugha zetu za Kiingereza na Kiswahili. Waheshimiwa Wabunge wakiangalia matokeo ya mitihani wanafunzi wetu wanafanya vibaya katika masomo yetu yote mawili ya lugha, Kiingereza na Kiswahili na tulio huko maofisini tunaona hata namna ya watendaji Serikali wa ngazi ya juu kabisa wanavyoandika mambo kwa Kiswahili kibovu, wacha tu Kiingereza, Kiswahili kibovu. (*Makofî*)

Kwa hiyo, sisemi wote lakini baadhi yao wanaandika Kiswahili kibovu, Digirii wanazo. Kwa hiyo, *approach* au mwelekeo ambao tunauchukua ni kulishughulikia tatizo la ufundishaji wa masomo hayo ya lugha. Na katika mtaala mpya muda hapa hauniruhusu, lakini katika mtaala mpya ambao Kamati ya Huduma za Jamii tulitolea maelezo, jambo hili limetazamwa upya kabisa na kuweka utaratibu mpya unaofaa wa kufundisha masomo haya ya lugha. (*Makofî*)

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge walipe zoezi hili muda wa kutosha tutaanza kuona matokeo mazuri na vijana wetu watakavyomudu vizuri Kiingereza, Kiswahili pamoja na Hisabati kupitia mtaala mpya tunaoundaa sasa. (*Makofî*)

Na. 330

### **Tatizo la Maji eneo la Mkwajuni/Mwambani**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna matatizo ya maji ya siku nyingi katika mji mdogo wa Mkwajuni na Mwambani unaotokana na ongezeko kubwa la watu na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la matumizi na mahitaji ya maji:-

- (a) Je, Serikali itasikiliza kilio cha wananchi wa maeneo hayo na kuwachimbia visima kukidhi mahitaji yao ya maji?
- (b) Je, kwa nini Serikali isikarabati vyanzo vya maji vilivyopo ili kuondoa kabisa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO  
(K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo haja ya kuchimba visima kwa ajili ya mji mdogo wa Mkwajuni na kijiji cha Mwambani ili kukidhi mahitaji ya maji katika eneo hilo. Chanzo cha maji katika eneo hili ni chemchem zilizopo Mwambani ambapo sehemu ya maji hayo husukumwa kwa pampu hadi mjini na mengine hufika kwa mtiririko. Vile vile kipo kisima kwenye kijiji hicho ambacho hakitumiki kwa sasa baada ya mtambo wake kuibiwa.

Mheshimiwa Spika, wakati mradi wa Mkwajuni unabuniwa mwaka 1973, eneo la mji wa Mkwajuni na kijiji cha Mwambani lilikuwa na idadi ya watu wapatao 5,000 na mahitaji yao ya maji yalikuwa ni mita za ujazo 268 kwa siku. Hivi sasa eneo la Mkwajuni na Mwambani kwa pamoja linakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 11,000 na hivyo kufanya mahitaji ya maji ya eneo hili kufikia mita za ujazo 500 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji hayo, Serikali ilifanya uchunguzi wa maji katika eneo la Mkwajuni na Mwambani mwaka 1995 na kubaini kuwa upo uwezekano wa kupata maji zaidi chini ya ardhi kwa kuchimba visima virefu. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya inatafuta fedha kwa ajili ya kuchimba visima hivyo katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge na kukarabati kisima kilichoibowi mtambo wake ili kukidhi mahitaji ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashauri wananchi wa Mkwajuni na Mwambani kuunda Kamati ya maji na Mfuko wa Maji ili wajiandae kumiliki na kuendesha mradi huo punde utakapojengwa na kuzuia kabisa tatizo la wizi wa mitambo kama ilivyotokea katika siku zilizopita.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili. Kwa kuwa kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, wananchi wa Kijiji cha Mwambani wamepeleka umeme lile eneo la kisima kwa kuchimba kusaidiana na TANESCO na kwa kuwa tatizo ni mashine ya maji, kisima kile kinaonekana kina maji mengi kama alivyosema. Je, Serikali inaweza kusaidiana nao kwa sababu maji ni tatizo sana kwa kijiji kile cha Mwambani na maeneo inayoizunguka?

Swali la pili, mji wa Mkwajuni kama ulivyosema mwenyewe ni kwamba sasa ni mji mdogo kwa kuwa umekidhi hadhi ya mji mdogo na kwa kuwa maeneo ya Majengo, Kaloleni, Kamficheni, Polisi, Bomani na Mjini maji ni tabu sana kwa akina mama wanachota maji ya mtaro na kwa kuwa yale matenki yapo yanaonyesha kuwa yangewenza kukarabatiwa na yale machache yasipotee njiani. Je, Serikali inaweza kusaidiana na Wilaya kuweza kuyakarabati na kupatikana kwa maji pale Mkwajuni? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO  
(K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza lazima nitamke kuwa kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Ntwina kufuutilia suala la maji katika Wizara hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kuleta mafanikio katika Jimbo lake la uchaguzi na ndiyo maana hata huu mpango ambao tumekubaliana kusaidiana na Halmashauri wa kupeleka mtambo mwingine pale umefanikiwa kutokana na jitihada zake. (*Makofi*)

Lakini la msingi ni lazima tuzingatie sera yetu ya maji inasema nini. Hivi sasa Sera ya Maji unapojengwa mtambo au na Halmashauri au kwa Serikali Kuu mtambo ule unakabidhiwa mara moja kwa kijiji husika kama ni mji mdogo husika ili wao wenyewe waweze kuutunza ndiyo maana tunasema bila Kamati za Maji, bila Kamati hizo kufungua Mfuko wa maji ambao unashirikisha wananchi wenyewe, wananchi hawatapata ule uchungu wa kulinda mradi huo. Ndiyo maana mashine zinazotusaidia zote zinaibiwa na kila mmoja anajiona wala hahusiki anasubiri kuja kulaumu serikaloi baadaye kwamba wananchi wanapata matatizo. (*Makofi*)

Kwa hivyo, yale aliyoazungumza ya Mkwajuni kwenye swalii (b) la kusaidia mashine baada ya wananchi kuvuta umeme kwa kushirikiana na *TANESCO* yanawezekana tu tukiwahimiza ndugu zetu wa Mkwajuni na Mwambani kuunda Kamati za Maji na Mfuko ya Maji, wachangie bila ya shaka mitambo hii tunayoifunga itakuwa inasimamiwa na wenyewe na vitu vidogo vidogo pampu vinaweza tu vikashughulikiwa na mfuko ule wa maji.

Na. 331

#### **Tatizo la Maji - Mji wa Sumbawanga**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga kuna mtandao wa maji uliioachwa na wakoloni tangu 1961 na kufanyiwa ukarabati kidogo mwaka 1974 wakati Mkoa wa Rukwa unazaliwa:-

(a) Pamoja na maombi ya siku nyingi ya kuimarisha upatikanaji wa maji katika mji huo. Je, mpaka sasa ahadi za Serikali za tangu 1998 zimeishia wapi?

(b) Je, kwa nini Mikoa iliyokuwa katika awamu moja na mji wa Sumbawanga ikiwemo Shinyanga, Lindi, Mtwara, imepata wafadhili wakati Sumbawanga bado na nini hatma ya baadaye ya mji huo kupatiwa mfadhili?

(c) Kama imeshindikana kupata mfadhili toka nje. Je, kwa nini Serikali isitumie fedha zake za ndani kuunusuru mji huo ambao unaongezeka na kukua haraka kuliko miji mingi ya hapa nchini kwa kuupatia huduma hiyo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO  
(K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Ni kweli kwamba kulikuwa na ahadi ya ufadhili kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank (ADB)*) kugharamia mradi wa maji mjini Sumbawanga pamoja na miji ya Lindi, Mtwara na Shinyanga. Mfadhili huyo alijitoa kufadhili miji hiyo kwa sababu zake mwenyewe hivyo kuifanya miji hii kukosa mfadhili madhubuti. Kama hatua ya maandalizi, Wizara iliamua kufanya uchunguzi wa awali (*Pre-Feasibility Study*) kwa mji wa Sumbawanga ili kupata ripoti ambayo ingetumika kuombea fedha kwa wafadhili wengine. Ripoti hiyo ilikamilishwa na iliwasilishwa Benki ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Kiarabu kwa Afrika (*Arab Bank for Economic Development in Africa (BADEA)*) ambayo imeonyesha nia ya kugharamia mradi huo. Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na mfadhili huyu.
- (b) Mheshimiwa Spika, miji ya Shinyanga, Lindi na Mtwara ambayo ilikuwa katika awamu moja na Sumbawanga nayo haijapata wafadhili wa nje. Miji yote hii minne inaendelezwa kwa juhudini za Serikali. Kutokana na ukosefu wa ufadhili ili kuboresha utoaji wa huduma ya maji, miji yote hii bado iko katika daraja C miongoni mwa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mjini ambapo Serikali bado inagharamia matengenezo, uendeshaji pamoja na mishahara ya watumishi.
- (c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya juhudini nyingi ili kuimarisha hali ya upatikanaji wa maji katika mji wa Sumbawanga. Juhudi hizo ni pamoja na kuundwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Sumbawanga ambayo ina majukumu ya kuhakikisha kuwa wakazi wote wa mji wa Sumbawanga wanapata huduma ya majisafi na salama na uondoaji wa majitaka. Aidha, Wizara imeendelea kuisaidia Mamlaka hiyo fedha za kuimarisha miundombinu yake kama ifuatavyo:-

Mwaka 2202/2003 jumla ya Sh.40,592,128 zilipelekwa kwa ajili ya kununulia mabomba, viungio na mita za maji. Mwaka 2003/2004 jumla ya sh.10,000,000 zilipelekwa kwa ajili ya kuchimba kisima cha maji katika Bonde la Lwiche. Mwaka 2004/2005 jumla ya sh.31,000,000 zilipelekwa kwa ajili ya kuchimba kisima cha pili na ununuzi wa pampu ya maji, dira, mabomba na viungio vyake. Mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara imeomba jumla ya shilingi milioni 120 kwa ajili ya ukamilishaji wa visima, ulazaji wa bomba, ujenzi wa tanki na ununuzi wa dira za maji. Kutokana na juhudini nilizozitaja, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kuwa Serikali inafanya jitihada za kutosha ili kuhakikisha kwamba wakazi wa mji wa Sumbawanga wanapata majisafi na salama.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri la kutia matumaini. Swali langu la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imetenga shilingi 120 milioni kwa ajili ya kusaidia mji wa Sumbawanga katika kipindi hiki. Je, Waziri atakubaliana nami ya kwamba kwa sababu kuanzia mwezi ujao hali ya maji itakuwa mbaya katika mji huo sasa tungeomba mkandarasi ambaye atakuwa amepewa kazi hiyo aanze kushughulikia ikiwezekana

haraka iwezekanavyo awamu kwa awamu ili tusije tukapata madhara ya kukosa maji katika eneo hilo?

Swali la pili, kwa kuwa bado kuna haja ya kuomba mfadhili na makisio ya awali ilionekana kwamba gharama itakuwa zaidi ya milioni 600 ili kukamilisha mradi mzima. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami ya kwamba pamoja na jitihada za Serikali bado umuhimu wa kupata wafadhili ili kukamilisha hiyo kazi bado uko pale pale na tuombe Serikali ikazane kuhakikisha hilo linafanikiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia kwamba hizi milioni 120 tulizoomba kiasi chote kitakachokuwa kinapatikana kutoka Hazina kitaanza mara moja kwenda kupunguza tatizo la maji mjini Sumbawanga.

Kuhusu umuhimu wa mfadhili nataka nimhakikishie kwamba katika miji ile ya Lindi, Mtwara ambayo tunazungumza na *JICA* mji huu wa Sumbawanga bado tunaendelea kuzungumza na *BADEA* ili tuone kwamba miji yote ambayo ipo katika daraja la C kwa mujibu wa mfumo wa majisafi na majitaka iweze kupanda na tatizo la maji liwe ni historia katika nchi yetu.

Na. 332

#### **Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Magumu**

**MHE. PAUL P. KIMITI (K.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo watoto wengi wanaoishi katika mazingira magumu na kwa kuwa zipo taasisi binafsi na vituo vya kulelea watoto hao kama *Friends of Donbosco – Dar es Salaam* na vingine vingi ambavyo huhangaika pia kuwasomesha kuanzia shule ya msingi na kuendelea:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isichukue jukumu la kuendelea kuwasomesha watoto hao hasa wanapofaulu kuendelea na elimu ya sekondari?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha kwa ajili ya kusaidia watoto wa aina hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa wapo watoto wengi wanaoishi katika mazingira magumu kama ilivyobainishwa na Mheshimiwa Nyami. Kutokana na hili Serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni imetenga fedha kwa ajili ya ada ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu waliochaguliwa kujiunga na shule za sekondari za Serikali.

Serikali kwa kupitia Wizara yangu hutenga fedha kwa ajili ya kuwapatia mahitaji muhimu watoto hao ikiwa ni pamoja na sare, nauli na vifaa vingine vya shule.

(b) Kwa kutegemea uwezo wake, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia watoto walio katika mazingira magumu. Serikali pia, imekuwa na itaendelea kuzijengea uwezo familia zenyenye dhiki ili ziweze kujiendeleza kiuchumi na kuweza kuendelea kuwasaidia watoto wao. (*Makofî*)

Vile vile, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa wanaoendesha Makao ya Watoto Yatima na wanaoishi katika mazingira magumu kwa lengo la kuchangia gharama za kuwatunza watoto hao. (*Makofî*)

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la upungufu wa fedha katika Serikali ni tatizo ambalo kwa kweli ni sugu na kwa kuwa kuna mashirika ya kimataifa mengi ambayo yanasaidia watoto wanaishi katika mazingira magumu pamoja na yatima tunajua orodha iko kubwa?

Je, Waziri anaweza kutusaidia na kusaidia Bunge, Taasisi au Mashirika yanayoshughulikia watoto yatima pamoja na watoto wanaishi katika mazingira magumu ili tujue angalau anwani zao wapi tunaweza kuwapata ana kwa ana kama inawezekana. Unaweza kutuletea Bungeni angalau tukajua tuanze kuwasiliana nao moja kwa moja kabla ya kipindi cha Bunge hiki hakijaisha?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJALNA NA M ICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali peke yake hatuwezi tukahudumia matatizo yote yanayowakabili watoto ambao wako kwenye mazingira magumu. Hata hivyo tunapenda kuishukuru sana shirika la *UNCEF* ambalo limekuwa karibu sana na sisi katika masuala hayo *AXIOS* na *NGOs* za watu binafsi na taasisi za dini ziko nyingi tu hapa nchini. Lakini Mheshimiwa akiwa anahitaji tupate Mashirika yote ya kimataifa nataka nimdhibitishie kwamba tunae hapa leo Waziri anasoma hotuba yake na wataalamu wake wa Ustawi wa Jamii wapo bila shaka Waziri atapokuwa anazungumza zungumza jioni pengine kama atakuwa tayari anaweza akatoa orodha ya mashirika hayo.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nilipenda nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na mpango huu mzuri wa Serikali kuna tatizo kwamba wanaofaidika mara nyingi huwa katika maeneo yanayotambulikana hasa katika miji mikubwa na maeneo yaliyo karibu maeneo kama hayo?

Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwatambua hao watoto wanaishi katika mazingira magumu kutoka sehemu mbalimbali za nchi hasa mpaka wilayani kama Chunya na maeneo mengine kama hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tulianza katika wilaya chache mwaka wa fedha uliyoishia Juni, 30 mwaka huu tukaongeza wilaya lakini hivi sasa tunataka kuingia nchi nzima na nitamwomba Mheshimiwa Mbunge astahimili asikie mpango huo mpya aliouzungumzia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, basi tunaendelea na yanayofuata. Kwanza tangazo moja la kikao cha Kamati ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mwenyekiti wake anawatangazia Wabunge, Wabunge ambaa ni wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 25 kikao cha Kamati hiyo kitafanyika katika ukumbi Na. 231 kuanzia saa 4.30 asubuhi hii, tangazo moja tu, tunaendelea na *Order Paper*.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006**

#### **Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo**

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii inayohusu Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kuitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Mbunge wa Handeni, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda na Waziri wa Fedha Mbunge wa Rombo, Mheshimiwa Basil Pesambilii Mramba, kwa Hotuba zao nzuri zilizoweka mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2005/2006. Malengo, maelekezo na vigezo vilivymo kwenye Hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2005/2006. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sofia Simba (Mb.) iliyojadili makadirio ya matumizi ya Wizara yangu tarehe 30 na 31 Mei 2005. Ushauri uliotolewa na Kamati utaiwezesha Wizara kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kwake kuwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia CCM na Mheshimiwa Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais akiwa mgombea mwenza, na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar kwa kuchaguliwa kwake kuwa mgombea Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia CCM. Napenda pia kutumia nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa vifo vya aliyejewa Mbunge wa Kilombero Mheshimiwa Abu Towegele Chiwanga na aliyejewa Mbunge wa Viti Maalumu Margret Bwana na kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao walifiwa na wazazi wao au ndugu zao na pia wale walionusurika katika ajali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutoa maelezo ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu katika muktadha wa dhamana ya Wizara yangu, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi 2000 na baadaye kufanya mapitio ya utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu katika kipindi cha 2004/2005 na matarajio ya utekelezaji katika kipindi cha mwaka 2005/06

Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu 1995 – 2005, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Wizara yangu imepata mafanikio makubwa chini ya uongozi wa Jemedari wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio haya yafuatayo yanatokana na Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 1995 na 2000, na utekelezaji wa Sera sahihi za Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria za Kazi, mwaka 2000 Wizara ilianza kuzifanyia mapitio Sheria za Kazi tulizokuwa nazo, ambazo nyingi zilioneekana zimepitwa na wakati na haziendani na mfumo wa uchumi tulio nao hivi sasa, yaani uchumi wa soko (*Market Economy*). Sheria hizo ni pamoja na:-

- Sheria ya Ajira, Sura 366 ya mwaka 1956.
- Sheria ya Usalama Kazini, Namba 62 ya mwaka 1964 Sura 574.
- Sheria ya Kiinua Mgongo, ya mwaka 1962 Sura 487.
- Sheria ya Kanuni za Mishahara na Masharti ya Ajira Sura 300.
- Sheria ya Mahakama ya Kazi, Namba 41 ya mwaka 1967.
- Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi, Namba 10 ya mwaka 1998.
- Sheria ya Afya na Usalama Kazini.

Aidha, Sheria hizi zimefanyiwa marekebisho na kuandaa Sheria mbili ambazo tayari zimeshapitishwa na Bunge la Aprili 2004 na kupatikana Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Namba 6 ya Mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kusimamia Kazi, Namba 7 ya Mwaka 2004, sheria zilizobaki zinaendelea kufanyiwa kazi.

Kutokana na kuanza kutumika kwa Sheria Na.7 ya Taasisi za Kusimamia Kazi, mafunzo yanayohusu sheria za kazi, usuluhishi na utatuzi wa migogoro yamefanyika kwa Maafisa Kazi pamoja na wadau wetu (waajiri na vyama vya wafanyakazi wapatao 90).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki jumla ya rufaa za kazi 4,992, migogoro ya kikazi 641, madai ya fidia 3,846, madai/malalamiko 1,905 na kaguzi 525 za kawaida na za mishahara ilishughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, Mikataba (*Conventions*) ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya *Tatu Wizara iliridhia mikataba ifuatayo*:

- Mkataba Na. 87 kuhusu Uhuru wa kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri wa 1948 ambao umeridhiwa mwaka 2000.
- Mkataba Na. 100 kuhusu Malipo sawa kwa Ujira sawa (*Equal Remuneration Convention*) wa 1951 ambao umeridhiwa mwaka 2002.
- Mkataba Na. 111 kuhusu Ubaguzi katika Ajira na Fani za Ajira (*Discrimination in Employment and Occupation Convention*) wa 1950 ambao umeridhiwa mwaka 2002.
- Mkataba Na. 138 kuhusu Umri wa chini unaoruhusiwa katika Ajira (*Minimum Age Convention*) wa 1973 ambao umeridhiwa mwaka 1998.
- Mkataba Na. 182 kuhusu Ajira Mbaya ya Mtoto (*Worst Forms of Child Labour Convention*) wa 1999 ambao umeridhiwa mwaka 2001.
- Mkataba Na. 154 kuhusu Majadiliano ya Pamoja (*Collective Bargaining Convention*) wa 1990 ambao umeridhiwa mwaka 1998.
- Mkataba Na. 170 kuhusu Kemikali (*Chemical Convention*) ambao umeridhiwa mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, Uratibu na Usimamizi wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri baada ya kuanzisha mfumo wa vyama vingi na pia mabadiliko makubwa ya kijamii na kiuchumi nchini na duniani kote, kulihitajika pia kuangalia upya suala la muundo wa vyama vya wafanyakazi na mahusiano yake na serikali na vyama vya siasa. Ndipo mwaka 1990 ilipotungwa na kupitishwa Sheria Na. 10 ya Vyama Huru vya waajiri nchini, ambapo lengo lake ni kutambua uhuru wa Wafanyakazi na waajiri wa kuunda na kuanzisha vyama vya wafanyakazi na waajiri. Wizara imesimamia uanzishwaji na usajili wa vyama huru vya wafanyakazi 18, Shirikisho 1 la Vyama Huru vya Wafanyakazi (*Trade Union Congress of Tanzania (TUCTA)*) na Chama cha Waajiri (*The Association of Tanzania Employers (ATE)*).

Mheshimiwa Spika, Kampeni ya Ukomeshaji wa Ajira ya Mtoto Wizara, kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani, ilianza kuratibu utekelezaji wa mpango wa Ukomeshaji wa Ajira ya Mtoto kuanzia mwaka 1995. Kadhalika kuna utekelezaji wa Mpango wa Muda Maalum (*Time Bound Programme*) dhidi ya utumikishaji mbaya wa watoto ulioanza mwaka 2002. Mpango huu wa Muda Maalum ulihusisha Wilaya 14. Shughuli zilizofanywa chini ya mpango huu wa muda maalum zilihusu uhamasishaji, uwezeshaji (*Capacity Building*), kinga na kuwaondoa watoto zaidi ya 10,400 kwenye kazi zenye mazingira ya hatari. Watoto hao walipewa shughuli mbadala ikiwa ni pamoja na elimu, elimu ya stadi mbalimbali za kazi na huduma za Afya. Aidha, mpango uliweza kuzisaidia familia masikini 530 ambazo watoto wao walajiriwa katika kazi za hatari kwa kuwawezesha kuanzisha shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, Kukuza na Kuendeleza Huduma za Ajira, mwezi Aprili 1997 Wizara ilipitisha Sera ya Taifa ya Ajira. Sera hii ilitoa malengo na mkakati wa utekelezaji pamoja na kuainisha wadau wakuu wa utekelezaji wa sera hiyo, pamoja na kuwepo na Baraza la kumshauri Waziri wa Kazi kuhusiana na masuala ya Ajira. Aidha mwaka 1999 Wizara ilipitisha Sheria Na. 9 ya Huduma za Ajira (*The National Employment Promotion Services Act' No. 9 of 1999*), Sheria hii ilifuta ile ya matumizi ya Nguvu Kazi Na. 6 ya mwaka 1983. (*Human Resources Deployment Act 1983*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) iliandaa na kutekeleza mikakati na miradi mbalimbali yenye lengo la kukuza ajira na kupunguza umaskini hususan kwa vijana. Mikakati na miradi hiyo ni pamoja na:-

- Mpango wa kukuza ajira (*Country Action programme CAP*) wa mwaka 2001. Mpango huu umeanisha maeneo na miradi inayoweza kukuza ajira hapa nchini.
- Mpango wa kuendeleza mafunzo ya watu kujiajiri na kuondoa umaskini (*Demand Driven Skills Training*) wa mwaka 2001. Mafunzo hayo yanalenga kuwapa wananchi mbinu na ujuzi mbalimbali na vifaa vya kuanzia kazi wanapomaliza mafunzo ili waweze kujiajiri wenyeewe. Mradi huu umekwisha tekelezwa katika Wilaya 35 za Tanzania Bara na Wananchi wapatao 974 wamepatiwa mafunzo na vifaa.
- Kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi, Wizara iliendesha mradi wa (*Labour Market Development Project*) ambao ulilenga watumishi waliokuwa wanastaafishwa (katika zoezi la kupunguza wafanyakazi) kwa kuapatia mafunzo na mbinu za kujiajiri/kujitegemea ili kupunguza makali ya maisha.
- Wizara imeendesha pia miradi kadhaa kwa makundi maalum kama vile Mradi wa Kuongeza Ajira ya Wanawake kwa lengo la kutokomeza Ajira ya Watoto, kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika jamii na kuondoa umaskini. Mradi huu uliendesha kwenye Mikoa ya Mbeya, Dar es Salaam na Tanga.
- Wizara ilifanya utafiti wa nguvu kazi na wa ajira ya mtoto mwaka 2000/2001. Matokeo ya utafiti huo yamebainisha ukubwa wa tatizo na kasi ya ukuaji wa tatizo la ajira, na kutupatia takwimu ambazo ni muhimu katika kupanga mipango ya taifa.
- Wizara imanzisha Ofisi ya Huduma ya Ajira katika Jiji la Dar es Salaam mwaka 2001. Shughuli za ofisi hii ni kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri. Jumla ya watafuta kazi 9,881 wameandikishwa. Kati yao watafutakazi 4,189 wameunganishwa na waajiri na kati ya hao waliounganishwa, 330 wamepata ajira. Mipango ipo mbioni kuanzisha ofisi nyingine katika Jiji la Mwanza kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu na Wazee, katika kipindi cha 1995-2005 Wizara imeweza kuandaa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 na Sera ya Huduma na Maendeleo kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004. Sera hizi

ni Dira katika utoaji wa huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu katika jamii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Mafunzo na Utengemao kwa Watu Wenye Ulemavu, hadi Septemba 2004 jumla ya wanafunzi wenye ulemavu 612 walipatiwa mafunzo ya stadi za kazi ikilinganishwa na wanafunzi 213 waliopata mafunzo hayo mwaka 1994. (*Makofit*)

**Aidha, Wizara chini ya mwavuli wa Baraza la Taifa la Ushauri National Advisory Council inaendesha mfuko miwili, ambayo ni National Fund for the Disabled ulioanzishwa chini ya Sheria Na.3 ya mwaka 1982 na Disabled Persons Trust Fund ulioanzishwa mwaka 1990 ikiwa ni juhudhi za wananchi kuchangia huduma kwa watu wenye ulemavu.**

**Tangu uanzishwe, mfuko huu umekwishatoa jumla ya Shilingi 25,000,000/= kwa ajili ya shughuli za uendeshaji kwa vyama vya watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (UWZ). Fedha hizi zimetumika kwa shughuli za mafunzo kwa viongozi, utawala na uhamasishaji.**

Mheshimiwa Spika, Utambuzi wa Watoto Yatima na Walio Katika Mazingira Magumu, kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la kuhudumia watoto (*UNICEF*) na *AXIOS Fundation*, Tanzania inaendesha mpango wa kuwatambua na kuwashudumia watoto yatima na walio katika mazingira magumu kwenye misingi ya kijamii (*Community Based Care and Support to Orphans and vulnerable children*).

Wizara iliwatambua watoto 57,541 katika Wilaya za Bagamoyo, Karagwe, Kisarawe, Magu, Makete, Musoma Vijiji, Rungwe, Manispaa ya Mbeya, Muheza, Temeke, Iringa Mjini, Jiji la Mwanza, Mtwara Mikindani, Ngara, Masasi, Bunda, Singida Mjini na Singida Vijiji. Huduma zilizotolewa kwa watoto yatima ni pamoja na kuwapatia malezi ya kambo, kuwapatia chakula, ada za shule na vifaa vya shule.

Aidha, Msaada wa Rais kwa akina mama wanaojifungua watoto watatu au zaidi kwa mara moja ultolewa kwa wanawake 1,144. Hili ni ongezeko la zaidi ya mara tano ambapo mwaka 1994 ni akina mama 213 tu waliweza kusaidiwa. Aidha kiasi cha fedha wanachosaidiwa kila mmoja kimeongezeka kutoka Shs.32,184/= hadi 150,000/=

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Malezi Katika Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo vya Mchana na Malezi ya Kambo na Kuasili, katika kipindi cha mwaka 1995 – 2004, Wizara imesimamia na kuratibu utoaji huduma katika vituo 1250 vyenye jumla ya watoto 49,708 wakiwemo wa kike 25,086 na wa kiume 24,622. Vituo vingine 102 vilisajiliwa, na jumla ya vyuo 11 vilitoa mafunzo kwa walezi 682. Wizara pia imeanza kutekeleza mradi wa majaribio wa Malezi ya Awali na Uchangamshi katika Wilaya ya Kibaha. (*Makofit*)

Aidha, Wizara inaratibu na kusimamia huduma zinazotolewa na Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Dini na watu binafsi yanayotoa huduma kwa Watoto vituoni pamoja na makao ya Taifa Kurasini. Wizara imeandaa mwongozo wa kuboresha utoaji wa huduma kwa jumla ya Makao 58 yaliyopo. Jumla ya maombi 7,740 ya walezi wa kambo yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, 2,500 yalikuwa na sifa za kupatiwa watoto wa kulea pia watoto 940 waliasiliwa.

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ya Vijana, ili kukuza ajira binafsi na uzalishaji mali kwa vijana, Wizara imehamasisha vijana kuanzisha vikundi vya vijana vya kuzalisha mali kwa lengo la kuongeza idadi ya vijana wanaojajiri wenyewe, kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira na kuongeza tija. Hadi sasa Wizara inaratibu zaidi ya vikundi 4,000 vya uzalishaji mali vya vijana ikilinganishwa na vikundi 2,898 vilivyokuwepo kabla ya 1995. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Wizara iliratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulioanzishwa katika mwaka wa fedha wa 1993/94 kwa mtaji wa shilingi millioni 300. Madhumuni makubwa ya mfuko huu ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana kwa lengo la kukuza mitaji ya kuanzisha miradi mipyau kuimarisha ya zamani. Kutokana na uhamasishaji na umuhimu wa mfuko huu kwa maendeleo ya vijana, Serikali imekwishatoa jumla ya Shilingi 1,685,770,000/. Aidha Halmashauri za Wilaya zinachangia asilimia 10 ya mapato kwenye mfuko huu na zimehamasishwa na kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kusimamia vizuri mfuko huu ili kuleta tija kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru. Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya tatu, Mbio za Mwenge wa Uhuru zimetumika vema katika kuwashamasisha wananchi katika kujiletea maendeleo yao. Katika kipindi hicho wananchi waliweza kuchanga jumla ya shilingi 3,589,470,691.80. Aidha Miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi 183,494,992,210 ilizinduliwa, ambayo ililenga zaidi katika elimu, afya na barabara.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Michezo, Wizara iliweza kuandaa na kuchapisha Sera ya Maendeleo ya Michezo ambayo ndiyo inayotumika kama Dira ya kuendesha na kuendeleza shughuli za michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa kuanzisha na kusimamia ujenzi wa uwanja wa michezo wa kisasa unaoendelea kujengwa katika eneo Changamani Jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mkandarasi kutoka China. Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa aliweka jiwe la msingi la Uwanja huu tarehe 18 Julai 2005. Ujenzi wa uwanja huu utakamilika mwezi Januari 2007 na Serikali itakabidhiwa mwezi Februari 2007. (*Makofi*)

Vijana chini ya umri wa miaka 20 walishiriki mashindano ya nchi huru za Afrika na Jumuiya ya *SADC* yaliyofanyika Msumbiji na kupata medali 6, kati yake 3 za Dhahabu na 3 za fedha. Aidha timu ya wanawake ya mpira wa miguu (*Twiga Stars*)

walishiriki katika mashindano ya timu za Mpira wa miguu kwa wanawake katika Afrika. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kushiriki mashindano hayo. (*Makofi*)

Aidha, Michezo imeendelea kupewa umuhimu na Serikali kwa kuwezesha vikundi, vilabu na wanamichezo kushiriki katika mashindano ya ndani na nje ya nchi. Mwaka 1998 katika michezo ya Jumuiya ya Madola iliyofanyika mjini Kuala Lumpur Malaysia Tanzania ilipata medali 3 za Dhahabu, 1 ya fedha na 1 ya Shaba. Mwaka 2002 katika mashindano kama hayo nchini Uingereza, Tanzania ilipata medali 1 ya Dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Timu za michezo za watu wenye ulemavu pia ziliiletea heshima kubwa nchi yetu kwa kupata medali tisa kwenye mashindano ya riadha ya watu wenye ulemavu mwaka 1995, medali tano nchini Marekani mwaka 1999 na medali 18 kwenye mashindano ya riadha na mpira wa miguu Dublin, Ireland mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo Katika Fani Mbalimbali, Wizara kwa kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii imefanikiwa kufanya yafuatayo:-

- Kufundisha masomo katika fani ya Ustawi wa Jamii (*Social Work*), Uongozi Kazi (*Labour Studies*) na Rasilimali Watu (*Human Resources Management*) katika ngazi ya Cheti na Stashahada ya juu kwa kuwapatia wanafunzi stadi za kisasa kulingana na mahitaji ya soko katika fani husika.
- Kumekuwepo na ongezeko la idadi ya wanafunzi kutoka 147 mwaka 1995/96 hadi kufikia wanafunzi 653 mwaka 2004/2005.
- Kuanzishwa kozi mpya 4 katika fani za Ustawi wa Jamii, Rasilimali Watu na Uongozi Kazi katika ngazi za Cheti (rasilimali watu), Stashahada ya juu (rasilimali watu), Stashahada ya uzamili ya (Ustawi wa Jamii), Stashahada ya Uzamili ya Sheria na Usuluhihi na Utatuhi.
- Aidha Taasisi imeanza mchakato wa kuifanya Taasisi kuwa Chuo Kikuu kishiriki.

Mheshimiwa Spika, Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi iliundwa chini ya Sheria Na. 1 ya Mwaka 1994 kwa lengo la kutoa, kuendeleza na kusimamia elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana wanaomaliza shule za msingi na sekondari ili waweze kujiajiri wenyewe au kuajiriwa katika Sekta Rasmi. Aidha mafunzo yanayotolewa pia yanalenga katika kukuza stadi za wafanyakazi ili waweze kuinua tija katika sehemu zao za kazi.

Ili kufanikisha malengo yaliyotajwa, mkazo mkubwa umewekwa katika kutoa mafunzo katika stadi zinazohitajika katika soko la ajira. Aidha, kozi zinazotolewa sasa zinalenga zaidi kuwawezesha vijana kuhitimu na kujiunga katika vikundi kwa lengo la kujiajiri.

Aidha mafunzo kwa wasichana yamewekewa uzito wa pekee ili uwiano wa wawulana na wasichana ulingane. Kwa upande mwingine wafanyakazi walioajiriwa katika sekta mbalimbali wanapatiwa mafunzo baada ya saa za kazi yanayolenga kuendeleza stadi zao kwa lengo la kukuza tija. Katika kipindi cha miaka kumi, Serikali imefanikiwa katika maeneo yafuatayo:-

- Wizara kwa kupitia *VETA* imefanikiwa kuongeza vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini kutoka vyuo 17 mwaka 1995 kufikia vyuo 21 mwaka 2004. Pia imefanikiwa kusajili vyuo vinavyotoa elimu ya mafunzo ya ufundi stadi kutoka 415 mwaka 1995 hadi kufikia 794 mwaka 2004.
- Idadi ya wanafunzi katika vyuo hivyo imeongezeka kutoka 3,500 mwaka 1995 na kufikia 17,172 mwaka 2004, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 391. Wanafunzi katika vyuo viliwyosajiliwa na *VETA* wameongezeka pia kutoka 35,490 mwaka 1994 na kufikia 50,075 mwaka 2004, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 41.
- Aidha, uwiano kati ya wawulana na wasichana katika vyuo umeongezeka kutoka asilimia 8 mwaka 1995 na kufikia asilimia 38 mwaka 2004.
- Idadi ya fani za mafunzo zinazofundishwa zimeongezeka kutoka fani 38 mwaka 1994 hadi 90 mwaka 2004.

Aidha ongezeko hilo la idadi ya washiriki linatokana na ukarabati, ujenzi na kupanuliwa vyuo vya ufundi stadi vya Mara, Kagera, Oljoro (Arusha), Mikumi na Songea na kuongezeka kwa fani zinazofundishwa.

Mheshimiwa Spika, Usalama na Afya Mahali pa Kazi, katika kipindi hiki cha awamu ya tatu, Wizara ilianzisha Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi mwaka 2001, Wakala huu umeanzishwa kwa lengo la kuboresha afya, usalama na ustawi wa wafanyakazi na maeneo yao ya kazi.

Katika kipindi cha mwaka 1995-2005 Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi umetekeleza yafuatayo:-

- Jumla ya kaguzi 40,249 za usalama na afya sehemu za kazi zilifanyika ikilinganishwa na lengo la kufanya kaguzi 20,517. Aidha, kati ya kaguzi hizo, 21,043 zimefanywa tangu kuanzishwa kwa wakala mwaka 2001.
- Wakala umetoa mafunzo ya uhamasishaji wa afya na usalama mahala pa kazi kwa waajiri katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Shinyanga. Mafunzo haya yamehusisha jumla ya sehemu za kazi 325. Mafunzo kama haya pia yalitolewa kwa njia ya televisheni, magazeti, redio na vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Jamii, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii lina majukumu ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kulipa mafao kwa wanachama. Aidha, ili kuboresha mafao, Shirika huwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali kama vile dhamana za Serikali na mabenki, mikopo, hisa za makampuni yaliyosajiliwa kwenye soko la Hisa la Dar es Salaam (*DSE*) na katika ujenzi wa nyumba na ofisi za kupangisha au kuuza. Katika kipindi cha miaka kumi Shirika lilipata mafanikio makubwa yafuatayo:-

- Shirika libadili mfumo kutoka Akiba (*NPF*) na kuwa mfumo kamili wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Mfumo huu mpya unatoa mafao saba kwa wanachama wake tofauti na mfumo wa zamani ambao ulikuwa unatoa mafao matatu tu. Mafao hayo saba ni Pensheni ya Uzeeni, Urithi, Ulemavu, Msaada wa mazishi, Mafao ya Uzazi, Mafao ya Kuumia Kazini na Mafao ya Matibabu.
- Thamani ya jumla ya rasilimali za Shirika imeongezeka kutoka shillingi bilioni 72.9 mwaka wa fedha wa 1995/1996 na kufikia shilingi bilioni 434.9 mwaka 2004/2005. Ongezeko hili limetokana na uwekezaji sehemu mbalimbali na kukua kwa makusanyo ya michango ya wanachama.
- Michango toka kwa wanachama na waajiri iliyokusanya kila mwaka imeongezeka kutoka shilingi bilioni 14.3 mwaka 1995/1996 na kufikia shilingi bilioni 97.4 mwaka 2004/2005. Hivyo kuvuka lengo la kukusanya shilingi billioni 95.0 kwa asilimia 2.5.
- Mapato kutoptaka na vitega uchumi mbalimbali vya Shirika yaliyokusanya kila mwaka yameongezeka kutoka shilingi bilioni 9.3 mwaka 1995/96 na kufikia shilingi bilioni 20.9 mwaka 2004/2005.
- Vitegauchumi vyote vya Shirika kwa ujumla vimeongezeka kutoka shilingi bilioni 54.3 mwaka 1995/96 na kufikia bilioni 373.4 mwishoni mwa mwaka 2004/2005. (*Makofii*)
- Aidha, miradi mikubwa ya ujenzi iliyokamilika katika kipindi cha mwaka 1995/96 mpaka 2000/2005 ni pamoja na *Water Front House*, *Mabibo Students Hostel*, *Mwalimu Nyerere Pension Tower*, *Quality Group Building*, Ujenzi wa Nyumba za Bei Nafuu: *Mikocheni Executive Apartments*, *Ubungo Plaza*, *Social Security House*, na *Mbezi Housing Scheme*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kuratibu na Kuboresha Tija Kitaifa, Wizara kwa kuitia Shirika la Tija la Taifa (*National Institute of Productivity (NIP)*) imefanikiwa kuratibu shughuli za kuboresha Tija na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi kama ifuatavyo:-

- Liliboresha tija na ufanisi kazini katika Taasisi za Umma, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Makampuni Binafsi kwa kutoa huduma 509 za mafunzo ambazo ziliwanufaisha watumishi 5,595 na huduma za uelekezi 49. (*Makofii*)

- Limejenga uwezo wa kufanya utafiti wa mishahara (*Tanzania Remuneration Survey*) na ubora wa huduma (*Tanzania Customer Satisfaction Survey*).
- Limeandaa Mpango wa Taifa wa Kusimamia na kuratibu Tija (*National Productivity Management Programme*)

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kazi Tanzania, Mahakama ya Kazi Tanzania ilianzishwa kwa Sheria Na. 41 ya Mwaka 1967 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 1990 kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji wenye tija kwa kusimamia haki na uhusiano kati ya waajiri na wafanyakazi mahali pa kazi nchini. Katika kipindi cha miaka 10 Mahakama hii ilikamilisha mashauri 903 kama ifuatavyo:-

Migogoro ya Kikazi 136 iliamuliwa, Migogoro ya Uchunguzi 443 iliamuliwa, Mikataba ya Hiari 206 ilisajiliwa, Maombi ya marejeo 88 yalirejewa, Ushauri ultolewa kwa Serikali mara 4, Makubaliano ya suluhu 3 yalisajiliwa, Malengo 8 yalisajiliwa, Hukumu 14 zilikaziwa, na Tafsiri ya uamuji 1 ilifanyika.

Aidha, katika kipindi hicho ofisi mbili za Kanda za Nyanda ya Juu Kusini (*Mbeya*), na Nyanda ya Kati (*Dodoma*) zilikamilishwa. Ofisi ya Kanda ya Kaskazini (*Arusha*) ilipatiwa Naibu Mwenyekiti na Ofisi za Makao Makuu zilipanuliwa. Vile vile Mahakama imeanzisha na inatekeleza taratibu ya kufanya vikao vya Mahakama katika Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Iringa, Tabora, Morogoro, Dodoma na Tanga.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2000 – 2005), Kazi na Ajira, Serikali imeendelea kurekebisha sheria za kazi ambazo zimepitwa na wakati. Sheria mbili ikiwa ni pamoja na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi ya Kusimamia Kazi Na. 7 ya mwaka 2004, zilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ili kupambana na umaskini na kukuza ajira na tija katika sekta isiyo rasmi, Serikali imeanzisha mpango maalumu wa kutoa mafunzo ya ujuzi wa kazi kwa vijana ili kuwapa ujuzi wa kazi na uwezo wa kuajiri, kupambana na umaskini na kukuza ajira na tija katika sekta isiyo rasmi.

Kituo cha Ajira, Dar es Salaam kimeimarishwa na kimeendelea kutoa huduma zake ambapo watafuta kazi 9,881 walijiandikisha, 4,189 kati ya hao waliunganishwa na waajiri na 330 walijiriwa. Idadi ya kazi zilizotangazwa kuitia Kituo hicho ilikuwa 4,468. Kwa kutumia kituo hicho, Serikali iliratibu mpango wa ajira kwa wanawake ambapo wanawake 1,027 waliandikishwa na kati yao 565 waliunganishwa na waajiri na 101 kuajiriwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Msaada kwa Makundi Maalum, Serikali imetoa msaada kwa akinamama wanaojifungua watoto watatu na zaidi kwa mara moja, watoto wanaozaliwa wakiwa wameungana na akinamama wanaopata ulemavu baada ya kujifungua. Katika kuhakikisha kwamba wazee na watu wenye walemovu wanapatiwa huduma zinazostahili katika jamii, Serikali iliandaa Sera ya Taifa ya Wazee na Sera ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye ulemavu.

Aidha, Katika jitihada za kuendelea kuboresha maisha ya makundi maalum ya wananchi, Serikali imetoe mafunzo kwa watu wenyewe ulemavu na wasiojiweza ambao wapo ndani na nje ya makazi. Watoto yatima na watoto katika mahabusu wamepatiwa huduma za chakula, dawa, mavazi na vifaa vya kulia chakula ambapo Shilingi zaidi ya 200 milioni zimetumika. Serikali imenunua sare, vifaa vya shule, kulipa ada, michango ya shule na vyuo, vifaa vya kufundishia na vyombo katika vyuo vya ufundi kwa walemaru. Watoto 675 wanaosoma elimu ya msingi na walemaru 612 wanaosoma katika vyuo saba vya ufundi, wamenufaika na huduma hiyo.

Serikali pia imetoe mafunzo kwa wawezeshaji haki (*Community justice facilitators*) katika ngazi ya jamii na hivyo kuhamasisha jamii kuhusu maendeleo ya watu wenyewe ulemavu kupitia kipindi cha Televisheni cha “Wape Nafasi” kinachoonyeshwa na televisheni ya Taifa. Aidha, Serikali imeainisha mpango madhubuti wa kuboresha huduma katika mahabusu za watoto na shule ya Maadilisho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Vijana, katika kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Vijana, Serikali imeratibu na kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana unaota mikopo kwa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali. Mfuko huu hutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana kwa lengo la kukuza mitaji yao. Aidha, mwongozo mpya wa kuendesha Mfuko huo umetolewa na kuanza kutumika ambapo hadi mwishoni mwa 2004, Serikali ilitoa mikopo ya jumla ya Shilingi 1,685,770,000. Kila Halmashauri ya Wilaya nchini hupata kiasi cha Shilingi 3,089,756 kwa mwaka kutoka katika Mfuko huo kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya vijana. Aidha kila Halmashauri ya Wilaya itakayofanya marejesho kwa asilimia 100 itapewa mara mbili ya fedha hizo zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru zinazofanyika kila mwaka nchini kote. Mbio hizo pia hutoa hamasa kubwa kwa wananchi kuchangia shughuli zao za maendeleo ili kuondokana na umaskini. Kwa kutumia Mbio za Mwenge wa Uhuru, vijana wanahamasishwa kupambana na matatizo ya umaskini, ujinga, maradhi kama vile UKIMWI na kuleta usawa wa jinsia. Michango inayopatikana kutokana na mbio hizo, hubaki katika maeneo husika kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi mbali mbali ya maendeleo. Katika mbio za kila mwaka, Mwenge wa Uhuru hubeba kaulimbiu maalum ambapo wananchi hupata fursa ya kuelimika kuhusu mambo mbali mbali.

Aidha, Serikali imeanzisha wiki maalum inayoanzia tarehe 8-14 Oktoba ambayo lengo lake ni kuwawezesha vijana kuionyesha jamii shughuli wanazozifanya katika kupambana na umaskini, UKIMWI na ujinga. Wiki hiyo inakwenda sambamba na kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru. Warsha kwa viongozi katika vikundi vya vijana vya uzalishaji mali, ziliendeshwa na Serikali katika mikoa ya Pwani, Morogoro na Dar es salaam, ili kuwapatia vijana elimu ya kuwawezesha kuanzisha na kusimamia vikundi vyao.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Michezo, kwa upande wa maendeleo ya michezo, Serikali imeendesha zoezi la kuhamasisha Halmashauri, Manispaa na Wilaya

kuajiri Wasajili Wasaidizi wa Wilaya wa Vyama na Vilabu vya Michezo nchini. Hadi sasa, wilaya 65 zimepata Wasajili Wasaidizi. Wasajili hao na Maafisa Michezo wote Tanzania Bara wamepewa mafunzo ya kutekeleza kazi za usajili, kufanya utafiti na kuendeleza michezo ya jadi katika maeneo yao.

Serikali pia imeendelea kuhimiza utunzaji wa maeneo kwa shughuli za michezo na burudani ikiwa ni pamoa na kurejesha maeneo yaliyovamiwa ili yatumike kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali imeendelea kuorodhesha na kusimamia viwanja na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo. Serikali ilifanikisha ushiriki wa timu ya mpira wa miguu ya wanawake ya Twiga Stars katika mashindano ya Kombe la Afrika na ushiriki wa timu ya riadha kwenye mashindano ya Olympiki mjini Athens, Ugiriki. Serikali imeanza ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo Jijini Dar es Salaam. Uwanja huo utakuwa na uwezo wa kuchukua watu 60,000 wakiwa wamekaa kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (*VETA*), kwa upande wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (*VETA*), Serikali imefanikiwa kuongeza Chuo kimoja cha Ufundsi na hivyo idadi ya Vyuo kufikia 21 vilivyopo katika mikoa 17 ya Tanzania Bara. Aidha, Serikali imefanikiwa kuongeza idadi ya vyuo vilivyo sajiliwa na *VETA* vinavyotoa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kutoka vyuo 538 mwaka 2000 hadi 794 Desemba, 2004. Idadi ya wanafunzi waliopo katika vyuo vya ufundi stadi imelongezeka kutoka wanafunzi 16,232 mwaka 2000 kufikia 17,172 Desemba, 2004. Katika vyuo vilivyo sajiliwa na *VETA*, idadi ya wanafunzi imelongezeka pia kutoka wanafunzi 38,538 mwaka 2000 hadi 50,075 mwaka 2004. Uwiano wa wanafunzi wa kike na wa kiume umeongezeka pia kutoka uwiano wa asilimia 12 mwaka 2000 hadi asilimia 38 mwishoni mwa 2004. (*Makofit*)

Aidha, fani zinazofundishwa na *VETA*, zimeendelea kuongezeka hadi kufikia fani 90 mwaka 2004. Aidha, hivi sasa mafunzo yanayotolewa na vyuo hivyo ni bora zaidi kwa vile yanazingatia mahitaji ya soko la ajira na mitaala ya mafunzo inayoandaliwa kwa viwango vya utendaji mahali pa kazi kinyume na hali ilivyokuwa. Idadi ya walimu wa ufundi stadi waliofundishwa imefikia 130 na idadi ya watahiniwa waliofanya mitihani mwaka 2004 ilikuwa 22,000 ambapo asilimia 70 walifaalu.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2004/2005 na Mipango ya Mwaka 2005/2006 napenda sasa kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu na ahadi zilizotolewa na Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 na kazi zitakazotekelawa katika mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kazi, Wizara kupitia Idara ya Kazi ina majukumu ya kuratibu na kusimamia Sera na Sheria za Kazi ili kuleta amani sehemu za kazi, kwa kulinda haki na wajibu wa Wafanyakazi na Waajiri, kupunguza na kutatua migogoro ya kikazi, kukuza majadiliano kwa azma ya kuwezesha ukuaji wa uchumi, ajira, tija na kulinda kazi ya staha (*decent work*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 majukumu yafuatayo yalitekelezwa:

- Iliratibu utekelezaji wa Mpango wa awamu ya kwanza ya marekebisho ya Sera na Sheria mpya za Kazi, ambazo ni:-
  - Sheria Na.6 ya Ajira na Mahusiano Kazini, pamoja na sheria Na.7 ya Taasisi za Kusimamia Kazi zilizopitishwa katika Bunge lako Tukufu la Aprili 2004. Sheria ya Taasisi za Kusimamia Kazi imeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Februari, 2005. Chini ya Sheria hii, Taasisi zinazotakiwa kuundwa ni pamoja na:-
  - Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii (*Labour Economic and Social Council (LESCO)*)
  - Kamisheni ya Usuluhishi na Utatuvi wa Migogoro, (*Commission for Mediation and Arbitration (CMA)*)
  - Kamati za Huduma Maalum (*Essential Services Committees*) na
  - Mahakama ya Kazi kuwa Idara ya Mahakama Kuu.
- Ilikamilisha uchapishaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii.
- Kutokana na kuanza kutumika kwa Sheria hii mafunzo ya stashada ya uzamili yanayohusu Sheria za kazi, usuluhishi na utatuvi wa migogoro, yametolewa kwa Maafisa Kazi pamoja na wadau wapatao 90 ambaao ni Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi.
- Mafunzo ya Stashahada ya juu katika masuala ya kazi (*Advanced Diploma in Labour Studies*) kwa Wakaguzi wa Kazi yanaendelea.
- Ukarabati wa ofisi 6 za kazi umeanza kwa kupata michoro ya ofisi hizo zitakazojumuisha pia ofisi za CMA. Ukarabati huu utafanyika kwa awamu kuanzia mwaka huu wa fedha na utaanza na ofisi za Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.
- Uteuzi wa wajumbe wa Baraza la kushughulikia kima cha chini cha mishahara kwa sekta ya huduma za nyumbani na hotelini umechapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 27 Mei, 2005 na utaanza kufanya kazi katika mwaka 2005/06.
- Kusudio la kuanzisha Baraza la Kima cha Chini cha Mishahara katika sekta za kilimo na madini limechapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 22 Aprili, 2005. Uteuzi wa wajumbe utafanyika katika mwaka 2005/06.
- Majadiliano na nchi za Kenya na Uganda kuhusu utekelezaji wa makubaliano ya Itifaki ya Ushuru wa pamoja (*Customs Union*) katika nchi za Afrika Mashariki yanaendelea. Aidha Wizara ilishiriki katika kikao maalum cha

kujadili Rasimu ya Itifaki juu ya Hadhi za Maafisa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Taasisi zake.

- Ilisimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi nchini ambapo:-
  - Jumla ya rufaa 236 za masuala ya kazi kati ya 246 zilizowasilishwa zilitolewa uamuza.
  - Migogoro ya kazi 27 na mikataba ya hiari 25 ilipokelewa na kushughulikiwa.
  - Madai ya fidia ya kuumia kazini kwa watumishi wa umma 189 yenye thamani ya Shilingi 20,412,000/= yamelipwa.
  - Mabaraza ya wafanyakazi 8 yalisimamiwa uchaguzi wake na mafunzo 6 ya kuimarisha mabaraza hayo yaliendeshwa.
- Mpango wa kupambana na ajira ya mtoto unaendelea kutekelezwa katika Wilaya 11 nchini. Mwongozo wa Kaguzi za ajira ya mtoto umechapishwa na kusambazwa kwa watendaji amba ni Maafisa Kazi, Wakaguzi wa Kazi, Wakaguzi wa Afya na Usalama Kazini, na Makatibu wa Vyama vya Wafanyakazi. Ufutiliaji unaendelea katika Wilaya kuhusu utekelezaji wa mradi wa kupambana na utumikishwaji watoto mashambani (*COMAGRI*).
- Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imemteua mtaalam atakayesimamia ukusanyaji wa taarifa kutoka Taasisi mbalimbali kuhusu mbinu zinazotumika katika kupambana na janga la UKIMWI sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kusimamia utekelezaji wa Marekebisho ya Sheria za Kazi awamu ya kwanza kwa kukamilisha uundaji wa Taasisi za kusimamia kazi, kutoa mafunzo kwa Maafisa Kazi, ukarabati wa ofisi tatu na uundaji wa Bodi za Kima cha Chini cha Mishahara Kisekta.
- Itakamilisha uandaaji wa mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii, na pia kufanya utafiti katika Mikoa wa jinsi ya kupanua wigo wa huduma za Hifadhi ya Jamii nchini. Aidha itapanga mikakati ya kuwaelimisha wananchi juu ya utaratibu wa Hifadhi ya Jamii.
- Kukamilisha na kuendelea kushughulikia migogoro ya kikazi, rufaa, maombi ya malipo ya fidia, na malalamiko ya wadau.
- Kusimamia mpango wa ukarabati wa majengo ya ofisi za kazi unaofanywa kwa msaada wa Serikali ya Denmark.

- Kujenga uwezo wa Idara kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa wa Kazi katika masuala ya kazi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sheria yanayoendelea.
- Kushughulikia kikamilifu utekelezaji wa mikataba ya viwango vya kazi ya *ILO, AU, SADC* na *EAC* tuliyoridhia ili kuenda sambamba na matakwa ya viwango vya kazi vya kimataifa.
- Kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani na Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa mpango wa kukomesha ajira ya watoto, kuendelea kuratibu kampeni za kitaifa dhidi ya ajira ya mtoto na aina mbaya za ajira ya mtoto na kuangalia ukubwa wa shughuli za biashara za watoto katika mipaka minane ya nchi yetu.
- Kukuza uwezo wa watumishi kiutendaji na kupambana na rushwa ili kudumisha Uongozi Bora na Utawala wa Kisheria.
- Kusimamia uundaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi na kuelimisha vyombo vya ushirikishwaji ili kuwezesha kuwepo kwa majadiliano kati ya wafanyakazi na waajiri.
- Kutoa elimu juu ya janga la UKIMWI kwa wafanyakazi na waajiri sehemu za kazi.
- Kudumisha UTATU kwa madhumuni ya kuboresha mahusiano mema kazini.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ajira, Idara ya Ajira ina jukumu la kushughulikia masuala ya ajira nchini, pia kuainisha na kupendekeza maeneo muhimu ya kukuza ajira na hatimaye kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 majukumu yafuatayo yalitekelezwa:-

- Iliendelea na awamu ya pili ya marekebisho ya Sera na Sheria za Kazi na Ajira. Hatua hii inahusu maeneo ya Usalama na Afya sehemu za kazi, Huduma za Ajira, Kukuza Ujuzi, Hifadhi ya Jamii na Taarifa za Soko la Ajira (*Labour Market Information*). Baadhi ya Marekebisho haya yapo katika hatua ya kuandaliwa Rasimu ya Sheria.
- Kituo cha ajira kilisajili watafuta kazi 1,087, kati yao watafuta kazi 540 waliunganishwa na waajiri kwa ajili ya usaili, ambapo kati yao 130 wamepata ajira kuitia kituo hiki.

- Ili kuboresha uwezo wa watafuta kazi, Wizara iliwapa mbinu za kufanya vizuri katika usaili watafuta kazi 150, mafunzo ya namna ya kujitafutia ajira kwa ufanisi watafuta kazi 361 na kutoa ushauri nasaha kwa watafuta kazi 64.
- Kituo kimeanza kutumia mtandao wa Kompyuta (*Automative Services*). Aidha Kituo kipo katika hatua za mwisho za kuanzisha tovuti yake kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa taarifa za kituo na soko la ajira kwa wananchi wengi zaidi.
- Maandalizi ya awali ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanzisha tawi la kituo cha ajira katika jiji la Mwanza yamekamilika.
- Ilisiriki maonyesho ya Sita ya Sekta isiyo Rasmi (nguvu kazi/Jua Kali) kwa nchi za Afrika Mashariki yaliyofanyika mjini Mombasa-Kenya yenye lengo la:-  
 - Kubadilishana ujuzi na uzoefu katika utengenezaji wa bidhaa.  
 - Kuboresha, Kuimarishe na kupanua masoko katika jumuiya ya Afrika ya Mashariki.  
 - Kuwa ishara ya ukumbusho wa kufufua Jumuiya ya Afrika Mashariki na  
 - Kudumisha ushirikiano baina ya nchi jumuiya.
- Jumla ya maombi 4,899 ya vibali vya ajira ya wageni yalishughulikiwa, kati ya hayo, maombi 1,617 chini ya taratibu maalumu kuitia kituo cha uwekezaji (*TIC*) na maombi 2,991 chini ya taratibu za kawaida yalikubaliwa. Aidha maombi 219 yalikataliwa na maombi 67 yanaendelea kushughulikiwa.
- Iliratibu mafunzo ya ujuzi wa watu kuweza kujiajiri na kuondoa umaskini. Mafunzo haya yamefanyika katika Wilaya 57 na jumla ya wananchi 1,259 wamenufaika kati yao wanaume walikuwa 669 na wanawake 590.
- Iliendesa semina ya mafunzo kwa Viongozi wanawake 20 wa vikundi vya biashara kwa lengo la kuwawezesha kuboresha usimamizi wa biashara zao.
- Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), Chama cha Wafanyakazi wa Mashambani (*TPAWU*), Chama cha Waajiri (*ATE*) na Asasi zisizo za Kiserikali (*NGOs*) iliendelea kutekeleza mradi wa Kuboresha na Kuongeza Ajira binafsi kwa Wanawake na Kutokomeza Ajira ya Watoto katika Halmashauri za Wilaya za Tanga, Korogwe, Handeni, Kinondoni, Ilala, Temeke na Rungwe. Jumla ya akina mama 940 na watoto 1,361 walinufaika.
- Aidha mradi uliwawezesha wanawake kujiunga na vikundi mbalimbali vya uchumi na pia kuwapatia mafunzo katika kilimo bora cha matunda, mboga, ufungaji wa kuku, usindikaji matunda na mboga na mafunzo kuhusu masoko; masomo ya afya ya jamii na elimu ya watu wazima.

- Wanawake 1,200 kati ya 1,700 wameweka akiba na wanaweza kukopa benki kwa masharti nafuu. Baadhi yao wana uwezo sasa wa kukopa mpaka Shilingi 1,000,000/= kutoka Shilingi 50,000/= za awali
- Jumla ya Vijana 642 kati yao wasichana 309 na wavulana 333, wa umri kati ya miaka 15-17 waliibuliwa toka kwenye ajira mbaya na zisizo salama na wasichana 65 waliokuwa katika biashara ya ngono/ukahaba wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali na stadi za kazi na hatimaye kujiunga na ajira mbadala.
- Jumla ya Watoto 1,361 kati yao wasichana 659 na wavulana 711 wa umri kati ya 6 - 13 waliibuliwa na kutoka katika ajira mbaya na kujiunga na shule za msingi au ufundi stadi.
- Jumla ya vijana wa kike 29 wamepelekwa katika vyuo vya ustawi wa jamii kusomea kufundisha na kuendesha vituo vya kulelea watoto wadogo sehemu za kazi, kwa lengo la kuwa walezi wenye sifa stahili za kuendesha vituo 22 vilivyoanzishwa katika maeneo ya mradi.
- Aidha, viongozi 195 wa vikundi vya wanawake walengwa wamepatiwa mafunzo ya kuanzisha na kuendesha *SACCOS*.
- Katika utekelezaji wa Ripoti ya Tume ya Ulimwengu ya Utandawazi, Wizara kama mjambe wa Kamati ya Wataalam katika kuandaa Mpango wa Kitaifa (*Plan of Action*) wa utekelezaji, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji imeainisha maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa ripoti hiyo. Maeneo hayo ni pamoja na yale yenye kuongeza na kukuza ajira hususan kwa vijana, viwango vya kazi (*Labour Standards*) na Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara kwa kupitia Idara itatekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha marekebisho ya Sera ya Ajira.
- Kuendelea kufanya utafiti katika sekta mbalimbali ili kupima kasi ya ukuaji wa ajira nchini na ule wa Nguvu kazi pamoja na ajira ya watoto.
- Kuendeleza awamu ya pili ya marekebisho ya Sera na Sheria za Kazi na Ajira pamoja na kuandaa mikakati ya utekelezaji.
- Kuendelea kutathmini na kutafuta njia ya kuboresha na kuwawezesha wananchi kunufaika na nafasi za kazi zinazopatikana katika soko la ajira, pamoja na kupanua wigo wa huduma za Ajira kwa kuanzisha tawi la Kituo cha Ajira jijini Mwanza.

- Kuendeleza mpango wa mafunzo juu ya utaratibu wa watu kuweza kujiajiri na kuondoa umaskini.
- Kuendeleza ajira ya makundi maalum ya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu.
- Kutekeleza programu za masuala ya ajira na kuondoa umaskini wa kipato.
- Kushiriki Maonyesho ya Saba Saba ya bidhaa za Viwanda na biashara maonyesho ya washiriki wa Sekta isiyo Rasmi kwa nchi za Afrika Mashariki yatakayofanyika Kampala – Uganda Novemba, 2005.
- Kujenga uwezo wa Idara ili kuboresha tija na ufanisi katika utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, Dara ya Ustawi wa Jamii, Wizara yangu kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii imetoea huduma kwa makundi yaliyo katika mazingira magumu zaidi zinazolenga kutetea, kulinda na kushawishi ustawi wa familia, wazee, wasiojiweza, watu wenye ulemavu, watoto yatima, watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, watoto walio katika mkinzano na sheria na huduma za majaribio na ujenzi wa tabia. Aidha Idara iliendelea kuratibu uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, na huduma za malezi, makuzi na uchangamshi wa awali wa mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 majukumu yafuatayo yalitekelezwa:-

- Kwa kushirikiana na wadau, iliendelea kuihamasisha jamii na Asasi mbalimbali juu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee.
- Ilifanya maandalizi ya uandaaji wa mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu.
- Ilikamilisha taratibu za kuiwezesha Serikali kuridhia kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Fursa Sawa kwa Watu Wenye Ulemavu.
- Imekamilisha Rasimu ya Mwongozo wa Malezi na Ulinzi wa Watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika jamii.
- Ilitoa na kuboresha huduma katika makazi 17 ya wazee, watu wenye ulemavu na wasiojiweza, Makao ya Taifa ya watoto wenye shida Kurasini, vyuo 7 vya watu wenye ulemavu, Kituo cha Mama na Mtoto Ilonga, Chuo cha Malezi Kisangara, mahabusi 5 za watoto na Shule ya Maadilisho Irambo.
- Kwa kushirikiana na mradi wa “SHIA” ilitoa mafunzo ya lugha ya alama kwa walimu 14, Maafisa Ustawi 8 na watumishi wa kada nyingine 8.

- Ilitoa mafunzo ya stadi za kazi kwa watu wenyewe ulemavu 280 katika vyuo vya ufundi vya Yombo, Mirongo, Masiwani, Singida, Masasi, Chang'ombe na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Anatoglu.
- Kwa kushirikiana na *UNICEF* ilitoa mafunzo kwa Wawezeshaji Haki Jamii 486 katika Halmashauri za Bagamoyo, Kisarawe, Magu, Makete, Mtwara – Mikindani, Bunda Karagwe, Songea, Singida, Iringa, Temeke, Masasi, Mwanza, Musoma Vijijini Singida Vijijini na Kibondo.
- Ilitoa huduma za Majaribio na Ujenzi wa Tabia kwa washitakiwa 1,476 wakiwemo watu wazima 293, watoto 734 na vijana 449.
- Imetoa elimu na ushauri nasaha kwa watoto 1,698 na vijana 728 kuhusu athari za madawa ya kulevyaa na namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika mahabusi 5 na Shule ya Maadilisho-Irambo.
- Jumla ya watoto 64,954 wanaoishi katika mazingira magumu zaidi wametambuliwa katika Halmashauri za Wilaya 21 hapa nchini, ambazo ni Bagamoyo, Karagwe, Kisarawe, Magu, Makete, Musoma Vijijini, Rungwe, Manispaa ya Mbeya, Temeke, Muheza, Iringa Mjini, Jiji la Mwanza, Mtwara – Mikindani, Masasi, Ngara, Bunda, Singida Mjini, Singida Vijijini, Kibondo, Songea na Ilala. Huu ndio mpango ambao Mheshimiwa Njelu Kasaka hatimaye utafika Chunya.
- Kwa kushirikiana na Shirika la *Axios International*, imeandaa mwongozo wa kuwahudumia watoto wanaoishi katika Makao ya Watoto na imeendelea kuwahudumia watoto yatima katika Halmashauri za Rungwe, Mbeya Mjini na Muheza.
- Iliratibu uendeshaji wa makao ya watoto yatima na wenyewe shida, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, vituo vya watoto wa mitaani, pamoja na vyuo vya walezi ili kuhakikisha ubora wa huduma.
- Ilitoa misaada kwa akina mama waliojifungua watoto watatu au zaidi kwa mara moja. Jumla ya akina mama 45 wamepata msaada huo.
- Jumla ya mashauri 6,137 ya ndoa zenyeye mifarakano, mashauri 9,964 ya matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa na mashauri 5,668 ya matunzo ya familia zilizofarakana yalishughulikiwa.
- Kwa kushirikiana na *UNICEF*, imetoa mafunzo kwa wawezeshaji 42 wa walezi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika Wilaya 7 za Kisarawe, Bagamoyo, Magu, Musoma Vijijini, Karagwe, Makete na Bunda.
- Katika kuratibu huduma za Malezi ya Kambo na Kuasili, jumla ya watoto 4 waliasiliwa na watoto 17 walichukuliwa na wazazi wa kambo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 majukumu yafuatayo yatakelezwa:-

- Itakamilisha maandalizi ya mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenyе Ulemavu.
- Itahamasisha jamii na asasi mbalimbali juu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee.
- Itakamilisha taratibu za kuiwezesha Serikali kuridhia Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Fursa Sawa kwa watu wenyе ulemavu.
- Itatoa na kuboresha huduma za Ustawi wa Jamii katika makazi 17 ya wazee, watu wasio na uwezo na watu wenyе ulemavu, vyuo 7 vya Ufundı kwa watu wenyе ulemavu, Makao ya watoto yatima na wenyе shida, mahabusi 5 za watoto, shule ya Maadilisho Irambo, Kituo cha Mama na Mtoto Ilonga na Chuo cha Mafunzo ya walezi Kisangara.
- Itafanya maandalizi ya marekebisho ya Sheria za Ajira na Matunzo kwa watu wenyе ulemavu kwa kushirikiana na *Help Age International*.
- Itafanya maandalizi ya utoaji wa fedha za msaada wa maisha kwa wazee.
- Itatoa mafunzo ya stadi za kazi kwa watu wenyе ulemavu, watoto mahabusu, waadiliwa, watoto wa makazi na watoto yatima wanaotunzwa katika makao ya watoto Kurasini.
- Itaanza maandalizi ya utambuzi wa watoto wenyе ulemavu.
- Itafanya mashauriano na Wizara ya Afya kwa lengo la kujumuisha masuala ya wazee na watu wenyе ulemavu katika mitaala ya mafunzo ya wataalamu wa afya.
- Itafanya mashauriano na wadau kwa lengo la kuandaa mwongozo wa ajira isiyo na ubaguzi kwa watu wenyе ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu.
- Itatekeleza malengo yaliyo katika Muongo wa Afrika wa watu wenyе ulemavu.
- Itawatambua na kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika Halmashauri 5 za Tanzania Bara.
- Itatoa misaada kwa watu wenyе ulemavu na akina mama waliojifungua watoto zaidi ya wawili kwa mara moja.

- Itaratibu uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, vituo vya watoto wa mitaani, vyuo vya malezi ya watoto na makao ya watoto yatima na wenye shida.
- Itakamilisha mwongozo na kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji wa malezi, makuzi na uchangamshi wa awali wa mtoto.
- Itaratibu huduma za malezi ya kambo na kuasili.
- Itatoa ushauri kwa vijana waathirika wa pombe na madawa ya kulevyia.
- Itafanya utafiti katika mahabusi za watoto na watu wazima ili kujua idadi na hali halisi ya watoto walio katika mkinzano na sheria.
- Itafanya ukarabati wa baadhi ya mahabusi za watoto, shule ya Maadilisho na itahuisha Bodi ya shule hiyo ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Vijana na watoto Sura ya 13 ya mwaka 1937.
- Itafanya mapitio ya Mtaala wa mafunzo ya Walezi wa Watoto katika Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo vya Mchana.

Idara ya Maendeleo ya Vijana, kwa upande wa Idara ya Maendeleo ya Vijana, Wizara yangu ina jukumu la kuweka sera na taratibu zinazojenga mazingira endelevu yanayowawezesha vijana kujiimarisha kiuchumi, kijamii na kisiasa na hivyo kukua katika maadili mema.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Idara ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

- Ilifanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 1996 kwa kuwashirikisha vijana na wadau mbalimbali. Lengo kuu lilikuwa ni kuandaa Sera ya Vijana inayolenga kutoa mwongozo bora na endelevu kwa wadau wote wanaojishughulisha na masuala ya vijana.
- Ilisimamia na kuratibu shughuli za kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru kilichofanyika mkoani Lindi tarehe 14/10/2004, ambapo jumla ya miradi ya maendeleo 1,596 yenye thamani ya shilingi 65,618,874,479.20 ilizinduliwa, kufunguliwa au kuwekewa mawe ya msingi. Katika ujenzi wa miradi hiyo wananchi walichangia jumla ya Shilingi 5,428,883,907.0 ambazo kwa utaratibu ulivyo, fedha hizo hubakia katika Wilaya husika ili kuendeleza miradi ya maendeleo ya wananchi. Kauli mbiu ya mbio hizo ilikuwa Vita dhidi ya UKIMWI (UKIMWI haubagui sisi tunabagua) na ukuzaji wa sekta isiyo rasmi kama njia ya kuondoa umaskini na kufikia malengo ya maendeleo ya milenia.
- Aidha uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2005/2006 zilifanyika mkoani Kigoma tarehe 08/06/2005. Ujumbe wa Mbio za Mwenge mwaka huu ni Vita dhidi ya Ukimwi na Uchaguzi Mkuu, wenye kauli mbiu “Tuwahifadhi Wasichana

na Wanawake dhidi ya maambukizi ya UKIMWI” na “Tujitokeze kupiga Kura kwa Amani”.

- Iliratibu shughuli za Wiki ya Vijana kuanzia tarehe 08/10 – 14/10/2005 mkoani Lindi. Vijana walioshiriki walipata nafasi ya kuonyesha na kutangaza shughuli zao za uzalishaji mali na masuala muhimu kuhusu maendeleo ya jamii. Aidha, Jumla ya vijana na watu wengine 395 (wanawake 35 na wanaume 365) walijitokeza kupima UKIMWI kwa hiari. Kati yao watu 23 ambao ni sawa na asilimia 5.82 walikutwa na virusi vya UKIMWI.
- Tathmini ya Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2004/2005 ilifanyika Mjini Zanzibar kwa lengo la kurekebisha mapungufu yaliyojitekeza na kuboresha Mbio za mwaka 2005/2006.
- Kwa kushirikiana na *UNICEF*, iliendelea kukusanya takwimu zinazowahusu Vijana mahali walipo na shughuli wanazozifanya. Mpango huu uliainisha jumla ya vikundi 3,884 vya vijana vya uzalishaji mali katika Wilaya 76 nchini. Aidha Orodha ya vikundi na asasi za vijana *Youth Directory* imeandaliwa kwa lengo la kuzitambua, kuwasiliana na kuandaa mipango mbalimbali ya asasi za vijana.
- Ilitoa mikopo ya maendeleo kwa vijana. Jumla ya Halmashauri 119 zilipatiwa jumla ya Shilingi 367,680,964. Katika marejesho, Halmashauri 10 za Wilaya zilirejesha mikopo yao kwa asilimia 100 ambazo ni Geita, Ksimba, Musoma, Singida, Rungwe, Lindi, Tabora, Hanang, Kasulu na Manispaa ya Arusha. Baada ya marejesho haya Wilaya hizi zilipewa mara mbili ya fedha zilizorejeshwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana wengi zaidi Wilayani. Kwa ujumla zoezi hili linalenga kuboresha utaratibu wa mikopo kwa kuhamasisha kukopa na kurejesha ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika na mikopo hii.
- Ukarabati wa majengo katika vituo vya mafunzo vya Ilonga, Sasanda na Marangu ulifanyika kwa kushirikiana na *COSTECH*. Wizara imeanzisha Tovuti ya mawasiliano juu ya masuala ya vijana kwenye Kituo cha Mafunzo ya Vijana cha Ilonga yenye jina la [WWW.infoyouth.or.tz](http://WWW.infoyouth.or.tz). Huduma hii inalenga kuboresha mafunzo ya ujenzi wa Stadi za Kazi na maisha kwa vijana na jamii inayoizunguka kituo hicho na Vijana walio vijijini. Aidha Mafunzo ya matumizi ya kompyuta yameanza kutolewa na kituo kwa vijana kwa wastani wa vikundi 10 kwa mwezi.
- Ilishiriki kwenye kongamano la kimataifa Kuhusu kampeni ya miaka 10 ya kukuza ajira kwa vijana *Youth Employment Summit (YES)*. Kongamano hilo likiwa ni kwa ajili ya kujadili mikakati ya kukuza ajira katika mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania.
- Iliwezesha vikundi vitatu vya Tanzania kushiriki katika mashindano ya Vikundi vya Vijana vya Uzalishaji Mali kutoka nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Youth Gold and Silver Award*). Kikundi kimoja kutoka Wilaya ya Mbinga kiitwacho KIBUVI (Kikundi Bunifu cha Ufundu cha Vijana)

kilishinda katika ngazi ya kanda ya Afrika. Kikundi hiki kitapata tuzo ya paundi 1000, Cheti pamoja na Medali kutoka *CYP*.

- Kwa kushirikiana na Benki ya Dunia chini ya mradi wa *Tanzania Multisectoral Aids Project (TMAP)*, ilitoa mafunzo kwa Kamati ya Wizara inayoshughulikia masuala ya UKIMWI. Aidha upembuzi yakinifu umeanza kufanywa kuhusu hali ya UKIMWI ndani ya Wizara na kuandaa vipeperushi na vijarida vya kutoa elimu ya UKIMWI kwa watumishi wa Wizara na jamii kwa ujumla.
- Kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleao la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), ilianda na kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanaojitolea iliyofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 08/12/2004. Kauli mbiu ilikuwa “Jitolee katika vita dhidi ya UKIMWI”

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 majukumu yafuatayo yatakelezwa.

- Itachapisha Sera ya Maendeleo ya Vijana iliyofanyiwa mapitio na kuisambaza kwa vijana na wadau wengine katika ngazi zote. Vile vile itaandaa mikakati ya utekelezaji wa sera hiyo.
- Itaandaa taratibu za kisheria za kuanzisha Baraza la Taifa la Vijana.
- Itaendelea na ukusanyaji wa takwimu za vijana na shughuli zao kwa wilaya 43 zilizobakia. Aidha zoezi la uandaaji wa orodha ya vikundi vya vijana (*Youth Directory*) ya vijana litakamilishwa.
- Kuimarisha uzalishaji katika vikundi vya uzalishaji mali vya vijana kwa kuwapatia vijana mafunzo katika nyanja za ukuzaji wa biashara na masoko, ufundu, uongozi na utawala wa miradi.
- Kuendeleza ukarabati wa vituo vya mafunzo vya Ilonga, Sasanda na Marangu na pia kuendelea kuimarisha kituo cha mtando wa mawasiliano (Tovuti ya Vijana) kilichopo Ilonga na kuwashamasisha vijana wengi zaidi kukitumia.
- Kuendelea kuratibu utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa Halmashauri za wilaya, Miji na Manispaa ili kuvijengea uwezo vikundi vya vijana wa kuijendesha na hivyo kuongeza tija.
- Kuendelea kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru, Wiki ya Vijana na kilele chake itakazofanyika mkoani Singida tarehe 14/10/2005.

- Kuandaa na kutekeleza mpango wa malezi utakaojumuisha vijana na viongozi wa *NGOs* za vijana katika masuala ya ushauri nasaha, stadi za maisha, afya ya uzazi na vita dhidi ya UKIMWI. Aidha mpango wa kudhibiti UKIMWI mahali pa kazi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia utaendelea kutekelezwa.
- Chini ya mtando wa Kitaifa wa kukuza Ajira kwa Vijana Duniani, itaandaa warsha kwa ajili ya Mashirika na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali yenye lengo la kuhamasisha mbinu za ukuzaji wa ajira kwa wadau wa vijana kote nchini.
- Kwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali itaandaa mpango wa majaribio utakaowawezesha vijana walio nje ya shule kuendelea na masomo ya ufundi na hata Sekondari kwa njia ya mawasiliano (*Distance learning education*).
- Siku ya wanaojitolea itaendelea kupewa umuhimu, kwa kuwahamasisha vijana na jamii kwa ujumla kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa kujitoleana hasa katika shughuli za kuongeza vipato na kukuza uchumi.
- Kwa kupitia Kituo cha Ujasiri-Marangu itaratibu na kuweka mipango mbalimbali ya mafunzo ya ujasiri kwa vijana na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maendeleo ya Michezo, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara iliendelea na jukumu la kuendeleza michezo kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo, kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kusimamia ujenzi wa uwanja wa michezo wa kisasa na ukarabati wa uwanja wa Taifa wa zamani. Jiwe la Msingi la uwanja wa kisasa liliwekwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 18/07/2005.
- Kwa kushirikiana na Baraza la Michezo ilisimamia uchaguzi wa chama cha mpira wa miguu nchini (*TFF*) ambapo uongozi mpya umepatikana na hali ya utulivu imerejea katika chama hicho. Nia ya Serikali kwa sasa ni kulijengea uwezo wa kiutendaji Shirikisho hilo kwa kuwapatia mafunzo viongozi wake wakuu.
- Ilifanikisha ushiriki wa timu ya Taifa kwenye mashindano ya Olimpiki yaliyofanyika Athens Ugiriki. Jumla ya wanamichezo 9 na maofisa, walimu na viongozi 9 walishiriki.
- Ilitoa mafunzo kwa wataalamu 332 wa michezo mbalimbali yaliyofanyika katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na vituo vya Arusha na Songea. Mafunzo haya yalihusu matunzo na matumizi bora ya viwanja, ukocha wa mchezo wa netiboli na usajili wa vyama vya michezo, ukocha wa mpira wa mikono, uongozi wa vyama vya michezo, ukocha wa mpira wa wavu kwa watu wenye ulemavu na mapambano dhidi ya ukimwi.

- Jumla ya vyama na vilabu 226 vya michezo mbalimbali vilisajiliwa.
- Ilitoa ushauri kuhusu marekebisho ya Katiba za Vyama na Vilabu ili kupunguza migogoro michezoni.
- Jumla ya Mikoa 10 ilipewa ushauri wa kitaalamu juu ya kuboresha na kuimarisha miundombinu ya michezo. Matunda ya ushauri huu yameanza kuonekana kwani viwanja vya michezo vimeanza kuwa bora zaidi.
- Ilifanya Ukarabati wa majengo ya Chuo cha Michezo Malya na kununua vitendea kazi katika chuo na vituo vya michezo vya Arusha na Songea.
- Iliwawezesha jumla ya watu wenye ulemavu wa akili 500 kushiriki mashindano ya Taifa ya michezo kwa watu wenye ulemavu yaliyofanyika mkoani Mwanza.
- Aidha wachezaji 2 wa Paralimpiki waliwezesha kushiriki katika mashindano huko Athens Ugiriki.
- Ilihamasisha ushiriki wa wanawake michezoni kwa kuhakikisha idadi sawa ya wanawake na wanaume katika mafunzo.
- Iliendeleza Mikataba ya ushirikiano wa kimichezo na nchi za Cuba, Korea ya Kusini na Rwanda.
- Ilipima afya za wanamichezo na kutoa matibabu na ushauri kwa wenye matatizo. Jumla ya wanamichezo 370 wa mkoa wa Dar es Salaam na 66 wa mkoa wa Tanga walipimwa. Upimaji ulifanyika pia kwa wanamichezo 427 wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) na waamuzi 100 wa mpira wa miguu. Aidha, Makatibu Wakuu wa Wizara zote na Makatibu Tawala wa Mikoa yote walipimwa afya zao na kupewa ushauri huko Mwanza.
- Ilipambana na maambukizi ya UKIMWI kwa kuwa na programu za mafunzo kwa wafanyakazi. Aidha, mafunzo ya vijana nje ya shule yajulikanayo kama “Muongoarika la Wanamichezo” yaliyofanyika katika Wilaya za Kibaha, Makete, Kilombero, Magu na Mafinga ambapo jumla ya washiriki 184 walinufaika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, majukumu yafuatayo yatakelezwa:-

- Kuendelea Kusimamia ujenzi wa uwanja wa kisasa unaojengwa jijini Dar es Salaam na kukamilisha ukarabati wa uwanja wa zamani ifikapo Oktoba, 2005.

- Kuziwezesha Timu za Taifa za michezo mbalimbali kushiriki michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika nchini Australia.
- Kutoa mafunzo ya utaalamu wa ukocha, uamuzi, uongozi na huduma ya kinga na tiba ili kuinua viwango vya ufundishaji, uamuzi na utawala bora katika vyama na vilabu.
- Kuvishauri vyama na vilabu kuzihuisha Katiba zao na kuzifuata ili kuleta amani na utulivu michezonii.
- Kudurusu Katiba mpya za vyama na vilabu na kuzisajili.
  
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu kuboresha miundombinu ya michezo hasa viwanja ili kuinua viwango vya ufundishaji na uchezaji.
- Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Michezo - Malya na vituo vya Arusha na Songea.
  
- Kuwawezesha watu wenyewe ulemavu kushiriki mashindano ya kimataifa na kitaifa, ambapo timu ya Paralimpiki itashiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola huko Australia, na ya Olimpiki Maalum itashiriki mashindano ya Taifa huko Mbeya, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kushiriki mashindano ya kimataifa huko China mwaka 2007.
  
- Kupima afya za wanamichezo, kutoa matibabu na ushauri wa kuboresha afya zao. Aidha, kwa kushirikiana na Chama cha Madaktari wa Michezo (*TASMA*) itafungua matawi mikoani ili huduma hii iwafikie wanamichezo wengi zaidi nchini.
  
- Kuwahamasisha wanawake kujiunga na vyama na vilabu vya michezo ili kuongeza ushiriki wao michezonii. Aidha, kukiimarisha Chama cha Michezo kwa Wanawake ili kiwahamasishe wanawake wengi zaidi kucheza, kuchezesha na kuongoza shughuli za michezo.
  
- Kutekeleza programu za mapambano dhidi ya maambukizo ya UKIMWI kwa wanamichezo kwa kuendeleza mafunzo ya Muongoorika la Wanamichezo kwa Wilaya zile ambazo hazijapata mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii lililoanzishwa kwa Sheria Na. 28 ya mwaka 1997 ni moja ya Taassisizilizo chini ya Wizara ambayo iliendelea na majukumu yake ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza fedha za wananchi katika miradi yenyeye kuleta faida na kulipa mafao kwa wanachama. Aidha ili kuboresha mafao ya wanachama Shirika litaendelea kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali kama vile dhamana za Serikali,

mabenki, mikopo, hisa za makampuni yaliyosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (*DSE*) na katika ujenzi wa nyumba na ofisi za kupangisha au kuuza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005, Shirika lilitekeleza yafuatayo:

- Lilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 97.4 ikiwa ni michango kutoka kwa waajiri na wanachama. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 102.5 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 95.0.
- Lililipa mafao ya wanachama jumla ya shilingi milioni 24,565.7 ambayo ni sawa na asilimia 132 ya lengo lilokusudiwa la kulipa shilingi milioni 18,603.5.
- Lilikusanya jumla ya shilingi milioni 165,145.8 kutoka kwenye vyake mbalimbali vinavyojumuisha mapato kutoka kwenye vitega uchumi, vitega uchumi vilivyokomaa na michango ya wanachama. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 96 ya lengo la kukusanya shilingi milioni 172,736.2.
- Semina mbalimbali zilifanyika na mafunzo yalitolewa ili kuwawezesha wananchi kuuelewa mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii. Semina na mafunzo hayo yalitolewa kwa waajiri na wanachama wa *NSSF*.
- Shirika lilikamilisha ujenzi wa awamu ya pili ya mradi wa nyumba 91 za gharama nafuu katika eneo la Kinyerezi – Dar es Salaam.
- Matayarisho ya kuanza kutoa Mafao ya Matibabu kwa wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yalikamilishwa na mafao hayo yamezinduliwa mwezi Julai, 2005.
- Liliendelea na ujenzi wa jengo la *Mafuta House*.
- Uwekaji wa kompyuta katika ofisi mbalimbali na kuziunganisha unaendelea. Wataalamu wa kuweka mifumo ya kompyuta na mawasiliano kupitia mtandao wa kompyuta kwa shughuli zote za Shirika ili kuboresha huduma wameanza kazi hiyo.
- Linaendelea kuboresha uwekaji wa kumbukumbu mbalimbali za wanachama. Vituo vya kutunzia kumbukumbu vinajengwa katika Mikoa ya Mtwara, Morogoro na Mwanza.
- Lilikamilisha ujenzi wa ofisi katika Wilaya ya Nzega – Tabora.
- Lilishiriki katika maonyesho ya 29 ya Biashara ya Kimataifa (sabasaba) katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere na kufanikiwa kuwa mshindi wa kwanza katika Sekta ya Huduma na Biashara na mshindi wa pili wa jumla.

- Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu kwa mradi wa daraja la Kigamboni ameshateuliwa na atawasilisha ripoti yake mwishoni mwa mwezi Julai, 2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Shirika linakusudia kufanya yafuatayo:-

- Litakusanya mapato yanayofikia shilingi bilioni 202.5 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali nya mapato na kutumia kiasi hicho hicho cha fedha.
- Elimu itaendelea kutolewa kwa wanachama, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii.
- Litatoa mafao saba likiwemo fao la matibabu kwa wanachama wa mfuko wa Hifadhi ya Jamii.
- Uwekaji na uunganishaji wa kompyuta katika ofisi mbalimbali za Shirika utaendelea.
- Vituo nya kuweka kumbukumbu mbalimbali za wanachama vitaendelea kujengwa, na katika mwaka huu wa fedha Shirika limepanga kujenga vituo vitatu katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Tabora.
- Ujenzi wa ofisi katika Jiji la Mwanza, Mkoa wa Kagera na Wilaya za Mbozi na Njombe utafanyika.
- Shirika litaendelea na ujenzi wa *Mafuta House* na *Ex-Tazara*.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi (*VETA*), kwa kuititia *VETA*, Wizara inasimamia na kuratibu shughuli za elimu na mafunzo ya stadi za kazi nichini kwa kutoa mafunzo ya stadi mbalimbali zinazochangia kukuza ajira na kusajili vyuo vyote vinavyotoa mafunzo ya aina hii. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi (*VETA*) ianzishwa kwa Sheria Na. 1 ya 1994

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, *VETA* imetekeleza yafuatayo:-

- Mkandarasi kwa ajili ya ununuzi wa vifaa nya mafunzo kwa vyuo vilivyokarabatiwa nya Mara, Kagera, Mikumi, Songea na Oljoro amepatikana na vifaa hivyo vitanunuliwa mwaka wa fedha 2005/2006.
- Washauri wa Ujenzi kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa vyuo nya *VETA* nya Shinyanga, Mpanda, Tabora, na Ulyankulu pamoja na ujenzi wa vyuo vipyta nya Singida na Arusha wamepatikana na wameshaanza kazi mwaka 2004/2005.
- Ujenzi wa chuo cha *VETA* Kigoma umekamilika na kozi fupi fupi zitaanza kutolewa mwezi Agosti 2005. Aidha Ununuzi wa vifaa vyote nya mafunzo

(*tools and equipment*) kwa ajili ya kozi za muda mrefu utaanza mara baada ya kukamilisha taratibu za kutia saini Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Korea ya Kusini.

- Jumla ya washiriki 40,881 kutoka vyuo vya *VETA* na visivyo vya *VETA* wamehudhuria mafunzo ya kozi fupi fupi ikilinganishwa na washiriki 37,984 mwaka 2003/2000/2004. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 8.
- Mafunzo ya stadi za kazi kwa ajili ya wasichana yameendelea kuimarishwa na kupanuliwa. Idadi ya wasichana waliojiunga katika mafunzo ya kozi ndefu na fupi katika vyuo vya *VETA* na visivyo vya *VETA* imeongezeka kutoka 19,645 mwaka 2003/2004 na kufikia washiriki 20,627 mwaka 2004/2005.
- Mafunzo ya Walimu wa Ufundu Stadi yanayotolewa katika chuo cha Morogoro yameendelea kuboreshwa, hususan yale yanayotolewa chini ya utaratibu wa kusoma wakati mwalimu anaendelea na kazi zake (*off-campus*). Idadi ya wanaofaulu mitihani imeongezeka kutoka asilimia 48 mwaka 2003/2004 na kufikia asilimia 84.3 mwaka 2004/2005. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 88.3.
- Taratibu za usajili na ithibati wa vyuo vya ufundu stadi zimeboreshwa kuanzia Januari 2005.
- Mfumo mpya wa utoaji mafunzo umezidi kuimarishwa, hususan katika vyuo vya Taasisi za Kidini, watu binafsi na Taasisi zisizo za Kiserikali. Jumla ya Shilingi bilioni 1.74 zimetumika kununulia vifaa vya kufundishia (*tools and equipment*), mafunzo ya walimu ili kuboresha viwango vya utekelezaji pamoja na misaada mingine ya kitaalamu.
- Ujenzi pamoja na ufungaji wa mitambo ya mafunzo katika kitengo maalum cha mafunzo kwa ajili ya sekta ya nyama (*Meat Industry*) katika Chuo cha *VETA* Dodoma umekamilika.
- Maandalizi pamoja na taratibu za awali za Ujenzi wa vyuo vya ufundu stadi vya Pwani, Lindi na Manyara yamekamilika kwa kupata viwanja.
- Mafunzo yametolewa kwa Walimu wa ufundu stadi 200 chini ya mradi unaofadhiliwa na mfuko wa *OPEC*.
- Elimu ya maisha katika vyuo vyote vya ufundu stadi nchini imeendelea kupanuliwa na kuboreshwa. Jumla ya Waalimu walezi (*Guardian Instructors*) 333 na viongozi (*Peer educators*) 758 wamepatiwa mafunzo.
- Mkakati wa kuboresha mfumo wa sasa wa utoaji mitihani (*Trade Testing*) umetekelizwa, Rasimu ya kanuni za mitihani katika mfumo mpya

*(Competence Based Training, Assessment and Certification)* zimetayarishwa na hivi sasa zinajadiliwa.

- Ushirikiano baina ya *VETA* na Zanzibar katika suala la utoaji mitihani ya ufundi stadi na biashara umeendelea kuimarishwa. Jumla ya watahiniwa 309 kutoka Zanzibar walifanya mitihani hii mwaka 2004 na kati yao 200 ambao ni sawa na asilimia 64 walifaalu.
  - Chuo cha *VETA* Kihonda kimeendelea na ushirikiano wake na Shirika la kuhudumia wasioona kutoa mafunzo kwa vijana wenyе matatizo ya kuona. Vijana hawa sasa wamejumuishwa na wanafunzi wa kawaida badala ya kuwatenga katika kazi maalum kama ilivyokuwa hapo awali. Walimu wanaendelea kupatiwa utaalam juu ya kuendeleza mafunzo ya aina hiyo.
  - Utekelezaji wa Mitihani ya Ufundi Stadi na Biashara (*Trade Test na NABE*) umeendelea kuimarishwa. Jumla ya watahiniwa 22,617 walifanya mitihani hii katika madaraja mbalimbali na kati yao 13,849 au asilimia 61.23 walifaalu. Idadi ya watahiniwa imeongezeka kwa asilimia 2.5 ikilinganishwa na waliofanya mitihani hii mwaka 2003/2004.
  - Mitihani katika mfumo mpya (*Competence Based Assessment*) ilitolewa kwa wanafunzi 8,317 hadi kufikia Desemba 2004. Idadi ya watahiniwa imeongezeka kwa asilimia 5.1 ikilinganishwa na waliofanya mitihani hii Desemba 2003. Katika mitihani ya biashara (*NABE*) jumla ya washiriki 1,536 walifaalu.
  - *VETA* imeshirikiana na *ILO* katika kutekeleza mradi unaolenga kuwaondoa na kuwazuia watoto walio chini ya umri wa miaka 18 kwenye ajira mbaya kwa kuwapatia mafunzo ya ufundi stadi ili waweze kujiajiri. Jumla ya watoto 3000 wamefaidika na mafunzo ya aina hii ambayo yametolewa katika Wilaya 11.
  - Mafunzo ya kozi ndefu katika vyuo vya *VETA* yameendelea kutolewa. Jumla ya vijana 8974 wamepatiwa mafunzo, ikiwa ni ongezeko la asilimia 5.1 kilinganishwa na idadi ya vijana waliojiunga na mafunzo haya mwaka 2003/2004. Aidha vyuo visiviyomilikiwa na *VETA* lakini vimesajiliwa na *VETA* vilitoa mafunzo ya muda mrefu kwa jumla ya vijana 27,853. Hili ni ongezeko la asilimia 5 ikilinganishwa na idadi ya Washiriki katika mwaka 2003/04.
- Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, *VETA* imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-
- Kufanya mapitio katika Sera ya Mafunzo na Ufundi Stadi nchini.
  - Kufunga vifaa vya kufundishia katika vyuo vya Ufundi stadi vya Mara, Kagera, Mikumi, Songea, Oljoro na Kigoma.

- Kuendelea na kazi ya kukarabati na kupanua vyuo vya ufundu stadi vya Shinyanga, Mpanda, Tabora na Ulyankulu na kuanza ujenzi wa vyuo vipywa Arusha, Singida, Pwani, Manyara, Lindi na kituo cha habari na mawasiliano (*ICT*) Chang'ombe - Dar es Salaam.
- Kuimarisha na kukuza utoaji wa idadi ya Kozi fupi fupi zinazotolewa.
- Kuendelea kuongeza idadi ya wasichana wanaojiunga na vyuo vya ufundu stadi.
- Kuimarisha, kuboresha na kupanua mafunzo ya ualimu wa ufundu stadi kwa kuanzisha kozi ya stashahada katika Chuo cha Walimu wa Ufundu Morogoro na kuanzisha mpango wa kuendeleza walimu wa ufundu kitaaluma (*skills upgrading and updating*).
- Kuboresha usajili wa vyuo vya ufundu stadi kwa kuzingatia utaratibu mpya wa usajili ulioanza kutumika 2005 ili kuboresha viwango vya mafunzo yanayotolewa.
- Kuendelea kuimarisha utekelezaji wa mfumo mpya wa mafunzo kwa kuimarisha mafunzo ya walimu, ukarabati wa karakana na kuboresha vifaa vya kufundishia.
- Kuanza kutoa mafunzo katika sekta ya nyama kwa kutumia kitengo maalum cha mafunzo kilichopo katika chuo cha *VETA* Dodoma.
- Kuboresha kanuni za utoaji wa mitihani ya ufundu stadi kwa lengo la kuunganisha *Trade Tests* na *CBET*.
- Kuendelea kutoa mafunzo ya kazi kwa wafanyakazi waliopo ili kukuza na kuboresha utendaji wao wa kazi na hivyo kuongeza tija.
- Kuendelea kukusanya takwimu kuhusu stadi za kazi zinazohitajika na kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanalenga katika kukidhi mahitaji hayo, hususani katika stadi zinazojitokeza kwa mara ya kwanza (*emerging skills*).
- Kuanza maandalizi ya awali ya chuo cha *VETA* Wilayani Igunga kwa kutumia majengo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rostam Aziz Mbunge wa Igunga. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri, katika kipindi cha Mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri nchini kwa mujibu wa Sheria Na. 10 ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

- Vyama viwili vya Wafanyakazi ambavyo ni Chama cha Wafanyakazi wa Mtandao wa Simu (*Telecommunication Workers Union of Tanzania (TEWUTA)*) na Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Ulinzi Binafsi (*Trade Union for Private Security Employees (TUPSE)*) vimesajili.
- Chama kimoja cha Waajiri (*The Association of Tanzania's Employers - ATE*) kimesajiliwa. Hivyo kufanya jumla ya vyama vya wafanyakazi na waajiri vilivyosajiliwa kufikia 20 ikiwa ni pamoja na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (*TUCTA*).
- Imeendelea kutoa ushauri kwa wafanyakazi juu ya haki ya kujiundia vyama vyao vya wafanyakazi. Jumla ya wafanyakazi 58 kutoka Sekta ya Mawasiliano ya Anga, Sekta ya Walimu, na Sekta isiyo rasmi na Sekta ya Nishati wamepatiwa ushauri. Serikali inatoa wito kwa Vyama vya Wafanyakazi kujitahidi kuwaelimisha wanachama wao pamoja na kuwashudumia ipasavyo kwa mujibu wa Kanuni na Katiba ili kuepusha migogoro ndani ya vyama.
- Kaguzi 52 za vyama hususani kumbukumbu za wanachama pamoja na vitabu vya mapato na matumizi katika mikoa ya Tabora, Mwanza, Mbeya, Iringa, Pwani na Tanga zimefanyika.
- Ilitoa elimu juu ya Sheria Mpya za Kazi. Jumla ya Makatibu Wakuu na Makatibu Wakuu Wasaidizi wa Vyama wapatao 35 wa vyama vyote vilivyosajiliwa walipatiwa elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kusimamia na kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri nchini.
- Kufanya Kaguzi za vyama vilivyopo pamoja na matawi yake yaliyopo nchini.
- Itaendelea kuvielimisha vyama kwa njia ya semina na mikutano ili viweze kuzielewa sheria, na hivyo kutekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Katiba na Kanuni na hivyo kupunguza migogoro inayozuka mionganii mwao.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), umuhimu wa Usalama na Afya ya wafanyakazi katika sehemu za kazi ulipewa uzito na Wizara.

Wizara pia imetumia mbinu mbalimbali kuhakikisha kwamba Sheria ya Usalama na Afya mahali pa kazi Na.5 ya Mwaka 2003 inafahamika kwa umma.

Napenda kuchukua nafasi hii, kuwakumbusha waajiri na wadau wote kwa ujumla kuwa, ni vyema kuzingatia sheria hiyo ili kuboresha afya na usalama sehemu za kazi hatimaye kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Wizara kuitia OSHA ilitekeleza yafuatayo:-

- Jumla ya kaguzi 2,150 za kawaida (*general workplace inspections*) zilifanyika na ushauri kutolewa.
- Kaguzi 2,905 maalum na za kisheria (*special and statutory*) ambazo zinajumuisha zana mbalimbali zitumikazo viwandani na sehemu zingine za kazi (*statutory plant inspections*), kaguzi za umeme (*electrical inspections*), upimaji wa afya za wafanyakazi (*Medical examinations*), upimaji wa athari za afya sehemu za kazi (*Industrial hygiene measurements*), uandikishaji wa viwanda au sehemu za kazi, uchunguzi wa ramani za majengo mapya yanayokusudiwa kuwa viwanda au sehemu za kazi (*scrutiny of industrial plans*) na uchunguzi wa ajali sehemu za kazi (*accident investigations*) zilifanyika.
- Kwa kushirikiana na Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani kanda ya Afrika Mashariki, pamoja na vyama vya wafanyakazi na waajiri ilianda na kuadhimisha kitaifa siku ya Afya na Usalama mahali pa kazi Duniani (tarehe 28 Aprili 2005) ikiwa ni kampeni maalumu ya kimataifa ya kuwataka wadau wote na umma kwa ujumla kujenga utamaduni katika nyanja ya usalama na afya (*safety and health culture*).
- Mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi kwa waajiri na wafanyakazi yalitolewa kwa njia ya semina katika mikoa mbalimbali. Aidha mafunzo ya aina hiyo yalitolewa pia kwa njia ya redio, televisheni, magazeti na vipeperushi.
- Kwa kushirikiana na wadau wengine imeandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Usalama na Afya mahali pa kazi.
- Imeshirikiana na Idara za Kazi katika nchi za Afrika Mashariki na Shirika la Kazi Duniani katika kutathimini na kuoanisha Sera na Sheria za Afya na Usalama sehemu za kazi kwa nchi zilizoko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 *OSHA* itatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kufanya kaguzi 2,500 za kawaida za usalama na afya sehemu za kazi.

- Kufanya kaguzi 3,025 maalumu na za kisheria za usalama na afya mahali pa kazi.
- Kuhakikisha kwamba vifaa vyta kupimia athari mbalimbali za kiafya na usalama sehemu za kazi vinapatikana.
- Kuimarisha ofisi za kanda ya Arusha na Mwanza kati ya sita zinazohusiana na usalama na afya mahali pa kazi.
- Kutoa mafunzo ya afya na usalama mahali pa kazi kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo redio, televisheni, magazeti na vipeperushi ili kuwafikia walengwa kwa wingi zaidi, hili litafanyika chini ya msaada wa *DANIDA*.
- Kutengeneza taratibu za kupata taarifa kuhusu magonjwa na ajali zitokanazo na kazi.
- Kuendelea na taratibu za ukarabati wa jengo la ofisi sehemu ya maabara, kliniki, chumba cha mafunzo, mikutano na maktaba.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii (*ISW*), Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambayo ni Chuo cha Elimu ya Juu katika masuala ya Ustawi wa Jamii Kazi na Rasilimali Watu iliendelea na shughuli zake za kitaaluma kwa kuzingatia malengo yaliyomo kwenye mpango wake (*Institute Strategic Plan*) wa mwaka 2002/2003 – 2006/2007. Taasisi hii ilianzishwa kwa Sheria Na 26 ya mwaka 1973.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, majukumu yafuatayo yalitekelezwa:-

- Ilisajili jumla ya wakurufunzi 400 katika kozi ndefu, na wakurufunzi 72 katika kozi fupifupi.
- Shughuli za upanuzi na uboreshaji miundo mbinu zilifanyika ambapo ujenzi wa madarasa mawili ya kisasa umekamilika na kuanza kutumika. Ujenzi wa madarasa mengine mawili upo katika hatua za mwisho. Kukamilika kwa madarasa hayo kumeiwezesha Taasisi kupunguza tatizo la uhaba wa madarasa kutokana na ongezeko la wakurufunzi kutoka 450 kwa mwaka 2003/04 hadi kufikia 653 kwa mwaka 2004/2005.
- Aidha maandalizi ya michoro ya maktaba kubwa ya kisasa (*Information Resource Centre*) yapo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji.
- Ilianza kutoa Stashahada ya Uzamili ya Sheria, Usuluhishi na Uamuji (*Postgraduate Diploma in Law, Mediation and Arbitration*). Jumla ya wakurufunzi 90 kutoka Idara ya Kazi, Shirikisho la Vyama vyta Wafanyakazi (*TUCTA*), Chama cha Waajiri (*ATE*) wamepatiwa mafunzo.

- Ilifundisha mafunzo ya muda mfupi katika fani za Kompyuta, malezi na ushauri nasaha. Ili kufanikisha masomo ya kompyuta, Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*) imetoa kompyuta 43 na mitaala wa masomo ya jioni umekamilika
- Jumla ya tafiti 3 kuhusu Ajira mbaya ya Watoto zimefanyika katika Mashamba ya Chai, Mkonge, Tumbaku, Maua (*Horticulture*), Migodini na katika sekta isiyo rasmi.
- Ilifundisha wakurufunzi na vikundi mbalimbali katika fani mbalimbali kutoka katika mashirika yasiyo ya Kiserikali kuhusu madhara yatokanayo na UKIMWI na mihadarati.
- Ilijumuisha (*Integrating*) masuala yanayohusu utawala bora kwenye mitaala ya fani zote zinazofundishwa katika Taasisi hii. Kufundisha na kufanya tafiti mbalimbali kuhusu wazee, watu wenyewe ulemavu, watoto yatima, athari zitokanazo na ukimwi na namna ya kupambana nazo.
- Ilifundisha mambo muhimu yanayohusu Sera ya Vyama Huru vya Wafanyakazi na Sheria mpya za kazi na ajira hususan miundo mbalimbali ya vyama hivyo katika soko huria na nafasi ya vyama vya wafanyakazi katika kuinua uchumi katika sehemu za kazi na Taifa kwa ujumla.
- Kubainisha machimbuko ya matatizo ya kijamii na kuainisha mbinu mbalimbali za utatuzi wake kwa njia ya tafiti za kina.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 majukumu yafuatayo yatakelezwaza:-

- Kupanua programu za mafunzo kutoka Stashahada ya Juu kuwa Shahada pamoja na kuanzisha mitaala ya kozi fupi fupi na masomo ya jioni ili kutoa nafasi kwa watanzania wengi zaidi kupata elimu ya juu hasa inayohusu masuala ya kazi, rasilimali watu na ustawi wa jamii.
- Kuongeza idadi ya wakurufunzi wa ndani na nje kutoka 653 hadi 850, ili kuwapa wananchi wengi zaidi nafasi ya kupata elimu ya juu itakayowawezesha kumiliki vyema uchumi wa Taifa.
- Kukamilisha ujenzi wa madarasa mawili na Maktaba kubwa ya kisasa (*Information Resource Centre*).
- Itatoa mafunzo maalum (*Executive programme*) ya Sheria mpya za Kazi kwa Maafisa Kazi waandamizi 30, mafunzo ya miezi mitatu kwa wadau wengine 90 na mafunzo ya stashahada ya uzamili katika utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya kazi kwa wakurufunzi 30.

- Kudhibiti kasi ya kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI kwa kuielemisha jamii juu ya athari za UKIMWI, kufanya tafiti na kuendesha Warsha na Semina mbalimbali mahali pa kazi.
- Kufanya maandalizi ya uanzishwaji wa Kituo cha Ushauri Nasaha na Malezi (*Counseling Centre*) kwa wadau mbalimbali hususan waathirika wa virusi nya UKIMWI.
- Kufanya maandalizi ya uanzishaji wa Kituo cha Uongozi kazi (*Centre for Labour Studies*) ambacho kitakuwa kitovu cha Uongozi kazi katika nchi za Afrika ya Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), katika kipindi cha 2004/2005 Baraza la Michezo la Taifa limetekeleza yafuatayo:-

- Limeelekeza na kushirikiana na Vyama nya Michezo kwa Watu wenye Ulemavu na Chama cha Michezo kwa Wanawake ili waunde Vilabu na Vyama nya Michezo katika ngazi mbalimbali kwa ajili ya kuongeza idadi ya washiriki.
- Liliwasiliana na Vyama nya Michezo 25 nya Taifa kuhimiza uanzishwaji wa timu za Vijana wadogo ambapo Vyama nya *TAHA, TBA, CHANETA, TFF* na *TTA* vimefanikiwa kuendesha mashindano ya Taifa kwa Vijana. Aidha, ilikusanya maoni ya mapendekezo na imeandaa Rasimu ya mkakati wa michezo kwa Vijana.
- Limesimamia na kuendesha chaguzi za Vyama nya Michezo ambapo Vyama nya *TOA, TSA, SPUTANZA* na *THU* vilifanya uchaguzi.
- Limeendesha Semina na Mikutano kwa Vyama nya Michezo 11 kuhusu masuala ya Utawala Bora na utatuzi wa migogoro katika Vyama nya Michezo.
- Kwa kushirikiana na Vyama nya *SAD, Right to Play* na *IPC* limeshiriki katika uendeshaji wa Semina na Bonanza yenyre lengo la kuwaelimisha Wanawake na Wanamichezo wenye Ulemavu kuhusu elimu ya UKIMWI na Afya njema kwa Wanaparalimpiki.
- Liliratibu kikamilifu ushiriki wa Timu za Tanzania katika mashindano ya Olimpiki, Paralimpiki (Olimpiki ya watu wenye ulemavu), Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa Vijana wenye Umri Chini ya Miaka 17, Timu ya Taifa ya Vijana ya kriketi kwenye mashindano ya Dunia kanda ya Afrika na Mpira wa Mikono.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006, Baraza la Michezo la Taifa litatekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha mkakati na kutoa mwongozo wa utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Michezo kwa Vijana.
- Kuanzisha utaratibu wa kuihusisha jamii kuhusika zaidi na michezo au Vikundi vya Michezo katika maeneo wanayoishi (*Community Sports*) kama njia bora ya kuiwezesha jamii kuweka misingi imara ya ushiriki katika michezo, kugharamia shughuli za michezo na kuibua vipaji vya wanamichezo na kuviendeza.
- Kuhamasisha jamii, wafanyabiashara na Umma kwa ujumla kuona uwezekano wa kuanzisha Vilabu vya Michezo ya kulipwa.
- Kusimamia na kuendesha chaguzi za vyama vitano vya michezo.
- Kuuelimisha Umma namna ya kuepukana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kupitia michezo.
- Kuvielimisha vikundi mbalimbali vya wanamichezo namna ya kuvigeuza vikundi vyao kuwa vya michezo na uzalishaji mali. Maeneo haya yanaweza kuwa msingi mzuri wa kupunguza umaskini mionganoni mwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa: (*NIP*), Wizara yangu kupitia Shirika la Tija la Taifa lililoanzishwa kwa Sheria Na. 17 ya Mwaka 1969 lina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za kuboresha Tija katika Taifa letu, litakalowezesha kuongozeka kwa pato la Taifa na hatimaye kuleta maendeleo ya kiuchumi na maisha bora kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005, Shirika la Tija la Taifa liliendelea na majukumu yake ya kuboresha tija na ufanisi kazini katika Taasisi za Umma, mashirika yasiyo ya kiserikali na makampuni binafsi kwa kupitia huduma zake za mafunzo, uelekezi na utafiti.

- Liliendesha mafunzo 71 kati ya 80 yaliyopangwa ambapo zaidi ya watanzania 700 kati ya 960 waliotegemewa kutoka katika sekta mbali mbali walipata mafunzo yanayolenga kuwapa mbinu za kisasa za kuboresha utendaji kazi katika sehemu zao za kazi.
- Lilifanikiwa kutoa huduma ya uelekezi kwa wateja 12 kati ya 10 waliotegemewa. Wateja hao walitoka katika Taasisi za Umma, Makampuni Binafsi na Mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani liliendelea na matayarisho ya mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Tija (*National Productivity Management Programme*).

Mheshimiwa Spika katika mwaka wa fedha 2005/2006, Shirika la Tija la Taifa litatekeleza yafuatayo:-

- Litatoa mafunzo 80 ya kuboresha ufanisi na tija kwa watu 1,000 kutoka katika taasisi za umma na binafsi.
- Limeandaa Rasimu ya mradi wa kuwafundisha jinsi ya kujinadi kwa waajiri. Rasimu hii kwa sasa ipo katika hatua ya kutafuta ufadhili.
- Kufanya utafiti wa mishahara kwa sekta na kada mbalimbali (*Tanzania Remuneration Survey*) na utafiti wa ubora wa huduma (*Tanzania Customer Satisfaction Survey*) kwa sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kazi, Mahakama ya Kazi kama chombo cha kitaifa kilichoundwa kwa Sheria Na.41 ya Mwaka 1967 na kufanyiwa marekebisho mbalimbali, imeendelea na majukumu yake chini ya sheria hiyo ambayo ni kusimamia haki, tija na mahusiano kati ya waajiri na wafanyakazi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Mahakama ya Kazi ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

- Jumla ya mashauri 212 kati ya 363 yaliyokuwepo na kupokelewa yalitolewa maamuzi kama ifuatavyo:-
    - Migogoro ya Kikazi 6 kati ya 8 iliyokuwepo ilitolewa Uamuzi.
    - Migogoro ya Uchunguzi 144 kati ya 247 ilitolewa Uamuzi.
    - Mikataba ya Hiari 17 ilisajiliwa kati ya 22 iliyokuwepo.
    - Maombi ya Marejeo 44 yalitolewa uamuzi kati ya 88 yaliyokuwepo.
    - Mkataba wa makubaliano 1 ulishughulikiwa.
  - Kwa msaada wa *DANIDA* imeanzisha na kutekeleza mpango wa ushirikiano kati ya Mahakama ya Kazi ya Tanzania na Mahakama ya kazi ya Denmark. Ushirikiano huu utasaidia kuimarisha Mahakama iwe ya kisasa kwa kukarabati majengo na kutumia vifaa vya kisasa.
- Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 majukumu yafuatayo yatakelezwa:-
- Kuhakikisha Sheria za Kazi zinazingatia uhusiano wa usawa na haki katika masuala ya kikazi na kwenye vyombo vingine vya kazi.

- Kuhakikisha uwajibikaji katika kutoa haki makazini kati ya waajiri na waajiriwa ili kuzuia rushwa, kuendeleza usawa wa kijinsia na kudhibiti UKIMWI kwa watumishi.
- Itawaelimisha wadau wa Mahakama kuhusu haki na majukumu yao na pia kuhusu majukumu, utendaji na mafanikio ya Mahakama ya Kazi.
- Kutokana na mabadiliko ya Sheria za Kazi zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu katika utekelezaji wake, Mahakama itakuwa Idara ya Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala, Idara ya Utawala na Utumishi ina majukumu mbalimbali yakiwemo ya kuajiri, kusimamia utendaji kazi, kutoa mafunzo ya utendaji kazi, kupambana na rushwa na ugonjwa hatari wa UKIMWI mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005 majukumu yafuatayo yalitekelezwa:-

- Iliendelea kuboresha utendaji kazi kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi, kudumisha maadili ya utumishi sehemu za kazi na kuboresha mfumo wa menejimenti na utoaji huduma bora kwa jamii.
- Imeanzisha Kamati ya Ajira ya Wizara itakayohusika na ajira mpya, kuthibitishwa kazini, upandishwaji vyeo na nidhamu ndani ya Wizara.
- Imejiri watumishi 66 wa kada mbalimbali ili kukabiliana na upungufu wa watumishi na kuongeza ufanisi.
- Imetoa Mafunzo kuhusu mabadiliko ya utendaji kazi (*OPRAS*) kwa watumishi zaidi ya 250 wa mikoa ya Arusha, Tanga, Mbeya, Morogoro na Dodoma.
- Imeendesha mafunzo kuhusu janga la UKIMWI sehemu za kazi kwa watumishi zaidi ya 250 wa Wizara. Aidha zaidi ya asimilia 90 ya watumishi wamepatiwa mafunzo kuhusu mapambano dhidi ya rushwa katika Kanda ya Mashariki, Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini, Kusini na Kati.
- Imeendesha vikao 2 vya Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, majukumu yafuatayo yatakelezwa:-

- Kuhakikisha kuwepo kwa mchanganuo mzuri wa kazi ya kila kada ndani ya Wizara ili kuwezesha mfumo mzuri wa utendaji kazi.
- Kuhakikisha kuwepo kwa utaratibu wa mfumo wa maendeleo ya watumishi.

- Kuhakikisha sera ya mafao ya uzeeni na pensheni kwa watumishi wanaostaifu inatekelezwa ndani ya wizara ili kuondoa kero kwa watumishi wastaaful.
- Kuendelea kutoa mafunzo ya *OPRAS*, Maadili, madhara ya ugonjwa na UKIMWI na Sera Mpya ya Utumishi wa Umma kwa watumishi wa Wizara.
- Kuandaa mchakato wa kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma kwa umma.
- Kuendelea kuandaa na kusimamia vikao vya Baraza la Wafanyakazi.
- Kuzindua mkataba wa huduma kwa wateja (*Client Service Charter*) baada ya kukamilika kwa sheria ya kazi na sera mbalimbali za wizara.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho, huduma zinazotolewa na Wizara yangu zinamgusa kila mwananchi kwa njia moja au nyingine. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao mbalimbali ya mawazo na ushauri walioutoa ndani na nje ya Bunge hili kwa Wizara yangu kwa nia ya kuboresha huduma tunazotoa.

Wizara iko tayari kuyapokea na kuyafanya kazi mapendekezo, ushauri na maoni watakayoendelea kuyatoa Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kusaidiana katika kuboresha huduma hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, majukumu yote niliyoyaeleza yametekelawa kwa ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda pia nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo pamoja na Mashirika na Taasisi zake kwa juhudhi zao kubwa walizozionyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa.

Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir Mbunge wa Mchinga, na Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa msaada na ushauri wake wa karibu.

Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Bwana Abubakar S. Rajabu, Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara na Bodi zao ambaao wameshirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wote ambaao kwa namna mbalimbali wametuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu, na kwa njia ya pekee naomba niitaje Kamati Maalumu ya kurekebisha

Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Jaji John Mrosso wa Mahakama ya Rufaa kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya ya kurekebisha Sheria za Kazi na Ajira, Bodi ya Ushauri wa Kazi (*Labour Advisory Board*), Bodi ya Ushauri ya Wizara (*Ministerial Advisory Board*), Shirikisho la Waajiri Tanzania (*ATE*) na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*) kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Mwisho katika mtiririko wa shukrani zangu lakini sio mwisho kwa umuhimu, naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Urambo Magharibi kwa ushirikiano wanaonipa na uchapakazi wao, sifa ambazo zinafanya kazi ya kuwatumikia iwe rahisi. Wizara yangu inatambua na itaendelea kutambua michango mbalimbali ya wahisani ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yetu.

Kwa kuwa siwezi kuwataja wahisani wote, kwa uchache naomba Shukrani za dhati ziende kwa Serikali za nchi na Mashirika ya Kimataifa ya Denmark, Marekani, Japan, China, Sweden, Canada, Ujeruman, Finland na Korea ya Kusini, *ILO*, *UNDP*, *UNFPA*, *UNIDO*, *UNICEF*, *FES*, *SHIA*, *ADB*, *ADF*, *OPEC*, *ABBORT* Pharmaceutical and Laboratories, Help Age International, *AXIOS*, *SIDE* by *SIDE*, *JICA* na Mashirika na makampuni ya hapa nyumbani ambayo ni *VODACOM*, Mpango wa Taifa wa Kuthibiti UKIMWI (*NACP*), *Africa Youth Alliance (AYA)*, Kahama Mines Ltd. na Kagera Sugar Ltd. Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Wizara, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2005/2006, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 37,954,287,300 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo chini ya Fungu 65. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 1,261,327,800 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo chini ya Fungu 60. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. HAROUB SAID MASOUD - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kanuni ya 88 (1), naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2004/2005 ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2005/2006 ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa salamu zangu za rambirambi kwa Wananchi na familia za marehemu waliokuwa Wabunge amba wamefariki katika kipindi hiki, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero, aliyeferikia Dunia tarehe 2 Juni, 2005 na Marehemu Mheshimiwa Margereth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa, aliyeferiki Dunia tarehe 23 Juni, 2005 wakati tunaendelea na vikao vya Mkutano huu wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, vifo hivi ni msiba mkubwa kwa Bunge letu Tukufu, kwa familia zao na kwa Wananchi wa maeneo waliyokuwa wakiwakilisha. Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. *Amina*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa salamu zangu za rambirambi, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya , Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa kuwezesha Tanzania kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kimataifa, ambayo itasimamia matumizi ya michezo kuleta maendeleo na amani Duniani. Kamati hii ina jumla ya nchi 12. Aidha, tunapongeza juhudhi zilizofanywa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani, Kanda ya Afrika Mashariki na Somalia, Ndugu Ali Ibrahim, kwa kufanikisha ujenzi wa Makao Makuu ya Shirika hili katika Kanda ya Afrika Mashariki, ambapo shehere za kuweka Jiwe la Msingi katika jengo hili zilifanyika tarehe 25 Mei, 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao katika kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Sophia M. Simba, Mwenyekiti Mbunge, mimi mwenyewe, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Omar Mohammed Mwenda , Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mheshimiwa Teddy L. Kassel-Bantu, Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde, Mheshimiwa Janeth E. Mashele, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye na Mheshimiwa Kisyeri Chambiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo ya taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2004/2005, pamoja na mapendekezo ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2005/2006 ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, tarehe 30 mpaka 31 Mei, 2005 Jijini Dar es Salaam. Mambo yaliyojadiliwa katika taarifa hiyo ni pamoja na Dira ya Wizara, Majukumu ya Wizara, Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Mapato na Matumizi kwa kipindi kilichopita cha 2004/2005, Mafanikio na Matatizo yaliyojiteza wakati wa utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika katika kipindi cha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hatua mbalimbali za utekelezaji zilizofikiwa na Wizara katika kutekeleza maagizo na ushauri uliotolewa na Kamati wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata maelezo na kupitia mapendekezo ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2005/2006 Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za kununua vifaa vya kujimudu kwa wanafunzi wa vyuo vya watu wenye ulemavu kutoka shilingi milioni tano kwa mwaka wa fedha 2004/2005 hadi kufikia kiasi cha shilingi 19,250,000 kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Hata hivyo, kutoptaka na mahitaji mengi ya vifaa kwa wanafunzi katika vyuo hivyo, fedha hiyo haitoshi. Kamati inashauri juhudi zaidi zifanyike ili Serikali iweze kuongeza kiasi kikubwa zaidi cha fedha.

Pili, Serikali ifanye maandalizi mazuri kwa vyuo vya watu wenye ulemavu kuweza kupata elimu nzuri na yenye ubora sawa na vyuo vingine kama vilivyo chini ya *VETA*.

Tatu, Kamati inaipongeza Serikali kwa utaratibu wa kuanza kuwalipa malipo ya saa za ziada watumishi na walimu wanaowahudumia watu wenye ulemavu, ikiwa ni pamoa na wale wanaowahudumia wazee na watoto waishio katika makambi. Hata hivyo, malipo haya hayatoshi ikilinganishwa na kazi wanazozifanya. Kamati inashauri Serikali kuona uwezekano wa kuwalipa malipo maalum (*Special Allowance*) au malipo ya mazingira magumu (*Hardship Allowance*).

Nne, walimu wanaopendekezwa kufundisha katika vyuo vya watu wenye ulemavu, wawe na sifa za utaalamu wa fani husika ili kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi sahihi na kupata soko la bidhaa zao mara wanapomaliza mafunzo yao.

Tano, hali ya vyuo vya watu wenye ulemavu ni mbaya sana na vingine kufungwa na hivyo kupunguza nafasi ya watu wenye ulemavu kujiunga na vyuo hivyo, ambavyo ni Chuo cha Lwanzari Tabora, kimefungwa karibu miaka tisa sasa lakini walimu wanaendelea kulipwa mishahara; Chuo cha Mihayo Mwanza kimefungwa, Chuo cha Mtapika Masasi, kimegeuzwa kuwa Sekondari na hakuna sababu zozote za wazi kwa nini kimegeuzwa kuwa Sekondari na Chuo cha Singida Mjini hali yake ni mbaya. Kamati inashauri Vyuo hivyo, vifanyiwe ukarabati na vilivyofungwa vitafutiwe ufumbuzi ili viendelee kutumika. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Kamati ilibahatika kutembelea Mradi wa Kuendeleza Usawa wa Jinsia na Ajira Bora na Salama, unaoendeshwa na ufadhili wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Kamati ilisikitishwa sana, kuona hali mbaya walionayo vijana ambaa ndio nguzo ya Taifa katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Vijana hawa ni wale wanajishughulisha na biashara ya ngono na uuzaaji na utumiaji wa madawa ya kulevyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaupongeza Mradi wa Kuendeleza Usawa wa Jinsia na Ajira Bora na Salama, kwa juhudi zake za kuwatoa vijana hawa katika ajira hiyo mbaya. Aidha, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

- Kupitia Taasisi mbalimbali za Mashirika, iangalie uwezekano wa kuwapatia makazi maalum na yenye heshima, vijana waliotoka katika biashara haramu ya ngono na

madawa ya kulevyta, kwani inakuwa vigumu kuachana kabisa na vitendo hivi wakiwa katika mazingira yale yale;

- Kutoptaka na vijana wengi kuwa na nia ya dhati ya kuacha kutumia madawa ya kulevyta na ambao tayari wameshaathirika, Kamati inashauri Serikali kufanya juhudhi za makusudi ili kuwanusuru vijana hawa kwa kuwapatia matibabu dhidi ya madawa haya ya kulevyta; na

- Mheshimiwa Spika, eneo la uwanja wa fisi lililopo Manzese Dar es Salaam, ndio maarufu kwa vijana watumiao madawa ya kulevyta na biashara mbaya ya ngono, ina watoto zaidi ya 100 waliozaliwa bila kutarajiwa na wanaishi katika hali ngumu na ya kusikitisha sana. Watoto wengine hawalewi hata mama zao wanaishi wapi, hali hiyo imepelekeea watoto hao kuishi kwa mateso na mbaya zaidi kuiga tabia za wazazi wao na wao kujikuta wanafanya biashara ya ngono na kubakwa katika umri mdogo sana. Kamati inashauri Serikali kupatia Serikali za Mitaa kuangalia uwezekano wa kupata eneo la kujenga kituo cha kulelea watoto hawa ili kuwaokoa kabla hawajaathirika vibaya zaidi. Hii pia itakuwa njia bora na nzuri ya kuwasaidia wazazi wao katika jitihada za kujikwamua kiuchumi na kijamii kwani watakuwa na nafasi ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujilettea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii pia ilionana na akina mama watu wazima ambao wanaishi eneo la uwanja wa fisi, ambao wametolewa kutoka katika biashara mbaya ya ngono na madawa ya kulevyta. Wengi wao walieleza sababu za kufanya biashara hiyo kuwa ni pamoja na mfarakano katika ndoa. Kamati inashauri jamii kutotelekeza familia zao na kusababisha madhara makubwa kwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuendeleza Usawa wa Jinsia na Ajira Bora na Salama, umeonesha mafanikio makubwa Mkoani Dar es Salaam. Kamati inashauri Mradi huu usiishie Dar es Salaam tu uende pia katika Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na ongezeko la watu katika makambi ya wazee wenye ukoma na wasijiweza. Ongezeko hili linatokana na kuzaliana kwa wakazi hao, hali inayosababisha upungufu mkubwa wa huduma zitolewazo. Kwa ujumla hali ya makambi ni mbaya. Kamati inashauri Serikali kuona uwezekano wa kuwasaidia watoto na vijana, wanaozaliwa katika makambi haya, wapate mafunzo ya ufundi ili waweze kujitegemea na kupunguza mzigoto kwa Serikali wa kuendelea kuwahudumia wakiwa makambini. Kutoptaka na makambi mengi kutokuwa na mipaka (*fence*), Wananchi wamekuwa wakiingilia na kumega sehemu ya makazi haya kwa mfano, kambi ya watu wenye ukoma Musoma Vijijini, imeingiliwa na mwekezaji. Kamati inashauri Serikali kuona uwezekano wa umuhimu wa kuyawekea mipaka maeneo hayo.

Pili, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za kugharamia chakula, mavazi, malazi na madawa katika Taasisi zinazohudumia watu wenye ulemavu, wazee na watoto kutoka shilingi 204,568,100 kwa mwaka wa fedha 2004/2004 hadi shilingi 408,085,000 kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Hata hivyo, kutoptaka na ongezeko la watu katika makambi haya, kiasi hiki bado hakitoshi, Kamati inaiomba Serikali kuwa na uwezekano wa kuongeza fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kumaliza mgogoro wa uongozi katika Shirika la Mpira wa Miguu (*TFF*). Aidha, inaupongeza uongozi wa *TFF* kwa kukubali maelekezo ya Serikali na kuyafanya marekebisho Katiba yao ili kukidhi mahitaji ya wadau. Kamati inaipongeza Serikali vile vile kwa hatua iliyofikia katika ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo ambao Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, aliweka Jiwe la Msingi tarehe 18 Julai, 2005. Hata hivyo, Kamati inashauri juhudui iongezwe zaidi ili uwanja huo uweze kukamilika kama ilivyopangwa Januari, 2007.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Ajira (*Labour Exchange Centre*), Kamati inakipongeza kituo hiki kwa kazi nzuri ya kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri. Kuanzia 2001 hadi mwaka 2005, kituo kiliandikisha watafuta kazi 9,877, kati yao 4,808 wamefanikiwa kupata kazi. Hata hivyo, Kamati inashauri huduma hiyo, iende hadi Mikoa mingine isiishie Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na migogoro inayoendelea ndani ya Mamlaka ya *VETA*, chombo ambacho ni mkombozi kwa vijana wetu. Ili kuinusuru Mamlaka hiyo, Kamati inashauri Serikali isimamie na ihakikishe migogoro hiyo inamalizika haraka iwezekanavyo. Kutokana na bidhaa nyingi zinazozalishwa na *VETA* kuuzwa kwa bei ya juu, kwa sababu ya mchakato wa ununuzi wa malighafi, Kamati inashauri Serikali iruhusu Taasisi za Umma ndogondogo kama *VETA*, zinunue malighafi kutoka viwandani kama inavyoruhusu Wakuu wa Shule za Sekondari, ili kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kuuza bidhaa kwa bei za ushindani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inalipongeza Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), kwa juhudui zake inazozifanya katika kuwekeza. Moja kati ya miradi yake mikubwa ni *Mafuta House* lililopo Jijini Dar es Salaam. Mheshimiwa Spika, mradi wa jengo hili ulianzishwa na Shirika la Taifa la Maendeleo ya *Mafuta* (*TPDC*) na Shirika la Nyumba la Taifa *NHC* mwaka 1995. Ujenzi wa jengo hili ulikwama 1999 kutokana na ukosefu wa fedha, baada ya kukosa mnunuzi na mbia wa kuendeleza Mradi huu. Serikali iliamua kuukabidhi Mradi huo kwa *NSSF*, kwa nia ya kuuendeleza hapo Mei, 2004. Uamuzi huo ulifikiwa katika kikao kilichofanyika katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kilichowahusisha Viongozi wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wizara ya Fedha, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Nishati na Madini, pamoja na Viongozi wa Mashirika ya *NSSF*, *TPDC* na *NHC*.

Hata hivyo, *NSSF* ilikabidhiwa Mradi huu kwa masharti yafuatayo: ilipe madeni yote ya Mradi yapatayo shilingi bilioni 4.3; iangalie uwezekano wa kuendelea na washauri, pamoja na makandarasi waliopo ili kuharakisha utekelezaji wa Mradi na kunusuru gharama zaidi; Mradi uanzu kutekelezwa mara moja na taratibu za kuhamisha umiliki wa jengo zianze mara moja. Ni mategemeo yetu kuwa, hilo limeshatekelezwa kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini hapa Bungeni. Mradi huu unatarajiwa kuigharimu *NSSF* shilingi bilioni 23.299.

Mheshimiwa Spika, katika jengo hili kuna sehemu iliyokuwa imetengwa maalumu kwa shughuli za kuhifadhi kumbukumbu za utafiti kwa ajili ya *TPDC*. Sehemu hii ina ukubwa wa mita za mraba 550 na ziko katika ghorofa ya chini ya *Block A*. Kwa kuzingatia umuhimu wa sehemu hiyo kwa *TPDC*, Shirika la *NSSF* liliamua kuwapatia sehemu hii kwa matumizi yao kama yalivyokusudiwa bila malipo yoyote. Taarifa hii ilitolewa kwa wahusika na ukaguzi wa kitaalam kufanyika na timu ya pamoja ya wataalam wa mashirika hayo mawili.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa, lina kazi kubwa ya kutoa mafunzo ya kuongeza tija sehemu ya kazi. Shirika hili lilikuwa na kiwanja cha kujenga ofisi eneo la Mbezi - Jijini Dar es Salaam na tayari lilikwisha tumia shilingi milioni 113,903. Kwa kuendeleza kiwanja hicho, Kamati inaishauri Serikali kuwa, fedha zilizotumika katika kuendeleza eneo hilo zirejeshwe kwa shirika, pamoja na kupatiwa kiwanja kingine kinachokidhi mahitaji ya shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni na ushauri, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, inaunga mkono mapendelekezo ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Fungu Namba 60 na 65 kama ifuatavyo: Fungu 60 - Matumizi ya Kawaida shilingi 513,490,9000; Miradi ya Maendeleo shilingi 732,000; jumla shilingi 144,222,900. Fungu 65 - Matumizi ya Kawaida shilingi 5,742,283,200, Miradi ya Maendeleo shilingi 12,500,000; jumla shilingi 18,242,283,200.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge Mchinga, Katibu Mkuu, Ndugu Abubakar Rajabu na wafanyakazi wote wa Wizara, kwa maandalizi mazuri ya taarifa na pia kwa ushirikiano ambao wameutoa kwa Kamati hii wakati wote. Napenda niyashukuru Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa kutoa ushirikiano mzuri mbele ya Kamati. Mashirika hayo ni Shirika la Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi (*VETA*), Shirika la Tija la Taifa (*NIP*), Taasisi ya Usalama wa Afya mahali pa Kazi (*OSHA*), Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Mahakama ya Kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru tena, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa juhudhi zao katika kutoa maoni na ushirikiano wao katika kupitia Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Naomba pia nimshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L.Foka, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake vizuri. Vilevile napenda kumshukuru Katibu wetu, Bibi Angelina Sanga, kwa kuihudumia vizuri Kamati hii, pamoja na kuandaa taarifa hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa njia ya pekee, naomba niwashukuru wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Koani, kwa kuniwezesha kuwa hapa kwa vipindi viwili na mategemeo yangu Mwenyezi Mungu akipenda na Mwenyezi Mungu atajalia vilevile, awape nia ya kunirudisha tena katika kipindi hicho cha mwaka 2005/2010.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, bora niwataje waliojiandikisha kuchangia ili wajiandae ni Mheshimiwa Athuman S.M. Janguo, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi na Mheshimiwa Mohamed H. Missanga. Ndio wanne wa mwanzo, watakaotumia saa moja ya kwanza ya majadiliano. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba mpokee shukrani zetu za dhati, kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa mwaka wa fedha 2005/2006, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 45(5) (b) (c), toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia, kuwapongeza wote ambao wameendelea kuteuliwa na vyama vyao kuingia katika kinyang'anyiro cha kutafuta ridhaa ya Watanzania kuongozza dola. Pia nawapongeza wale wote, ambao tayari wamebahatika kushinda kura za maoni kupitia vyama vyao kugombea nafasi za Ubunge, Uwakilishi na Udiwani. Naamini hizo ni dalili nzuri za kuelekea katika mafanikio.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Kamati nzima ya Uongozi ya Kambi hiyo, kwa kazi wanayoifanya ili kushiriki kikamilifu Bungeni licha ya mazingira magumu. Vile vile nawashukuru Mheshimiwa *Alhaj Profesa Juma Athuman Kapuya*, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wao, Bwana Abubakar Rajabu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi wanayoifanya na naomba wasichoke, japokuwa bajeti itolewayo na Serikali kwenye Idara zake nyeti kwa maendeleo ya Taifa haitoshi. Mbaya zaidi, ukiangalia fungu lililotengwa mwaka huu wa bajeti kwa ajili ya maendeleo ni karibu nusu ya bajeti ya mwaka uliopita, ambapo Bunge liliidhinisha shilingi 55,338,811,000, wakati mwaka huu wa fedha ni shilingi 27,664,219,000.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Bunge hili, tumeendelea kushuhudia migogoro mingi katika sehemu za kazi, wafanyakazi kutolipwa mafao wanayostahili na wakati mwingine kutolipwa kabisa, tumeshuhudia migogoro mingi ya kazi ikichelewa kutatuliwa kwa wakati na kusababisha wahusika kupata tabu na usumbufu mwingi wakati wanasubiri maamuzi toka kwa Mheshimiwa Waziri, Mahakama ya Kazi au Baraza la Usuluhihi.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Grace Kiwelu, akiwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani, kwenye Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tarehe 1 Julai, 2005, alieleza bayana, wasiwasi wetu dhidi ya

mfumo wa ajira na utendaji kazi wa Makampuni mengi ya nje, yanayofanikiwa kupata Mikataba ya kazi nchini kwa kutotii na kuheshimu sheria, kanuni na miongozo ya kiutumishi hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni aibu na fedheha, siku moja baada ya uwekaji wa Jiwe la Msingi katika Uwanja mpya wa Taifa, shuhuli kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kunafumuka mgomo, ngumi na kurushiana maneno mazito baina ya Wafanyakazi Wazalendo na Kampuni inayowaajiri ya Kichina. Chanzo kikubwa kikiwa ni maslahi na malipo duni. Tunashauri badala ya sisi viongozi wa juu wa Serikali kujitokeza haraka haraka na kutoa kauli zinazoonekana kuwatetea na kuwalinda hawa wageni, ni vema tukawa tunakaa kwanza na kutafakari chanzo cha tatizo. Mengi ya Makampuni haya ya Kigeni, yana mambo ya kimya kimya ya kiunyanyasaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ajira, wakati idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa, kuna maelezo kuwa, ajira pia inapungua kwa kasi hiyo hiyo. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, Tanzania hivi sasa ina watu wanaokadiriwa kufikia milioni 35. Idadi hiyo ni kubwa ikilinganishwa na watu milioni tisa waliokuwepo wakati Tanganyika inapata uhuru mwaka 1961.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati idadi ya watu inaongezeka, viongozi wa vyama vya wafanyakazi, wanazidi kulalamika juu ya kasi ya upungufu wa ajira inavyoongezeka. Tathmini ya kujua kama ajira inaongezeka au inapungua, haijafanyika lakini Watanzania wote tunaona inapungua, hasa ukiangalia idadi ya vijana wanaomaliza Kidato cha Nne na kufaulu bila kuingia Kidato cha Tano au wanaomaliza Kidato cha Sita na kufaulu bila ya kupata nafasi ya kuingia Chuo Kikuu. Hii yote ni nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa ajira isiyo rasmi ni moja ya dalili kuu zinazoonesha kwamba, Tanzania hivi sasa inakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa ajira iliyo rasmi. Takwimu zinaonesha kuwa, kati ya idadi ya watu wote 2,690,399 wanaoishi Dar es Salaam, asilimia 46.5 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi hawana kazi na katika bajeti ya Serikali haioneshi ni mikakati gani imewekwa ili kupambana na tatizo hilo. Ajira viwandani ni ndogo sana. Katika nguvu kazi ya Watanzania milioni 16 ni Watanzania wasiozidi 59,010 tu ndio wenye ajira katika sekta rasmi ya viwanda. Ajira rasmi katika sekta zote haizidi watu 800,000.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa ajira rasmi ni kigezo muhimu cha uchumi unaokua na kupunguza umaskini. Hii ni kutohana na ukweli kwamba, shughuli nyingine zote za kujiajiri zinategemea matumizi ya vipato vya wale wenye ajira rasmi kwa mfano, mkulima, seremala, fundi cherehani, kinyozi, mwuza duka na kadhalika, wote wanategemea mzunguko wa fedha ambao chanzo chake ni yule mwenye ajira rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mathalani, kikijengwa kiwanda mahali kinachoajiri wafanyakazi 1,000, ambao kwa wastani kila mmoja wao analipwa shilingi 100,000/= kwa

mwezi, kila mwisho wa mwezi kutakuwa na ongezeko la jumla ya shilingi milioni 100 kwenye mikono ya wafanyakazi hao, ambazo ziko tayari kutumiwa. Wapo wanaohitaji vitanda watakwenda kwa fundi seremala. Wapo watakaohitaji suruali au magauni watakwenda kwa fundi cherehani. Wapo watakaohitaji mchele, maharage, unga, mchicha na kadhalika, watakwenda sokoni. Fundi seremala naye ili aweze kuchonga vitanda vyta watu, atahitaji kununua na kuchaniwa mbao. Fundi cherehani atahitaji kununua vitambaa na nyuzi. Mchuuzi wa sokoni atahitaji mkulima amwuzie nafaka na kadhalika, ili mradi ajira rasmi 1,000 zinaweza zikatengeneza mlolongo wa ajira tegemezi zinazoweza kuajiri watu wengine hata 5,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hali ya ajira ni soko. Tunasema mtu wa kuajiriwa lazima afiti katika ajira ya soko, hali hiyo inasababishwa na Serikali kushindwa kulinda baadhi ya ajira. Ili kulinda ajira za vijana wetu ni vema tukasisitiza mfumo wa kutoa mafunzo kazini (*In-service Training*), ambao utasaidia kuongeza ujuzi wa ufanisi wa watu walio kazini badala ya kuwatimua huku ikifahamika hawatakuwa na nafasi ya kupata ajira tena popote pale kutokana na ushindani katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, mfano ni Kiwanda cha Bia cha Kibo Moshi, ambacho baada ya Serikali kushindwa kukilinda, kilinunuliwa na wafanyakazi wote wakapoteza ajira. Madhara ya wafanyakazi kupoteza ajira, yameingia moja kwa moja hadi kwenye sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inasema ikipata ridhaa ya Wananchi, italinda ajira za wafanyakazi, Serikali inao uwezo huo amba ni kuzuia wafanyakazi kutoka nje kuingia nchini kuchukua kila kazi hata zile zinazoweza kufanywa na Wazalendo. Hivi sasa wageni wanaruhusiwa kuanzisha karakana za magari, kuuza maua, kuendesha migahawa na kadhalika; hivi Watanzania wasipolindwa kuyafanya hayo watakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, tutapanua wigo wa ajira na kutofautisha maeneo ya kuwekeza ili kuwasaidia Wananchi wetu mbalimbali na hususan vijana wetu wanaohitimu katika vyuo mbalimbali vyta Elimu ya Juu na Wananchi waliopunguzwa kazi, walio wabunifu na wenye mawazo mapya kujilingiza katika shughuli za kujajiri kuititia biashara na uzalishaji. Serikali itaanzisha Mfuko rasmi wa kulea na kukuza biashara na uzalishaji viwandani (*Trade and Manufacturing Incubator Funds*).

Mheshimiwa Spika, ajira ya Serikali, pamoja na kwenye Mashirika ya Umma na yale ya Binafsi ni asilimia 4.8 tu. Pamoja na uchache wao, wafanyakazi hao wanapata mishahara midogo ambayo haiwezi kukidhi mahitaji halisi ya kila siku. Kwa sasa kima cha chini kilichotangazwa katika bajeti hii ni shilingi 67,500/=.

Mheshimiwa Spika, mbali na kima hicho kuwa kidogo wakati wa kutoa nyongeza, Serikali pia haizingatii mahitaji ya mfanyakazi kwa mfano, mwenye familia ya watoto sita, ambaye pia anapanga chumba mjini cha shilingi 5,000/= kwa mwezi na

akiwa na vyumba vitatu maana yake ni shilingi 15,000/= kwa mwezi, anapewa nyongeza sawa na asiye na familia.

Mheshimiwa Spika, vijana ambao ni Wananchi wa chini ya umri wa mika 30, wanaunda asilimia 70 ya Wananchi wote nchini. Vijana ndiyo kundi lenye mchango mkubwa katika uzalishaji kuliko kundi lingine lolote na kwa maana hiyo, umuhimu wa kundi hili kwa jamii ni mkubwa mno. Serikali imelipuuza kundi hili kwa muda mrefu mno, sehemu kubwa ya vijana hawana fursa za ajira za kueleweka, kitu ambacho kinawasababisha walio wengi kujikuta wakilazimika kuingia katika vitendo viovu, kupambana na umaskini unaowakibili. Vijana wengi wamekata tamaa kabisa kiasi kwamba, wanadhani kwamba, njia pekee iliyobaki ya kujiletea maendeleo yao au kujipatia kipato ni wao kuondoka nchini au kufanya vitendo vya ujambazi ikiwa ni sehemu ya mtaji wa maskini ambapo ni nguvu zake mwenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hali hii haiashirii mazingira mazuri kwa maendeleo ya nchi na vita dhidi ya umaskini. Mtazamo wa Serikali kwa vijana ni wa ubabaishaji na mara nyingi huwa unalenga pale tu wanapohitajika ili kufanikisha malengo fulani fulani ya Serikali hususan wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, suala hili linaloitwa Maendeleo ya Vijana, bado limekuwa ni kero kubwa katika nchi yetu. Kupiga vita UKIMWI na kuandaa warsha za *NGOs* na *CDOs* na kukimbiza Mwenge, haviwezi kuleta maendeleo kwa vijana wetu bila kupanga mipango endelevu itakayowawezesha kupata elimu na hatimaye ajira itakuwa ni kazi bure. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia fedha nyingi za Serikali kwa kukimbiza Mwenge na hatimaye kutoa taarifa za miradi iliyofunguliwa wakati wa mbio hizo za mwenge ni kitendawili kinachotaka kuteguliwa. Kitu cha kujiuliza ni *sustainability* ya miradi hiyo na miradi hiyo inakuwa kwenye *programs* zipo za maendeleo. Mara nyingi miradi hiyo si mipya bali wahusika hutumia kivuli cha Mwenge ili waonekane wamefanya kitu, kumbe mradi ulibuniwa na watu wengine na kwa madhumuni mengine tofauti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hali ya michezo ya burudani nchini imekuwa siyo nzuri kwa muda mrefu sasa. Viwanja vyetu vya michezo viko katika hali mbaya na mbaya zaidi ni pale viwanja takriban 15 vinapohodhiwa na CCM, japo sisi sote tuliweka jasho letu katika ujenzi wa Viwanja hivyo, hata wakati wa ukarabati wa viwanja hivi kwa shuhuli maalum mfano, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Fedha za Serikali hutumika japo mmiliki wa uwanja tunaambiwa ni CCM. Suala hili si haki kwa wanamichezo na Watanzania kwa ujumla, kwani viwanja hivyo vinatakiwa kuwa ni mali ya Serikali na siyo mali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, wawakilishi wetu mbalimbali kwenye michezo ya Kimataifa, wanaendelea kufanya vibaya kila mara. Mara kadhaa timu zetu za Taifa, zimekuwa zikiokolewa na wafanyabiasha binafsi ili zisishindwe kuwakilisha Taifa. Hali hii ni ya kushangaza sana ikizingatiwa kuwa katika matumizi ya Serikali, kiasi cha shilingi

879,583,600 kilichotengwa katika bajeti ya michezo kwa kipindi cha 2005/2006 ni kidogo mno kwa ajili ya maendeleo ya michezo na shughuli za utawala.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ikipata nafasi ya kuunda Serikali, itahimiza ujenzi wa viwanja vipyta ya michezo na uboreshaji wa vile ambavyo tayari vipo. Katika hili hatutaki iwe siri, tuchukuapo Serikali Novemba, 2005, viwanja vyote vilivyoporwa na CCM vitarejeshwa Serikalini. Jukumu la kukamilisha azma hii litakabidhiwa kwa Mabaraza ya Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya, pamoja na vyanzo vingine vya fedha. Mamlaka hizo zitatafuta wabia wa kushirikiana nao kukamilisha jukumu hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ushindani zaidi katika michezo, Serikali ya Upinzani kwa kushirikiana na vyama vya michezo mbalimbali, itabuni mashindano ya ziada nje ya ligi za kawaida, ikiwa ni pamoja na kutafuta wadhamini wa uhakika wa kudhamini mashindano hayo. Aidha, Serikali itashauriana na *TF* juu ya kulifufua Kombe la Taifa, pamoja na kuweka mikakati ya kukisaidia chama hicho kupata wadhamini wa uhakika kwa ajili ya udhamini wa Kombe hilo. Katika kuweka changamoto katika mashindano hayo kama ifanyikavyo Kombe la Dunia, kila Mkoa utaruhusiwa kuwatumia wachezaji wa Mikoa yao wanaocheza *Club* za nje ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ili wanamichezo waweze kushindana kikamilifu na kuitumia michezo kama ajira, Taifa halina budi kukubali kuwa mabadiliko ya msingi ni lazima yafanyike katika sekta ya michezo ili wanamichezo wetu waweze kuitegemea michezo wanayocheza kama ajira. Serikali itawatumia wataalamu mbalimbali wa masuala ya michezo ili kupata mkakati bora wa kuasisi mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa ya Wananchi kuunda Serikali, itahakikisha kuwa, kunakuwa na mkakati unaoigusa jamii nzima katika kuhakikisha kuwa, viwango vya ubora wa washiriki wa Taifa letu katika medani za michezo na burudani vinapanda. Serikali pia itachukua hatua zifuatazo:-

(a) Itaboresha huduma za burudani na michezo mijini na vijijini na kusambaza wataalamu wa fani mbalimbali katika medani hizo ili kusaidia kutambua vipaji na kuviendeleza.

(b) Itashawishi ushiriki zaidi wa sekta binafsi katika kuwekeza katika huduma za burudani na michezo.

(c) Itashawishi vijana kuwa mstari wa mbele kuyaendeleza yale yote mazuri yanayopatikana katika tamaduni zetu na kupiga vita tamaduni mbaya za kigeni.

(d) Itashawishi vijana kushiriki kwa hiari yao katika harakati mbalimbali za kijamii kama vile uboreshaji wa mazingira na kuwasaidia wagonjwa, watoto, wazee na yatima.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha Sheria ya Haki Miliki, inapewa meno, kwani Serikali ya sasa pamoja na kuwa wasanii wamekuwa wakikosa mapato halali ya

kazi zao na wajanja wachache wamekuwa wakinufaika na kazi hizo za wasanii. Hivyo, lengo letu hasa si tu kupata medali kwenye mashindano mbalimbali, bali ni pamoja na biashara kama wenzetu wafanyavyo.

Mheshimiwa Spika, Sanaa ya Urembo hapa kwetu ni mpya katika mazingira na utamaduni wa Mtanzania na hilo nadhani halina ubishi wa aina yoyote ile. Hivyo basi, licha ya Tanzania kutoa washiriki katika mashindano mbalimbali duniani, lakini bado washiriki wameshindwa kuonesha umahiri wao na hii yote siyo kosa lao, ila kushindwa kwao tunaweza kukuelezea kuwa, kunatokana na tatizo la vigezo vitumiwavyo hapa kwetu, huenda haviendani na vigezo vitumiwavyo katika mashindano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumo katika utandawazi, kwa maana hiyo basi, hatuna budi kwenda na wenzetu sambamba. Kuna usemi unaotumika sana katika sanaa hii ya urembo usemao: “*Beauty with Purpose*”, hii siyo kuwa mzuri tu, uzuri wa umbo na sura bila ya kuwa na vipaji vingine pia uharaka wa akili katika kufikiri.

Mheshimiwa Spika, ili tuwe washindani na washindi katika fani hii, tunatakiwa kuondoa ubabaishaji wa waandaaji wa mashindano haya na hili linawezekana pale tu Serikali itakapoweka mkono wake, kwa kuangalia sifa za watu na makampuni yanayoandaa mashindano haya kuanzia ngazi za vitongozi mpaka Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani, katika kila watu 10 ulimwenguni, mmoja wao ni mlemavu. Kwa kuwianisha hii, ina maana kwamba, asilimia 10 ya watu wote Watanzania, yaani watu 3,700,000 ni walemavu wa aina moja ama nyingine. Kwa mtazamo wa aina yoyote ile, idadi hii ni kubwa mno, kiasi cha kuhitajika mipango maalumu inayolilenga kundi hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kutekeleza Sheria Namba 2 na 3 za mwaka 1982, zinazolinda ajira na matunzo kwa walemavu. Aidha, Serikali imeshindwa kuridhia Azimio la Umoja wa Mataifa Namba 149 la mwaka 1982 linalowahu walemavu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa ya Watanzania ya kuunda Serikali, itahakikisha kuwa, nchi yetu inaweka mazingira mazuri ya kupunguza matatizo yaletayo ulemavu, ambao kwa kiasi kikubwa, husababishwa na ajali na uzembe katika sekta nzima ya Afya. Aidha, Serikali itatekeleza Sheria Namba 2 na 3 za mwaka 1982 na kuridhia Azimio la Umoja wa Mataifa Namba 149 la mwaka 1982, linalowahu walemavu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ulioanzishwa wa kuwajengea makazi wazee ni mzuri, tunaipongeza Serikali kwa hilo, lakini kosa kubwa linalofanyika ni kuwatenga wazee hao na kuwaweka peke yao.

Mheshimiwa Spika, majukumu makubwa ya Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ni pamoja na kuandikisha wanachama kwa Mfuko wa Hifadhi, kukusanya michango ya

Wanachama, kulipa mafao kwa Wanachama, kuwekeza Mafao ya Wanachama kwenye vitega uchumi mbalimbali ili kuboresha mafao ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wakuu wa *NSSF* ni wafanyakazi wa kawaida, ikiwa ni pamoja na kundi kubwa la wafanyakazi wa ngazi za chini. Pamoja na mafanikio hayo makubwa ya Shirika hili, lakini Shirika limewasahau sana wachangiaji wake sahihi na matokeo yake wanaofaidi zaidi huduma zake siyo wale wanaolibeba kikweli kweli Shirika hili kupitia michango yao. Kambi ya Upinzani, pamoja na wachangiaji, tungelipenda kuelewa ni lini hasa pesa tunazoweka zitaanza kuzaa na wachangiaji kupewa gawio kulingana na mchango wa kila mwanachama, kwani ukiangalia kwa undani ni sawa na kuwekeza, ni sawa na kununua hisa. Shirika linatumia fedha hizo kwenye miradi mbalimbali inayozidi kuliingizia fedha nyingi, wanachama wanataka kupata gawio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kuwekeza mitaji ni muhimu lakini vilevile ni muhimu kufanyika kwa tahadhari kubwa na zaidi ni lazima maslahi ya wachangiaji yatangulizwe kwanza. Bodi ya Wadhamini, inapaswa iwe makini katika kusimamia majukumu yake. Kambi ya Upinzani hatusiti kusema kwamba, ubia na urafiki wa kasi kubwa unaondelea baina ya *NSSF* na mfanyabiashara Yusuph Manji, mwenye kumiliki *Quality Group*, ambapo amekuwa akikopeshwa mabilioni ya fedha za wateja na yeye kuingia Mikataba ya kuliuzia shirika hilo hilo vitu mbalimbali na mambo mengine mengi, ni mambo ambayo Bodi inapaswa iyaangalie kwa umakini na kwa uangalifu, vinginevyo mnanusa hali ya hatari siku za usoni hata ikibidi ni vema Tume iundwe kuchunguza kwa makini ni nini kinachoendelea humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi hali inavyoendelea na hususan kwa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii nchini, Kambi ya Upinzani, inaona ipo haja kubwa ya kuunda chombo cha kusimamia vizuri matumizi ya Mifuko hii, vinginevyo ipo siku itajikuta inapata matatizo makubwa na pengine kushindwa kulipa wanachama mafao yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Micheweni, kwa imani walijonayo kwangu na kwa ushirikiano walionipa kwa kipindi chote walichonichagua kuwa Mbunge wao. Nakishukuru Chama changu kwa kuniamini tena na kunteua kugombea tena Kiti cha Ubunge katika Jimbo la Micheweni tarehe 30 Oktoba, 2005. Kwa mshikamano nilionao, Wana-CUF na Wananchi wote wa Jimboni kwangu, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, *Inshallah*, nina uhakika kwa wale watakaopata ridhaa ya Wananchi wao na kuchaguliwa tena, tutaonana tena hapa Bungeni Novemba, 2005. Ahsante. (*Makofi*)

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha CUF. Chama kilichonipa tiketi ya kuwepo humu ndani, kuiongoza vema Kambi yetu bila migogoro wala fitina na kwa umakini na busara ya hali ya juu.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Chama kuwa Mwenyekiti na mwongoza kikosi cha kukitafutia chama

changu cha *CUF* ushindi mkubwa nchi nzima katika uchaguzi wa mwaka huu. Tunawaomba Wananchi wa Bukoba Mjini, waturejeshee Jemedari wetu huyu hapa Bungeni tarehe 30 Oktoba wakati wa Uchaguzi Mkuu.

Aidha, nawapongeza Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, toka kwa vyama vya CHADEMA, *TLP*, *UDP* na *CUF*, kwa kuilinda na kuivusha Kambi salama hadi mwisho wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wabunge wote, bila kumsahau Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Wafanyakazi wote wa Bunge.

Baada ya kuyasema hayo, kwa sababu Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya ni rafiki yangu wa karibu, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha na ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofî*)

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Napenda nitamke mwanzo kabisa kwamba, naiunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofî*)

Nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa *Alhaj* Profesa Juma Athumani Kapuya au Juma Athumani Janguo, Naibu wake, Ndugu yangu, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Katibu Mkuu Bwana Abubakar Rajab na Wasaidizi wao wote, kwa mambo mawili; kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara na pia kwa kutuletea hoja safi. (*Makofî*)

Labda nichukue nafasi hii vilevile nimpongeze Mjumbe wa Kamati yangu, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, kwa ndoto za mchana za kwamba, Kambi ya Upinzani itachukua Serikali mwezi Novemba. Nataka nimirahadharishe kwamba, Watanzania wanajua kuchagua mchele kando na chuya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo kwa Wizara, ninayo maoni machache ambayo hayana shabaha ya kukosoa bali ni kuboresha ili ziwavezeshe kufanya kazi zao vizuri. Mchango wangu unalenga katika maeneo yafuatayo: Sera na Mipango ya kukuza uzalishaji na ajira hasa kwa vijana; nidhamu ya kazi, haki na uwajibikaji kazini; uboreshaji wa michango ya makundi maalum katika jamii na huduma za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*).

Mheshimiwa Spika, Sera na Mipango ya Wizara hii hapana budi zilenge katika kukuza ajira hasa ya vijana ambao ndio nguvukazi ya leo na kesho katika Taifa hili kwa ajili ya kukuza uchumi wa Taifa letu. Ajira ya vijana hasa ile ya kujiajiri wenyewe kule vijijini, hapana budi ipewe kipaumbele, vinginevyo vijana watakata tamaa, wataendelea kumiminikia mijini, ujambazi utaongezeka, utulivu utaondoka na kwamba, MKUKUTA utakuwa umetekelozwa kwa maneno tu. Labda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuwa, siku hizi vijana wetu kila wanapokutana na Mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi, wanamwimbia wimbo wa ajira, ajira, ajira. Hii ina maana kwamba, kwao

wao hii ni kero kubwa sana na wana matumaini makubwa kwamba, huko tuendako kero ya ajira itapungua. Kwa hiyo, tusipokuwa na mipango thabiti ya ajira, utulivu wao kama nilivyosema mwanzo utaondoka, haitoshi kutueleza katika hoja hii kwamba, utaratibu upo wa kuangalia na kusimamia vikundi 4,000 vya Kambi za Vijana, wanataka pawe na ajira katika maeneo mbalimbali ya kujajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kule Jimboni kwangu Kisarawe, kila ninapokutana na vijana swalii kubwa ninaloulizwa ni Serikali ina mipango gani ya kuongeza ajira vijijini, sina jibu. Wanazo shughuli nyingi za kufanya katika kilimo, useremala, uchongaji vinyago, ususi wa mikeka kwa akina mama, ushonaji, ufumaji na kadhalika, lakini matatizo yao makubwa ni ukosefu wa mitaji, ujuzi na kutokuwapo masoko ya kuuzia bidhaa zao.

Kwenye bajeti ya 2004/2005 na bajeti hii tunayoizungumzia hivi sasa, Wizara imeweka malengo mazuri sana kuhusu mpango wa mafunzo ya watu kujajiri wenyewe na kuondoa umaskini. Wao wanasema *Demand Driven Skills Training Program*, lakini nasikitika kusema kuwa, malengo haya mazuri hayathibitishwi kibajeti. Kati ya bajeti ya shilingi 10,290,000,000 ya Matumizi ya Kawaida, maeneo yanayozingatia ajira hayakupewa uzito. Kwa mfano, Programu 40, *Social Services* imetengewa shilingi bilioni 390,000,000 sawa na asilimia karibu 30; Programu 50 Maendeleo ya Vijana imetengewa shilingi 1,138,000,000 tu, sawa na asilimia 10 na Sera na Mipango ambayo mimi naamini ndizo zinazoandaa maendeleo za kazi, zimepangiwa shilingi milioni 598 tu, sawa na asilimia 0.6. Kwa utaratibu huu, nauliza tutafika?

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina mpango mzuri sana wa kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Waziri. Lakini tofauti na ilivyo katika mfuko wa mikopo kwa akina mama kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, sikumbuki ni lini kwa mara ya mwisho vijana wa Kisarawe wamepatiwa mikopo hiyo. Wananiuliza lakini sina jibu, sasa wakati Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anajibu hoja zetu, namwomba kwa makini kabisa, awaambie vijana wa Kisarawe, ni lini watapata mikopo kupitia Wizara yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalie bajeti ya maendeleo ya mwaka huu na miaka miwili iliyopita kuanzia 2003/2004, kuhusu ajira na maendeleo ya vijana. Kwa miaka mitatu mfululizo, hakukutengwa kitu chochote kwa fedha zetu wenyewe, isipokuwa shilingi 1,789,000,000 zilizotengwa kwa *VETA* mwaka 2003/2004. Hapa napenda kumshukuru na kumpongeza sana, Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uamuzi wake wa busara kwamba, hataondoka madarakani kabla ya Uwanja wa Michezo wa Kisasa wa Karne ya 21 kuanza kujengwa. Kwa uamuzi wake huo, uwanja huo tangu bajeti iliyopita na bajeti hii sasa umetengewa shilingi 27,500,000,000 na ujenzi kama ilivyokwisha elezwa hapo mwanzo kwamba, unaendelea. Hongera sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitatu, sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo, sawa na shilingi 50,200,000,000, imetokana na wahisani wa nje, tunawashukuru sana lakini tungependa vilevile tuone fedha za Tanzania zinapangwa kwa ajili ya maendeleo.

Sasa nizungumzie nidhamu na uwajibikaji. MKUKUTA una malengo makuu matatu, kama tunavyofamu, Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, Kuboresha Maisha ya watu wetu, Utawala Bora na Uwajibikaji. Wizara hii inahusika sana na malengo haya makubwa ya nidhamu kazini na uwajibikaji wa waajiriwa na waajiri ni nyenzo muhimu za kuongeza uzalishaji na kukuza uchumi hivyo, kupunguza umaskini. Haki na wajibu ni vielelezo vya Utawala Bora, kwa hiyo, Wizara hii ina jukumu kubwa la kusimamia nidhamu, haaki na wajibu mahali pa kazi. Nitamke tu kwamba, kwa hili, ningependa kuipongeza Wizara kwamba, imefanya kazi nzuri katika eneo hilo. (*Makofî*)

Wametuletea Bungeni hapa Sheria mbalimbali za kazi na marekebisho yake, kama inavyoelezwa katika ibara ya saba ya hotuba ya Waziri. Wamesimamia majadiliano baina ya Wafanyakazi na Menejimenti na hivi juzi tu na ninapenda kumshukuru Waziri kwamba, amesimamia na kushuhudia Mkataba wa Uelewano baina ya Menejimenti ya *TANESCO* na Wafanyakazi. Nafikiri utaratibu huu wazidi kuuendeleza. Lakini namshauri Waziri pale *NBC* nadhani mambo bado hayajawa sawa, hebu tupia macho ili ufanye kama vile ulivyofanya kule *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu utakua kwa haraka sana na umaskini utapigwa vita kama hatutayaacha nyuma, makundi yaliyonyongea katika nchi hii, yaani ni pamoja na wanawake, watoto, walemovu na wazee. Ninafahamu kwamba, kama ilivyosemwa katika hotuba hii kwamba, tayari tunayo mipango mizuri kwa wanawake na vijana, lakini kwa upande wa wazee na walemovu naona bado kunahitajika kuongeza nguvu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu walemovu, naipongeza Serikali kwa kuwa na Makambi ya Walemovu, lakini kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia hoja hii ni kwamba, bado maeneo mengi yanatakiwa yatiliwe nguvu. Nashauri kuwa, Serikali vilevile isimamie sekta binafsi ili yale ambayo Serikali imeyaweka kwa kuboresha utendaji kazi na kuondoa matatizo ya walemovu, yafanyike vilevile katika sekta binafsi ambayo sasa hivi bado haijazingatia sheria tulizopitisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi sana kujenga shule na makazi maalum kwa walemovu. Huduma mbalimbali zinatolewa lakini kama nilivyosema kwamba, haya hayatoshi kwa sababu naambowi ziko Kambi kama 17 tu. Je, Mikoa yote hii itakuwa inategemea Kambi hizo 17?

Mheshimiwa Spika, kwa harakaharaka kabla kengele haijanililia, ninapenda kuupongeza Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, ikiwemo Bodi ambayo baadhi ya Wakurugenzi wake wapo hapa Bungeni na Menejimenti ambayo inaongozwa na kijana shupavu sana, Dr. Ramadhani Dau. Mimi namfahamu sana Dr. Dau kwamba, ni mchapakazi hodari na ndiyo maana nilipokuwa katika Mamlaka ya Bandari, niliishawishi Bodi tukamnyakua kutoka Chuo Kikuu na ninafurahi kwamba, sasa kule *NSSF* mambo kwa kweli yanakwenda vizuri mno, nawapongeza ye ye na Menejimenti yake. Menejimenti imeweza kuboresha huduma za Mfuko na imeboresha vilevile maslahi ya wafanyakazi, kwa faida ya wanachama, wafanyakazi na Taifa kwa ujumla, kama tunavyoolezwa katika ibara ya 27 ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa utendaji kazi wake mzuri, *NSSF* sasa imekuwa mwokozi wa baadhi ya Mashirika ambayo kwa sababu mbalimbali, yameanza kulegalega. Tumeshuhudia jinsi Shirika hilo lilivyookoa miradi ya *NASACO*, *TAZARA* na *TPDC*, baada ya mashirika hayo kushindwa kukamilisha miradi yao hasa pale *Leaders Club*, *TAZARA*, Jengo la *NASACO* ambalo sasa limepewa jina la *Water Front* na *Mafuta House*, ambayo Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ameizungumzia.

Lakini napenda kuitahadharisha Serikali, ijizue katika kulishawishi Shirika hili au kulishinikiza kuingia kwenye miradi ambayo haikufanyiwa upembuzi yakinifu wa kiuchumi (*Economic Analysis*), vinginevyo si muda mrefu, Mfuko huu utatumbukizwa kwenye janga la kuwa mufilisi, kama ilivyotokea kwa Benki yetu ya Biashara kabla hatujabinafsisha. Benki ya Biashara, ililazimishwa kutoa mamiloni ya shilingi ya mikopo kwa *National Milling Corporation* na baadhi ya Vyama vya Ushirika, matokeo yake ni kwamba, Vyama vya Ushirika vilikufa na *National Milling* ilikufa na *NBC* ikadidimia hapo tulipoibinafsisha.

Tujifunze kutokana na makosa yetu ya nyuma, mfano wa kuifanya *NSSF* kuwekeza katika Jengo la *Mafuta*, mimi binafsi sikuupendelea na hasa pale ambapo kunawekwa kikao cha Mawaziri wazito sana chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, unafikiri Menejimenti inaweza ikasema kwamba, hapana? Halafu ya kuifanya iweze kulipa madeni ya nyuma na kuendelea kujijenga ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kama nilivyosema, mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Pili, napenda kuipongeza Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa *Alhaj Profesa Juma Kapuya*, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kutuandalia hotuba nzuri, yenye ufanuzi na matarajio ya yale ambayo tunafikiria kwamba, yatatendeka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru ushirikiano nilioupata kwa miaka mitano, pamoja na kwamba, sikuwa kwenye Kamati ya Kudumu yao, lakini kwa upande wangu, ndiyo Wizara Mama inayoshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu, ambapo mimi humu ndani ndiyo mwakilishi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kwa kweli tumeshirikiana, kurekebishana na kukumbushana, ni jambo la kawaida kwa sababu wote tulilenga kujaribu kuleta maendeleo mema kwa jamii inayohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, nitachangia machache katika kukumbusha ili yawekwe sawa, awamu ijayo iendeleze mambo hayo. Nitajikita zaidi kwenye suala la watu wenye ulemavu, maana ndilo ambalo nina ujuzi nalo kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza, kuipongeza Serikali na Wizara, kwa kukamilisha Sera ya Maendeleo ya Watu wenyе Ulemavu. Hii nakumbuka ilikuwa hekaheka mwaka 2002 mpaka nilitaka kutoa shilingi, lakini ndiyo hivyo, tulikuwa tunashauriana tu. Mchakato umeendelea, sera ile imekamilika na sasa angalau tunaweza tukaanza kuitumia.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa ninachokiomba ni Serikali kuweza kuchukua hatua madhubuti kwa kweli kuelimisha sera hii kwa wadau mbalimbali ili wafahamu yaliyomo mle ndani, waweze kusaidia hata kushauri nini kifanyike katika hiyo mikakati ambayo Serikali imeshasema hapa kwamba, ndiyo inaandaa mikakati ya utekelezaji wake. Kwa sababu wapo wadau na wanajua pia, kwa hiyo, ningeomba hili liweze kufanyika kwa sababu sijaona limeanza *seriously* baada ya sera ile kupitishwa au kukamilika na imetafsiriwa hata kwa lugha ya vidoti doti ili wenzetu wasioona waweze kuisoma. Sasa inapendeza ikifahamika vizuri kwa wadau wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, pia nadhani sheria hii pamoja na swalı langu la tarehe 16 nilijibiwa kwamba, hakuna haja ya sheria kutungwa bali kanuni. Basi hizo kanuni ziharakishwe ili tuone utekelezaji wake ukianza *seriously*.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka katika bajeti ya 2003/2004, Serikali iliahidi kwamba, baada ya ukamilifu wa kisera, basi itaendelea na michakato na kuhakikisha kwamba, inakamilisha kuridhiwa kwa Mkataba wa Kimataifa unaohusu Kanuni na haki za watu wenyе ulemavu duniani na kule mwanzo tuliridhia. Mimi ninaombra na mchakato huu pia uendelee kusudi uendane na yaliyomo kwenye sera na uendane na hizo kanuni tuone mabadiliko ya watu wenyе ulemavu yakiwa na kasi ya kuonekana na kutekelezwa kwake.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia, naishukuru sana sana Kamati ya Maendeleo ya Jamii katika ukurasa wake wa tano mpaka wa nane, ilivyofafanua kinaganaga masuala ya watu wenyе ulemavu na matatizo waliyoyaona nadhani kwa kipindi cha miaka mitano iliopita. Hapa nazingatia umuhimu wa Vyuo vya Ufundı vya Watu wenyе Ulemavu vyote, kufunguliwa na vyote kuendelezwa vizuri. Wenzangu wamesema Lwazari Tabora kuna hata Masiwani Tanga, kimefungwa kabisa na hapa ninachoomba kufahamu, kwa nini Mtapika Masasi Chuo kilichokuwa cha Walemau Wasioona, wanapata stadi za kazi kimebadilishwa kuwa Sekondari.

Mheshimiwa Spika, nimesikia tu sasa ninaombra Wizara ituthibitishie hilo na inieleze sababu za kutosheleza, kwa nini mabadiliko hayo yametokea ili basi tuweze kushauriana. Labda Hal mashauri zime-force kwamba, hayo majengo na nini, lakini, je, wale ambaو walikuwa wanasoma wa Kanda ile ya Kusini kule sasa watakwenda wapi? Ndiyo waende Tabora, ndiyo waende Dar es Saalam, mbona huduma na gharama zitakuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, ningependa kufahamu kabisa sababu za Mtapika Masasi kubadilishwa matumizi kuwa ni *Secondary School*. Nimesikia lakini naamini ni kweli kwa sababu Kamati imeuliza hivi sababu zake ni nini? Nataka kufahamu ili tuweze basi kwa pamoja, kuona ushauri wake utakuwa nini.

Mheshimiwa Spika, ni mwaka 2003 na 2004, tulipitisha sheria za ajira mpya, ambazo kweli nilifurahi kwa sababu zielekeza kwamba, hapatakuwa na ubaguzi wowote wa ajira kutokana na hali na mambo kama hayo na hata ulemavu ndani yake ukiwemo. Lakini kwa masikitiko, kama mchangiaji mmoja alivyosema, suala la ajira kwa watu wenyе ulemavu limekuwa gumi na nadhani litaendelea kuwa gumi kama kweli hatutakuwa na mikakati ya dhati. Waajiri binafsi wengi hata siku moja hawaamini kwamba, watu wenyе ulemavu, wanaweza wakatoa tija katika shughuli zao, isipokuwa nina mfano wa mwajiri mmoja wa Moshi kule kwenye kiwanda cha viatu, sijui yule ameingiwa sana na dini, lakini wengi wala hawana habari.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ajira ni za ushindani, mpaka mtu usailiwe na ushinde. Lakini mimi kwa kipindi cha mwaka 2004 na 2005, nimepata hata malalamiko kutoka kwa watu wenyе ulemavu waliohitimu kwenye Vyuo Vikuu kwamba, wanapokwenda kwenye usaili, hawaambulii kitu pamoja na kwamba, wamesoma sawa na wenzao. Lakini bado zile fikra kwamba, watu wenyе ulemavu hawawezi kuwa na tija katika kazi bado ipo kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ninao ushauri wala siyo kulalamika, ni kwamba, basi Serikali ichukue jukumu lake la kwanza kabisa, ikishirikiana na uongozi wa Vyama vya Watu wenyе Ulemavu, labda kuendelea kuelimisha jamii kwa ujumla, kuhusu masuala ya watu wenyе ulemavu, mahitaji yao, haki zao, labda tuone nini kinawenza kikabadilika. Vinginevyo, bado fikra ni zile zile hakuna kinachowezekana, lakini uwezekano upo.

Mheshimiwa Spika, lingine kuhusiana na ajira, kuna suala la kujajiri. Hapa nirudie kama wenzangu walivyosema, tatizo kubwa ni mtaji. Katika Wizara hii, kuna Mfuko wa Vijana wa Mikopo, lakini nasikitika kusema kwamba, Halmashauri zilizo nyingi ambazo ndiyo Wakala wa Mfuko huu, hazitoi mikopo kwa vikundi vya watu wenyе ulemavu. Hiyo ni fikra kwamba, wenyе ulemavu hawarejeshi mikopo na hao hawawezi kazi. Sasa watu wenyе ulemavu kwa hali zao, sitaki kurudia kuyasema mengi, kwa sababu kwa miaka mitano nimeimba. Wenyе ulemavu ndiyo wana matatizo zaidi ya wenzao. Kama vijana wengine wana matatizo na kama wanawake wengine wana matatizo, wanawake na vijana wenyе ulemavu, wana matatizo mara 10, ndiyo ambao wanapaswa kupewa kipaumbele waweze kujikwamua katika hali zao duni na hapo ndipo umaskini umejikita. Kwa hiyo, hawana hiyo nafasi ya kupewa mikopo, kwa sababu Halmashauri nyingi kwa kweli hazijali, kuna Halmashauri chache ambazo zimejitalidi kuweza kuwawezesha, lakini Halmashauri zilizo nyingi hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Spika, labda hapa pia niweze kushauri, pamoja na sheria tulizozipitisha, pamoja na matatizo ya mikopo, labda Serikali ione uwezekano wa kuweza kutoa motisha kwa waajiri mbalimbali, wanaowaajiri watu wenyе ulemavu, waweze kupewa kitu cha kuweza kuwavutia ili labda tatizo hili liweze kupungua, vinginevyo mambo si mazuri.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kuona kwamba, uwanja wetu mpya kule Dar es Salaam unakidhi mahitaji ya sisi walemaru kuingia bila wasiwasi, tutaenda

maliwato bila wasiwasi, kwa kweli huo ni mwanzo mzuri. Kwa sababu michezo nayo ni afya, michezo husaidia kuleta mahusiano, hata vyama vyetu vya kisiasa huko nyuma vilianza katika viwanja vya michezo.

Kwa hiyo, hiyo ni nafasi hasa kwa wale wa Dar es Salaam wataweza kuingia huko na kuona na kutumia vile viwanja, hata kukiandaa kwenye michezo mbalimbali ambayo tumeambiwa hapa kuna *Special Olympics* na kadha wa kadha. Kwa hiyo, hili ninalipongeza sana na naomba tu kwamba, ule uwanja uishe na Mungu akinijalia, niwe wa kwanza kabisa kuingia na kuyaona hayo yaliyomo kwenye ramani yametimizwa na wenzangu waweze kufaidika nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini hapa basi kwa sababu Wizara na Serikali ni moja, ningombua tu mwanzo huu mzuri, tuiione Serikali yetu kwa ujumla inaboresha maeneo yote ya umma, kuweza kuitika bila tatizo na watu wenye ulemavu. Kuhusu michezo, naomba Serikali itoe kama ruzuku ya kutosha hasa kwenye maandalizi ya michezo ya watu wenye ulemavu. Kwenye *olympic* na nini wanaleta sifa nchini hapa, lakini maandalizi yake mara nyingi sana yanakumbwa na ukwasi, kwa hiyo, mambo yanakuwa siyo mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa leo niseme tu kwamba, mengi yameniridhisha, lakini ninachosikitika kidogo tena ni kwamba, duniani sasa hivi kuna mchakato wa kuwa na Mkataba wa Haki na Ustawi wa Watu wenye Ulemavu Duniani huko New York. Katika Mchakato huo, Serikali zinashiriki. Kwa masikitiko makubwa, nchi yetu ya Tanzania haina mtu anayekwenda kule kwa *capacity* ya Serikali, akatoa msimamo wa nchi kwamba, tunasema nini katika suala hili. Naambiya kwenye kiti chetu, sijawahi kwenda huko, kwenye kiti chetu ni bendera inapepea *with absence*. Sasa Tanzania yenyе hadhi Kimataifa, tushindwe hilo nalo la kulishiriki ili baadaye turidhie vitu vya kupita tu. Wanakwenda wachache kwa kupidia mgongo wa *NGOs*, lakini mawazo yao hayachukuliwi kwamba, hiyo ni *context* ya Serikali, yanabaki tu kuwa mawazo. Kwa hiyo, naomba kabisa kwanza, nifahamishwe labda Serikali haijui kwamba, mambo hayo yanaendelea na kama linafahamika, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi baada ya kuligundua nimelipeleka Serikalini na kujaribu kuwaambia kwamba, jamani kuna hili inakuwaje, mpaka leo nakiri kusema kwamba, sijapata maelekezo wala maelezo ya nini kinachoendelea. Sasa kwa ujumla unaweza ukasema basi tunadharauliwa kwa sababu ni mchakato wa watu wenye ulemavu, mbona mazingira walishiriki. Sasa mawazo kama haya, hayapendezi na hayawesi yakatupeleka mahali pazuri. Kwa hiyo, naomba hili Serikali ilione na inieleze leo hasa tatizo ni nini ili nisizidi kuumia kumbe mambo yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda tu kumalizia kuhusu Elimu ya Juu. Nilisema kwenye Wizara inayohusika, kila kipengele cha watu wenye ulemavu kwa kweli nilikisema katika sehemu zake kwa miaka yote mitano. Suala la watu wenye ulemavu, nasema kwamba ni Mtambuka kwa sababu ni sehemu gani ambapo hutaona mlemavu, atahitaji matibabu, atahitaji sijui nini, yaani ni Mtambuka kama tunavyosema Jinsia. Kwa hiyo, kila mahali kwa kweli walemavu wapo na ninaishukuru sana Kamati,

imeeleza mengi sana na yote yale ninakubaliana nayo, imeweza kusaidia na huo ni ushiriki au ushirikiano mzuri ambaao tulikuwa nao.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Bunge linaishia ishia, napenda kutoa shukrani kwako, kila nilipoomba nafasi ya kuchangia hata kama kulikuwa hakuna nafasi, nadhani nilikuwa napata upendeleo wa namna fulani, kwa sababu nilikuwa mwakilishi pekee ili niyaseme yafahamike na naamini katika kuzungumza kwangu, niseme ukweli Waheshimiwa Wabunge, wamefaidika. Sasa wanafahamu ulemavu ni kitu gani na wengi wamesaidia sana hata kwenye Majimbo yao, wametoa *wheelchairs*, wameshiriki, yaani kuna *sense* ya kufahamu zaidi masuala hayo ya ulemavu kwa miaka mitano. Hiyo nini, walnikubali, walikuwa wanansikiliza na ulikuwa unanipa nafasi ya kusema hapa ndani kwa ukamilifu kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa hilo, umetuongoza vizuri. Licha ya shukrani hizo, napenda kabisa kabisa kuwashukuru, Waheshimiwa Wabunge wote, tangu *back benchers* mpaka Mawaziri. Nimefarijika kwa miaka mitano walnipenda sana, kweli kabisa nakiri walnipa ushirikiano mno hata wakati wa kupanda ngazi kama msichana wangu hayupo, Mawaziri walikuwa wanansaidia kupanda ngazi, si kawaida. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa ananikuta mara nyingi kwenye kona fulani pale lazima atasimama Mheshimiwa Margareth Mkanga hujambo, yaani nilikuwa sehemu kwa kweli ya wote waliokuwemo humu ndani ya Bunge. Mimi nawashukuru sana na sitasahau. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Baada ya kuwashukuru wengine wote, niwatakia kheri ya kurudi tena humu Bungeni. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

Mheshimiwa Spika na mimi niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, kwa kazi wanazozifanya. Lingine leo ninasimama kuchangia katika Wizara hii na hasa katika masuala ya Vijana na kwa vile mimi ni kijana, kwa hiyo, nina uhakika yale nitakayoyasema ni mawazo yao kwa usahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa niwaombe Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, tuelewane vizuri katika hoja nitakazozitoa. Maana siwasemei wao, kwa yale mazuri ambayo wameyafanya, wameshayasema kwenye hotuba yao. Ni bahati mbaya kwamba, kuna mengine ambayo pengine Wizara haikuyafanya, hawakuyataja. Nitakapoyataja hayo nina uhakika, waamini kwamba, ninausema mfumo mzima wa Kiserikali au mfumo mzima wa sisi Wananchi wa Tanzania na siyo kama namsema Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya au Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya hayo, nilikuwa najaribu kuangalia hii Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anazungumzia kama kutanzua migogoro iliyopo kazini, mahali ambapo kazi tayari zipo

sasa awashughulikie wale walioko pale na migogoro yao na maslahi yao. Lakini pengine nilitaka kufikiri kwamba, Wizara hii iko pale kwa kuhakikisha kwamba, kila Mtanzania ikiwezekana kwa kushirikiana na Wizara nyingine, anayo kazi ya kufanya na kama kazi hana anaundiwa mazingira ya kupata kazi ile na siyo kwamba, mtu anakaa hapo kwenye kijiwe, hana cha kufanya wakati tuna Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Spika, sasa nimeangalia na wametoa takwimu kwa Dar es Salaam, kwa maana kwamba, hawajaenda kwingine. Mheshimiwa Waziri, amesema kulikuwa na watafuta kazi 9,881 wakajiandikisha kwenye Kituo kinachohusika, waliounganishwa na waajiri walikuwa 4,189 na waliopata bahati ya kuajiriwa walikuwa 330. Kwa hiyo, 9,511 hawakuajiriwa kwa pale Dar es Salaam. Sasa inakuwaje kwenye maeneo kama Mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga, Rukwa, Mara, Arusha na kwingine ambako Kituo hiki hakikuwepo. Kwa dalili hii ya kwamba, walioomba walikuwa karibu 10,000 wakaajiriwa 330, inaonesha kwamba, kwa kweli tuna kazi kubwa na tuna kazi ngumu ambayo inatukabili na kwamba, Wizara sasa pengine haijajipanua kufikia kule.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, tukubaliane kwamba, unaweza kwenda katika Kijiji labda pengine pale Ukerewe au Rarya au Kitwe, ukizungumza Wizara ya Afya, watu wanaona manesi pale, ukizungumza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wanaona Polisi wanapita, ukizungumza Wizara ya Elimu na Utamaduni wanawaona walimu wako pale, lakini ukizungumza Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo sina uhakika kwamba, kwenye ngazi ya Vijiji au Kata, kuna mtumishi anayehusika katika kuwakusanya vijana kwenye vikundi na kuwaambia mambo kadha wa kadha yanayohusu wao kupata ajira na kufanya kazi mahali pale walipo. Nadhani huo ni udhaifu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninaamini hata *plan* zetu hapa za jinsi ya kuwapatia vijana kazi haiko wazi, kwa sababu hakuna mpango maalum. Ukitaka kuwapatia kazi lazima uangalie ni sekta zipi na kila sekta sasa kwa kushirikiana na Wizara iliyopo mnawapatiaje kazi hao. Mathalani kwenye Sekta ya Kilimo, unaweza ukasema kilimo hapo na unaimba kilimo, lakini kuna vijana wamemaliza shule hawana ardhi, hawakwenda shuleni, hawakwenda *VETA*, hawategemei kuajiriwa Polisi, hawategemei kuajiriwa popote, lakini wamekaa pale, ardhi hawana, ardhi iliyopo ni ya baba zao, lakini siyo kwamba, Tanzania hatuna ardhi, ardhi ipo kubwa tu na hata hivyo, ukiwaambia waende wakachukue mapori, sasa waende kwenye mapori hivi hivi tu bila msaada, Serikali haiwajui, hatua ya kwanza miezi sita ili iwafikishe pale, hakuna barabara wala hakuna nini. Sasa mambo haya lazima tuyaaingalie, vinginevyo tunajiwekea bomu ambalo litatulipukia na tutashangaa, kile tunachojivunia hakitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ametuambia hapa masuala ya maendeleo ya vijana kwamba, mpaka 2004 mwishoni, Serikali ilitoa shilingi bilioni moja na milioni mia saba hivi kwa ajili ya kuwakopesha vijana na kwa mantiki hiyo, kila Wilaya ilipata kwenye shilingi milioni tatu. Sasa najuliza, mathalani Wilaya ya Karagwe ina watu 500,000, kule Geita nadhani wako 600,000, sasa kila Wilaya ikiipatia

shilingi milioni tatu kuwakopesha vijana, tuseme kila Wilaya ina Kata 30 na kwenye kila Kata kuna vikundi vya Vijana sijui kimoja, vitano, sielewi.

Lakini inavyoelekea hizo shilingi milioni tatu ukitaka kila mtu umpe shilingi laki moja, utawakopesha watu 30 au vikundi 30 na kama ni vikundi wataambiwa kwanza, waombe maombi wayapeleke Wilayani, kwa hiyo, hizo ni gharama, wataambiwa kama wamekubaliwa, wapige picha wazipeleke kwenye benki na kwa sababu iko mbali, wataambiwa wajaze fomu, wataambiwa waende kufungua akaunti na wataambiwa waende kupeleka watia saini kule kwenye Benki. Sasa kutegemea na umbali wa nchi hii, hao watu uliowapa shilingi laki moja sijui wako 10, sijui wako wangapi, sijui wauze maandazi, sijui wauze vitumbua, mimi sielewi. Sasa hiyo shilingi laki moja unawapa hicho kikundi wafanyie nini labda pengine wanunue mpira?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa tunachokifanya nadhani tunafanya mzaha. Ni neno sahihi kabisa na nadhani sisikitiki kwa kusema kwamba, tunafanya mzaha, kwa sababu *there is no impact at all* na hizo shilingi milioni tatu ili ziweze kugawanywa, lazima Kikao cha Halmashauri wakae, kama kuna Madiwani 40 walipane posho ya kikao sijui shilingi 30,000 na ile *per diem* sijui shilingi 30,000, kwa hiyo shilingi 60,000 ukizidisha mara 40 sijui zinakuja shilingi milioni ngapi, mnakwenda kugawa shilingi milioni tatu. Pamoja na kwamba, yanaweza kutolewa maelezo kwamba na Wilaya nazo wameziambia zichangie.

Sasa wakipitia njia zote hizo na picha zote na ushauri na nini, hizo shilingi milioni tatu ni hewa na wala hazipo. Sasa kwa nini hiki kifungu hatukifuti, badala yake tunakiweka hapa halafu tunaanza kufanya mambo ambayo hayapo. Ninapendekeza Serikali, itafute utaratibu mwingine wa kuhakikisha kwamba, kama ni vijana mnawasaidia namna gani.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia hii wanayouza vipande vya *Umoja Fund*, hata kama haihusu Wizara hii. Hata hivyo, wanapotangaza wanawatangazia watu wa Mjini, ambako ndiko kuna mabenki ndiyo wanaonunua. Kwa sababu *SACCOS* hazikupewa madaraka hayo na kuna watu wengine kama hawajui, nilikuwa naangalia wakati napitapita pale, wako watu kama Polisi kwa sababu hata kule Polisi kuna vijana. Kuna wengine wako kwenye mapori lakini sijawaona pale hata vijana wengine wako kwenye Jeshi la Kujenga Taifa kule na Jeshi la Wananchi. Sasa wangefanya sensa ni wangapi wanafika pale kununua hivyo vipande, hawapo ni watu tu wamekaa pale mjini, hata kama wengine wanasiliza redio. Lakini hili la kwamba, wanasiliza redio, hakuna mikutano na watu wanakaa kule kwenye Vijiji wala hawaelezani, ni jambo ambalo ni tabu na wanaonunua vile vipande ni wale ambao walionacho wataongezewa. Sasa hata wale ambao hawanacho, angalau na wao wasaidiwe kidogo kidogo, siyo kwamba wanyang'anywe kabisa.

Mheshimiwa Spika, Baraza la kima cha chini cha mshahara katika Sekta za Kilimo na Madini, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameeleza kwamba, wanajaribu kulizungumza suala la kima cha chini cha mshahara na imeelezwa hapa kwamba, waajiriwa katika Serikali, Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi ni asilimia 4.8

ya watu wote wanaofanya kazi za kwao. Lakini kima cha chini cha mshahara ni shilingi 69,000. Nadhani hii tunafanya mzaha kwa sababu Mashirika yote sasa hivi, hasa yale yaliyobinafsishwa, kila mwaka wanatangaza faida, *NSSF* inatangaza faida, ukienda Tanga Sementi wanatangaza faida, kila mahali tu, *TBL* wanatangaza faida. Lakini huyo mfanyakazi yeye ndiyo wanampa mshahara kidogo, hivi hiyo faida wanayotutangazia kwene magazeti halafu huyo mfanyakazi wanampa shilingi 69,000 maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, nadhani ni mzaha, unajua kuna watu wengine kwa sababu ya *nature* ya kazi yao kwamba hawawezi kuandamana, hawawezi kununa, sijui watu wa Redio Tanzania wanapata ngapi, unaona mtu anaamka asubuhi, usiku bado yuko pale mpaka saa sita usiku, watu wote mpaka msinzie. Wale watu wa magazeti sijui tunaishije maana yake kama ukiamka asubuhi, akasema magazeti leo hayapo na Redio zote zimefungwa, nadhani mtu mwingine atakimbia atasema nchi imepinduliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini siamini kama kuna magazeti yale makubwa makubwa yamefilisika. Watakwambia wamepata faida na wanafungua gazeti lingine, kesho kutwa anafungua gazeti lingine, redio zinazaliana kama uyoga, kila mtu anatangaza habari. Lakini ukiwauliza hayo maslahi mnawapa watu kulingana na kazi wanazozifanya na hii ni kwa sababu watumishi katika Idara hizo, hawawezi kuandamana wala kugoma kama walivyogoma Madaktari. Ina maana Madaktari wasingegechachamaa, nadhani mngewapuuza. Lakini kwa nini tusubiri mtu aandamane, wakati anakufanyia kazi ambayo wewe unazalisha na kila siku unatangaza.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ustawi wa Jamii, imeelezwa hapo inaangalia wazee wasiojiweza na walemvavu, wamesema hapa waliotangulia. Lakini hili naamini tunalifanyia mzaha na bahati nzuri, sijui bahati mbaya, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, wao ni walemvavu pia. Lakini pamoja na wao kuwa walemvavu na nina ushahidi bado hatujaweka mkakati wa kuwasaidia walemvavu. Tunazo Tume kama *TACAIDS* pale, sijui Umoja wa Mataifa, Bush wanaleta fedha wanalandika pale.

Sipigi kwa sababu tunawasaidia walioathirika na UKIMWI. Hivi huyu aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu au akapata ajali yeye anapita hapa Dodoma anaomba na akituomba tunakasirika, tunanuna, tunaona anafanya karaha! Hivi hao ni haki yao waendelee kukaa humo mitaani na ni haki ya Serikali inayokusanya kodi za wenzao na nyingine za mjomba wake, isiweke huko. Haiwezi kuwatengea kifungu maalum kama ilivyo *TACAIDS*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii ndiyo inatushangaza, maana yake wako wengi na ushahidi ni hapa Dodoma. Sasa wenyewe mnawaweka wapi au tunasubiri Bush aje atuamshe kwamba, fanya hivi nitawapa fedha halafu na sisi tunafanya. Ina maana watu wengine wafikiri kwa niaba yetu? Naona Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, ananiangalia yeye ni mlemavu, kwa sababu akitoa hiyo miwani yake, haweziz kusoma vizuri kama wale ambao hawana mikono hawawezi kulima na wale ambao hawana miguu hawawezi kutembea, ndiyo maana yangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, wawafikirie hao nao ni watu kama tunavyowafikiria wengine kabisa kwamba, tutawaagizia dawa za kurefusha maisha kwa watu walioathirika, tutafanya semina na wale wasio na mikono na wasioona wako hapa tunawaona, siyo kuwafukuza kwenye mitaa kwamba wao ni kero, tunataka kuwapeleka msituni. Tunawapita kila siku hata hapa Bungeni wanakuja halafu sisi tunachecha tu. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri na ye ye anasema akitoa miwani hawezi kusoma vizuri, nadhani atakubaliana kwamba, *concern* hii tuwasaidie hao na tuwaweke katika sera na lile la vijana walipe umuhimu, kama wao wanaendelea kulichezea, baada ya miaka 10 watakuja kuona tulichokuwa tunakisema ni nini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawapongeza Mawaziri na ninaunga mkono hoja hii na ninaunga mkono kwa sababu ninajua wewe kama unapewa fimbo, sana sana unaweza kupiga nyoka au sungura, lakini fimbo haiwezi kuua simba mpaka wakupe bunduki. Kwa hiyo, hii bajeti ya shilingi bilioni 38, haya tunayoyasema hayawezi kuyafanya.

Kwa hiyo, siwalaumu wao ila mfumo mzima na ndiyo maana tunawaambia na mfumo mzima wasikie kwamba, ili waweze kusambaa na kwenda katika nchi nzima na kufanya *logistics* na kufanya *studies*, kuwashawishi watu na kuwapa maelekezo na elimu, lazima wawe na bajeti ya kutosha, waweke hapo na tukubaliane hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofî*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hii hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa *Alhaj* Profesa Juma Kapuya. Baada ya shukrani hizo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Ndugu Abubakar Rajab, kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nataka nijielekeze katika mambo matatu; Sheria za Kazi, Sera ya Wazee na nitamalizia na masuala ya michezo.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria za Kazi, sitazungumzia sana ila kwa kifupi tu nataka niseme tu kwamba, naendelea kutoa masikitiko yangu kwamba, Sheria ya Fidia au Sheria ya Kiinua Mgongo, nimekuwa nikiipigia kelele toka nimeingia katika Bunge hili na Mheshimiwa Waziri alipoleta marekebisho yale ya sheria nyingine zilizopita, aliahidi kwamba, ile Sheria ya Kiinua Mgongo, ingefanyiwa marekebisho mapema, lakini sasa tunamaliza Bunge sheri hiyo haijaja.

Nasema hiyo ndiyo sheria nyeti kwa sababu inawahusu wafanyakazi wengi na inawaumiza na kwa kweli inatia kichefuchefu. Kama ambavyo nimesema, vipi wanam-compensate mtu aliyekufa kwa shilingi 84,000? Vipi wanam-compensate kwa shilingi 108,000 ambayo ana total incapacitation. Haiwezekani, huo unaweza ukaita ni unyonyaji na dhuluma kwa njia moja. Sasa nilitazamia kwamba, kabla Bunge hili

halijaisha, kwa kweli sheria hii ya fidia ya wafanyakazi, ingekuwa ni moja ya sheria ambayo ilikuwa iletwe na ifanyiwe marekebisho ili Wananchi hawa wanaohusika ambao wanadhirika, waweze kupata haki zao kama inavyostahili. Sasa naendelea kusikitika kwamba, jambo hili halijafanyiwa kazi na Bunge ndio limemalizika, sasa Mheshimiwa Waziri, atatueleza labda ana mkakati gani juu ya hilo?

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie habari ya Sera ya Wazee. Kwanza, nataka niipongeze Serikali kwa kutunga hiyo Sera ya Wazee, ambayo ndani yake kwa kweli ina mambo mazuri sana yanayohusu wazee. Ni bahati mbaya kwamba, sera hii mpaka sasa haijaleweka vizuri kwa wazee na wazee wamekuwa wakipiga kelele juu ya sera hii. Kama wangeelimishwa vizuri, wakaelewa maudhui yaliyomo kwenye sera hii, nina hakika wazee wangeipongeza sana Serikali ya CCM na Wizara inayohusika. Sasa kwanza, niombe jitihada zifanywe na Wizara inayohusika katika kuwaelimisha wazee juu ya sera hii, kwa sababu ndani yake mna mambo mazuri ambayo yanatanzua vilio vya wazee, ambavyo sisi tunaopita huko majimboni, wazee wanauliza mbona Serikali ya CCM imetusahau. Kumbe tayari uko mpango mzuri ambao utawasaidia hawa wazee. Kwa hiyo, nahimiza au nasisitiza elimu itolewe juu ya sera hii.

Katika mambo ambayo ni mazuri mle ndani, ukiacha namna ya kuwatumia wazee katika jamii, liko suala sugu la matibabu kwa wazee na sera inabainisha wazi kwamba, wazee watapata matibabu bure hasa wazee ambao hawana uwezo. Tatizo hapa ni kwamba, haijaleweka utaratibu gani utakaofanyika ili huyo mzee aweze kupata matibabu bure. Bado wazee kule wanahangaika na kwa bahati mbaya, bado wako Madaktari wengine katika hospitali, wanawapuuza na kuwadhalilisha hawa wazee wanapokwenda katika zahanati zetu. Hili ambalo tunasema kwenye sera ambalo linaimbwu siku zote kwamba wazee watapata matibabu bure hawapati matibabu bure. Sasa ningeomba Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa kushirikiana labda na Wizara ya Afya na TAMISEMI, itoe utaratibu unaoeleweka wa kuwawezesha hawa wazee wanaosema watapata matibabu bure ili waweze kuelewa hasa baada ya kujulikana kwamba, mzee ni yule ambaye amefika miaka 60, lakini kwa minajili ya matibabu ni mzee ambaye hana uwezo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile katika sera hii, liko suala la mikopo kwa wazee. Wazee walikuwa wanalamika mbona akinamama wanapata mikopo, mbona vijana wanapata mikopo, ingawa mikopo yenye ni kiduchu, lakini angalau wanapata. Sasa wazee hawa walikuwa hawapati kitu na walikuwa wanalamika sana. Lakini ndani ya Sera ya Wazee, kama sikosei kifungu 3.4, mnawenza mkanisahihisha, inaelezwa mle ndani kwamba, wazee sasa nao watapata mikopo, kwa maana ya kwamba utaundwa Mfuko ambao ni *Revolving Fund* ili wazee hawa waweze kukopa. Sasa niombe basi hiyo itekelezwe. Swali langu ni kwamba, je, katika bajeti hii ambayo sasa tunaizungumzia na tunaipitisha, Mfuko huo tayari umekwisha anza au utaanza katika mwaka huu wa fedha au itabaki ni hadithi tu kwamba kutakuwa na mikopo kwa wazee wakati hamna chochote kinachofanyika?

Ningependa nimwombe Waziri, atakapokuwa anamaliza hoja yake hii, aeleze kama Mfuko huu unaanza lini na kama unaanza katika mwaka huu wa fedha. Lakini pia

utaratibu wa namna ya kumuwezesha huyo mzee aliyepo huko sijui Sepuka, Ihanja, Ikungi, Puma na hata Urambo, atapataje huo mkopo na taratibu zake zikoje. Hiyo nayo ibainishwe ili kuondoa utata ambao unaweza kuwafanya wazee wakose haki yao hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo kwanza, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais au niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa hatua kubwa aliyochukua ya kutujengea au kuhakikisha kwamba, tunapata Kiwanja cha Kimataifa, nampongeza sana juu ya hilo. Kitendo hicho ni kielelezo thabiti kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Tatu, imesikiliza kilio cha Wananchi na imepania katika kudumisha na kuendeleza michezo hapa nchini. Kila mtu amefurahia, wenzangu wamesema sitaki kurudia, mategemeo yangu ni kwamba, Mradi huu utakamilika katika wakati uliopangwa. Wakati ujenzi huu unaendelea, ningeomba hatua za kuwafundisha wataalamu watakaoendesa kiwanja hiki nazo zichukuliwe, ziende sambamba na maandalizi au na ujenzi wa kiwanja. Tusingojee kiwanja kikamilike halafu tutafute wataalam na wataalam wawe ambao wamebobea katika masuala ya kutunza viwanja.

Tuna matatizo ya utunzaji wa vitu vyetu vingi tu, iwe barabara na kadhalika. Sasa naomba na hili katika viwanja nalo lishughulikiwe. Kwa mfano, Meneja ambaye tunamtazamia awe Meneja wetu wa uwanja ule lazima apewe msasa, afundishwe kikweli kikweli na ikiwezekana ajue lugha sizizopungua tatu, ajue Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kwa sababu Mameneja wanaokuja au viongozi wanaokuja, ama wanamichezo wanaokuja, aidha wanazungumza Kiingereza, Kifaransa au Kiarabu. Itakuwa vizuri Meneja tutakayempata au wataalamu tutakaowapata pale, wawe ni wale ambao wanajua lugha hizi kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano kati ya wanamichezo na makundi yao na sisi hapa.

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile kusema kwamba, pamoja na ujenzi wa kiwanja hicho, naomba katika Awamu ya Nne inayokuja, hasa katika *phase* ya kwanza ile ya miaka mitano, waangalie kuboresha viwanja vingine na hasa Uwanja wa Kirumba uwe katika *standard* ya Kimataifa. Kwa sababu uwanja huu peke yake hautoshi, tunahitaji uwanja mwingine ili tupate sifa ya kuandaa mashindano ya Kimataifa makubwa. Sasa wakati uwanja unamalizika, huu ambao umejengwa na tunapata kwa hisani ya Mheshimiwa Mkapa, mipango ianze kwa ajili ya *ku-improve* Uwanja wa Kirumba. Nimesema Uwanja wa Kirumba, kwa sababu kwa kweli una *facilities* nyingi na una kila sababu ya kuwa *improved* ili uweze kuwa uwanja wa pili wa Kimataifa na sasa tuweze kupata sifa ya kuandaa mashindano ya Kimataifa. Inawezekana kazi iliyoko pale sio kubwa sana ukilinganisha na viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, nataka niwapongeze sana wadau wote waliotia *pressure* mpaka uchaguzi wa *TFF* ukafanyika. Tulifika mahali hata Serikali yenyele ilianza kugwaya, haikujulikana kama kweli uchaguzi utafanyika. Lakini *pressure* ambayo ilifanywa na wadau wa mpira, ndio ambayo iliwezesha uchaguzi wa *TFF* kufanyika. Nawapongeza sana wadau wote walioshiriki katika hali hiyo. (*Makofit*)

Nampongeza sana Rais wa *TFF*, Ndugu yangu Tenga, kwa kuukwaa huo Urais, lakini kwa kazi nzuri ambayo anaifanya hadi sasa. Nampongeza yeye na viongozi

wenzake wote kwamba, wanafanya kazi nzuri na kazi inaonekana. Ni matumaini yangu kwamba, watafanya vizuri katika kusimamia mambo mbalimbali. Mapungufu ambayo yanajitokeza hayakosekani, lakini yanadhibitiwa na tena yanadhibitiwa katika wakati wake. Ili *TFF* waweze kufanya kazi vizuri, wanahitaji msaada. Kwa bahati nzuri *TFF* iliyopo sasa, imejitahidi kuhakikisha kwamba, yale mahusiano mabaya yaliyokuwepo kati ya Chama cha Mpira na Serikali, sasa hayapo. Sasa ni wakati mzuri wa Serikali yenyewe nayo kuliona hilo na kuisaida *TFF* kikamilifu.

Kwa mfano, yako madeni ambayo *TFF* wamerithi, makubwa tu ya *CAF*, *CECAFA* na inawezekana hata ya *FIFA*. Madeni ambayo kama wataendelea nayo, yatawapunguzia uwezo wa kufanya kazi zao sawa sawa. Niiombe Serikali, watafute kila aina ya uwezekano wa kuwasaidia *TFF* ili kusudi waondokane na madeni haya ili watekeleze mipango yao ambayo iko mbele yao, lakini vile vile wasaidiwe katika kuhudumia timu zetu. Timu yetu ya *under 20* iko katika mazoezi, mashindano yao yatafanyika Agosti, Serikali iangalie namna ya kuwasaidia. Kuna *Senior Challenge Cup* Desemba, Serikali iangalie namna ya kuwasaidia. Wenzetu Nigeria kule licha ya kwamba, wanapata Dola 250,000 kutoka *FIFA*, Serikali inaongeza kiwango kile mara kumi, yaani 2.5 USD milioni wanapata. Zambia na Zimbabwe wana-finance mashindano yale ya Kimataifa asilimia mia moja. Tufike mahali na sisi Serikali yetu isaidie katika hilo. Kwa kutegemea tu fedha za mlangoni, nakuhakikishieni kabisa kwamba, mambo yetu hayawezi kuwa mazuri na daima tutakuwa nyuma katika mipango yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hili suala la kufuta madeni uko mfano kulikuwa na OFUMA, ambayo ilifanya kazi vizuri, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza, alitoa Kombe la OFUMA na madeni yakafutwa. Nadhani hapo ndio mahali pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo katika Chama cha Ngumi. Yako matatizo ya muda mrefu na malumbano makubwa. Uchaguzi ulifanyika tarehe 22 Juni, 2003 kama nakumbuka, uongozi ule ukawekwa pale na uongozi uliwekwa pale kwa kweli kinyume na Katiba, kwa sababu Katiba inasema wanachama ni Mikoa, lakini waliofanya uchaguzi ni vilabu tena vya Dar es Salaam, hilo ni tatizo. Wakapewa jukumu la kuiandaa Katiba katika kipindi cha miezi sita, sasa ni miaka miwili au mwaka mmoja na nusu hakijafanyika kitu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aliangalie. Kwa sababu msisahau ngumi ndio ilikuwa chama cha kwanza kutuletea medali ya *Olympic* hapa Tanzania. Chama cha kwanza kabisa. Marehemu Titus Simba, ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kutuletea medali hapa. Sasa ni vizuri kukumbuka mambo kama haya na kuwasaidia pale ambapo pana mizozo. Watu hawaelewani, Katibu Mkuu aliyepo nasikia ameenguliwa, hafanyi kazi sawa sawa, *TOC* wanamtambua Katibu Mkuu, Msajili anamtambua Katibu Mkuu na BMT, lakini hafanyi kazi sawa sawa. Kwa hiyo, haya ni baadhi ya matatizo ambayo yanatokea. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aliangalie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri na Serikali waangalie tena muundo wa Wizara hii, hasa katika upande wa michezo. Wizara hii kimichezo iko Makao Makuu Wizarani, chini huku hakuna kitu. Mikoani na Wilayani, nani atakayesimamia suala zima la michezo kuhamasisha vijana na kadhalika. Kwa hiyo, hebu angalia sana muundo. Ukiangalia upande mwingine, unaweza kukuta kwamba,

kuna *duplication* ya kazi kati ya Baraza la Michezo na Idara yetu ya Michezo pale Wizarani. Hebu tuangalie tunaweza tukaona mambo haya hayapo. Baraza la Michezo la Taifa, Mwenyekiti wake anateuliwa na Rais, mtu wa kawaida mwenye uwezo aliyebobea katika michezo, mkoani ni *RAS* au *DAS*. Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, hana ubavu wa kumwelekeza *RAS*, kufanya mambo ambayo yeye kama Waziri, angetaka yafanyike. Hilo ni tatizo. Muundo au *Organisation Structure* katika Taasisi yoyote ile katika falsafa ya Menejimenti ni muhimu katika kufanikisha azma na madhumuni ya Taasisi hiyo. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia kwa sababu huku chini hakuna watu. Ukiongeza na sasa mashuleni wanafunzi hawafanyi mashindano wanachezacheza tu, lakini kama mashindano hakuna kunakuwa na tatizo kubwa namna ya kuibua vipaji vya watoto wetu huko chini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Kazi, Maendeleo na Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze sana Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu wake, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir na watendaji wao, Katibu Mkuu, pamoja na timu yake, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia matatizo ya vijana na baadaye nitamalizia kwa kuzungumzia malengo mbalimbali ya Wizara hii. Tatizo kubwa la vijana ni elimu. Elimu ya Msingi kwa miaka mingi kabla marekebisho hayajafanywa kwamba, sasa elimu hiyo itolewe bure, yamesababisha vijana wengi kukosa elimu na vijana hao sasa wapo, hawana elimu na hawana ajira. Tukienda katika Elimu ya Sekondari, bado kuna matatizo, kabla ya marekebisho ya Serikali kupunguza ada katika Shule za Sekondari, vijana wengi wameshindwa kulipiwa ada na wazazi wao katika Shule za Sekondari na hivyo, kuongeza idadi ya vijana wasiopata elimu, sasa ya Msingi na hata ya Sekondari. Lakini vile vige vijana wengi wamepata matatizo hasa vijana wa kike, kushindwa kumaliza Elimu ya Msingi na ya Sekondari. Kwa sababu hiyo basi, kuendeleza kuongeza idadi kubwa ya vijana ambao hawana elimu. Kwa hiyo, tatizo letu kubwa la vijana kwanza ni kukosa Elimu ya Msingi na Sekondari. Katika Elimu ya Sekondari, hili tatizo pia linaongezeka kwamba, tumekuwa na idadi ndogo ya Shule za Sekondari na kwa hiyo, vijana wengine hata kama watakuwa wamefaulu katika elimu yao ya Msingi, wanakosa nafasi ya kuendelea na Elimu ya Sekondari. Hili ni tatizo la Kitaifa na kwa hiyo, Taifa lina matatizo kwa vijana wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningezungumzia kidogo suala la Sekondari. Pamoja na jitihada ambazo sasa hivi zinafanywa za kuongeza idadi ya Shule za Sekondari ili vijana wetu waweze kupata elimu ya kiwango hicho cha Sekondari, bado kuna matatizo ya vijana ambao wanakosa kabisa hii Elimu ya Sekondari kwa sababu mbalimbali. Wilaya ya Muheza ni moja kati ya Wilaya ambazo zimekuwa na matatizo ya upungufu mkubwa wa Shule za Sekondari. Ili kuboresha kiwango hicho cha Elimu

ya Sekondari kwa vijana wetu, hivi karibuni tumefanya dhifa moja pale Dar es Salaam ya kuchangisha fedha kwa ajili ya kuongeza idadi ya Shule za Sekondari. Kwa nafasi hii ya pekee, naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, kusaidia Wilaya ya Muheza kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa Shule za Sekondari. Katika hafla ile, pamoja na ahadi na fedha zilizopatikana, jumla ya shilingi 245 milioni zilikusanywa. Nampongeza sana. (*Makof*)

Naomba pia kuchukua nafasi hii, kukipongeza Chama cha Maendeleo ya Wilaya Muheza (*Muheza Development Trust Fund*), chini ya uongozi wa Kamishna Adadi Rajabu, kwa kuandaa hafla ile ambayo ilifana sana na kwa kweli matarajio yetu ni kuona kwamba, Muheza inapata *High School* ya kwanza, itakayotokana na kazi kubwa iliyofanywa katika kipindi cha wiki mbili zilizopita. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la vijana linaleta tatizo kubwa la Kitaifa na hili ni tatizo la ajira, kukosa Elimu ya Msingi na Sekondari, lakini kukosa kazi pia kuna tatizo kubwa la ajira. Sasa tatizo hili ndilo linalochangia vile vile kufanya hali ya michezo hapa nchini kushuka, bila ya kupata chakula cha kutosha vijana wanashindwa kushiriki kikamilifu katika mazoezi, hata katika mchezo wa ngumi ukishiriki kama hujashiba vizuri basi ngumi nyepesi ya kidevuni unaanguka chini, *technical knock out*, mchezo umekwisha katika raundi ya kwanza. Kwa hiyo, ajira ni muhimu sana, kuwezesewa vijana kushiriki kikamilifu katika mazoezi. Lakini ajira vile vile itawawezesha vijana kujipatia vifaa vya michezo. Bila uwezo huo basi, vijana wanakuwa wanyonge sana katika kushiriki katika michezo kwa sababu hawapati vifaa. Siku zote vijana wanatafuta wahisani, wafadhili wa kuwanunulia jezi, mpira kila ukipasuka mfadhili, kwa sababu hawana ajira. Sasa ni vizuri tukaangalia na tukaiunga mkono mpango ule unaoitwa *Mini-Tiger Program*, inayoanza Kitaifa. Tuiunge mkono sana kwa sababu ina shabaha ya kuongeza ajira na hii itasaidia sana vijana kupata ajira na kuwa na uwezo wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, ningombwa tufikirie sana uwezekano wa kuongeza bajeti ya Wizara hii. Fungu hili wanalopata haliwatoshelezi kutekeleza yale ambayo tunakusudia kuyatekeleza. Mfano katika Mfuko ule wa mikopo ya vijana, kila Halmashauri inapewa wastani wa shilingi milioni tatu kwa mwaka. Lakini zipo Wilaya zina Kata 35, ukizigawa fedha hizi maana yake ni kwamba, Kata moja itapata angalau shilingi 90,000 tu. Kata yenye vijiji zaidi ya kumi, yenye vikundi zaidi ya 150 shilingi 90,000, kwa vijana unasema umewasaidia, nadhani hatujawasaidia. Kwa hiyo, tuongeze bajeti ili tuweze kuongeza viwango hivi. Viwango hivyo kwa kweli kwa mikopo ya vikundi, tunawadanganya na tunajidanganya, haiwatoshelezi na hatuwasaidii kitu.

Mheshimiwa Spika, ningombwa pia kuzungumzia jambo lingine ambalo hivi karibuni niliwahi kuuliza swali kuhusu majengo ya *Welfares*, ambayo awali yalikuwa yanatumika na wapiganaji wa vita vya dunia. Pamoja na kwamba, Serikali haikuwa na uwezo wa kuyarejesha majengo haya kama tulivyopendekeza kwa wazee, ningombwa basi Wizara hii ifanye mambo yafuatayo: Katika mfumo huo wa Sera ya Wazee, basi tutenye fedha kwa ajili ya kuwakopesha wazee ili nao waweze kufanya miradi yao. La pili, tunaomba Wizara hii sasa ifanye jitihada na hatua za mwisho baada ya marekebisho

ya chama kile cha wazee, basi tufanye mikakati ya kuhakikisha wazee wale wanaendelea kupata posho zao zilizokuwa zimeahidiwa. Sijaona mahali popote jambo hili likizungumziwa, kwa hiyo, nadhani ni wakati muafaka tuwasaidie. Tumewasaidia katika kuwezesha uchaguzi kufanyika katika chama kile, basi tuendelee kufuutilia Serikali ya Uingereza ili fedha zile ziweze kuja na wazee hawa waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimekuwa nikilizungumza kila ninapochangia katika Wizara hii ni maombi niliyoyapeleka Wizarani huko kuhusu Wilaya ya Muheza kupata Chuo cha *VETA*. Shabaha kwa kweli ni kuwa na *VETA* katika kila Wilaya. Umuhimu wa *VETA* katika kila Wilaya upo. Pamoja na kuwepo kwa vyuo vingine vya ufundi katika Wilaya ya Muheza, kwa mfano, lakini stadi zinazotolewa katika vyuo hivyo hazitoshelezi. Chuo pekee ambacho kina stadi nyingi ambazo vijana wengi wanazipenda na wanataka kuzifahamu ni *VETA*. Leo ukienda katika gereji nyingi wanazozia gereji za chini ya miti na kadhalika, utakuta zimeajiri vijana wengi ambao hawalipwi hata mishahara. Wanafanya kazi kwa nia ya kutaka kujifunza kazi za ufundi wa magari. Hii ni elimu inayopatikana *VETA*. Kwa hiyo, kuna kikosi kikubwa au idadi kubwa ya vijana wanaotaka kujua kazi hii lakini hawana mahali pa kujifunza. Gereji hizi za chini ya miti, watafanya kazi kwa zaidi ya miaka minne, mitano, pamoja na kukaa kwa muda mrefu huo hawatapata yeti. Kwa hiyo, si rahisi kutambua uwezo wao wa kifundi walioupara kwa miaka yote mitano wanayofanya kazi katika gereji za chini ya miti. Bado naikumbusha Wizara kwamba, Muheza tunahitaji pia kuwa na Chuo cha Ufundu cha *VETA*.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu, kupongeza jitihada zinazofanywa katika ujenzi wa uwanja mpya wa kisasa. Pamoja na mambo hayo, naomba nikumbushe mambo yafuatayo katika klabu zetu za mpira ni lazima yazingatiwe ili mchezo wa mpira wa miguu pamoja na michezo mingine yote hapa nchini iweze kushamiri: La kwanza ni uongozi bora, uongozi wa upeo wa juu na uongozi bunifu. Hizo ndiyo sifa, ubunifu ni lazima uwepo. Lakini la pili, ni uaminifu katika uongozi, uaminifu katika kuweka kumbukumbu sahihi za mapato na matumizi ya klabu zetu. Hili ni muhimu lazima lizingatiwe. La tatu, ni kuhakikisha kwamba, utaratibu wa kuweka kumbukumbu unaheshimiwa, unazingatiwa na ruhusa inakuwepo ya kufanya ukaguzi katika mahesabu hayo. La nne, ni kwamba, lazima viongozi wakubali na kuheshimu maslahi ya wachezaji wao. Bila kujali maslahi ya wachezaji tutakuwa tunajidanganya tu.

Hivi karibuni tumeona baadhi ya wachezaji kutoka nje ya nchi, wamekuja nchini lakini wametoa kauli na mimi nakubaliana na kauli zao. Wanasema wanakuja Tanzania kama njia ya kupata nafasi ya kwenda kucheza soka Ulaya; maana yake ni nini? Maana yake lazima tutambue kwamba, michezo ni ajira, ili uweze kupata ajira lazima useme wewe umewahi kucheza wapi na wapi. Kwa hiyo, wamecheza Uganda sasa wanataka kucheza Tanzania, baadaye watacheza Zambia, hatimaye watakwenda kucheza Ulaya. Kwa hiyo, hilo lazima tulitambue.

La mwisho, lazima tuhakikishe kwamba, hawa wachezaji wanatimiziwa masharti yao. Tuwajali na tunahakikisha walimu wa michezo katika klabu zetu wanapatikana.

Tukiyazingatia hayo tutakapokamilisha uwanja ule, basi nina uhakika kwamba, tutakuwa na timu nzuri zitakazoweza kutujengea heshima hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba nitoe pongezi kwa Taasisi zifuatazo: Kwanza, *UNICEF*, wamesaidia sana katika kusaidia watoto yatima kupata Elimu ya Sekondari na kuwapatia vifaa lakini vile vile Shirika hili la *AXIOS International*, ambao pia wanafanya kazi nzuri Wilayani Muheza ya kusaidia watoto yatima, wamesaidia ukarabati wa ujenzi wa Hospitali yetu Teule ya Muheza na kwa kweli wanafanya kazi nzuri, wanastahili kupongezwa sana. Yote wanayoyafanya haya yanalenga katika kuboresha ustawi wa vijana wetu. Japokuwa tunasema hao wanaowasomesha ni watoto yatima, lakini hao ndio watoto tunaowategemea, ndio vijana wetu. Tukiwaboresha vijana hawa, basi tutakuwa tunajenga msingi mzuri wa Taifa la kesho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie kukushukuru sana na kuwashukuru sana viongozi hawa. Ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie kwenye hiyo hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kuipongeza sana hii Wizara ambayo kwa upande wangu, naona shughuli wanazoshughulika nazo na hasa za vijana ni nyeti. Kimeru tunaamini kwamba, ng'ombe wasio na watoto hawana uendelevu na hawana maisha. Vile vile katika jamii vijana wao ndio kama tunavyosema kwenye vigezo vingine kwamba, ndio mgongo wa Taifa, nisingewaita mgongo ndio Taifa. Kama sensa inavyoonesha kwamba, asilimia karibu 60 ya Taifa la Tanzania ni kati ya miaka 15 mpaka 30, kwa hiyo, kwa kweli hao ndio Taifa la Tanzania. Hii Wizara ndiyo ambayo inatunza na kuendeleza hilo Taifa.

Nashirikiana na wenzangu kwamba, nani pia kama wao siridhiki na jinsi ambavyo tunaonesha uzito wa hii Wizara katika bajeti ambayo tunaigawia ya shilingi bilioni 10 na ukitazama ile Programu Namba 50, gawio linalotolewa pale ni shilingi bilioni 1.1 na ambayo karibu nusu yake inakwenda kwenye *subsection* moja tu, na nadhani watazidi kutuelekeza tutakapofikia mahali hapo.

Mheshimiwa Spika, inaenda kwenye *other goods and services, not classified above* ambayo ni karibu milioni 405, ambayo ni karibu nusu ya bajeti nzima ya programu hiyo ya *youth development*. Ukitazama hii *population* tunayoizungumzai na unyeti wake na Ilani ya Chama ya Vijana, kwa kweli naona hapa kuna haja ya kulifikiria zaidi na ombi langu ni kwamba kuna haja ya *ku-strategize* zaidi katika hii sekta ya vijana.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetumwa na wananchi wa Jimbo langu la Arumeru Mashariki miaka miwili na ushehe iliyopita. Tulipata ajali ya vijana wetu 11 kwenye ajali ya trekta, walikuwa wanakwenda kwenye mchezo wa soka. Wamenituma nitoe shukrani ambazo Wizara hii ilionyesha kwa jinsi ambavyo walishiriki katika hilo suala la maafa yaliyotupata Arumeru Mashariki. Iilitokea kijiji cha Sakila, Kata ya Kikatiti. Uzito walilolipa katika ushiriki huo tunamshukuru mno Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya,

ye ye mwenyewe alifika binafsi, salaam zake zimetumwa, kumpa shukrani hizo za wana Arumeru Mashariki na katika ushiriki huo kuna ahadi ambazo zilitolewa na Wizara pamoja na vyombo vyake na tuna imani kwamba ahadi hizo zilifanyiwa kazi na huenda hizo ahadi nyingine zimeshatekelezwa kwa viwango ambavyo huenda mimi sijapata taarifa yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hizo ambazo zimeshatekelezwa tunashukuru na ambazo huenda hazijatekelezwa tungeomba zitolewe kauli ya matumaini kama kuna uwezekano, maana wangependa wasikie, je, kuna matumaini bado ya kusuburi? Tungependa tusikie kutoka kwa wahusika ili walengwa wazidi kuendelea kuwa na matumaini kama bado hayajatekelezwa. Kama yameshatekelezwa tunatoa shukrani zetu za dhati sana kwa juhudhi hizo ambazo zimefanyika.

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu masuala ambayo ni ya hili Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). *Technically* Shirika la *NSSF* ni shirika la kifedha, mimi nalionia lile kama Taasisi ya Fedha. Kuna kuwepo na mchanganyiko au mkanganyiko kati ya kuifikiria kwanza, je, ni Taasisi ya Fedha na kwa hiyo, iwe chini ya vyombo vyaa fedha na kwa hiyo, iwe chini ya *Financial Institution Act* au iendelee kuwa chini ya Wizara ya Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, watu wengi tunakuwa na mawazo kwamba huenda kuna haja ya kuifikiria zaidi. Je, kama *PPF* ingekuwa vizuri zaidi ikafanywa kama ilivyo kwamba ni Taasisi ya Kifedha na shughuli zake ni za kifedha kikweli kweli. Kwa hiyo, ikasimamiwa kama Taasisi ya Fedha na ikawa utendaji wake unasimamiwa na vyombo husika vyaa Taasisi za Fedha chini ya *Financial Institution Act*.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba kuna taratibu ambazo zinafanyika huenda za kisheria, lakini hazijafanyika bado, lakini hilo Wizara nyie mnaonaje? Ingekuwa vizuri tukafahamu kwamba nyie mnalionaje hili.

Pili, ni kuhusu fedha ambazo *NSSF* inakusanya kutoka kwa waajiri pamoja na wafanyakazi, ni fedha nyingi si kidogo. Kama ambavyo inatolewa kwenye kitabu cha hotuba kwa mwaka huu wa fedha wa 2004/2005 imekusanya bilioni 24.5, na imegawa karibu robo ya hiyo fedha kwa wajumbe wake. Sasa hiyo si hela kidogo kwenye nchi ya hali ya kwetu. Hizo si fedha kidogo nadhani na ingekuwaje kama kwa mfano ingefanya utaratibu ili wanachama wake wakaweza kufaidi hizo fedha kwa njia moja au nyingine, kuzifaidi kwa kuzitumia kwa njia ya maendeleo yao. Kwa sasa hivi kuna vijana jinsi ambavyo mgao unaopatikana kupitia mfuko ambaa unatumwa kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya vijana kukopa.

Lakini je, hizi zao zenyewe ni zao? Wamepeleka kwenye *NSSF* wanazingojea mpaka waje kuzipata wakati wanastaafu wazipate kwa njia moja au nyingine, lakini kuna utaratibu kwa mfano kama wanavyofanya *PPF*. *PPF* wanatumia Benki ambayo sitaitaja jina lakini wao wana-channel fedha zao kupitia Benki ya Biashara ambayo ile Benki mtu yoyote anayehitaji zile fedha kwa njia ya kuzitumia kwa shughuli ya maendeleo anakwenda kule lakini anapata zile fedha kwa njia taratibu za kibiashara anawenza

akazipata zile fadha zikamsaidia kwenye shughuli za kibashara bila kwenda moja kwa moja kwenye ule mfuko wa *PPF* kwa mfano.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* wanaweza wakafanya kitu kama cha aina hiyo kwa mfano sio lazima wao wenye maana yake kuziweka hela za wananchi kwenye shughuli ambazo zitafanya iwe *risk* sana kwa ajili ya wananchi wao waje kukosa fedha zao itakuwa matatizo zaidi hiyo inaeleweka. Lakini inawezekana sana kwamba wanaweza wakahakikisha kwamba wananchi wenye waneza wanaweza wakafaidi zile fedha kwa jaili ya maendeleo yao na hasa vijana.

Mheshimiwa Spika, kingine kinahusu suala la utamaduni, labda ni kukuza hii dhana ya maendeleo ya vijana. Je, maendeleo ya vijana kama waliotangulia wanavyozungumza kwa kweli ni pana na ninaimani kwamba linahitajika kuwa ni pana zaidi kuliko ambavyo labda linatumika sasa hivi. Wizara ninaimani kwamba wanalionna hivyo lakini kiutendaji mimi ninavyoona ni kwamba linatumika kwa ufinyu zaidi. Kwa *VETA* wanaofaidi kwenye mafunzo ya kupanua *development skills*, ni wale ambao wanakuwa bahati nzuri wao wamepata bahati ya kupata elimu ya msingi au nyingine.

Kuna ambao labda hawana njia ya kuweza kupata bahati kama hiyo, wengine ambao tuko kule vijijini tunaona hii hali lakini hakuna njia ya kuweza kuhakikisha kwamba wao wanaweza wakafaidi fursa kama hizi ambazo zinaweza zinaweza zikapatikana kuititia Wizarani, lakini wao hawana njia ya kufikiwa.

Je, Wizara ina mpango gani kuhusu hawa ambao maendeleo yao yanahitaji kwa kweli yaanzie kwenye misingi ambayo si *tradition* kama ambavyo tumezoea? Kuna mikakati yoyote ya kuweza kupenyeza kwenye maeneo ambayo labda hatukuyazoea na ambayo si *traditional* kama ambavyo tumezoea?

Mheshimiwa Spika, mimi nawaunga sana mkono Waheshimiwa viongozi wa hii Wizara, wanafanya kazi nzuri na kwenye eneo ambalo ni nyeti. Hii Wizara ndiyo pekee, ni kati ya Wazara nyeti ambazo kwa kweli zinaweza zikatuokoa kwenye tatizo ambalo ni *potentially time bomb* la matatizo ya vijana ambao tuko nao na kama sasa hivi ahadi ambazo wanazingojea.

Mheshimiwa Spika naunga hoja na nawatakia utekelezaji mzuri na naomba nitumie fursa hii kuwatangazia Waheshimiwa wapigakura wangu wa Arumeru Mashariki kwamba nami nipo nao, nawashukuru kwa kipindi hiki cha miaka mitano na ninaimani wanansubiri waniambie nirudi tena.

Mheshimiwa Spika na ndugu zangu, nawatakia kheri sana. Ahsanteni sana. (*Makofit*)

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kupata nafasi hii ili na mimi niungane na wenzangu katika kuchangia bajeti ya Wizara iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nataka nitoe pongezi kubwa kwa Waziri, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Wataalam wake kwa jinsi wanavyofanya kazi zao nzuri kushughulikia

migogoro kila mara ya mipira, na mpaka nchi inakuwa na amani ni kutokana na jitihada zao za ushirikiano. Kwa hiyo, naendelea kuwapongeza na kwamba si katika hilo tu bado kuna mambo mengi ambayo wanapaswa kuingia na kuzamia katika utekelezaji wake ili kuwaokoa hawa vijana wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani pia kwako Spika, Mheshimiwa Pius Msekwa, kwa jinsi unavyojitahidi kutuelekeza kazi mbalimbali humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nakutakia kila la kheri, afya njema na kazi njema na kila mara Mungu akujalie uwe mstari wa mbele katika utekelezaji wako. (*Makofi*)

Natoa pongezi pia kwa Katibu wetu mgeni, Ndugu Damian Foka, kwa jinsi anavyojitahidi kufanya kazi na kuwa msikivu kwa sababu mimi mwenyewe nimekuwa na matatizo lakini amenisikiliza mpaka ameyatatua. Pamoja na Wakuu wa Idara na watendaji wote na Makatibu wetu hawa walioko mbele na wengine ambao zamu yao itakuwa baadaye, nawapongeza na nawatakia kila la heri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inawezekana sitapata nafasi ya kusimama tena ukiangalia muda wenyewe wa Bunge ndiyo unakwenda, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi wa ndani ya CCM Mkoa wakiwemo na Makatibu wa Wilaya na Makatibu Watendaji, kwa jinsi wanavyofanya kazi vizuri na kutetea sera za CCM kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Isdori Shirima, jinsi anavyotekeleza sera ya CCM. Nataka nthibitishe katika Bunge hili kwamba sisi Mkoa wa Mtwara kwa sasa hivi tunaye *RC* ambaye ni kada ambaye yuko mstari wa mbele kutekeleza Ilani ya CCM na akiungana na Watendaji wake, Ma-*DC* kila Wilaya, Makatibu Kata na hata viongozi wa Vijiji wamekuwa wakishirikiana kwa sababu mambo mengi ambayo tumefanikisha tusingewenza kufanikisha kama si ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia viongozi wa Halmashauri za Wilaya zote tano za Mkoa wa Mtwara za Newala, Masasi, Mtwara Vijijini, Mtwara Mjini na Tandahimba. Kwa ujumla hawa wote niliowapa pongezi, wamekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na mimi. Shughuli za Ubunge ni ngumu, tunapokuwa kwenye ziara tunakuwa na matatizo mengi, lakini wamekuwa wakisaidia yale ambayo yalioko ndani ya uwezo wao.

Kwa hiyo, ninayo kila sababu ya kuwashukuru na kuwatakia kila la kheri na kwamba waendelee na moyo wao hata wengine watakao kuja kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wanawake wa Mkoa wa Mtwara, wamenisaidia sana kazi zangu, wamekuwa wavumilivu na wakati wote kwenye ziara wameweza kutoa huduma, chakula, kuhudhuria vikao na kuwa wasikivu katika yale ambayo nilikuwa ninayatoa. Kwa hiyo, mimi ninawashukuru na ninawapongeza pia na moyo wao uendelee.

Mheshimiwa Spika, mbele yetu sasa tuna uchaguzi wa kura za maoni za Wabunge, natoa wito kwa wajumbe wote katika Wilaya zote ndani ya Mkoa wangu kutoka Mtwara Mjini, Mtwara Vijijini, Tandahimba, Masasi na Newala, viongozi akinamama wajitokeze siku hiyo kwenda kupiga kura kwa sababu kupiga kura ni haki yao na kuchagua viongozi. Wachague viongozi bora, wasichague bora viongozi.

Mheshimiwa Spika, nipongeze Wizara kwa maana nataka nitoe mchango kwa ujumla lakini kwa haraka haraka upande wa walemovu na wazee, dira inasema wanataka kushughulikia shughuli zao. Mimi nashauri kwamba kama tutakuwa tunafumba macho, tukaendelea kuimba wimbo tu kwamba Serikali itakuwa tayari kuwasaidia walemovu bila kuchukua hatua, bado hatujatenda haki.

Mheshimiwa Spika, wazee wametoka mbali, wamefanya kazi nyingi katika nchi hii, lakini makabrasha yanawazungumza sana kwamba tutawalinda wazee, tutawasikiliza wazee, mimi nataka niseme kwamba bado hatujajikita katika utendaji kuona jinsi gani hawa wazee tunawasaidia kuona mipango yao inakaa vizuri. Mimi ninao wazee waliostaafu wako wengi tu japokuwa hapa tunapokea majibu kwamba sasa hivi wastaafu wote wanalipwa, mimi nataka niseme hivi wako wazee walio wengi bado hawajalipwa maslahi yao. Sasa hiyo ni moja ya sehemu ya kazi hii kuwaangalia wazee pamoja na kwamba kuna Kanuni, Katiba, Dira, twende sasa moja kwa moja kumwangalia huyo mzee, je, mahitaji yake anayapata kulingana na wakati au tumekaa tu tunatarajia kuweka malengo ya matarajio? Bado mimi nasema kwamba twende tuone tunawasaidiaje.

Mheshimiwa Spika, wazee sasa wameitika wito wa Serikali kuungana kwa pamoja kuunda vikundi vyao, wanatoa mafunzo ya UKIMWI, wanawashawishi vijana wafanye kazi za kilimo. Hayo mambo yako ndani ya Mkoa wangu, lakini wanapokuja pengine kutafuta mahitaji, kutafuta mikopo, miradi mbalimbali, wamekuwa wakikwama. Sasa sijui ni kwa sababu Idara hii ina kazi nyingi, lakini kwa sababu leo tunazungumza, Serikali basi ione jinsi gani inajikita kuona mipango hii inakwenda sambamba na mahitaji yale ambayo tunakusudia kuwasaidia Wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kutoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Awamu ya Batu kwa utekelezaji wake wa Maazimio au na ahadi ambayo Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa aliitoa kwa ujenzi wa Uwanja wa mpira Dar es Salaam amba makandarasi wake ni wa kutoka China. Mimi naomba Wizara hii pamoja na kumpongeza Waziri alikwenda kuwaona vijana wetu waliofanya mgomo. Bado wasicheze mbali, waendelee kukaa na vijana wetu na wale makandarasi ili wafanye kazi zao kwa uhakika na ule Uwanja uishe kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, wachezaji walio wengi wa mpira, historia imejiandika walitoka Mikoa ya Kusini na Mikoa hiyo ni Mtwara yenewe, Lindi, Ruvuma na hao ndiyo walioliwezesha Taifa hili kujulikana. Lakini hao hao ndiyo wanaokuwa na mazingira magumu. Sasa basi, naiombia Serikali iweke historia, Uwanja wa Dar es salaam ukiisha, sasa wakajenge Mtwara Uwanja mwagine na Uwanja huo mimi napendekeza hapa nikiwepo Bungeni, sitakuwepo lakini kwa sababu itaandikwa

kwenye *Hansard* ukaitwe jina la Mheshimiwa Rais wetu aliyeko madarakani sasa hivi; Benjamin William Mkapa. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hilo nadhani mmelisikia na naomba likae kama lilivyo kwa sababu hiyo hiyo kwamba historia ilijiandika na tunayo kila sababu, kwa nini bado wachezaji watoke Mtwara, Kanda ya Kusini wakastawishe Taifa, sio kweli Taifa lenyewe Dar es Salaam, Dar es Salaam. Twende tukawajengee Uwanja wao Kusini ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, leo vijana walio wengi wanacheza mpira, hata vijana wadogo utakuta wanacheza mpira, lakini wanacheza maeneo ambayo hayana uhakika. Tumezungumza humu ndani ya Bunge mpaka sasa tunamaliza miaka mitano, kwamba vijana watengewe maeneo ya kucheza mpira. Lakini ukienda kwenye miji mikubwa utakuta wanacheza mahali pamevana, hapo hapo pamerundikana magari, pana vichuma vya kuweza kujiuimiza na tangu tuliongea kwamba wapewe viwanja, mimi nimeona bado viwanja vile vinazidi kupotea, vinazidi kuchukuliwa na watu. Hivi ni kweli tunafanya nini? Kwa nini sasa tusione viwanja vya vijana wanaocheza vizuri na kuwasaidia watoto wapate viwanja vizuri, nadhifu wacheze mpira kwa sababu hao vijana ndiyo wanaotakiwa waende Taifani. Sasa kama hatuwasaidii kutoka vijijini watafikaje Taifani? Ingawa leo hiyo itikadi ndiyo inakufa, wanachukuliwa walioko huku Dar es Salaam, wale wa vijijini mtawachukua lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vijana hawa ambao sasa hivi wanatuletea heshima, wanacheza mpira mpaka wa Kitaifa, ukiangalia kule vijijini wanakotoka, niungane na wenzangu na mimi nina mifano hai, wanacheza bila viatu, wanacheza hawana jezi. Lakini Miji mikubwa ya nchi hii sina sababu ya kuitaja wote tunajua, wahisani wamerundikana wanatoa zawadi kwenye Miji mikubwa. Jezi wanatoa kwenye Miji mikubwa, viatu, huduma na kadhalika. Sasa kama Serikali haikutoa maelekezo kwamba ninyi wahisani sasa geuka angalia vijijini au geuza sasa nenda Mikoani Kusini mkatoe huduma ya kuwapa vifaa, atatoa nani?

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, ninapotembea kwenye maeneo ya Jimbo lile katika kila Wilaya kwa taarifa ya kikao hiki, vijana ndiyo wanasukuma gari. Wako tayari kusukuma gari ninayokaa mimi hata kilometra mbili hata nawaonea huruma. Lakini nataka tujiulize, kwa nini wanasukuma gari, wanasukuma gari kwa matumaini kwamba Mheshimiwa Mbunge atatusfadhilli, sasa mimi nitawafadhili nini?

Mheshimiwa Spika, nitatoa kitu gani kuwasaidia wale vijana? Matokeo yake tunazungumza lugha tu kwamba vijana hoyee! Vijana safi! Sina kitu cha kufadhili, lakini anayeweza kufadhili ni Serikali. Serikali iingie, ijikite iwasaki die wale vijana. Leo hapa tunalamika na mimi nataka nilalamike kuiambia Serikali kwamba Idara hii iongezewe fungu la fedha ili wafanye kazi zao vizuri. Lakini je, nitakapo sema waongeze ili wafanye kazi, wanafanya kazi gani? Timu hii inakwenda vijijini, mbona mimi sijaiona Mkoani kwangu? Kama basi inashindwa kazi nyingi, basi nipewe mimi fungu hilo! (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, fungu litakaloongezwa leo kama wao hawawezi, wanipe mimi niende nikawagawie vijana wangu kule vijijini. Vijana hawana miradi, Serikali inatoa maelekezo na mimi nakubali, naiafiki, siwezi kukataa kwamba vijana wetu wategeme Halmashauri, lakini Halmashauri ina uwezo? Halmashauri haina uwezo. Mimi ninayezungumza natoka huko iliko Halmashauri. Halmashauri haiwezi kwenda kuangalia kila sekta, kila sekta ikawa na uwezo. Uwezo uko Serikali yetu Kuu, isijitoe kuwalea vijana. Vijana ndiyo walio wengi, vijana ndiyo walioko vijijini. Kwa hiyo, ninarudia, inawezekana bado sijasikika, ninasema hivi, baada ya hapo kuongeza fungu ambalo tunaomba kwa sababu eti mna kazi nyingi hamuwezi kwenda hasa Mikoa ya Kusini, Mtwara, basi nikabidhiwe mimi fungu na nitatembea kuwagawia vijana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi sijui kama ninaeleweka hapa nikiongea! Kwa sababu suala la vijana kuwasaidia imekuwa kama ni wimbo wa Taifa. Tutaimba wimbo mpaka lini, twende kwenye vitendo. Vijana hawa hawa ndiyo wanawekea Pato la Taifa kupitia miradi yao, uzalishaji kupitia kilimo, uzalishaji kupitia viwanda vidogo vidogo na ndiyo tunaandikia taarifa humu, uzalishaji uko jinsi kadhaa, asilimia kadhaa lakini mimi ninachosema wanaishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, katika sera hii ya CCM iliyopo, wameitika wito wa kilimo na kufanya hizo biashara ndogo ndogo. Lakini sisi tunaoczunguka kwenda kuwaona, bado wana matatizo na wakiishazalisha hawana masoko. Vitu wamekaa navyo tu hawana masoko. Sasa hili nadhani ni moja kwa moja kwamba Wizara ione hilo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *SIDO* inafanyakazi nzuri, lakini *SIDO* bado isaidiwe. Kule nyuma baada ya Uhuru kila Wilaya au Mkao, walijenga majengo mazuri ambayo vijana wetu walikuwa wanakwenda kujifunza shughuli tofauti tofauti. Sasa majengo hayo hayafanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda haraka haraka, muda umenikimbia. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge ndiyo tunafikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha kikao cha leo. Kwa hiyo, kama kawaida tutaendelea na mjadala wa jumla mpaka saa 11.30. Kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00.

(*Saa 6.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kama ilivyowasilishwa hapa asubuhi.

Awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na watumishi wake ndani ya Wizara hii kwa kazi nzuri ya kusimamia shughuli za michezo pamoja na shughuli nzima ya mambo ya kazi. Wanajitahidi japo tunajua tatizo la msingi kwa kweli ambalo hivi sasa linaikabili nchi nyingi zinazoendelea na hasa tukizingatia mchakato mzima wa mabadiliko ya kiuchumi ni tatizo la ajira. Tatizo la ajira ni sugu kwa Mataifa mengi na halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Ukiacha jinsi linavyotukabili katika nchi yetu, naamini ni pamoja na Mataifa mengine yanayoendelea, japo naamini dawa itategemea ni *approach* ipi ambayo inatumiwa na hasa *Decision Makers* katika kupanga *policy*, katika kupanga mikakati ya ndani na ile inayoweza kuathiri kutoka nje naamini ndiyo inaweza ikawa *solution*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huo, naamini hata ambao wanazungumza lugha ya haraka haraka kwa misingi kwamba ajira hakuna matatizo watashughulika nayo, naweza kusema labda hayo tuyachukulie kama ni maneno ya kisiasa na ni maneno ya kujitafutia kura, lakini kimsingi tatizo la ajira si la kumalizwa na mtu mmoja, bali ni mchakato wa watu mbalimbali na sekta mbalimbali na kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri njia mbili za kuweza kukabiliana na tatizo la ajira. Mojawapo, ningeomba Serikali yetu, Taasisi mbalimbali na vyombo vingine ambavyo viko chini ya Serikali na mamlaka tofauti tungejitetahidi kwanza kuheshimu *initiative* au ubunifu wa watu binafsi. Serikali iheshimu *initiatives* za watu binafsi, isizione kama ni vitu vya kupigwa vita au ni vitu ambavyo vinapaswa kuwa ni ugomvi kati yao na Serikali. Badala yake, Serikali kwa kushirikiana na watu wanaokuwa wamebuni vyanzo mbalimbali vya ajira wakae pamoja au Serikali isaidiane nao kuboresha au kuweka katika taratibu nzuri, naamini hiyo inaweza ikawa vile vile chanzo kizuri cha kukabiliana na tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mmoja unaojirudia tangu huko nyuma, lakini angalau hivi sasa umekwenda unatatuliwa japo bado una matatizo. Inapotokea kwa mfano, kijana wa pale Bukoba Mjini akajitahidi kujiajiri, akaachana na suala la kufikiria kuiba, akaona yeeye kwa nguvu zake kama mtaji wake akaamua kwamba anaanza kujipatia kipato kwa kuendesha baiskeli, naamini kwamba kwa ubunifu wake huo, kwa mawazo yake hayo ya kutaka kufanya usafiri wa baiskeli kwa kusafirisha abiria uwe chanzo cha kupata kipato chake, badala ya Serikali kumuona huyu ni adui, huyu hafai, huyu hapaswi kuendesha shughuli hiyo pale mjini, ninaamini kazi ya Serikali ni kuichukua *initiative* hiyo kama *challenge* kwamba inawezaje suala la biashara ya baiskeli ikawa ajira, lakini lisiathiri taratibu nyingine au sekta nyingine zilizoko pale au mahali pale ambako shughuli hiyo inataka kuanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kijana atatoka kijijini kama Izimbya huko Bukoba Vijiji au Muleba huko, hajui Sheria za Usalama Barabarani, hajui barabara kwamba hii ni *one way*, hajui *round about* inapaswa kutumikaje, vibao vya barabarani vinatumikaje, nafikiri jambo la awali ni Serikali kumwekea utaratibu kwamba kabla hujaanzisha biashara hiyo ni vizuri akapita mafunzo katika Taasisi fulani na hiyo Taasisi ikathibitisha kwamba sheria angalau za jumla jumla ameweza kuzifahamu na kisha

amehitimu vizuri na anaweza akaanzisha shughuli hiyo kwa kupata mapato yake, lakini vile vile na masuala ya usalama yanakuwa yameangaliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali inapotoka huko kichwa kichwa ikamuona huyu bwana ni adui, badala ya kumsaidia au kumpa maelekezo au kuweka taratibu za kuboresha kazi hiyo ukaja unampiga, unamnyang'anya hata hiyo baiskeli labda ambayo ameingia nayo mjini kama mtaji wake, nafikiri kwa namna hiyo tunakuwa tunatengeneza uadui kati ya Serikali na wale watu wanaokuwa wanabuni namna ya kuanzisha ajira wao binafsi au inapotokea kijana akaanza mradi wa kuosha magari, tunajua kuosha magari holela holela kunachafua mji, lakini siyo sahihi moja kwa moja ukaenda kumzuia au unamfukuza au unam-*arrest* badala ya kumwekea utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri yakatengwa maeneo yanayotambuliwa na mamlaka husika kwa ajili ya kuoshea magari ili yule anayetaka kuosha magari akapata ajira, lakini vile vile na taratibu zinazolinda miji yetu, zinazolinda masuala ya mazingira zikawa zimefuatwa. Kwa hiyo, narudia tena kwamba *challenge* mojawapo ambayo naomba Serikali ichukue ni kwamba badala ya hizi *initiatives* za vijana wetu wanazoanza nazo kuziona kama zinapingana na taratibu zetu na tukazona ni za kiuadui, nafikiri tungekuwa tunazikaribisha na tunaanza nazo kama *challenge* za kutafuta namna ya kuziboresha, naamini pande zote mbili zitanufaika na itakuwa sehemu mojawapo ya kutafuta ajira kwa ajili ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini njia nyingine pia ni kwamba, hili suala la ajira, suala la kazi, niliwhi kusema hapa kwamba si vyema kuliacha mikononi mwa Wizara moja kuona kama inaweza kupata *solution* katika kulitatua. Suala la ajira ni suala linalogusa sekta zote, Wizara zote kama jinsi ambavyo lilifanywa suala la UKIMWI kwamba kila Wizara, kila Taasisi imeelekezwa hatua za kuchukua ili kukabiliana na suala la UKIMWI.

Pamoja na hilo, naona hata suala la ajira kwa vijana wetu au ajira kwa wananchi wetu ni suala linalopaswa kugusa kila Taasisi, kila Wizara, kila Sekta kuweza kukabiliana nalo. Ni pale ambapo itakuwa wadau wote wameshirikishwa katika kulijadili, kujaribu kufanya brainstorming, kujaribu kushirikishana katika *ku-create* vyanzo vya ajira, naamini inaweza ikasaidia kutatua suala la ajira.

Mheshimiwa Spika, suala hili nalizungumza katika msingi mmojawapo kwamba, kwa kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, Serikali inaweza ikatoa *directives* kwamba kila mtu anayeanzisha hoteli kwa *grades* mbalimbali, mpaka hata Mama Ntilie akapewa *grade*. Anaweza akaelekezwa kwamba kila *grade* wewe unapaswa kumwajiri mtu labda ambaye amechukua mafunzo ya *hotel management* na iwe ni lazima kabla hajapewa leseni. Matokeo yake ni kwamba kila mwenye hoteli itamlazimu kupata kijana ambaye amepitia katika mafunzo hata japo ya mwezi mmoja au miwili ya kujuu namna ya kutoa huduma katika hoteli yenye *grade* fulani au kimgahawa chenye *grade* fulani.

Mheshimiwa Spika, kupitia Wizara ya Ujenzi, Serikali ikiweka mkakati na maelekezo na utaratibu wa kuwalazimisha *contractors* wote kwa *grades* mbalimbali za madaraja yao ya ukandarasi, naamini wanaweza wakaelekeza na wakaweza kupangiwa

taratibu za kuwaajiri vijana wanaomaliza mafunzo kupitia kwenye vyuo mbalimbali badala ya kuwaachia holela holela watu wakaajiri hata mjomba kwa misingi kwamba anajua tu kujenga au ana idea ya kujenga akawa ndiyo fundi wake. Ninaamini kwa njia hiyo hata vijana wetu ambao wanamaliza mafunzo wanawenza wakapata ajira bila wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwa ndugu zetu wa *TFF* na hasa uongozi mpya ambao umechukua nafasi hivi majuzi. Kwa kweli nizungumze kwamba, ni watu ambao wameanza kwa mwamko mpya na kwa mwelekeo mpya wa kuweza kutatua suala la michezo. Lakini kama ambavyo wameanza kutafuta maoni, kuweka mikakati ya kuweza kurekebisha Katiba yetu ya Chama cha Mpira, naamini inaweza ikawa ni mojawapo ya *solution* ya matatizo ambayo yamekuwa ni ya muda mrefu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Katiba mpya ambayo imeshirikisha watu mbalimbali kutoa michango yao nafikiri ni mwelekeo mzuri, mwelekeo ambao umekuwa unapiganiwa na watu wengi na ninaamini kwa mwendo huo wanakwenda vizuri kabisa na tunawapongeza. Ndiyo maana sisi kuanzia mwanzo hata wakati wameanza mikakati ya kuilea ile *Serengeti Boys*, japo mambo yalikuja yakaenda vibaya vibaya ndiyo maana tuliwaunga mkono moja kwa moja kwa kutoa michango mbalimbali kutoka kwenye vyama vyetu katika *ku-support initiative* walizonazo katika kuendeleza mpira wa miguu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjaminn Mkapa kwa kuweka *record*, kwanza ya kumaliza akiwa na *initiative* ya kujenga uwanja mpya na wa kisasa katika nchi yetu. Ni mwanzo mzuri, ameonyesha mfano na naamini hata tutakapochukua Serikali sisi mwezi Novemba, 2005 ni *challenge* nzuri. Yeye ameweza katika miaka kumi kujenga kiwanja kimoja, sisi tunaamini kila Mkoa utakuwa na kiwanja cha namna hiyo. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze kwa kauli yake ya juzi akiwa Zanzibar ambapo ametamka bayana kwamba: "Hakuna chama chochote chenye hatimiliki ya kuitawala nchi hii." Kwa kweli maneno yale yalikuwa na uzito wa kipekee na ninafikiri yametoa somo kwa watu wengi ambao walikuwa wanafikiri wamebeba hatimiliki ya kuendelea kutawala nchi hii milele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika kumalizia, kwa kuwa huenda itakuwa ni nafasi yangu ya mwisho ya kuchangia, sitegemei kuomba tena, kwa kweli mimi binafsi napenda nikupongeze sana. Nimekuwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni ambaye nilimpokea ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, umenipa ushirikiano mzuri. Mahali pengine watu wengi walikuwa wanana laumu labda kwa lugha au kwa mawasilisho ambayo yanabeba dhana kali kali, lakini nasema ndiyo kibarua changu nilichokabidhiwa kukalia kitie hiki, si makosa yangu na ninafikiri hata kulipwa kama Kiongozi wa Upinzani Bungeni ninalipwa kwa sababu ya kuyazungumza hayo niliyokuwa nayazungumza na kuyatetea yanayonipa kibarua. Kwa hiyo, nawaombeni wale ambao walikuwa wanajisikia vibaya vibaya au wanafikiri labda lugha kali..."

**MBUNGE FULANI:** Wakusamehe.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Hakuna haja ya kusameheana, ndio kazi zenyewe na hata mwingine yeote ambaye anaweza akabeba shughuli hiyo naamini ataendeleza yale ambayo niliweza kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, pia, kwa kweli niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano mzuri sana walionipa. Kambi ya Upinzani ina Wabunge kutoka vyama vinne, lakini jinsi ambavyo tumeendesha shughuli hii naamini wengi wangefikiri tunatoka katika chama kimoja. Lakini hiyo yote ni njia ambayo ilikuwa inapatikana kutokana na ushirikiano ambao kila mmoja alikuwa ananipa, kuheshimiana. Naamini wengi wanazidhi umri, lakini nilipokuwa nazungumza kama Waziri Mkuu Kivuli ninayeongoza, walikuwa wananiha heshima hiyo na ndio siri ya mafanikio yetu mpaka tukavusha kambi yetu mpaka mwisho wa Bunge hili. Nashukuru hayo yote nimeyafanya, si kwamba nimepita chuo chochote, ni kutokana na uzoefu na ushirikiano walionipa wenzangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mchakato mzima ambao umejitalidi kuendesha Bunge hili ndani ya mfumo huu wa Bunge la Vyama Vingi, tuone kama *transition*, tunategemea Bunge lijalo ambapo wenzetu wengi hawa watakuwa hapa wachache, sisi tutakuwa wengi huko, naomba taratibu nyingine nzuri ziwepo ili kuweza kuendeleza nchi yetu. Ahsante sana. (*Makof*)

**MHE. AZIZA S. ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii, nakushukuru sana.

Pili, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, kaka yetu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, kwa kazi nzuri ambayo wameweza kuifanya na katika hali ngumu zaidi. Vile vile, kuwapongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nasema Waheshimiwa Mawaziri hawa wamefanya kazi ngumu kwa sababu katika kufanya kwao kazi, bajeti ambayo walikuwa wakipewa na bado wanaendelea kupewa ni ndogo sana. Kwa hiyo, walikuwa na kazi ngumu, lakini wameweza kuifanya kwa fedha kidogo walizokuwa nazo. Tunaweza kuwalauku, lakini katika lawama ni lazima tuangalie ni kipi walichopewa cha kuweza kufanya kazi kwa muda wa miaka mitano au kwa muda wa mwaka mzima. Kwa hiyo, hii ni kusema kuwa Serikali ni lazima ielewe na kuamini kuwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ni sawa na Wizara nyingine, inabidi kupewa kipaumbele na wao kuangaliwa katika bajeti yao ili iweze kulingana na bajeti za Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, wanapopata fedha ndogo wanaweza wasifikie malengo ya kazi zao wanazozifanya, matokeo yake vijana na wengine wakawalaumu kwa kutokufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, naomba niseme kuwa Serikali ni lazima iangalie suala hilo na ninawapa pole sana kaka yangu Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya kwa kazi ngumu ambayo ameifanya na kaka yangu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. Kuna

ule usemi wanaosema kwamba: "Mzigo mzito mpe Mnyamwezi." Lakini pamoja na uzito, basi mumuongezee fedha yeze Mheshimiwa Profesa Kapuya, pamoja na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii pia kuchangia kuhusu suala la migogoro kazini. Nimekaa kwa muda ambao nimejifunza mambo mengi yanayosababisha migogoro kazini. Lakini tuna uwezo wa kutatua migogoro hii. Ni lazima Watanzania waweze kuamini na kuelewa kuwa tupo katika utandawazi na kama tupo katika utandawazi ni lazima tukubali kubadilika. Suala la kuandamana, suala la kufanya migomo ni moja ya mambo yatakayofanya Watanzania tusiendelee mbele, tuzidi kurudi nyuma katika maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu kuna utaratibu wa sheria na Katiba na katika kazi pia kuna utaratibu. Kama wafanyakazi wanaona kuwa hawatendewi haki katika maeneo yao, wana haki ya kufuata sheria kwa kutumia wanasheria wetu ambao tuko nao ili kuweza kuomba madai yao wanayoona yana mapunjo ili waweze kuongezewa. Lakini kwa kuandamana na kupiga kelele ni jambo mojawapo litakalosababisha nchi yetu kurudi nyuma na hata wale wawekezaji wanaohitaji kuja kuwekeza katika nchi yetu wakaogopa kutokana na fujo au vishawishi wanavyoweza kuvipata. Wao wanaona ni mojawapo ya vitu vizuri, lakini ni kitu ambacho kinapoteza sifa ya nchi yetu na sifa ya wafanyakazi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, naamini kuwa wapo vijana ambao wana uwezo wa kufanya kazi na wapo vijana ambao wana nafasi na bado wanahitaji nafasi. Kwa hiyo, wale ambao wanajiona wana nafasi ya kuwa wanafanya migomo, basi watoe nafasi kwa wale ambao wanahitaji kuajiriwa ili waajiriwe kwa sababu bado tuna vijana wengi ambao hawana ajira. Nina imani wengi wanaweza kuona kuwa nimewaambia wafanyakazi au vijana wenzangu wanaoamua kugoma, lakini si sawa, ni lazima tuambizane ukweli pale panapofanyika makosa ili tuweze kurekebishana au kusaidia nchi yetu iepukane na migogoro ambayo haina sababu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili ambalo nataka kuongelea ni kwamba, katika vijana kuna nafasi pia za vijana wanawake. Vijana wanawake ni lazima tuangaliwe. Katika bajeti iliyopita niliuliza swalii lililohusiana na vijana wa kike wanaopata mimba wakiwa shuleni. Mheshimiwa Waziri alinijibu na kusema: "Ni kutokana na uhuni wa yule msichana mpaka akapata mimba." Lakini suala hili hili pia limetokea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo pia linanitisha kwa hivi sasa na linanihuzunisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa hoteli katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nina imani kuwa mfanyabiashara yejote anapokwenda kuangalia biashara yake aiweke wapi ni lazima aangalie kuna vivutio vyaa gani ambapo ataweka biashara yake. Hata kama akiweka soko, akiamua kuweke hoteli au maduka, ni lazima aangalie ni maeneo gani ambayo kutakuwa na vivutio zaidi. Sasa inanishangaza zaidi, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kujengewa hoteli itakayokuwa *Kilimani City Hotel*, je, pale wameangalia vitu gani ambavyo vina vivutio vyaa biashara ya hoteli?

Mheshimiwa Spika, nina imani kuwa wao wamechukulia uhitaji wa kupata pesa na si kuhitaji maendeleo au kuangalia athari ambayo itatokea pale. Wameona kuwa vivutio vikubwa vilivyopo pale ni wale wasichana wanaosoma katika chuo kile. Inasikitisha kwa sababu wameshindwa kupeleka hoteli katika eneo la bahari, lakini wanaamua kupeleka hoteli ndani ya Chuo Kikuu! Je, ni nini lilichowavutia zaidi?

Kwa hiyo, wapo ambao watashawishika kwenda pale. Ndiyo maana ya kusema kwamba, vijana wengi wa kike wataathirika kielimu kwa sababu pale ni sehemu ambayo itakuwa ni ya kishawishi kwa vijana wavulana na pia hata wazee kwenda kupanga pale na kuweza kusababisha vijana wa kike kurudi nyuma kielimu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie suala hilo na laiti kama itaendelea ile hoteli kujengwa na kufanya kazi pale, tuna imani kuwa vijana wengi wa kike watakuwa hawajapata haki zao kwa sababu watashawishika kwa mambo mengi yatakayofanyika pale. Tunaomba kama vijana wa kike, Serikali iangalie zaidi hoteli ile isiwepo pale. Kuna mambo mengi ya kufanya pale, si lazima hoteli.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika dunia masuala ya utalii ni masuala ambayo yako juu katika maendeleo. Ni kwa nini tusiweze kujenga Chuo chetu cha Utalii? Tanzania ni moja ya nchi ambayo ina vivutio vya utalii vingi sana. Vinavyojulikana ni vinne tu, lakini viko 14 ambavyo vingeweza kusaidia hata vijana wa nchi za nje kuja katika nchi yetu kujiunga na Chuo hicho cha Utalii kitakachoanzishwa kutoa *Degree* na *Masters* ambapo wengi watakaokuja kujifunza hapa watajifunza wakiwa darasani na bado watajifunza wakienda katika *field* itakayowaonyesha dhahiri kuwa utalii wa Kitanzania ukoje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba Serikali badala ya kujenga hoteli iangalie kubadilisha ili kuweka Chuo cha Utalii kiweze kuwasaidia vijana wetu wa Kitanzania waweze kuelimika kuliko kuwawekeea hoteli ambayo itawanufaisha watu wachache zaidi. Nina imani kuwa suala hili limefika na litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maafisa Vijana, hili naliongelea, lakini kutokana na bajeti finyu nina imani kuwa hata hawa Maafisa Vijana ndiyo maana wanakuwa hawapo katika Mikoa na hawapo katika Wilaya, matokeo yake wanatumia Maafisa Utamaduni ndiyo wanaofanya kazi za Maafisa Vijana. Kwa hiyo, ninaomba utaratibu huu uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la vijana kuweza kupata ajira. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza *ITV* na *TVT* kwa nafasi yao ambayo wameweka vipindi maalum vya vijana. Vipindi hivi ambavyo nimekuwa nikivifatilia sana kwa kweli vina mafunzo mbalimbali kuhusu vijana ni namna gani wanavyoishi na ni namna gani wengine wanavyopata ajira. Hiyo ni njia mojawapo ya kuwasaidia vijana wengine kujifunza wenzao wanafanya vitu gani katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, naomba pia Serikali iwasaidie vijana. Wanaambiwa kila siku vijana waweze kujajiri wenyewe, je, Serikali imewaandalia utaratibu gani wa vijana kujajiri wenyewe au imewapa mafunzo gani? Si lazima kwenda kumpa mafunzo kijana mmoja mmoja, lakini inaweza pia ikatumia nafasi hii ya *ITV* na *TVT* na redio kuweza kuwafunza au kuwaelimisha vijana mambo mbalimbali ili waweze kujajiri wenyewe.

Kuhusu suala la vijana na masuala ya uzoefu wakiwa kazini, hili nalirudia mara ya pili, katika bajeti iliyopita nililiongelea pia. Kijana anapoenda kuomba kazi anaambiwa ni lazima uwe na uzoefu usiopungua miaka mitano/sita/saba na kuendelea. Je, kijana ambaye ni sasa hivi ametoka kupata *Degree* au *Masters* yake, hii inampa nafasi gani ya kuweza kuelewa au amejifunza katika chuo gani? Nina imani hata sisi wenyewe Madiwani, Wabunge, hata Urais, hakuna chuo ambacho kiongozi yejote ameenda kujifunza apate kugombea Udiwani au apate kugombea Ubunge au apate kugombea Urais. Kila mmoja anachukua fomu na mafunzo yanakuwa huko huko anakokwenda. Kama hivi hata mimi leo nimesimama sjafundishwa kusimama kuongea katika Bunge, hakuna chuo kilichonifunza. Lakini wewe mwenyewe unajituma na mwisho unazoea kusimama na kuongea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado Serikali iangalie vijana wale waweze kupewa nafasi. Suala la kipengele cha kusema uzoefu kiondoke. Hakuna ambaye anaweza kutokuzoea, kila mmoja anazoea huko huko. Lakini bado mpaka sasa kipengele hicho kipo na hata kwenye magazeti wanakiandika. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kipengele gani hicho?

**MHE. AZIZA S. ALI:** Hata kwenye magazeti wanaandika kuhusu suala la uzoefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naona Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kule Mchinga wamezoea kuandika suala la uzoefu, naona amelifurahia sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuweza kuwapongeza vijana wote ambao wameshiriki katika Bunge lako kwa hii leo kuweza kuhudhuria katika bajeti iliyokuwa ikiwasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa sababu wamevutiwa sana na Wizara hii na hii ndiyo Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, naona unahangaika, hapa kulia kwangu ndiyo wale vijana wamekaa. Kwa hiyo, ninawapongeza sana kwa mahudhurio yao mazuri sana. Hii inaonyesha vijana ni namna gani ambavyo wanashawishika kuja kuhudhuria Bunge kujua Bajeti ya Vijana au imepewa pesa kiasi gani, ni uzoefu ambao huwa wanaanza kuzoea jamani, msianze kusema kuwa bado hawajazoea.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya, lakini bado niwashukuru wananchi wake ambao wamempigia kura na kuweza kufika katika Bunge hili.

Pia, lazima nikubali kuwa wananchi waliompigia kura Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya ndiyo wananchi ambao wamenipigia kura mimi. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo walikuwa wakiifanya na pili kuwashukuru wananchi Mchinga kwa kuweza kutuchagulia Kaka yetu Mudhihir Mudhihir na bado nina imani watakuwa na imani naye ya kumchagua tena. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgaywa uliomba dakika tano. Unaweza kuchangia kwa dakika tano.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili, naomba niwashukuru watoa hoja ambao ni Mheshimiwa Waziri pamoja na Msaidizi wake kwa hoja ambazo zinatugusa vijana wote wa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa vile muda hauniruhusu, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. La kwanza ni ajira. Kwa kweli ajira ni tatizo kubwa. Hii Wizara ina kazi nzito ambayo inabidi itafakari kwa kina. Sasa kwa kupitia hoja hii ninaiomba Wizara yetu hii ya Mheshimiwa Ndugu yetu Profesa Juma Kapuya kwamba tunaomba *tax relief* kwa viwanda vinavyojengwa Vijiji. Mimi nina utaratibu, kama Mungu atapenda labda kama nitarudi ninaendelea sasa hivi kufanya eneo moja katika Vijiji vya Jimbo langu Kijiji cha Igundu ninakifanya kiwe *industrial area*. Lengo langu ni kuhakikisha kwamba vijana hawaji tena Dar es Salaam kuhangaikia kazi. Vijana wa Jimbo langu ni mwiko kwenda Dar es Salaam kuhangaikia kazi. Kwa hiyo, ninaamini kwamba kufikia mwaka 2006 mwishoni tutakuwa na *industrial area* kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitaarifu Bunge lako kwamba niliwhi kuahidi kwamba tunafanya *research* kubwa sana ya kuanza kuzalisha gari yetu. Niliwhi kulitamka na huwezi kuliongopea Bunge, ninaomba nitamke wazi kwamba kazi hiyo imekamilika. Mungu akipenda mwakani Januari tunaweza kuwa na gari letu Watanzania lililotengenezwa Tanzania la bei ndogo kabisa ambalo tutaweza kulimiliki Watanzania. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nikutaarifu kwamba Taifa lako la Tanzania lina vijana wenye vichwa. Mimi nimefanya *research* sijui wanaita MKUKUTA, katika mkakati wa gari, nimefika mpaka huko Japan kwa wenzetu wanakotengeneza hayo magari, nimeingia kwenye viwanda vyao Korea, lakini nimegundua kwamba Watanzania wana akili, vijana wana akili, tatizo lililopo hatuwaonyeshi njia waone wapite njia ipi. Tumewaacha kama walivyo, wanahangaika wanatapatapa hawana mwelekeo. (*Makofi*)

Sasa naomba nitoe *challenge* kwa Wizara ya Profesa Juma Kapuya kwamba, kuna haja ya kuweka mwelekeo mzuri kwa vijana wetu. Mimi mwenyewe wakati ninafanya kazi moja ambayo nafikiri muda sio mrefu nitawakabidhi Waheshimiwa Wabunge, niliyoahidi kwamba nitatoa *science kit* kwa ajili ya Shule zetu zote Tanzania na hizi

*science kits* zitakuwa hapa tayari siku ya Alhamisi ambazo niliwaambie kuwa zina thamani ya Shilingi milioni 120 na nitazikabidhi kwa heshima ya kazi niliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo, kama nilivyowaahidi kwamba nliifanya *research*, siyo hapa Tanzania nimekwenda India, Uingereza, nchi zaidi ya nne. Nilipofanya nao kazi waliamini kwamba kweli Tanzania tuna vichwa. Kuna Mzungu mmoja aliniuliza swali moja ambalo leo hii najiuliza; akasema, kama Tanzania ina watu wanaochapa kazi kama wewe ni kwa nini ni maskini? Aliniuliza hilo swali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilifanya kazi, wale Wazungu wakachemsha. Nimefanya nao kazi masaa 48 sikulala, hilo naomba nikuhakikishie. Niliokuwa nafanya nao kazi nilistukia wamesinzia, hao Wazungu, nikabaki peke yangu, lakini nikajitahidi. Ndiyo maana ya hiyo *science kit* tukaipata kama nilivyowaambia kwamba ni *science kit* ya kwanza kwa nchi za Afrika na kwa dunia nzima zinazalishwa nchi tatu tu, ambazo ni India, Uingereza na Tanzania. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, ninaomba nimalizie kwa hoja hii nyingine kuhusu *VETA*. Tunaomba *VETA* ipunguze gharama. *VETA* ndiyo *challenge* ya kumsaidia Mtanzania ambaye hana uwezo na ambaye hawezi kwenda Sekondari. Gharama zimekuwa ni kubwa mno. Sasa imekuwa kama biashara, lakini *VETA* nia yake ilivyokuja haikuwa biashara, ilikuwa ni kuwasaidia vijana kupata ajira/ujuzi utakaowasaidia katika maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kwamba mimi natoka familia ya wakulima na pia ni mkulima, tukaona kwamba sasa kuna haja pia ya wazee wetu wakulima waingizwe kwenye utaratibu wetu wa *NSSF* kwa maana kwamba wazee wetu wanafikia wanapata shida sana wanapokuwa wazee, hawana tumaini la maisha yao ya baadaye. Akimaliza kulima, kazeeka ndiyo hivyo tena, hana nguvu za kulima, vijana labda kusomesha au hana basi ndiyo maisha yake yamekwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukaomba kwamba waingizwe katika utaratibu wa *NSSF*. Kulingana na mazao watakayokuwa wanazalisha, basi wakatwe *percentages* fulani ambayo kwenye uzee wao wataanza na wao kulipwa hata kama ni Sh.10,000/= zitawasaidia kwa ajili ya matibabu na mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo huenda ni la mwisho, ni kuhusu michezo. Michezo ni burudani na ni ajira. Tumeomba Serikali yetu muda mrefu kwamba ni kwa nini tusianze *practise* ya kwenda hata *Soccer* la kulipwa? Sasa kwa kupitia uwanja huu ni *challenge* pia kwamba sasa tunaweza kuanza hata *Soccer* la kulipwa. Kuanza *Soccer* la kulipwa huwezi kuanza na mabilioni kama wanayolipa kule Uingereza. Tunaweza kuanza hata kwa shilingi 50,000/= hata kwa mashindano ya mbuzi. Watu ni *Soccer* la kulipwa hilo tunakwenda kwenye *practise* ili vijana wetu waone kama ni ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ninaomba nikupongeze wewe, ni mzee wetu kwa kweli umetulea, leo hii mimi nina miaka kumi Bungeni. Niliingia hapa nikiwa kichanga, lakini umetuelekeza, umetupa njia mpaka leo tunajiona sisi na wenyewe

wakiitwa wazee Bungeni na mimi nasimama. Siyo wazee wa umri, wazee wa Bungeni kwa maana nina miaka kumi. Kwa hiyo, nimepata uzoefu mzuri. Kwa hiyo, ninaomba nikushukuru. Pia naomba niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa hoja zeo walizokwishatoa na ambao bado wanaendelea. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, Wabunge wenzangu mimi niko pamoja na ninyi sambamba kwa mema na mazuri, ninawatachia kila zuri Mungu atujalie neema na afya njema tujaliwe kurudi. Ahsanteni sana. (*Makofî/Kicheko*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naitumia nafasi hii kuipongeza sana hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa hotuba yao hii nzuri iliyojaa ufanisi mzuri ambao unaleta matarajio mema ya maendeleo ya Taifa letu hili katika sekta nzima inayohusiana na masuala ya kazi, maendeleo ya vijana na michezo.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, maafisa na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi hii nzuri ambayo mmejitahidi kuisimamia na kuiongoza. Naiunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kumteua Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuiongoza na kuisimamia Wizara hii muhimu kwa maisha, maslahi na maendeleo ya watu na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mawaziri hawa wawili kuonyesha kuwa mmoja ni mpenzi mkubwa sana wa klabu ya Simba na mwengine ni mpenzi mkubwa sana wa klabu ya Yanga, wanafanyakazi zao vizuri sana, kwa ushirikiano mkubwa na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii kama ukiiangalia ipasavyo utagundua kuwa imegawanyika katika sehemu tatu muhimu, zinagusa maisha, maslahi na maendeleo ya watu na Taifa letu la Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza inahu masuala ya kazi, sehemu ya pili inahu siana na maendeleo ya vijana na sehemu ya tatu inahu siana na michezo. Sehemu zote hizi tatu ni muhimu kwa maisha, maslahi na maendeleo yanayohusuwatu na nchi kwa ujumla. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara yetu hii kuimarisha mipango na sera zake ili iweze kuleta mafanikio yaliyokusudiwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri imagusia maeneo mbalimbali ambayo yanaigusa jamii yetu na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa saba wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri inaeleza kuhusu kampeni ya ukomeshaji wa ajira ya mtoto. Ninaipongeza sana Serikali na Serikali kuwa na kampeni hii ili inayowahusu watoto. Pia ninaiomba Wizara kutueleza kampeni hii imefanikiwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa ishirini na mbili, hotuba inaeleza juu ya kazi na ajira.

Mheshimiwa Spika, nikiinukuu sehemu hii inaeleza kuwa, Serikali imeendelea kurekebisha sheria za kazi ambazo zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuendelea kurekebisha sheria hizi za kazi hasa tukiangalia hali halisi ya mabadiliko mbalimbali yaliyotokea na yanayoendelea kutokea hapa duniani tangu kuanza kwa karne hii ya ishirini na moja.

Mheshimiwa Spika, karne hii imeleta mabadiliko na maendeleo makubwa katika kazi (Ajira) na ktika suala zima la uchumi na maendeleo ambapo suala la kazi ni moja katika sekta ianyosimamia maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda niiulize Wizara na Serikali, je, hizi sheria zinazofanyiwa marekebisho wafanyakazi wanazijua? Kama wanazijua ni njia gani zinazotumika kuwafahamisha? Kama hawazielewi ni kwa nini hawaleleweshwi?

Mheshimiwa Spika, ni jambo la msingi wafanyakazi kuzielewa sheria zinazosimamia kazi zao, maslahi yao na kadhalika. Kwa hiyo, hatua zichukuliwe ili wafanyakazi wazielewe sheria zinazohusu kazi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, anaelezea juu ya maendeleo ya vijana. Ninaipongeza sana hotuba hii kuelezea juu ya maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara hii na Serikali yetu kuongeza juhudi zake na mipango imara kujenga misingi thabiti itakayowapatia vijana maendeleo makubwa ya kiuchumi, kielimu na kitaalamu pamoja na kipato (fedha).

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa ishirini na sita, unaelezea juu ya maendeleo ya michezo kwa kusema kuwa Serikali imeendesha zoezi la kuhamasisha Halmashauri, Manispaa na Wilaya, kuajiri wasajili wasaidizi wa Wilaya wa vyama na vilabu vyta michezo nchini. Ninaipongeza sana Serikali kwa kuendesha zoezi hili lakini naiomba Serikali katika kuzihamasisha Halmashauri, Manispaa na Wilaya hizi kusiweze kuajiri wasajili wasaidizi wa Wilaya wa vyama na vilabu vyta michezo tu bali pia usimamizi na uendeshaji mzuri katika vyama na vilabu hivyo katika maeneo hayo yaliyoainishwa yaani Halmashauri, Manispaa na Wilaya zetu zote hapa nchini. Kwa hiyo, kama zipo kasoro katika kulifanikisha hili naomba zirekebishwe haraka sana ili kuleta maendeleo ya kweli katika michezo hapa nchini na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuandika mchango wangu huu mdogo, napenda nirudie kusema kuwa hotuba hii ninaiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Nawapongeza Waziri Alhaji Juma A. Kapuya na Naibu Waziri Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, kwa hotuba yao. Pia ninawapongeza watendaji chini ya Katibu Mkuu Abubakar S. Rajabu. Baada ya hayo nachangia maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utambuzi wa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, naipongeza Serikali kwa utambuzi mbali na mikakati ya kuwasaidia bado kasi ni ndogo. Kazi kubwa inaonekana na taasisi na mashirika binafsi.

Mheshimiwa Waziri ni utaratibu gani wa kudumu ili wasaidiwe hasa hawa watoto wa mitaani? Kazi kubwa inafanywa lakini ni jinsi gani wazazi wanabanwa pindi wakifahamika wametelekeza watoto. Mara nyingi wanaume wanachangia pindi wanapowapa ujauzito hukana au pia wakiachana na wake zao na watoto hutelekezwa. Ni Sheria ipi itawabana? Wananchi wanalamika badala ya kuiambia jamii wasaidie kuelimisha, kuna umuhimu wa kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kutuwezesha kupata uwanja wa Kimataifa kule Dar es Salaam. Ni vyema viwanja vingine viangaliwe ikiwa ni pamoja na uwanja wa Mkwakwani, Tanga. Miaka ya 1970 Tanga ilivuma sana katika michezo hasa mpira wa miguu, sasa ni kama timu zimekufa.

Mheshimiwa Spika, viwanja bila wachezaji haiwezi kuelezeza. Kuna tatizo linajitokeza malalamiko kwa vijana kutowezeshwa kushiriki na kujifunza ili wapandishe/wakuze vipaji vya michezo kama *netball*, mpira wa meza, vikapu, ngumi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bado vijana wanalamika/kutambua umuhimu wa kuwepo kwa utaratibu wa yale mashindano ya michezo kwa shule za Sekondari na Msingi. Nashauri Wizara iandae mikakati mikubwa na endelevu ili michezo na mashindano haya yaende na kuweza kuendelea kwa kiteknolojia, badala ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kuona eti inashusha kiwango cha taaluma. Kwa nini Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Kazi na Michezo isikae pamoja na Wizara ya Elimu na Utamaduni mkamaliza tatizo hii?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikipo kwa vijana, Bajeti kwa Wizara katika Wizara hii na eneo hili ni kero, aidha, Serikali iongeze Bajeti hii au kuacha. Hii inaonekana kama kero hasa inapokuwa pesa ndogo imeletwa katika Halmashauri na vikundi vya vijana vingi, pesa yenye sana sana wamepata shilingi 20,000. Hii ni sawa na kuchukua maji katika kikombe na kumwaga baharini. Tunaomba itafutwe programu maalum ya kusaidia vijana badala ya kutegemea fedha ya Halmashauri asilimia 5.

Mheshimiwa Spika, sera ya wazee, tunaipongeza Serikali kwa hili lakini bila kusimamia utekelezaji, sera itakuwa hakuna maana. Ili kutekeleza bado Serikali iongeze Bajeti.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawapongeza wananchi/wanajamii kwa kushiriki kwa hali na mali kuwasaidia watoto/vijana wetu kwa kila hali. Napongeza pia Wizara kwa juhudhi zao, lakini ni dhahiri bado wanahitaji msaada zaidi kifedha na hali. Nawapongezeni tena Waziri, Naibu Waziri, Mungu awajalie mrudi tena Oktoba ili pesa tunayowapa leo iwe fimbo ya kuanzia ili mtekeleze majukumu yenu kwa ari mpya na nguvu mpya. Watendaji nawapongeza pia na kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba niunge mkono hoja.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri na hotuba yenyeye dira. Timu hii ya uongozi itakumbukwa kwa *legacy* ya uwanja wa kwanza Tanzania utakaokuwa na hadhi ya *Olympic*. Hii ndiyo *legacy* atakayokumbukwa nayo Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Mheshimiwa Waziri Profesa Kuma A. Kapuya. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita ilitokea ajali Jimboni Arumeru Mashariki ilitokea Sakila, Kata ya Kikatiti. Ilihusisha vijana wanamichezo, walikuwa wanasafiri kwenda kuchenza soka. Tunashukuru kwa jinsi Wizara walivyoshiriki kwenye msiba uliotupata. Jimbo zima linakumbuka kwa shukrani, heshima aliyyotupa Mheshimiwa Waziri Profesa Juma A. Kapuya kwa kufika mwenyewe na kushiriki kwenye hayo maafa yaliyyotupata. Vijana kumi na moja walipoteza maisha yao kwenye ajali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitoa ahadi kwa wafiwa kwenye ajali hiyo, uongozi wa michezo Taifa pia walitoa ahadi. Nina imani huenda jitihada za kutekeleza hizo ahadi zimeshafanywa natanguliza shukrani kwa niaba ya walengwa kama walengwa wameshafikishiwa walioahidiwa. Kama hizo jitihada za kutekeleza ahadi bado zinaendelea, basi ningeomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli ya kutoa matumaini kwa hao waliolengwa na ahadi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ningependa kuchangia linahusu Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). *Technically* hili ni tatizo la fedha, inakusanya bilioni 97.4 lilipa bilioni 24.5 (25% ya makusanyo). Ninapendekeza yafuatayo:-

(a) Je, ni kwa nini *NSSF* isiwe chini ya usimamizi wa *BOT* chini ya *Financial Institute Act*?

(b) Ufanyike utaratibu wa kuwawezesha wenyewe mfuko na hasa vijana waweze kukopa kutohana na fedha za mfuko kama vile wanavyofanya *PPF*.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniweka hai mpaka hivi leo.

Mheshimiwa Spika, ninataka nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Katibu Mkuu pamoja na Wizara yote kwa Bajeti yao nzuri na imechambua mambo yote na imegusia mambo mengi ambayo ni ya kweli. Naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia hoja hii na mimi kwa kuipongeza Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) kwa kweli shirika linafanya kazi zake vizuri na linawasaidia sana vijana na akinamama kweli kweli, shirika hili limefanya kazi zake Tanzania nzima kuanzia vijiji mpaka mijini kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Spika, ninao ushahidi mzuri kwa shirika hili kwenye ushahidi wa kwanza kwenye Jimbo la Kiwani wako akinamama wengi tu pamoja na vijana waliofaidika na mradi hivi sasa akinamama wanaendesha kazi zao vizuri hali kadhalika na vijana. Hivyo linastahili kupongezwa, mimi ninalipongeza sana na ningeombwa Serikali na masharika mengine waige mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuongeza fedha za kununulia vifaa vya kujimudu kwa wanafunzi wa vyuo vyenye ulemavu, lakini mimi ningeishauri Serikali kweli kweli imejitahidi lakini pale ambapo ilionekana upo uwezo basi Bajeti iongezwe, ukiunganisha mambo mengi au majukumu makubwa yaliopo ni vyema Bajeti hii iongezwe sana angalau wawezeshe kukidhi haya majukumu.

Mheshimiwa Spika, lingine ningeombwa Serikali kuhusu makambi yanayoishi wazee na watoto wasiojiweza kwa kweli kambi hizi zinasikitisha sana, haziridhishi hata kidogo, majengo yenyewe yamechakaa, idadi ya watu wanoishi humo imekuwa kubwa mno ukilinganisha na huduma inayokubalika humo, naiomba Serikali iziangalie sana sana kambi hizi na kama kuna uwezekano basi Bajeti ya nyongeza.

Kwa kweli Bajeti hii imeelezea ukweli mimi natilia mkazo zaidi kwamba Bajeti hii ipitishwe na kama kuna uwezekano basi iongezwe tena kwa sababu bado ni ndogo mno na majukumu ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninasikitishwa sana na migogoro inayoendelea ndani ya mamlaka ya *VETA*. Chombo ambacho ni mkombozi kwa vijana wengi, mimi ningeishauri Serikali ikasimamia kwa kina ili mgogoro huu umalizike haraka sana iwezekanavyo ili vijana wetu wafaidike na chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nalipongeza Shirika la *NSSF* kwa juhudhi kubwa sana kwa kuweza kununua jengo la *Mafuta House* ambalo lilishindikana kuendelezwa, namwomba Mungu awape nguvu zaidi ya kumaliza jengo hilo, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii mkono asilimia mia kwa mia. Ninaendelea kuwapongeza viongozi wote wa Wizara hii, ninaitakia mfanikio mema na waendeshe Wizara hii kwa mafanikio mema ili vijana wetu waendelee kufaidika na Wizara hii. Ahsante.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia machache kuhusu Wizara hii. Tangu tupate Uhuru, tulianzisha makambi ya vijana ambayo yalisaidia sana vijana kupata mafunzo ya uzalishaji mali na kuwaimarisha vijana nidhamu ya kazi. Mbozi tunalo kambi ambalo kwa sasa halitumiki kabisa. Naomba kama Serikali haina mpango wa kambi hili basi ilite Wilayani, litumike na liimarishwe kuwa Sekondari ya Bweni kwa wasichana. Wilaya iko tayari kuliendeleza.

Baada ya Wizara kupendekeza kuifuta sheria ya nguvu kazi, je, kuna mafanikio ya vijana kufanya kazi kwa hiari na kwa maendeleo ya Taifa letu? Lazima Taifa liwe na utaratibu wa kuwabana vijana waweze kubaki vijiji mara baada ya kumaliza elimu yao ya msingi na sekondari. Hivi litafanikiwa tu kama kila kijiji kitalazimika kisheria kuwapatia uwezo wa kumiliki ardhi kimila ili waweze kuzalisha na kutumia elimu ya kilimo wanayofundishwa wawapo shulen. Hili lita saidiwa vijana kubaki vijiji na kuendeleza vihamba vyao pale walipo wakijitegemea.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Wizara iandae utaratibu utakaowajengea vijana waamini kuwa kazi ni heshima ya utu wa binadamu. Kwa msingi huu basi Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi ili vijana wote wapimiwe maeneo yao pale walipo. Hili la kuwashauri wajunge vikundi vya uzalishaji si rahisi na ni lazima hufanyike uchambuzi kwa nini makambi ya Gezaulole yalitokomea bila mafanikio.

Wizara ichukue nafasi ya kudhibiti malalamiko ya wafanyakazi. Yapo malalamiko kwamba wafanyakazi wanafukuzwa kazi bila kujali kazi zao na wanapoffishwa Baraza la Mawaziri na kutakiwa warudishwe kazini kwa kuonekana kwamba walionewa, mwajiri hupuza maamuzi hayo na hakuna hatua zinazochukuliwa na Baraza ama Wizara. Ukweli huu umemtokea Bibi Fumbo aliyeachishwa kazi na uongozi wa Benki ya Posta Tanzania, walipuza hata maamuzi ya mahakama ya kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo kuhusu suala hili kwani habari hii anayo na vithibitisho vyote anavyo (nilimkabidhi). Vinginevyo naunga mkono hoja na kuwaomba wenzangu wote kuipitishe Bajeti hii. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na wataalamu wao wote kwa kuweza kuwasilisha Bajeti yao mbele ya Bunge lako hili Tukufu, kwa ufasaha na mwelekeo wa kupiga hatua ya maendeleo ndani ya Wizara hii.

Kwanza napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uamuzi thabiti na unaotekelzeza kwa kuamua na kudhamiria kujenga uwanja wa kisasa kabisa Tanzania wenye hadhi ya *Olympic*, ukweli katika nchi yetu ni sawa sawa na katuondoa kizani

Watanzania na kutuweka kwenye mwanga usiozimika. Hongera sana na fungu lako liko kwa mola aliyetuumba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Wizara za kuhakikisha vijana wanafaidika na matunda ya nchi hii, napenda kuikumbusha Wizara kilio cha vijana wa Zanzibar cha kupatiwa Chuo cha *VETA* kwani tunaamini *VETA* ni ya Watanzania lakini la kusikitisha bado haijawa ya Watanzania kwani upande wa pili wa Tanzania hawajafaidika wala kuziona faida zake. Kwa hali hiyo, ningeomba Wizara kufikiria *VETA* kufika Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wengi wanaoacha kazi wanasumbuka sana wakati wa kufuatilia mafao yao, kwani inakuwa tofauti na wakati wa makato huwa ni wa haraka, lakini wakati wa mafao huwa wa usumbufu. Ningeomba Wizara iangalie zaidi kwa namna gani inaweza kuondoa usumbufu huo ili kila mmoja wetu aipende mifuko ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi hapa nchini wamezoea mchezo wa mpira wa miguu, naishukuru Wizara kwa kuleta ushawishi kwa vijana kushiriki michezo mingine na kwa hilo Wizara imefanikiwa lakini la kusikitisha zaidi ni kuona vifaa vya michezo ndio vimeduwa vya bei ya juu sana kutokana na kodi za ushuru kuwa kubwa kwa hiyo kwa kuitia Wizara yetu inayoshughulikia michezo iiombe Serikali kufikiria kuondoa kodi katika vifaa vya michezo ili kuongeza hamasa kwa vijana waweze kuipenda zaidi michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache napenda kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE.PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya, Naibu wake Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Katibu Mkuu Ndugu Abubakar S. Rajabu, Wakuu wa Idara na watumishi wote kwa kazi nzuri pia kwa taarifa hii ya kina. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache kuhusu maeneo machache ya ufanuzi. Kwanza, kituo cha ajira kimeonyesha mafanikio na matatizo yapi ili kabla hakijafunguliwa katika kanda nyingine marekebisho yafanyike?

Mheshimiwa Spika, pili, sera ya vijana, je Wizara imeandaa mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo? Je, mkakati huo umehusisha vipi Wilaya, Mkoa na Vijiji? Kabla ya awamu inayokuja, Wizara ingesaidia maandalizi hayo maana hii itakuwa *agenda* kubwa kwenye kampeni za mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, tatu, sera ya wazee, mkakati wa utekelezaji nao umefikia wapi? Pia sera ya watu wenye ulemavu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bado kuna kazi kubwa ya kuendelea na jitihada za kupambana na magonjwa ya matumizi ya madawa ya kulevyia kwa vijana. Tunahitaji mikakati zaidi ili kuliepusha Taifa letu lisiingie katika janga hili.

Mheshimiwa Spika, ningefurahi kujua kama Serikali inashauriana vipi na shirika lasilo la kiserikali lijulikanalo kama *SOBER TANZANIA* ambalo linahusika na kuelimisha athari za ulevi na dawa za kulevyia?

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa uwanja wa michezo, limemjengea heshima Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Pia limejenga heshima kwa Wizara nzima, lakini tatizo la wafanyakazi na wajenzi limeanza kutia hofu kama hali hii ikiendelea. Je, Wizara inasema nini kwa wananchi ili kujua ukweli juu ya tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, je, mpango wa zamani wa kuimarisha michezo katika ngazi ya vijiji na shule za misingi kwa kuwapatia mipira kila kijiji, umeishia wapi?

Napenda kuipongeza *NSSF* kwa kazi nzuri inayofanyia nchi hii, lakini je, mpango wa *NSSF* wa kuanza kuwahudumia watu ambao siyo wafanyakazi rasmi nao umefikia wapi? Wapo wafanyabiashara, wakulima ambao wangependa kujiunga na mfuko huo wafanyaje? Wanatuuliza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa jitihada za *VETA* nchini, vituo hivi viendele kumilikiwa na Serikali. Ni mapema mno kuanza kufikiria kuvibinafsisha vyuo hivyo, tusikubali mpaka tufanye tathmini yake sisi wenyewe wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, naomba suala la ulemavu lipewe kipaumbele kwa hatua zifuatazo:-

(a) Kuongezewa Bajeti katika vyama vyaya walema.

(b) Kupewa elimu yenye kulingana na mazingira na ulemavu nao.

(c) Kuhakikisha miundombinu kama majengo na viwanja vinifuata hali halisi ya kuwasaidia walema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu, Tanzania viro viwanja vingi vyaya michezo hasa mpira wa miguu lakini viwanja hivyo vinamiliikiwa na Chama cha Mapinduzi. Lakini kulingana na uwezo wa chama ni mdogo kuvihudumia viwanja hivyo vina hali mbaya, hivyo nashauri Serikali ijiingize ubia na chama ili viwanja vipatiwe ukarabati kwa mtindo wa kisasa wa kuinua soka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo, ipo haja ya waamuzi wetu na viongozi wa vyama vyaya michezo wanapatiwa mafunzo na semina ili kuondoa malalamiko ya waamuzi katika michezo na migogoro katika vyama na vilabu vyaya michezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo ya Pasaka, lazima kwa makusudi Wizara ihakikishe michezo ya Pasaka inaimarishwa zaidi ili kuinua uhusiano wa kiundugu na michezo kwa Jamhuri yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo jeshini, ipo haja kwa Wizara kuhakikisha michezo uraiani inapata nguvu kama majeshini ilivyo kuliachia jeshi kuimarisha michezo ni kuvuruga misingi ya michezo uraiani, ipo haja Wizara ya Kazi, Wizara ya Elimu kushirikiana kuanzisha michezo mashulen, kazini na taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ligi ya Muungano, kuna michezo gani ya mbadala baada ya kuondosha ligi kuu ya Muungano. Ipo haja ya mfumo wetu wa michezo uangalie sana ushirikiano wa michezo katika soka kuwepo na ligi kama hii ambayo itatoa kasi na ubora wa kimichezo baina ya nchi zetu mbili, Pasaka, Muungano, Mufindi, haitoshi tuongezee ligi yenye msisimko zaidi Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti za vyama, vyama vingi vya michezo Tanzania vinategemea zaidi ruzuku kutoka Serikalini kujiendesha kwa hivyo, ipo haja kwa vyama vyetu kubuni mbinu za kujipatia fedha za kujiendesha ili visiwe tegemezi sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, *Serengeti Boys*, kwa muda mfupi Katibu wa *TFF* ametoa kauli kuwa watachukuliwa hatua wale wote waliosababisha kuwa Timu ya Serengeti kutolewa katika mashindano kwa kumchezesh mchezaji aliyekuwa na umri mkubwa (kijeba) lakini cha kushangaza hatua hizo hazijatajwa waliosababisha uzembe huo, naomba ufanuzi zaidi tu. Ahsante.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya, Naibu wake Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na Katibu Mkuu Abubakar Rajabu, kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali na hasa wadau kwa kufanikisha uchaguzi wa *TFF*. Nampongeza sana Rais wa *TFF*, Ndugu Tenga kwa kazi nzuri anayoifanya pamoa na Kamati nzima ya utendaji ya *TFF*. Ili *FAT* wafanikiwe lazima vilabu vyote viwe na utulivu (*stability*). Mizozo katika klubu ya Yanga na Simba itakwamisha jitihada za *FAT* kiunua kiwango cha mpira. Haipendezi na haifai kwa Serikali kufumbia macho mizozo iliyopo Yanga na Simba kwani wakorofii wanajulikana. Siku zote wako msituni, uongozi wowote unapokuwa madarakani kwa maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kutafuta njia ya kumaliza mgogoro katika vilabu hasa Yanga na Simba. Kuhusu sera ya wazee nasisitiza mfuko wa mikopo kwa wazee uundwe mapema na uwe wa kutosha. Utaratibu wa kumkopeshwa mwananchi hasa wazee shilingi 20,000 kama ndio mkopo wa kusaidia haufai na haukidhi haja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TFF* hasa Rais Tenga kwa kufanya marekebisho ya Katiba ya *TFF* hasa kwa kushirikisha wadau mbalimbali kama wananchi walivyosisitiza. Naomba Serikali iwawezeshe ili kukamilisha azma hii. Naunga mkono hoja.

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima kabisa kuchukua fursa hii maalum kwanza kukushukuru kwa kupata wasaa huu kuchangia hotuba ambayo inaelezea kuhusu Wizara hii ya Maendeleo ya Vijana na Michezo ambayo inaletwa asubuhi katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kitope kuunga mkono hotuba hii ya Bajeti kwa ukamilifu yaani asilimia mia kwa mia. Hotuba hii imeandikwa vizuri na Bajeti yake iliombwa inastahili kupewa yote ili utekelezaji wake uweze kufanyika kama ambavyo Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wenzao wote wameomba kwa ufasaha kabisa, kwa namna yake nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa utekelezaji wa Wizara hii umeonyesha vyema kuanzia mafunzo ya fani mbalimbali, kwa vikundi maalum, maendeleo ya vijana, maendeleo ya michezo, elimu ya mafunzo ya ufundi stadi ni mionganini mwa mambo yanayoonyesha uhai mzuri wa kubainisha Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2000. Aidha, namna ambayo majukumu ya kushughulikia ajira yameelezwa kwa uangalifu kabisa na yako bayana kabisa.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ustawi wa Jamii imeendelea kuhamasisha asasi zake katika utekelezaji wake wa sera ya Taifa ya wazazi pamoja na uwekaji wa taratibu na majukumu ya kuwawezesha vijana kujiimrisha kiuchumi na kisiasa kwa kuimrisha maadili mazuri.

Aidha, Wizara hii imeonyesha umahiri wake wa kupiga vita vya UKIMWI pamoja na utaratibu wa kuinua vita dhidi ya umaskini. Lengo la Wizara pia imeimarisha nia yake ya kuwalinda vijana hususani wa kike kuwalinda dhidi ya maambukizi dhidi ya UKIMWI na *HIV/AIDS*.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue fursa hii maalum kabisa tena kwa dhati kabisa niishukuru Wizara hii na Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kutimiza ahadi yake ya kujenga kiwanja cha sasa cha kimataifa cha michezo kwa ilani ilivyoagiza. Ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Benjamine William Mkapa, amekuja katika awamu ya kutekeleza ahadi za Chama cha Mapinduzi kwa mtiririko kama ambavyo waasisi wa Muungano huu wa Tanzania na awamu zake zote zimekua zinatekeleza.

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi wa Kitope hatuna pingamizi yoyote, hatuna hoja wala dawa na Bajeti yake na ninaiunga mkono hoja hii kwa nguvu zetu zote. Ahsante.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na nawatakia utekelezaji mwema wa malengo mliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya, kwa kumtuma Katibu Mkuu kwa kutembelea Kituo cha Walemavu cha Kolandoto na kuona hali halisi ya kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwenye Bajeti ya mwaka wa fedha 2005/2006 mambo mengi yatafanyika. Nashukuru kwa msaada alioutoa papo kwa hapo wa *blankets* na nguo ya kujikimu. Naomba sana Bajeti ya chakula iongezwe kwani shilingi 126/= kwa siku ni kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, Wizara iweke utaratibu wa kutoa vifaa vya michezo katika shule na shule za vijijini na wapenzi wachezaji wa mpira.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Naibu Waziri kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa ufasaha sana hata ilipokuwa maswali ya Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza watendaji wakuu wote wa Wizara kwa ushirikiano wa kutatua matatizo ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la neema katika kutekeleza malengo mliyojipangia.

**MHE. MWANAIDI HASSAN MAKAME:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na maafisa wote wa Wizara hii. Wizara hii ni muhimu sana kwa hiyo, naomba isimamie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuongeza fedha kwenye Bajeti ijayo ili iweze kufanya kazi zake vizuri, Serikali ifungue maduka ya vifaa vya kwenye maduka ya watu binafsi inakuwa bei ni kubwa jambo ambalo usababisha wana michezo wengi kushindwa kununua vifaa hivyo na wapo walemavu ambao wanashindwa kuijendeleza katika biashara zao kwa sababu hawajapata utaalamu wa kutosha hivyo ninaomba Serikali isimamie suala hilo.

Pia iundwe Kamati maalum, kila Wilaya itakayosimamia masuala ya michezo Kamati hizo wawemo na makundi ya vijana walemavu na wazee wenye uzoefu wa michezo, viwepo vifaa vya kuchezea watoto na vifaa hivyo viuzwe kwa bei nafuu kwa sababu wanafunzi uwezo wao ni mdogo na ikiwezekana baadhi ya vifaa Wizara itoe bure ili kuwapa moyo wanafunzi hao, Wizara isimamie vyuo vya ufundi kwa sababu wanafunzi wengi baada ya kumaliza kusoma na hasa wale wanaomaliza elimu ya msingi wengi wao hawana shughuli za kufanya hivyo ninaomba Wizara ijenge viwanda vya kutosha vya aina mbalimbali kwa ajili ya kujitafutia ili waweze kujitegemea na kupiga vita dawa za kulevya, hivyo Serikali iwachukulie hatua kali kwa wale watakaokamatwa na dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ule mpango wa kupanua Chuo cha *VETA*, Tabora ili kiweze kutoa mafunzo ya fani mbalimbali umefikia wapi? Vile vile ningependa kujua kile Chuo cha Walemaru wasioona cha Lwanzori, Tabora Wizara ina mpango gani wa kukitumia? Chuo hicho kwa muda mrefu hakitumiki na wafanyakazi wanapata mishahara bila kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wao kwa hotuba safi na kazi nzuri waifanyakazi katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimechangia kwa maneno lakini sikusema yote Bungeni. Kwa hiyo, napenda kuongeza yafuatayo katika baadhi ya yale maeneo manne niliyochangia kama ifuatavyo:-

(1) Sera ya mipango katika kukuza uchumi na ajira. Nimelalamikia mikopo kutokuwepo kwa vijana wa Kisarawe na Mkoa wa Pwani. Labda Wizara inatoa lakini utaratibu wa kuifikisha kwa walengwa ni mbovu. Nashauri uwepo ushirikiano baina ya Wizara yako na TAMISEMI kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha mgawanyo wa haki baina ya Wilaya na Mikoa ili vijana sehemu mbalimbali wapate migao yao.

(b) Kuhakikisha kuwa michango ya Halmashauri ya 10% inatolewa kwa nyakati zake.

(2) Nidhamu, haki na wajibu, nimewapongeza kwa utekelezaji wa jukumu kuu, muongeze jitihada katika maeneo yote.

(3) Mheshimiwa Spika, kuhusu makundi maalum.

(a) Kwanza watoto, kamati za mayatima na wasio na uwezo ziongozwe na zipatiwe nyenzo badala ya kuzitelekeza baada ya kuzianzisha.

(b) Pili, makazi ya walemaru hayatoshi kulingana na idadi yao. Baadhi yao yametelekezwa, vile vile kwa kuwa haiwezekani kuwaweka walemaru wote kwenye makambi au makazi, uwepo mpango wa kuwasaidia walemaru walio nje ya makambi.

(c) Tatu, kuhusu wazee wasio na uwezo wa kufanya kazi wawekwe chini ya *Welfare* ili watunzwe kikamilifu na wenye uwezo wa kufanya shughuli nyepesi, wapatiwe nyenzo ili wajihudumie na wazalishe.

Nne, kuhusu mfuko wa Huduma za Jamii, tuiachie bodi na menejimenti wawekeze kwenye miradi ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu (*Economic Analysis or Economic Viability Studies*). Tusiwalettee maamuzi ya kisiasa, tuige mfano wa Serikali zote za Ethiopia na Shirika la Ndege lao (*Ethiopia Air Line*). Wakati wote, uongozi wa shirika haupewi maagizo na Serikali ya nchi.

Tano, mambo mawili ambayo sikuyagusia kabisa ni suala la jukumu la kusimamia kambi za walemovu yangethamishiwa TAMISEMI ili uangalizi uwe chini ya Halmashauri kule ziliko kambi hizo na usuluhihi wa migogoro ya kimichezo. Hili linachukua muda wako na wa wasaidizi wako mwingi. Matokeo yake mnanyang'anya muda wenu wa kusimamia eneo la uzalishaji. Kwa hivyo, nashauri kuwa mamlaka kusika iliondoe katoka Wizara hii jukumu la michezo lihamishiwe Wizara nyingine. Bora zaidi iundwe Wizara mahsusii ya michezo na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri na ninaiunga mkono hoja yake. Ahsante.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufanuzi mzuri na wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo, kuhusu walemovu, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga Bajeti ya kutosha kusaidia watoto yatima kupata elimu na matunzo? Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha makambi ya walemovu kwa kutoa huduma bora zaidi na je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kusaidia shule za wasioona ikiwemo Shule ya Msingi ya Wasioona ya Buigiri, Dodoma?

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Serikali ijenge Shule ya Sekondari ya Wasioona Buigiri, Dodoma, shule itakayosaidia watoto wasioona Kanda ya Kati na mikoa mengine kupata elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Kazi, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha/kufungua ofisi ya Idara ya Kazi kila Wilaya na kuwapatia vitendea kazi vya kutosha na kuna sababu gani za kufuta/kufunga ofisi hizo katika wilaya? Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Ofisi za Ustawi wa Jamii katika Wilaya na kuwapatia vitendea kazi vya kutosha?

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, kwanza naipongeza sana *TFF* kwa kusimamia ligi kuu ya *Vodacom* vizuri. Ushauri wangu ni kwamba *TFF* iweke mikakati ya kuondoa migogoro mingi katika vilabu vyetu vya mpira wa miguu, migogoro ndicho chanzo kikubwa cha kurudisha nyuma na suala la michezo hasa mpira wa miguu hapa nchini. Pia naipongeza sana timu yangu ya Mji Mpwapwa kushiriki ligi kuu ya *Vodacom*, miaka nane mfulululizo nataka kuwahakikishia wanachama wapenzi wa Mji Mpwapwa

pamoja na kuanza msimu huu wa mwaka 2005 lakini haitashuka daraja tayari tumefanya marekebisho ili ifanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali vilabu vingi havina vyanzo vyatapato pamoja na *Vodacom* kusaidia vilabu vyatapato wa miguu vimeshiriki ligi kuu fedha hizo hazitoshi kwa mizunguko yote ya ligi kuu. Naomba Serikali itenye fedha kusaidia vilabu hivyo ili kuendeleza mchezo huo, marefa wanaoharibu/vurunda mchezo wa mpira wa miguu hatua kali zichukuliwe.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, shukrani nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara wote. Karibuni sana Dodoma.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kama ifuatavyo, vijana wana mkakati wowote ulioandaliwa na Serikali kuwakwamua kimaisha? Mikopo ya vijana inaongezeka au inapungua kwa kiasi cha fedha kuanzia mwaka 2000/2001 hadi mwaka 2005/2006 kwa asilimia ngapi?

Mheshimiwa Spika, vijana wanaojiedeleza mijini kwa nini wabomolewe maeneo yao na kunyanganywa mali? Pia vijana wanaopata ajira kwenye viwanda binafsi kulipwa chini ya kiwango cha kima cha chini. Kiwango chini ya kiwango kinaitwaje, shimonii?

Mheshimiwa Spika, viwanda ambavyo vina migogoro na vijana waliopata ajira wanapoonewa na matajiri mbona iko kimya? Vijana kunyang'anywa viwanja vyatapato ili kupisha matajiri kujenga nyumba tabia hii ni hujuma ya michezo. Kuhusu kiwanja, gharama ya kujenga kiwanja cha Taifa ni shilingi ngapi hadi kukamilika? Huu ni mikopo au msaada?

Mheshimiwa Spika, kuhusu jengo la *Mafuta House*, naomba Wizara yako ikae na Waziri wa Mkuu, Bodi ya NSSF na TPDC na watu wachache wenye vibali kama wewe ili kujadili upya swali hili, ili lisilette matatizo awamu ijayo kwa watu kupelekwa Mahakamani

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, Wizara yako ni mpenzi wa timu gani, Simba au Yanga ili wasitubabaishie kiushabiki?

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Jimbo langu la Siha naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Alhaj Profesa Juma A. Kapuya, Mbunge na Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Hotuba hii ina uchambuzi wa kina na inaonyesha namna Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 ilivyotekelizwa katika Taifa letu. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. Aidha, napenda kumpongeza sana Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge ambaye amekuwa msaada mkubwa kwa Waziri wake. Tunampongeza sana na kumtakia kila la kheri katika siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira katika nchi yetu ni suala la mahusiano ya uzalishaji mali katika mfumo ambao tumekubali kuutumia katika nchi yetu. Mfumo wa kibepari ambao ndani yake umebeba soko huria nia yake kubwa ni kutengeneza faida kibao (*super profit*). Lakini la pili ni kwamba jinsi teknolojia inavyozidi kukua ndivyo walio wengi huondolewa kazini na mashine kuchukua nafasi ya nguvu kazi. Hili ni suala la historia wala si la ufahamu. *Industrial Revolution* ilizalisha watu wengi wasio na kazi, bidhaa zisizo na wateja kwa kukosa uwezo wa kuzinunua (*poor purchasing power*) na pia tatizo la malighafi ya kutosheleza mahitaji ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, hili la ajira ambalo ni la kihistoria kwetu lazima tulitazame kwa uangalifu mkubwa. Ilani ya Uchaguzi ya CCM imesema Chama cha Mapinduzi kikichukua madaraka kitakachofanyika ni kuweka mazingira ambayo yatamwezesha kila mmoja wetu kujiajiri. Hii ina maana kuwa kazi yetu kubwa ni kubuni miradi mbalimbali ambayo ndiyo itasababisha kuwepo kwa ajira kwa ajili ya vijana wetu na watu wetu wote kwa ujumla. Hii ina maana kwamba kupatikana kwa miuondombinu kama umeme, maji, barabara, reli yenye tu itatuletea ajira na wakati huo huo itaweka mazingira ambayo yatasababisha watu wetu waweze kujiajiri, vinginevyo tunaweza kuwaacha watu wetu wakiwa na matumaini makubwa ya ajira hivyo kuzalisha vurugu nchini zisizo na misingi wowote ule. Kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo, kuimarishwa kwa kilimo kidogo kidogo kupitia ushirika wa uzalishaji mali ni miongoni mwa mambo ya kuzingatia ili tupate ajira. Sio hivyo tu, upatikanaji wa mikopo midogo midogo kwa ajili ya watu wetu kutasaidia sana katika uibukaji wa miradi mbalimbali ambavyo naamini itasaidia kuleta ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naompongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza ahadi yake ya kuona uwanja wa michezo wa Dar es Salaam wenye hadhi ya kimataifa unaanzishwa rasmi. Hongera Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa hotuba hii ambayo ina matumaini makubwa ya maendeleo kwa wananchi wetu na Taifa kwa ujumla. Nawapongeza wote ambao kwa njia moja au nyingine wanachangia katika uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya vijana, naipongeza Wizara hii kwa juhudzi za kutoa fedha kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya mikopo ya vijana. Hata hivyo kiwango hiki ni kidogo ukilinganisha na wingi wa vikundi vilivyohamasika. Ngudu Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba wapo vijana wengi wanaoendesha huduma ya daladala, husafiri kwa balskeli. Vijana hawa kama wangepatiwa msaada au mikopo wa kutosha wangaweza kuboresha huduma hii, wakawenza kununua hata *Bajaj*, pikipiki za miguu mitatu toka India. Pikipiki hizi ni nzuri hasa kwa usafiri wa vijijini kusikokuwa na barabara na magari yasikofika. Nafahamu kuwa mikopo hutolewa na Halmashauri ili iweze kutimiza wajibu wake huu, lazima iwe na uwezo. Naomba kupata ufanuzi Halmashauri inatakiwa ifanye nini ili hatimaye ipate msaada wa kutosha kwa kuweza

kutoa mkopo kwa miradi mikubwa kwa kikundi kikubwa kama hicho lakini chenye manufaa kwa wananchi wengi kama hao?

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya michezo, napongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa kwa kulipatia Taifa hili zawadi ya kiwanja cha kiwango cha *Olympic*. Ni chombo ambacho hakitasahaulika na bila shaka kitaitwa kwa jina lake. Ili kiwanja hiki kiwe na manufaa, hatuna budi kuwa na viwanja vidogo vidogo karibu na wananchi, viwanja ambavyo hatimaye vitatupatia wanamichezo watakaotumia kiwanja hiki kipyä na cha Kimataifa. Zawadi kwa Watanzania iliyotolewa na Rais wetu mpandwa wa awamu ya tatu ushauri wangu ni Wizara hii kuja na *master plan* ambayo hatimaye itakuja na mpango kama MMEM utakaojenga viwanja vya michezo ngazi ya Wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri na wananchi. Inawezekana kabisa. Ni imani yangu kuwa viwanja hivyo vitaibua ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya katika maendeleo ya michezo. Tukumbuke michezo hujenga afya na miili ambavyo hatimaye michezo hujenga afya na miili ambavyo hatimaye hujenga Taifa lenye afya na nidhamu kubwa.

Kuhusu mafunzo ya *VETA*, napongeza sana Wizara hii kwa mafunzo yanayotolewa kwa vijana kupitia *VETA*. Wahitimu wa mafunzo haya ni msingi wa maendeleo kitekinolojia na maendeleo ya kiumla ya karne hii. Mapendekezo, kwa vile vijana wengi wanatokea katika familia zenye vipato duni na zisizo na elimu ya awali ya ufundi wanaosemea vijana wao, basi utaratibu ungfanywa wahitimu washawishiwe kuanzisha vikundi kabla ya kutoka vyuoni wapewe mikopo, mitaji vitendea kazi ili wanapohitimu wataanza mara moja kuzalisha kama shirika dogo huku wakiwa chini ya uangalizi wa chuo chao. Bila msaada huo wahitimu huzagaa mijini wakitafuta ajira kwa kipindi kirefu huku taaluma yao ikipotea bure.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *NSSF*, naipongeza sana *NSSF* kwa miradi yake mbali mbali ya uwekezaji. Naomba sana kuelimishwa iwapo *NSSF* yaweza kuwekeana mikataba na Halmashauri zetu hasa katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Kama inawezekana ni upi utaratibu unaoweza kutumika ili wa umma kam walimu wauguzi na wengine wengi wanaoweza kukubali kukaa kwenye Wilaya husika kwa kipindi fulani miaka 10 au zaidi wakaweza kujengewa nyumba hizo na wakawa wanalipia kwenye mishahara yao. Nitafurahi kufahamu iwapo watumishi wa kwimba nao wanawenza kunufaika kwa mpango kama huo. Kuhusu wazee na walemovu, naipongeza Wizara hii kwa sera mahususi kwa jaili ya makundi maalum kama wazee na walemovu bado tunao wananchi wengi walio katika makundi haya ambayo yanahitaji msaada.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri, kwa vile baadhi ya ndugu hao wana jamaa na ndugu zao walio na uwezo kimapato, nashauri sheria itungwe itakayowataka ndugu au jamaa kuchangia katika ustawi wa makundi haya. Hii itapunguza uzito wa mizigo Serikalini. Mimi kwa niaba ya wapigakura wa Jimbo la Kwimba naunga mkono hoja hii.

**SPIKA:** Sasa ni zamu ya watoa hoja kuhitimisha hoja yao, namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo asaidie kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo hoja ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mimi nitajielekeza katika maeneo manne tu. Eneo la kwanza ni hili la *VETA* naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Rhoda Kahatano na Mheshimiwa Bujiku Sakila kwa mchango wao. Tunataka kuwathibishia kwamba tunachukua maoni yao yote. Hoja iliyotolewa na Mama Kahatano ni nzuri. *VETA* inachangia kupiga vita umaskini kwa kutoa mafunzo ya aina mbalimbali, kwa makundi mbalimbali kama ifuatavyo:- Kundi la kwanza ni wale wanaomaliza Vyuo vya Ufundis Stadi ambao mitaala yao ya mafunzo ya ujasiriamali. Vijana hao ama kwa kuungana wao wenyewe au wakisaidiwa na Halmashauri zao huunda vikundi vidogo vidogo na kupewa mikopo kutoka vyanzio mbalimbali na hivyo kuwa tayari kuwijirri pale wanapokosa ajira. Kundi hili pia limeanza kupatiwa vitendea kazi wanapomaliza mafunzo yao ili iwe rahisi kuwijirri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kundi la pili ni wale ambao hawana ujuzi wa ujasiriamali, kama vile vikundi katika Halmashauri mbalimbali. Wale vijana ambao hawana ujuzi wanawenza kuunda vikundi pia, halafu *VETA* ikavipa mafunzo kama ya ufugaji wa kisasa wa nyuki, kuku na kadhalika, halafu wakapewa msaada wa vitendea kazi na kuanza kuwijirri. Tayari hapa Mkoani Dodoma eneo la Dodoma Vijijini, Kata ya Chilonwa vijana 40 walipewa mafunzo ya aina hiyo na *VETA* na pia kupewa vitendea kazi, *VETA* ikishirikiana na Halmashauri hizi katika kutoa mafunzo haya.

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni lile la wanaojifunza kama saidia fundi. Hawa hukosa baadhi ya mafunzo kwa sababu ya kukosa mitaala katika maeneo hayo na kwamba sehemu hizo za mafunzo hutegemea aina ya kazi fundi aliyopata wakati huo. Tunatarajia vijana hawa kuwapatia mafunzo kwa njia ya masomo ya jioni au kozi fupi fupi ili kuwawezesha kupata stadi kwa viwango vilivyopo. Vile vile, mafunzo maalum hutolewa kwa watoto walio katika ajira mbaya ili kuwawezesha kuwijirri au kuajiriwa. Watoto hawa hupewa msaada kupitia mpango *ILO* na *IPEC* ambayo itawanufaisha kutoka kwenye ajira mbaya na ambao tayari wamepatiwa mafunzo ya *VETA* katika fani mbalimbali.

Halafu Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o amezungumzia suala la mafunzo ya ujasiriamali litiliwe mkazo kwa wanawake katika Halmashauri mbalimbali, hasa wale ambao tayari wana mwelekeo wa kujiunga katika *SACCOS*. Kutokana na taratibu zilizopo mikopo haipaswi kutolewa kabla ya walengwa kupewa mafunzo ya ujasiriamali. Kazi kubwa ambayo *VETA* inafanya ni kuhakikisha walengwa wanapata mafunzo hayo ili iwe rahisi kwao kupata mikopo, lakini iwe rahisi pia kurejesha mikopo.

Kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali za Wilaya, *VETA* inatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi ambavyo havijapata mafunzo ya aina hiyo. Wigo wa utoaji mafunzo haya hivi sasa unatanuliwa kwa kuviwezesha Vyuo vyote vya Ufundis Stadi, vile

vya *VETA* na visivyokuwa vya *VETA* viweze kutoa mafunzo haya katika vikundi vilivyopo katika maeneo hayo.

Mpango wa Taifa wa kufundisha Walimu wajasiriamali umeanzishwa katika Chuo cha *VETA* cha Ualimu wa Fundi Stadi kilichopo Morogoro. Hii itawezesha kupata Walimu wa kutosha katika stadi hizi.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo - Mbunge wa Tabora Mjini amezungumzia juu ya upanuzi wa Chuo cha *VETA* Tabora. Naomba nimhakikishie kwamba *consultant* ameshachaguliwa tayari, kazi imeanza na hivi sasa washauri hao wako hatua ya usanifu. Kwa hiyo, muda sio mrefu upanuzi utaanza.(*Makofî*)

Pia Mheshimiwa Herbert Mntangi - Mbunge wa Muheza yeye anaomba Wilaya ya Muheza ijengewe Chuo cha Ufundı Stadi. Ni ombi zuri, lakini tuliamua kwanza kila Mkoa upate Chuo na hivi sasa tunahakikisha kwamba Mikoa ya Lindi, Manyara na Pwani katika mwaka huu wa fedha inajengewa halafu tutaangalia ni Wilaya gani ya kuanza nayo baada ya kukamilisha Mikoa yetu yote.

Halafu Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe ameomba sana *VETA* ianzishwe kule Zanzibar. Tungependa kufanya hivyo, lakini kwa bahati mbaya masuala ya mafunzo ya Elimu ya Ufundı Stadi siyo ya Muungano, hata hivyo tunashirikiana na wenzetu katika kuandaa mitihani ambayo inakuwa ni ya aina moja. Hoja itakapojitokeza ya masuala haya kuunganishwa katika Muungano kwa taratibu zilipo tutafurahi kufanya hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, pamoja na Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah wameshauri kuhusu kumalizwa kwa mgogoro ndani ya *VETA*. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge wa Kamati, pamoja na Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah na Wabunge wote kuwa kilichotokea *VETA* haikuwa mgogoro ila kutokuelewa kwa Wafanyakazi wa *VETA* kuhusu utafiti uliokuwa unafanywa na mtaalam chini ya Wizara kwa madhumuni ya kufanyia marekebisho Sera ya Ufundı Stadi nichini. Baada ya kulijua hilo, Serikali pamoja na Bodi ya *VETA* walichukua hatua madhubuti kuwaelimisha Wafanyakazi wote wa *VETA* pamoja na wadau wa *VETA*. Kwa sasa hali ya *VETA* ni shwari baada ya juhudhi hizo kufanywa. (*Makofî*)

Halafu Mheshimiwa Talala Mbise - Mbunge wa Arumeru Mashariki, kuhusu kupatiwa mafunzo ya Ufundı Stadi kwa watu wasio na Elimu, *VETA* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ina utaratibu wa kutoa mafunzo kwa sekta isiyo rasmi. Mafunzo ya namna hii yanajumuisha watu wa aina mbalimbali wakiwemo wasio na Elimu ya uraia. Ndugu yangu Muttamwega Mgaywa, hee! Ameshaondoka! Yeye amechangia sasa hivi habari ya *VETA* kupunguza gharama. Nataka nimhakikishie kwamba Vyuo vya *VETA* gharama yake ni ndogo lakini bado tunawasaidia wale ambao wanaendesha Vyuo vya Ufundı Stadi, siyo tu kwa vifaa, lakini hata Walimu wao kuwapa Elimu ya Ufundı Stadi na namna ya kuifundisha Elimu hiyo pale Morogoro. Bado hivi sasa tunatoa Elimu ya

ujasiriamali kwa kushirikiana na Halmashauri kama tulivyofanya kwa Halmashauri ya Dodoma Vijijini.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ningependa niingie katika suala la vijana. Mheshimiwa Shoka Khamis Juma amezungumza mambo mengi, kwa kweli yale ya ushauri tunayapokea hatuwezi tukajibu kila moja.

Lakini lile la kusema kwamba vijana wamekata tamaa, tunahisi kama labda ni kauli ya kutiwa chumvi mno. Kwa sababu sio kweli kwamba Serikali imekaa kimya tu na yenyeWE imekata tamaa. Tunafanya shughuli nyingi za kuhakikisha kwamba tatizo hili la vijana linaondoka. Kama alivyo sema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, suala la kutatua matatizo ya ajira kwa vijana sio suala la kulala tu asubuhi likawa tayari. Sio suala la mtu mmoja tu akafikiria mimi naweza kulifanya hivi. Hili suala la mchekato ndiyo maana MKUKUTA unaingiza kwenye suala la Elimu, kwenye suala la kilimo, maji, ardhi, kila Wizara utakayokuta wewe kuna suala la MKUKUTA na haya yote nia yake ni kumwondoa Mtanzania katika suala hili la umaskini. Kwa hiyo, tunapoyazungumza haya wakati mwingine ni vyema tukawa tunaangalia hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shoka amesema Mwenge wa Uhuru ni kitendawili. Sisi tunafikiria kauli yake ndiyo kitendawili kwa sababu dhana hii ya Mwenge wa Uhuru si kitu kipyta, lakini Watanzania tufikie mahali na sisi tujivunie mambo yetu. Kwa sababu katika dunia masuala ya mwenge yako matatu tu, moja katika mashindano ya *Olympic*, kuna mwenge. Wenzetu hawa hawausemei na wanausifa haswa Mwenge wa *Olympic*, mzuri kweli! Lakini tuna Kifimbo cha Malkia kinakimbizwa nchi nzima hatujawasikia kupiga kelele. Mwenge wa Uhuru wa Tanzania ambao unajenga amani, unahamasisha maendeleo, wenzetu wanasema hiki ni kitendawili. (*Makofit*)

### **MBUNGE FULANI: Waambie!**

Miradi hii siyo ya kubabaisha. Kwa kweli miradi hii inayozinduliwa na mbio za mwenge ni miradi halisi, watu wanachangia kwa hiari yao, inajenga umoja, wanaibua uzalendo na kwa kweli akitokea kiongozi wa kisiasa ambaye hatapenda kuunga mkono jambo hili badala yake anaamua kulivuruga, kiongozi huyu hatakii mema nchi yetu, wala hatakii mema umoja na ustawi wa nchi hii. (*Makofit*)

Pia, Kaka yangu Herbert Mntangi amezungumza kwa uchungu sana kwamba huu umaskini tunaouona matatizo yake makubwa ni Elimu. Bila shaka ataungana na mimi kwamba jitihada za mpango wa MMEM na MMES na hii habari ya MKUKUTA ni jibu la matatizo hayo ambayo yalikuwa yakinukabili muda mrefu. Watu wenye akili wanasema ukigundua tatizo na suluhisho unalipata hapo hapo. Kwa hiyo, tatizo ambalo umeligundua suluhisho limepatikana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Maafisa Utamaduni/Vijana na ndugu yangu Aziza Sleyum Ali, naye amechangia vile vile. Ni kweli pale ambapo pana Afisa Utamaduni Afisa Vijana hayupo, tunamuunganisha. Pale ambapo kuna Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa Utamaduni hayupo tunamuunganisha, maadamu kazi zao zote karibu zinakaribiana na

tunajitahidi kama alivyosema Mheshimiwa Shamim Khan hapa asubuhi wakati anajibu swalii, wakati mwingine Maendeleo ya Jamii hulazimika kumpa Elimu ya Idara ya Maendeleo ya Jamii, Afisa Utamaduni au Vijana ili aweze kufanya kazi kwa maana ya Serikali ni ile ile moja na Halmashauri ni ile ile moja.

Lakini akazungumzia vile vile juu ya fedha za Mfuko wa vijana kuwa ni mdogo. Tunakubali, lakini udogo nao unaongezwa vile vile na tabia ya vikundi kutokurejesha mikopo. Maana huu Mfuko ni *revolving*. Sasa watu wanapewa wanachikichia tu wanakaa kimya. Tungependa kuwapongeza kwa kweli wale Viongozi wa Wilaya 10 ambao wameamua kurejesha mkopo huu kwa asilimia mia moja na sisi tumewapa mara mbili yake kwa maana ya milioni sita zaidi na fedha hizo bado zipo.

Kwa hiyo, kama Wilaya ambayo inaweza ikarejesha kesho. Tunawahakikisheeni keshokutwa tutampa *cheque* ya milioni sita. Sasa kwa wale ambao hawarejeshi, Mfuko utaendelea kuwa mdogo kila siku. Ningomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Waheshimiwa Madiwani, hivi vikundi wakati mwingine tukienda tukidai kwa nguvu tunaweza tukakosa kura, lakini ili tuwasaidie kupata wengi zaidi, basi hawa wachache waliopewa tuwabane warejeshe ili wengine waweweze kupata. Hata wale vijana wa Kisarawe nao waweze kupata, mimi naamini imekuwa ni tatizo kwa sababu kwa miaka mitatu mfululizo sasa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, haijafanya marejesho. Sasa tungeomba warejeshe. *Wallah* wakirejesha tutahakikisha tunawapa mara mbili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Margareth Mkanga anasema wapo baadhi ya watu ambao mikopo kwa walemaru wanaitoa kwa ubaguzi sana. Kama wapo wa namna hiyo, ni watu wa hatari kweli kweli, tunatoa wito kwa Halmashauri zetu. Tunapozungumzia vijana tunazungumzia umri wao na siyo jinsia wala siyo hali yao ya kimaumbile. Kwa hiyo, wale ambao wanafikiria walemaru hawastahili kupata mikopo hii wanafanya jambo la dhambi kinyume cha sheria na taratibu. Tunawaomba waitoe mikopo hiyo na maadam haitoki mifukoni mwao ni mikopo ya Serikali, basi waifikishe kwao. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Halinga unasema Mbozi mnataka Kambi ya Vijana ya Sasanda igeuzwe iwe Sekondari. Tunakuombeni mtuachie ndiyo maana tumeanza kulikarabati, tumeweka na umeme wa *solar* pale. Tunataka sasa kila kanda vijana tuwaweke pale wafundishwe kwa vitendo ili tupunguze tatizo ambalo Waheshimiwa Wabunge, wote wanalipigia kelele la vijana kukosa stadi za kazi. Kwa hiyo, nakuomba Mzee utasaidie kuhamasisha kwenye Halmashauri wakubaliane na sisi kwamba eneo hili tunalihitaji, tumeanza kulifanyia ukarabati na mwaka huu wa fedha tutaongeza ukarabati zaidi. Naamini Mheshimiwa Edson Halinga kwa sababu ni impenzi wa vijana, utatusaidia sana katika hili maana wale ambao wangkuja, Sekondari na wanaokuja kwa miradi ya vijana wote ni vijana wako. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Kaka yangu Semindu Pawa, Shemeji, tunapokea ushauri na maoni yako yote. Mfuko wa Vijana ambao ameuzungumzia kwa uchungu sana kwamba hautoshi, fedha zinakuwa kama mzaha na mwingine alitumia neno hili. Kwa kweli tatizo lile nililolizungumzia mwanzoni kama tutajitahidi vijana wetu warejeshe Mfuko huu sasa

hivi ungekuwa na mabilioni ndiyo maana sasa tumeamua Halmashauri ambayo haileti hatupeleki, lakini wakileta kile walichokopeshwa tunawarejeshea mara mbili kama njia ya kuhamasisha watu kutulipa fedha hizi ili ziwafikie na watu wengine. Maana zikilipwa haziendi hazina zinabaki kwenye Mfuko huo huo. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Bana Mbise, alisema vijana ndiyo Taifa la Tanzania, tunakubali vijana Taifa la leo. Lakini fedha zilizotengwa ni kidogo. Sisi tunakubali tunafurahia na *concern* aliyoonyesha kwetu. Lakini tunaamini kwamba kadri uchumi unavyoongezeka na Bajeti hii tunaongezewa walau kiasi kidogo na Waheshimiwa Wabunge msichoke kutupigia debe maana tunaamini kila mkipiga debe ndiyo fedha hizi zinaongezeka. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Aggrey Mwanri upatikanaji wa mikopo midogo midogo utasaidia kubuni miradi ya vijana. Tunaungana mkono kabisa na wewe na yale uliyotuandikia kwa sababu wewe ni mchumi wa vitendo siyo nadharia tunaamini tutaitumia busara hiyo uliyotupa ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Lydia Boma tunapokea maoni yako, lakini Halmashauri hizo hazitupwi kama unavyofikiria. Tunapeleka Mfuko wa Vijana, Mfuko wa Wanawake, asilimia kumi ambayo haitoshi. Lakini sasa tumeanzisha kupitia *VETA* kuleta Elimu hii ya ujasiriamali ili kuweza kuwasaidia hao vijana. Hata pale alipozungumza Mheshimiwa Mbunge, kwamba hata wachezaji wengi wa mpira wanatoka kule Mikoa ya Kusini, watu walianza kucheka wakaona kama ni hadithi. Wale waliocheka ni wale amba hawafuatilii historia ya mpira. Lakini watu kama akina Marehemu Chuma, Marehemu Dini, akina Oktaviani Mrope, akina Marehemu Selestine Sikinde Mbunga, akina Marehemu Muhaji Muki hao wote kwa kweli wametokea Lindi, Nchi Yetu, Tawi la Yanga Afrika. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Sijaamini tunashukuru sana kwa pongezi zake kwetu na ye ye mwenyewe ni Daktari ndiyo maana ameweka msisitizo mkubwa katika vijana kuelimishwa juu ya kukwepa maambukizo ya Ukimwi. Sisi tutautumia ushauri wake wote katika mawazo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye michezo naona muda unakwenda kweli. Kwa ujumla wengi wamempongeza Rais kwa uamuzi wake wa kutekeleza ahadi aliyoiweka ya uwanja wa kisasa. Wote waliota pongozi hizo tutazifikisha kunakohusika. Lakini Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud pamoja na pongozi amekwenda mbali zaidi kutaka na vifaa vya michezo kwamba vipunguziwe ushuru wa kodi ili wanamichezo Tanzania waweze kununua kwa urahisi. Tumepokea ushauri huo na tutawasiliana na wenzetu wanaohusiana na sekta hiyo. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Paul Kimiti, zaidi ya pongozi ameulizia vile vile ule mpango wa zamani wa kufikisha mpira, jezi kwenye timu za Vijiji umeishia wapi? Kweli kulikuwa na mpango huu kupitia nchi ya Korea, Norway na UNICEF, lakini ukasimama ghafla na sisi tunaendelea kuzungumza na wenzetu kwamba jamani kile mlichotuonjesha kilikuwa kitamu. Sisi hatujasema kichungu mbona mmekatiza? Lakini kuomba unajua

kuna raha yake. Kuomba lazima ubembeleze kwa lugha laini na wakati wenyewe tunafikiria namna ya kufikia huko. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Bi Mwanaidi Hassan Makame amesema Serikali ifungue maduka ya michezo ili kupooza bei ya vifaa. Kwa kweli hili tunashindwa kulifanya kwa sababu tulishajiondosha kwenye biashara. Lakini tunawaomba wawekezaji siyo tu kuagiza vifaa, lakini waweke hapa viwanda. Mheshimiwa Muttamwega kama anataka kuanzisha kiwanda cha kutengeneza magari kwa kweli wangetusaidia vile vile kutengeneza vifaa vya michezo wangetuondoshea sana matatizo. Kwa hiyo, tunaomba Watanzania wenyewe uwezo huo wafanye hivyo ili kutupunguzia matatizo kidogo. Ametutaka vile vile Mheshimiwa Mwanaidi Makame tuunde Kamati mbalimbali za michezo Wilayani. Kamati hizo zipo chini ya Sheria Na. 12 ya mwaka 1967 iliyofanyiwa marekebisho na sheria Na.6 ya mwaka 1997. Kwa hiyo, sheria hizo zipo, tunakushukuru sana kwa maoni yako hayo. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Semindu Pawa, tena amezungumzia gharama za kujenga kiwanja. Ni mkopo au vipi na ni kiasi gani? Gharama ya ujenzi wa uwanja huu ni Shilingi bilioni 54.6 ambazo zinachangiwa na Serikali ya China na Tanzania. Kwa hiyo, hatuna deni. Unaona kazi hiyo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Katibu Mkuu ameahidi kwamba hatatoka hapa mpaka amekamilisha maelezo haya yote na mkakati wa kutekeleza Bajeti hii, ninaamini haya mengine ambayo ninayo humu mkononi yatamfikia kila mhusika katika muda utakaotakiwa kabla ya Bunge hili kuvunjwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, basi niseme la ujumla, watani wetu asubuhi ya leo kupitia Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, wamejigamba tena kwa matao, kuwa eti watakapoingia madarakani watageuza kila kufeli kuwa kufuzu. Ingawa hii ni kauli yao ya kila kuchapo, sisi tunaona ni vyema kuwajibu. Laiti nafsi zetu siku moja zingepewa uwezo wa miguu yetu hapana shaka kuwa Ikulu ingejaa Marais pakuweka mguu pasipatikane. Lakini kwa bahati njema nafsi ni nafsi na miguu ni miguu. Maajabu makubwa sana haya ya mtu mzima kutamani kutandika mkeka, wakati mahali penyewe pa kutandika mkeka hana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiwaauliza msingi wa matarajio yao tarehe 30 Oktoba, 2005 wanakwambia eti kwa sababu wanaongozwa na Profesa. Ikiwa hoja ni uprofesa, hivyo CCM humu ndani tu wacha nje, tuna maprofesa wangapi? (*Makofi*)

Mwingine huyu hapa! Lakini Waswahili husema kuwa ndani ya kundi la wasioona akitokea mwenye chongo huyo huwa mfalme. Basi, imekuwa ndiyo wimbo, Profesa wee, Profesa, sisi tuna maprofesa wangapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niruhusu nikushukuru wewe binafsi na Wasaidizi wako wakuu, Naibu Spika na Wenyeviti wetu wawili wa Bunge kwa kutuongoza vyema humu

Bungeni. Tunapoingia humu ndani wengine hata Kanuni hatuzijui, lakini wewe kwa uvumilivu mkubwa unatulea mpaka tunafahamu Kanuni zinakuwaje. (*Makofi*)

Namshukuru pia Mheshimiwa Sumaye, Waziri Mkuu kwa uongozi na imani yake kwangu kiasi cha kunitfea kwenye Kamati ya Shellukindo iliyopitia na kutoa mapendekezo ya mafao ya wastaa fu ambao walishachukua mafao yao ya mkupuo na kuwarejesha katika utaratibu wa pensheni. (*Makofi*)

Kamati hii ya Shellukindo vile vile ambayo mimi nilikuwa Mjumbe wake, ilipitia na kutoa maoni juu ya mafao ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Shellukindo alituongoza kwa busara kubwa na kwake pia nimejifunza mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa walionipa ndani na nje ya Bunge. Shukrani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wa CCM ambao kwa vipindi viwili wamekuwa wakinichagua kuwawakilisha katika Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Alhaj Profesa Juma Athumanii Kapuya katika kipindi cha miaka mitano alikuwa kiongozi wangu na mwalimu wangu. Namshukuru sana kwa ushirikiano alionipa na namwombea kwa Mwenyezi Mungu ashinde kwa kishindo katika uchaguzi ujao. (*Makofi*)

Shukrani hizi pia zimfikie Katibu Mkuu wetu Bwana Abubakar Rajabu na timu yake yote. Kuwemo kwangu humu Bungeni kumetokana na wapiga kura wa jimbo la Mchinga. Nawashukuru sana kwa imani walioionyesha kwangu na ushirikiano mkubwa walionipa katika ujenzi wa Jimbo letu. Nimewaambia kuwa nimejimwaga tena uwanjani na wao wameniambia karibu tena. Sasa ikiwa kuna watu wanajua mbio mimi ndiyo nafahamu njia. (*Kicheko/Makofi*)

Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, niliunga mkono kabla sijaanza Nakushukuru. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa ili niweze kuelezea baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Kwanza naanza kwa kuwashukuru sana kwa michango yao mizuri ambayo imeimarisha hoja tuliyoileta leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Waliopata nafasi ya kuchangia ni wengi sana na ningependa wengi zaidi wapate nafasi ya kuchangia kutokana na utamu wa Wizara hii. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Profesa Henry R. Mgombelo, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Bujiku K.P. Sakila, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud,

Mheshimiwa Edson M. Halinga, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo, Mheshimiwa George M. Lubeleje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wengine ni Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Asha Ali Ngede na Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliopata nafasi ya kuchangia kwa mdomo au kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Haroub Said Masoud - Makamu Mwenyekiti wa Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma - Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wengine ni Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Talala B. Mbise, Mheshimiwa Lydia T. Boma, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali na Mheshimiwa Muttamwega B. Mgaywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya ya Maendeleo ya Jamii ya Kudumu ya Bunge, alipowasilisha mawazo ya Kamati yake. Kwa michango yao tumeipongeza na tumeipokea sana. Vile vile naomba nimshukuru sana msemaji wa upinzani, ndugu yangu Shoka ambaye anaunga mkono hoja hii kutokana na urafiki wake yeze na Waziri lakini nadhani aliunga mkono hoja hii kwa sababu hoja hii inajitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile napenda nimpongeze na yeze kwa uvumilivu alionao kama alivyozungumza Mheshimiwa Mudhihir hapa kwamba wataendelea kusubiri na kusubiri inatukumbusha sisi tuliosoma zamani, kitabu kile cha kwanza kuna mtu anaonyeshwa, anatembea anatupa mikono hivi, fisi anaafuata mkono akitamani mkono utaanguka, hauanguki. Kwa hiyo, wataendelea kusubiri. Siyo Novemba 2005, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naanza kuingia katika hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mohamed Missanga, alisema Sheria ya Fidia ifanyiwe marekebisho. Ni kweli Serikali inajua hii Sheria ina mapungufu na hivi sasa tayari tumeshaandaa rasimu ya kujaribu kulizingatia suala hili, kutaka sheria ya kiinua mgongo ifanyiwe marekebisho kwa kuwa imepitwa na wakati. Ni kweli na hiyo pia tunaiangalia katika hii *Law Reform* au urejeaji wa Sheria za Kazi ambaa unaendelea hivi sasa na kwamba katika Bunge linalokuja ni Miswada ambayo italetwa mapema sana katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, alisema kufuatilia usumbufu wanaopata wafanyakazi walioachishwa kazi baada ya kustaaful watu wanapata matatizo makubwa. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, kwamba Serikali hili imeshalitupia macho na hasa baada ya kuunda Mfuko wa Pensheni wa Serikali. Sasa hivi

mtu anapostaafu siku anastaafu anakabidhiwa na *cheaque* yake au kama anachukua likizo ya kustaaafu anaporudi kukamilisha likizo yake anakabidhiwa *cheque* yake. Wale ambao rekodi zao hazijakamilika ndiyo ambao huchukua muda kidogo kama wiki mbili tatu, lakini huo udhaifu umeshasahihishwa ndani ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, aliuliza Serikali ina mpango gani wa kufungua Ofisi za Kazi katika Wilaya na kuzipatia vifaa na vitendea kazi? Sisi hufungua Ofisi za Kazi mahala ambapo pana wingi wa kazi. Kwa hiyo, hatuendi tu kwa maana ya Wilaya, basi lazima tuwe na Ofisi ya Idara ya Kazi, hapana. Kwa hiyo, hivi sasa kwa mfano tuko katika Wilaya 11, tuko katika Mikoa yote lakini tuko katika Wilaya 11 kutokana na wingi wa kazi na tuna namna ya kupata takwimu ili kuhakikisha kwamba tunafungua.

Mheshimiwa Edson Halinga, kutotekelezwa kwa uamuzi wa Baraza la Usuluhihi na Waziri anapoamriwa mfanyakazi arudishwe, kwa mfano Bibi Fimbo aliyekuwa mfanyakazi wa Benki ya Posta hutokea haya masuala. Lakini kinachohitajika ni Afisa wetu wa *Labour* mahala pale afahamishwe ili akazie hukumu. Inapokaziwa hukumu kama hakutekeleza, basi huyo mtu anaweza akashitakiwa tena Mahakamani ama na sisi wenyewe Wizara ya Kazi kwa kuitia Afisa wetu wa *Labour* au ye ye mwenyewe mfanyakazi aliyeambiwa arudi kazini. Lakini mwajiri anakwenda kuleta upuuzi, kwa hiyo, ni haki yake na uamuzi wetu ni halali na uamuzi wa Waziri ni wa mwisho.

Serikali ina mpango gani wa kufungua Ofisi za Kazi? Hiyo nimeshazungumzia. Serikali kuanzisha chombo cha kusimamia hifadhi ya jamii, Serikali imetambua uwepo wa mapungufu katika uendeshaji na usimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii na hatua zifuatazo zimeanza kuchukuliwa, kuandaa na kufanikisha kuwepo kwa Sera ya Hifadhi ya Jamii. Sera hii inaelekeza pamoja na mambo mengine, kuundwa chombo kitakachoratibu na kusimamia shughuli za hifadhi ya jamii. Hili nalo litakuja katika Sheria ambazo hivi sasa rasimu zinaandaliwa.

Mheshimiwa Semindu Pawa, viwanda ambavyo vina migogoro na vijana waliopata ajira wanapoonewa na matajiri mbona Serikali iko kimya? Serikali haikai kimya kunapokuwa na migogoro. Serikali ikipelekewa migogoro inakwenda kwa wakati muafaka kabisa kutatua. Ambacho hakitoeki ni kwamba inawezekana hata siku tukisikia Kigoma kumetokea kitu fulani, basi moja kwa moja iende kule. Ni sawa sawa na Hakimu. Hakimu hawezi akapita barabarani anakuta watu wanagombana anasema sasa ndiyo ninahukumu hapa hapa. Haiwezekani!

Kwa hiyo, sisi tunasubiri taratibu za kazi zifuatwe. Kwanza pale kazini kuna Tawi, tukitoka kwenye Tawi tunakwenda kwenye Baraza la Usuluhihi, tukitoka kwenye Baraza la Usuluhihi ndiyo tunakuja mpaka kwa Kamishna wa Kazi kuitia kwa Waziri. Kwa hiyo, taratibu ndiyo hizo, siyo kama tunalegalega, hapana.

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali; je, hizi sheria zinazofanyiwa marekebisho ya wafanyakazi wanazijua? Kama wanazijua, ni njia gani zimetumika? Kama hawazijui kwa nini hawaelekezwi? Sheria hizi baada ya kutoka, kinachoendelea sasa ni uhamasishaji na uelimishaji wa wahusika. Hizi Sheria za Kazi haziwahu su tu

wafanyakazi zinawahusu hata Waajiri. Katika hili naomba niwapongeze sana *ATE* kupitia Mwenyekiti wao ambaye kwa bahati nzuri yuko hapa leo, wao wamekwenda hatua moja zaidi wametengeneza hata vitabu vidogo vidogo unatembea nacho mfukoni, kitabu kimoja kinahusu sheria zile za Taasisi za kazi, kitabu kingine kinahusu mahusiano kazini.

Kwa hiyo, inakuwa Mwajiri hana sababu tena kusema mbona sijaelewa hapa. Kwa hiyo, wanachukua hatua ya kuelimishana, *TUKTA* vile vile tunasaidiana nao kupitia kuelimishana na wafanyakazi. Kwa hiyo, kama zimekaa tu katika ma-shelf hapana.

Mheshimiwa Haroub alipokuwa akichangia kama Makamu Mwenyekiti, alizungumzia kuhusu watoto wanaoishi uwanja wa fisi. Aliuliza Serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia hawa watoto, pamoja na watoto wa Mitaani? Sisi kama Serikali tunawajua wale, tunawatambua na tunashirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) mara kwa mara tunawatembalea, lakini mpango endelevu ni kwamba tunajaribu sasa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ili wajue kwamba wale ni watoto wao, tunabuni mkakati wa kuweza kuishi nao pamoja.

Mheshimiwa Lubeleje tena aliuliza Serikali ina mpango gani wa kutenga bajeti ya kutosha kusaidia watoto yatima kupata elimu na matumizi mengine? Waheshimiwa Wabunge, kama mtakumbuka tulipoanza awamu hii mwaka 1995 hali ya fedha katika Serikali hii ilikuwa mbaya sana na leo hii mwaka 2005 ukiangalia jinsi bajeti zimekuwa zikiongezeka pamoja na Wizara ya Kazi ni kitu ambacho tunapaswa kumpongeza Rais wetu sana kwa ubunifu wake. (*Makofî*)

Vile vile tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amekuwa msimamizi wa shughuli za Serikalini kuhakikisha kwamba nidhamu ambayo inaongelewa katika ngazi ya juu inasimamiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Athuman Janguo ambaye alisema yeye ni baba yangu, sasa Mheshimiwa Janguo watu wakituangalia wanajua mbegu bora ni ipi. Sasa sijui wewe ndiyo baba mimi mtoto! (*Makofî/Kicheko*)

Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kusaidia Shule ya Wasioona Bwigiri? Hili Mheshimiwa Janguo tunashirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni na Halmashauri za Wilaya katika mpango wa uboreshaji wa elimu kwa ujumla hasa MMEM na MMES.

Mheshimiwa Paul Kimiti aliuliza Serikali inashirikiana vipi na Shirika lisilo la Kiserikali lijulikanalo kama *SOBA* Tanzania? Mheshimiwa Kimiti na Waheshimiwa Wabunge Serikali imeandaa Tume ya kudhibiti madawa ya kulevyta ambayo inakutanisha wadau mbalimbali, Wizara, NGOs ikiwa na pamoja na *SOBA* Tanzania, tunashirikiana nao *SOBA* katika Semina za kuandaa mikakati ya kupambana na athari ya matumizi mabaya ya madawa ya kulevyta.

Kuhusu Bajeti ya huduma kwa watu wenyе ulemavu kwamba iongezwe, hiyo kama nilivyokwishazungumza kwamba bajeti kidogo imeanza kuongezeka. Kwa mfano, tuchukue hata mwaka jana 2004, hili lilielezwa vile vile na Kamati ya Bunge. Bajeti ya chakula mwaka jana kwa watu wenyе ulemavu na makambi yetu ilikuwa Shilingi milioni 204. Mwaka huu tumetengewa Shilingi milioni 408 ikiwa ni ongezeko la asilimia 100. Ukichukulia kuboresha au kukarabati majengo yale, mwaka jana 2004 tulikuwa na sifuri kabisa! Mwaka huu 2005 tumepata Shilingi milioni 29. Madawa, mwaka jana tulipata Shilingi milioni taano, mwaka huu tumepata Shilingi milioni 15. Kwa hiyo, kama hali ya uchumi inavyozidi kuimarika katika Serikali, ndivyo ambavyo na sisi kama Wizara, hali yetu inazidi kuwa ahueni. (*Makofit*)

Kamati ya Bunge, Huduma za Jamii hali mbaya ya kufungwa kwa Vyuo vya watu wenyе ulemavu. Tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuhusu hali mbaya na kufungwa kwa Vyuo. Lakini hii ilitokana na bajeti kama nilivyozungumza, hali ya sasa inaendelea kuwa nzuri na baadhi ya Vyuo tumeanza kufungua. Nina hakika muda si mrefu Vyuo ambavyo vimefungwa vitafunguliwa. Lwanzari bado kimefungwa, mwaka huu wa fedha unaoisha sasa, kwenye *quarter* ya mwisho tumepeleka Shilingi milioni sita Lwanzari ili kuezeka upya paa ambalo lilikuwa limesombwa na upepo. Katika bajeti hii tumetengea Shilingi milioni 26 kuhakikisha tunakamilisha mipango ya maji na umeme ili baadaye sasa masomo yaweze kuanza. Huwezi ukaanza masomo katika mazingira ambayo katika Chuo hasa Chuo cha watu wenyе ulemavu hakuna maji, hakuna umeme.

Suala la Mtapika, kilichotokea pale Mheshimiwa Mkanga ni kwamba si chote kimebadilika kuwa Sekondari. Watu wa Sekondari kwa maana Halmashauri waliomba jengo moja, wamepewa jengo moja ambalo wanalitumia kwa kuazima. Lakini sehemu nyingine inaendelea kubaki kama Chuo. Tatizo lililopo ni kwamba, hata Chuo tulichonacho kule hakijai wanafunzi.

Mheshimiwa Mntangi, posho na mikopo kwa wazee, Chama cha *Tanzania Region Club* hii ina matatizo ambayo tunapaswa kushirikiana sisi na Wizara ya Mambo ya Ndani kulimaliza suala hili hasa kwa kuzingatia kuwa muda halali ya uongozi uliopo sasa umekwisha na hata Balozi wa Uingereza analijua hili, tunashirikiana naye kwa karibu sana. Anachosubiri Balozi wa Uingereza ni kuhakikisha kwamba tunapata uongozi kwa mujibu wa Katiba na kusimamia kwa karibu sana ili sasa kwa kushirikiana naye fedha kutoka Uingereza zianze kuingia nchini kuwahudumia wazee hao. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mkanga, ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa *UN* na wa *Convention* kuhusu haki kwa walemavu, ni kweli hatujahuduria. Lakini nchi hii ingehuduria Mikutano yote ya nje, basi bajeti yote ya Serikali ingekwenda katika kuhudumia safari tu. Sasa kinachotokea, pale ambapo tumekwama kabisa, tunao Mabalozi wetu kwa mfano kule *New York* tunao Mabalozi wale ambao wapo katika *UN* pale wa kudumu wanakwenda kuhuduria kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, haendi kama mtu binafsi, wanakwenda kwa niaba yetu. Sisi wanatupigia simu tunamweleza ambayo yanapaswa kuzungumza na yeze akimaliza kikao kile anatuletea *feedback*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mkanga siyo kama tumelipuuza. Lakini hata hivyo, kutokana na sasa inavyozidi kuwa bora, tutajitahidi kuhuduria safari hizi nyingine zinazokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa sera ya wazee, mikakati imeandaliwa, vikundi 205 vya wazee na Halmashauri za Wilaya 16 zimehamasishwa kwa sera. Wizara imetenga fedha mwaka huu 2005 kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji. Mfuko wa Wazee Wizara inaendelea kujadiliana na Hazina pamoja na Serikali kuititia *TASAF* imepeleka Shilingi milioni 35 kila Kijiji kwa ajili ya huduma za maendeleo kwa makundi maalum ikiwemo pamoja na wazee. Sasa huko nako tufanye kazi Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba wazee hawa nao wanapata nafasi ya kupata keki ambayo imepelekwa na Serikali.

Mheshimiwa Shoka Khamis amesema kuhusu wawekezaji kutotii na kuheshimu sheria na Kanuni na miongozo ya kiutumishi hapa nchini. Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo makisio yake tuone; kwanza pale *TIC* (Kituo cha Uwekezaji) tunaye mwakilishi ambaye anahakikisha mtu anapopata ile leseni yake kwenda kuwekeza na sheria za kazi anakabidhiwa na anaelekezwa. Pia kunakuwepo na Semina na warsha mbalimbali zinazolenga katika kuwawezesha wawezekaji wazingatie kanuni na sheria hizo.

Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali hufanya kaguzi za mara kwa mara ili kuona sheria na kanuni zinafuatwa. Tatizo tunalolipata wakati mwingine unawakuta Watanzania pale ukiwaliza maswali wanakuficha. Halafu wanakwenda kunung'unikia nje. Sasa hii inakuwa haitusaidii, wawe wa kweli Wakaguzi wetu wanapofika na hatua zitachukuliwa. Sheria za sasa hivi ukienda katika kitengo chetu cha Usalama Kazini, sheria inawawezesha kabisa kuchukua hatua. Idara ya Kazi yenye, Sheria inawawezesha kuchukua hatua. Lakini lazima tupewe ukweli.

Hapa narudia tena, ushirikiano tunaupata kutoka kwa Chama cha Waajiri, ni mkubwa sana. Nao wako tayari kuhakikisha kwamba wale waajiri wanaopaka matope jina lao wanaanza kuwashughulikia kwa maana ya kuwaelimisha zaidi kwa sababu wanawatia aibu.

Mheshimiwa Margareth Mkanga alisema bado walemavu hawajafikiriwa kwenye masuala mengi ikiwa ni pamoja na uwezo wao wa kuingia kwenye sehemu mbalimbali za majengo kama maliwato. Hii Mheshimiwa Mkanga, Serikali imekwishaona umuhimu wa kuwawezesha walemavu wafike kwenye sehemu mbalimbali za majengo kwa kuweka kipengele cha Sheria Na. 71 chini ya Sheria ya Afya na Usalama mahali pa kazi ya 2003 ambacho kinaagiza wajenzi wa majengo kuzingatia mahitaji ya wenye ulemavu wa viungo.

Hata *lift*, tumeshaagiza kutokana na Sheria hii kwamba *lift* zinatakiwa kuwa na namba maalum za *Braille* kwa ajili ya wasioona. Kwa hiyo, akifika akipapasa atakuta zinamwonyesha kwamba *floor number* ngapi na akifika pale inapiga kengele.

Mheshimiwa Talala Bana Mbise alisema kuwepo utaratibu utakaowawezesha wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuchukua sehemu ya fedha walizochangia katika Mifuko. Hili Serikali tumeshalionia kwamba lina ukiritimba. Katika Sheria mpya

tunategemea tutaondoa udhaifu huu. Mheshimiwa Mbunge ameshauri *NSSF* ihamishiwe Wizara ya Fedha kwa kuwa ni Taasisi ya Fedha.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mifuko ya pensheni sio Taasisi ya Fedha. Ni fedha za wafanyakazi na duniani kote zinasimamiwa na Wizara ama inayosimamia masuala ya wafanyakazi au Wizara ambayo inahusu Mifuko ya Pensheni yenye we na hata ukichukua chimbuko la *NSSF* ambayo inazungumziwa sana hapa sasa *NSSF* chimbuko lake ni kitengo kidogo kilichokuwa Wizara ya Kazi. Pale walipokiona kinakua wakaona ili wakipe kujitegemea, wakakimega kikakaa peke yake kikawa kinaitwa *National Provident Fund*.

Limepanuka dude hili kwa ubunifu wa viongozi waliokuwepo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mkulo kwa kazi mzito aliyoifanya mpaka kuliasisi Shirika lile mpaka kulifikasiha lilipofika, sasa limepanuka. Sasa kupanuka tu kwa sababu lina hela, siyo maana yake ni Taasisi ya Fedha. *This is a Social Security Institution, it is not a Financial Institution. (Makofî)*

Kambi ya Upinzani, wafanyakazi kutolipwa mafao kwa wakati, hilo nimekwishajibu. Kucheleta kutolewa kwa masuala ya wafanyakazi katika ngazi ya Baraza la Usuluhihi na Waziri; hii hutokea, sikatai, lakini kwa sababu hapa ni lazima makundi yote mawili yawepo tunapokwenda kusuluhihi, wafanyakazi wawepo na Waajiri wawepo. Sasa kila mtu anatoa sababu zake, mimi leo naumwa siji. Madhali ametoa taarifa, huwezi ukasema shauri yake na hata asipokuja bila taarifa lazima umpelekee *notice* tatu kama asipofika *notice* tatu ambazo unazipa nafasi ya mwezi mmoja mmoja ndipo unaweza ukasema tunaweza tukaamua bila yeye kuwepo. Kwa hiyo, lazima ukikiuka hizo tena hata uamuza wako utakuwa hauna maana.

Lakini vile vile kutokana na wingi wa wafanyakazi na kesi hizi kuwa nyingi na *labour force* tuliyonayo pale Wizarani, ni dhahiri faili itabidi zisubiri, siyo kwamba mtu mmoja anafanya hivyo kwa hiana au kwa roho mbaya, sio kweli.

Mheshimiwa Shoka Khamis, ucheleweshaji wa utatuzi, hili tayari. Mahakama ya Kazi, hii sasa nazungumzia Mahakama ya Kazi. Mahakama ya Kazi ilikuwa na matatizo yafuatayo:- Kwanza nafasi za kufanya kazi kwa maana ya majengo, sasa majengo yameongezeka; Pili, ilikuwa na upungufu wa wafanyakazi. Sasa wafanyakazi wameongezeka, walikuwa na Manaibu wa Mwenyekiti, walikuwa watatu, sasa ni sita na hivyo kuongeza idadi ya mashauri yanayoamuliwa kwa mwaka. Kubuniwa kwa mbinu za kumaliza mashauri. Lakini vile vile juhudhi zimefanywa kupata Wafadhili ambao wanasadidua kuboresha utendaji kazi wa Mahakama. Kukarabati majengo na kutoa mafunzo kwa watumishi.

Huu ni mpango ambao wanashirikiana na Serikali ya Denmark na nimezungumza hata vyombo vyta kutendea kazi vitakuwa vyta kisasa. Kwa hiyo, ni dhahiri basi wao wamejipa kwamba kwa mikakati hii Mahakama imejiwekea lengo la kumaliza mashauri

yanayoletwa Mahakamani ndani ya miezi sita. Hii ni hatua ya maendeleo ambayo imepigwa katika Mahakama yetu ya Kazi.

Ushirikiano wa karibu kati ya *NSSF* na wafanyabiashara Yusuf Manji wa *Quality Group*; katika vitu ambavyo vimeua baadhi ya Taasisi zetu ni kuingiliwa na wanasiasa. La kwanza kwa mfano unaagiza tu kanunue pale, hii haifai na la pili, ni kusema fanya biashara na huyu usifanye biashara na huyu. Hiyo vile vile haifai. *NSSF* katika Mashirika ambayo yanajitahidi kuwa na mfumo ulio wazi ili wanapofikia maamuzi kwamba tunachukua biashara hii na tunaacha biashara hii ni kitu ambacho unawenza ukakieleza bila aibu mahali popote. Hii biashara ambayo imefanywa na Manji imepitia tathmini mbalimbali wala siyo kwa kutathmini wao *NSSF* kwa kutumia watathmini au *valuers* ambao wameajiriwa na wamejajiri wengine wa kutoka nje na wengine wa kutoka ndani.

Walipothibitisha kwamba hii ni biashara safi, ikabidi *NSSF* wachukue. Lakini kwa nini walichukua? *NSSF* ni Shirika ambalo lazima lifanye biashara ili kuweza kukidhi haja ya mafao ambayo wanatoa kwa wafanyakazi au wanachama wao. Bila kufanya biashara, haiwezekani. Kwa hiyo, wanafanya biashara gani? Wanafanya biashara moja, ni hizi, *Treasury Bonds*, wanafanya na majengo wanajenga ya kudumu. Lakini vile vile wakaona biashara ya *EPZ* inavutia kwa sababu *EPZ* tunaweza tukapata hata pesa za kigeni. Sasa tunapata wapi *EPZ facilities* ambazo zimeshakamilika ambazo ziko karibu? Ndiyo katika kufanya *survey* walikuta kulikuwa na *Quality Group*, kuna nyingine *Millennium Park* na nyingine nyingi tu walipofanya tathmini kwa kutumia hawa *valuers* ambao wako na kwa kutumia mfumo wa uwazi na ukweli wakaona kwamba *Quality Group* inafaa ndiyo wakanunua.

Kwa hiyo, hakuna haja ya kuanza kutiliana mashaka kwa sababu hata ukienda katika mabenki, mabenki wana *customers* ambao wanasema *these are good customers*, wanajitahidi kuwashikilia kama mtu ambaye anafanya biashara nao ni msafi, hana matatizo wanafanya naye biashara. Sasa mkianza kusema aah!! Umeshafanya naye kazi mara moja imetosha, ukifanyanaye kazi mara mbili hakuna kitu; sio sahihi kabisa! Tuwaache *NSSF* wafanye kazi kama wanavyoona inafaa kwa kuzingatia maelekezo na sera za nchi za uchumi. (*Makofi*)

*NSSF* ni nyingi sana. Kwa nini zitumike kuwaendeleza wanachama? Nitalijibu baadaye. Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, ushauri kuhusu Serikali kuhimiza wananchi wote wenye uwezo wa kufanya kazi wafanye kazi, kufuata ushauri wa kimataifa kwamba kwa nchi maskini kama Tanzania kumlazimisha mtu kufanya kazi ni kosa, hiyo siyo sahihi. Anashauri Serikali ijitegemee katika suala hili na kupunguza umaskini, yaani tuachane na hiyo, tuseme tu lazima watu wafanye kazi.

Mheshimiwa Mbunge, ni kweli ni sahihi kabisa kwa watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi wafanye kazi. Lakini tukumbuke kwamba sisi siyo Kisiba. Tuna mikataba ambayo tumeingia. Lazima tuiheshimu, vinginevyo tutaonekana si waungwana. Kwa hiyo, bado tuna *legacy* ya kikoloni, nadhani kwamba kufanya kazi ni utumwa. Sasa

tutoke hapo tujaribu kuelimishana sisi kwa sisi mpaka tufike mahala tujue kwamba kazi ni kipimo cha utu na kwa wale wanaotoka ambao ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi, Sera yetu inasema kabisa kwamba kazi ni kipimo cha utu, kama hufanyi kazi wewe si mtu. Vyama vingine vingeiga pengine tungepiga hatua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali anasema *Dar es Salaam City* kuhatarisha usalama wa wasichana Chuo Kikuu. Mheshimiwa Mbunge, tunaamini wale wasichana pale Chuo Kikuu ni watu wazima, wameelimika, wanajua kwamba kupanga ni kuchagua na vile vile ukumbuke mpaka wamefika hapo wameruka vihunzi vingi tu. Kwa hiyo, kutumia uzoefu wa vihunzi walivyoruka, wataruka na hiki cha mwisho ili waweze kuhakikisha kwamba wanakamilisha elimu yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Aziza alielezea suala la uzoefu kwamba ni tatizo kwa ajira kwa vijana na vyema liondolewe katika matakwa ya ajira. Ni kweli suala la uzoefu ni tatizo. Lakini kuna baadhi ya viwanda limeanza kuliona hasa katika nchi changa kama hizi. Uking'ang'ania tu uzoefu, uzoefu ni tatizo, hata kupata wafanyakazi unaowahitaji. Kwa hiyo, unaweza kuchukua Watanzania ambao wamemaliza tu Vyuo, wanakwenda pale wanaajiriwa unaanza kuwafundisha. Mheshimiwa Aziza, lakini kuna kazi nyingine huwezi ukakwepa suala la uzoefu ni lazima lizingatiwe.

Sasa suala la Mheshimiwa Lwakatare anasema tatizo la ajira siyo la kumalizwa na mtu mmoja ni mchakato wa watu wengi. Sisi hatujasema hivyo, kwamba suala la ajira ni suala la Wizara ya Kazi tu peke yake. Sio kweli. Ni ushirikiano wa Wizara zote hasa ukishika MKUKUTA utakuta MKUKUTA umeni-cut across, ume-declare kabisa kwamba suala la kazi ni suala mtambuka. Kwa hiyo, sisi tunakubaliana lakini ungesoma MKUKUTA au ungekuwa unafuatilia yanayotokea ndani ya Serikali yanayofanyika katika Wizara ya Ujenzi ni sehemu ya kazi; yanayofanyika katika Maliasili na Utalii uliyozungumza ni sehemu ya kazi; yanayofanyika Wizara ya Elimu na Utamaduni wanapoajiri Walimu ni sehemu ya kazi na mambo kadha wa kadha. Ukienda Wizara ya Ardhi ndiyo kabisa!

Kwa hiyo, tunakwenda kwa kushirikiana, siyo kwamba Wizara ya Kazi basi ndiyo peke yake na ndiyo imepewa jukumu hili peke yake, hapana. Lakini napenda nikushukuru kwamba umempongeza vile vile Mheshimiwa Mkapa kwa kutamka rasmi kuwa hakuna Chama chochote chenye hatimiliki ya kutawala nchi hii. Mimi nakupongeza umeona kwamba kauli hiyo ina hekima. Lakini umesahau sehemu ya pili ya kauli hiyo.

Mheshimiwa Mkapa alisema kwamba bila kuwa na sera nzuri zinazoelezeka, zikaleta maana kwa Watanzania, hutaweza kupewa nafasi ya kuongoza nchi hii. Sasa kwa sababu sera zinazolewaka, sera nzuri, zinazoleta maana na kutafsirika kwa vitendo, ni Sera za CCM, bila ya kuwa na hatimiliki ya karatasi CCM itaendelea kutawala nchi hii miaka mingi sana ijayo. Sasa hili hukulisema Mheshimiwa Lwakatare. Ni vyema ungelisema hilo ili kukamilisha pongezi zako kwa Mheshimiwa Mkapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mgaywa umesema Serikali itoe *tax relief* kwa viwanda vinavyojengwa Vijijini. Hili wala halihitaji mkakati maalum. *TIC* ndiyo kazi yake hiyo, ukiangalia ile *incentive scheme* ya wawekezaji katika nchi hii inasemekana kama ndiyo ya kwanza katika Bara zima la Afrika. Sasa haibagui ile *package* ya uwekezaji ya kwamba ukijenga Mijini, ndiyo utapata hii *package*, ukijenga vijijini hapana, utatozwa kodi, sio kweli. Kwa hiyo, kama unao wawekezaji walete twende nao *TIC* watapata. Haibagui ile *package* ambayo haijapata kutokea katika bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Mgaywa, anasema wakulima waingizwe katika utaratibu wa *NSSF* kwani katika maisha yao baadaye wanapata taabu sana, tunakubaliana na wewe. *NSSF* imefanya utafiti wa awali wa kuwajumuisha watu walio katika sekta isiyo rasmi ikiwa ni pamoja na wakulima. Matokeo yameonyesha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuwaingiza katika Mfuko wa *NSSF* wa njia ya hiari. Hivyo *NSSF* ipo katika maandalizi ya kutekeleza mapendelekezo hayo pia kwa kuzingatia mfumo maalum kwa wakulima. Mheshimiwa Paul Kimiti, mafanikio na matatizo ya Kituo cha Ajira angependa kabla hatujakwenda kwingine tumesema mwaka huu tunataka kujenga kufungua Kituo Mwanza. Mheshimiwa Kimiti na Waheshimiwa Wabunge, mafanikio ni kama yafuatavyo:-

- (a) Kituo kimewapatia wananchi mahali wanapoweza kuunganishwa na Waajiri na kupata ajira kwa urahisi na bila kuhangainka kuandika barua nyingi za maombi na kuzunguka kwa Waajiri wengi;
- (b) Kituo kimewaunganisha na Waajiri watafuta kazi 4,189 au asilimia 42 ya watafuta kazi waliosajiriwa kituoni na hivyo kuwapa fursa ya kushindania nafasi zilizopo katika soko la ajira;
- (c) Kituo kimewawezesha watafuta kazi zaidi ya 345 kupata ajira. Hawa ni asilimia nane ya wanaotafuta kazi waliouanganishwa na Waajiri..
- (d) Mafanikio mengine makubwa ya Kituo kuwapa moyo na matumaini wananchi katika juhudzi za kutafuta ajira kwa kutoa huduma za kufundisha jinsi ya kufanya vizuri katika usaili wa kazi. Sababu hata usaili nao una matatizo yake, unapokwenda kuulizwa maswali unaweza kujibu unavyojibu maswali unavyoji-*present*, hata kuvalaa wakati mwengine ni tatizo. Kila kazi inastahili yake kama unakwenda kutafuta kazi ya Benki ukaenda umevaa *T-shirt* imeandikwa hi hi! Basi pale Meneja anakuona, anasema huyu! Basi ahsante sana. *Have your cup of tea and you leave this.* Kituo kimewapatia Waajiri mahali pa kupata wafanyakazi wenye sifa wanaozitaka kwa urahisi na ufanisi na hivyo kuwawezesha kuinua tija.

Matatizo yaliyokikabili kituo ni yafuatayo:-

- (a) Upungufu wa fedha;

- (b) Baadhi ya watafuta kazi hawana njia za uhakika na za haraka za mawasiliano kama simu au barua pepe hivyo inakuwa vigumu kuwapata wakati nafasi za ajira zinapopatikana. Watafuta kazi wengi hukosa ajira kwa sababu hii na hili nalo ni tatizo kwelikweli. *We have people of no fixed aboard!* Hawana anuani kamili, anafika anaandikisha anapotea halafu bahati nzuri ndio wengi ambao wanapata nafasi ambao wanasesma *I want this one*, unamatfuta huna pa kumpata. Sasa imekuwa ni matatizo. Sasa tungependa basi wajitahidi kuwa na anuani ya kudumu.

Mheshimiwa Athumani Janguo, ujuzi wa watu kuweza kujiajiri na kuondoa umaskini, *demand driven skills* kama nilivyoeleza katika hotuba yangu hata tarehe 30/6/2005 Wilaya 57 zimepatiwa mafunzo. Wakati huu Wilaya 20 zinaendelea na mafunzo na tumeonyesha kitakwimu jinsi ambavyo wanawake na wanaume wanavyofaidika na mpango huu. Mheshimiwa Shoka, takwimu zinaonyesha idadi ya watu wote Dar es Salaam ni 2,690,399, wanaoishi Dar es Salaam 46 katika bajeti ya Serikali haionyeshi mkakati gani ili kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Shoka ukiangalia Dar es Salaam ilivyo ni kwa sababu ya fursa zilizopo pale ndio maana watu wanafurika Dar es Salaam. Nadhani hizi *figure* ulizonazo wewe umefanya hiyo kwa hisia, ungekuja ukachukua takwimu zetu ambazo ziko katika Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa kutumia *labour force survey* utakuta ni asilimia 12, sio asilimia 46.

Mheshimiwa Mutungirehi, kati ya watafuta kazi 700 waliopata ni 300 tu. Sawa, lakini tatizo kubwa ni kwamba ushindani katika soko la ajira ni mkubwa na watu wenye sifa zinazolingana na matakwa ya Waajiri ndio wanaozipata nafasi chache za ajira zilizopo.

Mheshimiwa Aziza pia alizungumza suala la uzoefu kama unavyokumbuka. Sasa kwa kuzingatia hayo ndio maana sisi kwa Kituo chetu kile kimeamua sasa kuwa na mkakati wa namna mbalimbali ya kuwasaidia kama nilivyoeleza ili waweze kukidhi haja ya haya Makampuni au ajira wanaotafuta wafanyakazi.

Mheshimiwa Mkanga, amerudi kwenye shida yetu ya kazi inayowabana Waajiri kutoa asilimia mbili kuwaajiri watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Mkanga, kwa kweli ni kama imepitwa na wakati. Baada ya Serikali kujitoa kuwa Mwaajiri mkubwa, sasa tunaiangalia upya jinsi ambavyo tunaweza tukasaidiana na Waajiri hawa namna ya kuweza kuchukua, pengine suala la motisha kama ulivyo-suggest tunaweza tukaliangalia ili kuweza kuhakikisha kwamba Waajiri wanawafikiria watu wenye ulemavu.

Wageni sasa huruhusiwa kuchukua hata nafasi ambazo Watanzania wanazimudu, haya mazungumzo ya jumla jumla huwa hayasaidii. Kama unao ushahidi kwamba mahali fulani yupo Dereva ambapo hata Mswahili angeweza kuwa Dereva, tuletee sisi tutashughulika. Lakini sasa usije ukasema kwamba kwa mfano, unaweza ukakuta mpishi

anapika, lakini ni chakula cha kichina na kile kina *test* maalum ambacho hakipikwi kutokana tu na cheti, kinapikwa kutokana na uzoefu.

Sasa huyo huwezi ukasema wapishi wapo ambao tunawaruhusu kabisa kutokana na sifa zao. Mheshimiwa Mungai, ana Kiwanda cha Chai Bora. Yule mwonja chai ana *experience* ya miaka zaidi ya thelathini. Kwa hiyo, hii na ukisema mpaka umpate mtu mwenye cheti itakuwa matatizo. Wafanyakazi wapewe mafunzo badala ya kuwatimua. Inapofikia suala la kupunguza wafanyakazi kazini, ujue imebidi, lakini hatuwafukuzi tu hivi hivi wanapewa kwanza stadi za kazi ili waweze kujiajiri wanapotoka hapo. Ajira ya walemovu ni ngumu, nimeshalizungumzia. Kasi ya upungufu wa ajira inaongezeka hilo tumeshazungumza.

Mheshimiwa Shoka Khamis, tena kusahauliwa kwa wachangia halisi, Mfuko wa huduma, Mfuko kufaidiwa na wengine kwamba watu wanachangia *NSSF* lakini wanaofaidi sio wanachama. Kulingana na Sheria iliyoanzishwa na Mfuko wa *NSSF* wanachama wa *NSSF* wamepata mafao yaliyoainishwa katika Sheria kama ifuatavyo:- Mafao yenye ni saba.

Ni pensheni ya uzee, mtu anapostaafu akiwa ni mwanachama wa *NSSF* anapata pensheni mpaka kufa kwake. Kwa wale wa kima cha chini wanapata asilimia 80 ya kima cha mshahara wa wakati ule, wale wengine inapungua mpaka kufikia asilimia 67. Kuna pensheni ya ulemavu, kuna pensheni ya wategemezi, kuna mafao ya kuumia kazini, ukiumia kazini unapata asilimia 50 ya mshahara wako kwa siku ambazo ukwenda kazini. Ikizidi wiki 26 unapata asilimia 60, pensheni ya utegemezi hivyo hivyo, mafao ya uzazi, mishahara ya wiki 12 pamoja na huduma za matibabu, mafao ya ajira sasa vyote hivi kama *NSSF* ndio niliyosema *NSSF* lazima ifanye biashara.

Kama *NSSF* ingekuwa imebweteka tu, kwamba tumepokea michango, tumekaa pembeni isingeweza kumudu uzito wa madude haya. Ndio maana *NSSF* inavutia, *NSSF* inatisha katika soko la mifuko ya pensheni kutokana na mambo haya. Hata ukifiwa, kuna msaada wa mazishi kutokana na michango yako. Unaweza ukapata Sh.75,000/=, Sh.150,000/= hata Sh.300,000/= na unajua unapofiwa wakati mwagine kwa sababu kifo hakipigi simu kinatokea tu, kinakuja wakati ambapo wewe umekauka kweli kweli. Kwa hiyo, sio kweli wanaofaidi ni wengine, wanachama ndio kwanza.

Wakaja na utaratibu wa Mfuko wa Kujenga Nyumba za Bei Nafuu, walengwa walikuwa ni wanachama wao na hao wanachama wanaelekezwa hata namna ya kuweza kupata fedha za kuweza kukopa, kama hawataki kulipa kwa taratibu za hela za kila mwezi na swali liliulizwa na Mheshimiwa Mbise, kwamba *NSSF* ni Taasisi ya fedha, hakuna.

Fedha zinazokusanywa na *NSSF* ni nyingi sana kwa nini zisitumike, hii nimeshaizungumza. Kwa nini *NSSF* isifanye kama mifuko mingine ya hifadhi ya jamii kuweka fedha katika mabenki kwa ajili ya kuwakopesha wanachama mikopo nafuu kwa maendeleo yao? Akasema mfuko ambao siutaji wanatumia Mashirika mengine kama *PPF*. Pamoja na kutokutaja, Mheshimiwa Mbise na Waheshimiwa Wabunge *NSSF*

imewekeza katika Benki ya Azania kama ilivyowekeza hiyo hiyo *PPF* aliyoitaja katika Benki hiyo. *NSSF* ina hisa zaidi katika Benki hiyo kama ifuatavyo:-

- *NSSF* asilimia 41.29;
- *PPF* asilimia 35.98;
- *PSPF* asilimia 12.35;
- *EADP asilimia 6.79; na*
- Watu binafsi asilimia 3.59.

Kwa hiyo, kama ni sifa, Mheshimiwa Mbise usingewapa *PPF* ungewapa *NSSF* kwa sababu ndio wenyе *majority shares* katika Benki hiyo na ndio inatoa mikopo yenyе riba nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Bujiku Sakila, aliuliza: Je, kuna uwezekano wa watumishi wa Halmashauri za Wilaya kujengewa nyumba za bei nafuu na kuuziwa kwa mikopo kupitia Halmashauri zao. Wazo hili Mheshimiwa Sakila, tunalipokea lakini linahitaji kuchambuliwa zaidi ili tulifanyie kazi. Wizara na Shirika la *NSSF* wamelichukua suala kwa ajili ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa kunipa nafasi. Kama muda mnavyouona unatutupa mkono, niishie kwa kusema kwa yale ambayo hatujayagusia. Sio kwamba tumeyapuuza, hapa tunaendelea kuyafanya kazi kwa ajili ya kuimarisha huduma katika Wizara yetu ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Taasisi zake zote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 60 – Mahakama ya Kazi Tanzania**

Kif. 1001-*Administration and General*... . . . . . Sh. 408,581,700/=

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba radhi nitakuja kwenye kifungu 1001.

**MWENYEKITI:** Hii ni Mahakama ya Kazi kama.....

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Nasema naomba radhi nitakuja kwenye kifungu kile cha mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Basi hatujafika huko.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001-Arusha Zone ..... Sh. 74,407,900/=  
Kif. 2002-Dar es Salaam ..... Sh.46,338,200/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 65 – Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo**

Kif. 1001-Administration and General ..... Sh.1,449,074,000/=

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi baada ya kushindwa kupata nafasi wakati tulikuwa tunachangia kwa mdomo, nilizungumzia suala la migogoro iliyopo sasa kwenye Klabu ya Yanga na Klabu ya Simba kwamba migogoro hii inakwamisha maendeleo ya michezo hapa nchini na kwamba uongozi mpya wa *TFF* hata ukifanya nini kama utulivu na amani haupo kwenye klabu zetu hizi hasa hizi kubwa mbili hatuwezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ni kwamba mwaka 1974 hali ya utulivu ilipokuwa nzuri, Tanzania tulipata vikombe vitatu. Tulipata *Youth Challenge Cup* tukashinda, *Eastern Central Senior Challenge Cup Eastern Central* tukashinda na Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki tukashinda. Kwa sababu hali ilikuwa nzuri kwa utulivu na amani kwenye vilabu vyetu.

Sasa hii migogoro ambayo iko kwenye Yanga na Simba kwa muda mrefu na Serikali inasikia. Wasiwasi wangu ni kwamba, kwa mfano ukichukua Yanga, yako makundi mawili ambayo yanajulikana yanapingana kweli kweli, kila mtu anataka kutumia lile jengo. Wasiwasi wangu ni kwamba iko siku wataumizana, watakufa watu pale ndipo Serikali iseme sasa tumejifunza. Kwa sababu siku zote tukipata majanga ndio Serikali inasema sasa tumejifunza.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuchukua hatua thabiti ya kuondokana na migogoro hii? Kwa sababu kwanza wale wanaofanya migogoro kwa kweli wanafahamika, ni wale wale wa kila siku, wanafahamika tu. Simba wanafahamika, Yanga wanafahamika, sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa hakuligusia hili labda kwa sababu ya muda, atuambie Serikali inachukua hatua gani hasa kule Yanga, niondokane na mawazo potofu ambayo wapenzi wa mpira wanasema mgogoro ule ungekuwa Simba sasa hivi ulikuwa umeshamalizika kama ambavyo ulifurukuta na ukamalizwa. Sasa Yanga kuna nini? Hebu Mheshimiwa Waziri hao wanaokupaka matope kwa sababu eti wewe ndio hivyo, hebu wasaidie hao wanayanga tatizo lao liishe. Serikali inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili niligusia kidogo tu habari ya matatizo ya uongozi katika *TABA* na kwamba kuna matatizo pale, nafikiri walinielewa. Naomba Mheshimiwa Waziri aseme hatua gani wanachukua kuokoa mchezo wetu wa ngumi za ridhaa ambao kama nilivyosema tulipata medali ya kwanza mwaka 1970 chini ya Marehemu Titus Simba; Je, Serikali inafanya nini kuhusu hasa BMT au Msajili juu ya mgogoro uliopo katika Chama cha Mpira na cha Ngumi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na jibu tumeliandaa lakini kama tulivyosema kwa sababu ya muda tulishindwa kulielezea. Katika mchango wake wa maandishi Mheshimiwa Mohamed Missanga amesema: "Namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa jumla kutafuta njia ya kumaliza mgogoro katika vilabu hasa Simba na Yanga." Huu ndio mchango wake wenyewe maandishi na sisi jibu letu ni hili lifuatalo:-

Kwanza tumeshukuru juu ya maoni yake na *concern* yake juu ya dosari hizi za aibu katika medani yetu ya soka hapa nchini. Lakini tunesema vilevile kwamba maoni yake hayo yataendelea kutusaidia sisi katika jitihada ambazo tayari zimeshaanza kati ya Wizara, *BMT* na *TFF*, katika juhudi zetu namba moja za kurekebisha kasoro hii ya aibu, na kama tunavyofahamu sisi tusingependa kulikuza jambo hili lioneckane kwamba la wale watu wanaotajwa kila siku kwa sababu wanachama wa Simba na Yanga wako Tanzania nzima na sio Dar es Salaam tu na ndio maana tumeamua kuchukua njia za hekima zinaweza zikatuchelewesa lakini tutakapofikia muafaka utakuwa ni muafaka wa kudumu kama ule ambao ultiokena katika *TFF* yenye.

Hili la pili alilolizungumza la *TABA*, alikuwa na wasiwasi kwamba matatizo ya Chama cha Ngumi yanatokana na uongozi uliowekwa na vilabu badala ya Mikoa. Je, Serikali iangalie suala hilo? Sisi tunasema uongozi wa *TABA* ni uongozi halali na uliowekwa na vilabu kutoka Tanzania nzima na sio Dar es Salaam peke. Baada ya kubaini udanganyifu uliofanywa na waliokuwa wanajitiita Vyama vya Mikoa, kulikuwepo na Vyama viwili vya Mikoa vilivyosajiliwa viwili tu. Hivi sasa Mkutano umepangwa Agosti,30 mwaka huu 2005 ili pamoja na mambo mengine kupitia hiyo Katiba chini ya uongozi huu halali ili tuondoshe haya matatizo ya uongozi yanayojitokeza mara kwa mara. Nakushukuru sana.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini katika hili la pili pamoja na haya ambayo ameyasema, tatizo lililopo ni kwamba huyo Katibu Mkuu wa Chama hicho cha *TABA* ameenguliwa na hafanyi kazi yake ya Ukatibu Mkuu na kwamba mawasiliano sasa yanakwenda kwa uongozi mwingine, labda Mwenyekiti na kadhalika. Wakati Msajili mwenyewe na *BMT* na hasa *TLS* wamekataa kuwasiliana na mtu mwingine kwa sababu kwa utaratibu lazima wawasiliane na Katibu Mkuu wa hicho Chama na hapewi nafasi ya kufanya kazi. Sasa ukiacha hayo mambo labda mvutano na Katiba lakini bado liko tatizo kwamba Chama hiki hakifanyi kazi kwa sababu yule Katibu Mkuu aliyechaguliwa kihalali kama anavyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hapewi nafasi ya kufanya kazi

katika Chama hicho. Huo peke yake ni mgogoro. Je, hilo Mheshimiwa Waziri anasemaje?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na yeye kwamba viongozi wenzake wamemuengua Katibu Mkuu na wamemuengua kwa sababu huyu Katibu Mkuu anafanya kazi kwa kufuata Katiba na sio ubabaishaji ambao umezoleka ndani ya Chama hicho, lakini kwa bahati mbayo hao waliomuengua hawana uwezo wa kuwasiliana na Wizara, hawana uwezo wa kuwasiliana na Tanzania *Olympic Committee* wala hawana uwezo wa kuwasiliana na BMT. Mawasiliano yote ya vyombo hivi nya Serikali pamoja na *TOC* yanafanya kupitia kwa Katibu Mkuu huyu ambao wao wanafikiria wamemuengua.

Kwa hiyo, wamemuengua kwa maneno tu lakini utendaji wa Ofisi yote anayofanya ni huyu. Ndio maana hata huo Mkutano wa tarehe 30 Agosti, unasi mamiwa na huyu na wale Wajumbe watakaokuja, tutaendelea na Mkutano wetu na hao wengine basi wasubiri siku hiyo waone kama wataendelea kuwa na nguvu bado ya kwenda kinyume na Katiba waliyoikubali wenyewe.

Namwomba Mheshimiwa Missanga avute subira na kwa sababu na yeye ni mdau aliyetusaidia sana katika kutatua mgogoro wa *TFF* tunategemea sana ushirikiano wake pamoja na kwamba kipindi hicho atakuwa kwenye kinyang'anyiro kikali, lakini tunaamini ata-*spare* muda wake ili atusaidie kuondoa tatizo hili.

**MHE. DR. THADEUS M.LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante *Vote 65 program 10 sub-vote 1001 - Mshahara wa Waziri*. Kwanza naishukuru Serikali kwa kutenga makazi ya wazee na watu wasiojiweza na vile vile kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuwashudumia hawa wale mavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba tu nipaye ufanuzi. Wizara inafuutilia matumizi ya fedha kwa sababu katika Kambi ya N'nge kuna wale mavu pale, kuna watumishi wako pale wanalipwa mshahara lakini utakuta madawa hayaendi kwa wakati, chakula hakiendi kwa wakati, walengwa wanapata matatizo: Je, Serikali inafuutilia hali hiyo? Lengo lenyewe ni zuri lakini utekezaji kidogo unakwamakwama ningeomba ufanuzi.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua kipengele alichokieleza Mheshimiwa Dr. Luoga. Serikali inafuutilia matumizi, lakini tunafuutilia matumizi kwa kushirikiana na wenzetu wa Halmashauri ambao wako karibu. Sasa kama kuna mapungufu ya dhahiri, ya wazi wazi ambayo unayasema angetuletea ili tuweze kutuma sasa Tume maalum kutoka Makao Makuu ya Wizara twende tukaliangalie kutokana na hali halisi iliyoko pale. Lakini ufuutiliaji huwa tunafanya, hata ma-auditor wetu huwa wanafanya *pre-audit checks* lakini kutokana na hali halisi ya ukubwa wa nchi wakati mwingine inaweza ikapita miaka miwili mitatu hatujafika katika kituo fulani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*

*ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> .....	Sh. 294,723,800/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> .....	Sh. 598,255,400/=
Kif. 2001 - <i>Labour</i> .....	Sh. 1,867,489,900/=
Kif. 2002 - <i>Employment Division</i> .....	Sh. 972,628,100/=
Kif. 4001 - <i>Social Welfare</i> .....	Sh. 3,089,965,100/=
Kif. 5001 - <i>Youth Development</i> .....	Sh. 1,138,348,400/=
Kif. 6004 - <i>Sports Development</i> .....	Sh. 879,583,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 60 – Mahakama ya Kazi**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> .....	Sh. 732,000,000/=
---	-------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 65 - Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> .....	Sh. 40,400,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> .....	Sh. 9,377,579,900/=
Kif. 2001 - <i>Labour</i> .....	Sh. 312,018,900/=
Kif. 4001 - <i>Social Welfare</i> .....	Sh. 5,391,620,200/=
Kif. 5001 - <i>Youth Development</i> .....	Sh. 34,500,000/=
Kif. 6001 - <i>Sports Development</i> .....	Sh. 12,508,100,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mwaka wa fedha 2005/2006, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana  
na Michezo yalipitishwa na Bunge*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa Kikao cha leo. Kwa hiyo, Bunge linahairishwa mpaka kesho asubuhi saa tatu.

(*Saa 12:56 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne  
tarehe 26 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi*)